

M A P

# MAPINDUZI YAKO YA KIFEDHA

Nguvu ya kuwa Mwaminifu

I N D

# GARY KEESEE

U Z I



M A P

# MAPINDUZI YAKO YA KIFEDHA

Nguvu ya kuwa Mwaminifu

I N D

# GARY KEESEE

U Z I

**Your Financial Revolution**

*Power of Allegiance*, Kiswahili By Gary Keesee

© Gary Keesee, 2022

Originally published in English

ISBN: 978-1-945930-03-4

Faith Life Now

P.O. Box 779

New Albany, OH 43054, USA

You can reach Faith Life Now Ministries on the Internet at

[FaithLifeNow.com](http://FaithLifeNow.com)

**Mapinduzi yako ya Kifedha**

*Nguvu ya kuwa Mwaminifu*, Kiswahili na Gary Keesee

© Gary Keesee, 2022

Awali kilichapishwa katika lugha ya Kiingereza

ISBN: 978-1-945930-03-4

Faith Life Now

P.O. Box 779

New Albany, OH 43054, USA

Unaweza kufikia Faith Life Now Ministries kwenye mtandao kupitia

[FaithLifeNow.com](http://FaithLifeNow.com)

# **YALIYOMO**

<b>DIBAJI .....</b>	7
<b>UTANGULIZI .....</b>	9
<b>SURA YA 1: Ufalme .....</b>	19
<b>SURA YA 2: Ukungu Wa Rangi Ya Samawati .....</b>	51
<b>SURA YA 3: Tafadhalii MUNGU, Uturehemu! .....</b>	57
<b>SURA YA 4: Samaki Mkubwa .....</b>	81
<b>SURA YA 5: Ulikuwa Uamuzi Wa Nani? .....</b>	89
<b>SURA YA 6: Baraka Ya Bwana.....</b>	117
<b>SURA YA 7: Mlango .....</b>	133
<b>SURA YA 8: Nguvu Ya Kuwa Mwaminifu.....</b>	141
<b>SURA YA 9: Wapeni Ninyi Chakula .....</b>	149
<b>SURA YA 10: Kusanya, Wala Usitokwe Na Jasho .....</b>	161
<b>SURA YA 11: Kusafiri Kwa Ndege Ni Rahisi Kuliko Kutembea! .....</b>	167



# DIBAJI

Kwa miaka kadhaa sasa, nimetamani kuandika kuhusu safari ambayo Mungu ametupitisha mimi na Drenda. Maisha yetu yamebadilika sana! Tumeona miujiza yote ambayo Yesu alifanya katika Biblia ikitukia mbele ya macho yetu kwa miaka mingi: wafu kufufuliwa; waliopooza kuamka, kutembea, na kurudi kazini siku iliyofuata; wagonjwa kupona; na fedha kurejeshwa kwa mamia ya maelfu ya watu. Lakini miujiza mikubwa zaidi ambayo tumeona ilitokea katika familia yetu na maisha yetu binafsi.

Lengo langu ni kukupeleka kwenye safari, safari ya ugunduzi ambayo natumai itabertilisha maisha yako kama yangu. Hadithi hii haiwezi kusimuliwa kwa kitabu kimoja. Hiki ni kitabu cha kwanza kati ya mfululizo wa vitabu vitakavyokuongoza katika mapinduzi yako binafsi ya kifedha na kitaanza kufichua mafumbo ya Ufalme wa Mungu yaliyobadilisha maisha yangu. Kwangu mimi, ni safari ya kusisimua ambayo haitaisha. Sote tutaendelea kujifunza! Ujuzi wa Ufalme hauwezi kwisha.

Namshukuru sana Mungu. Rehema Zake ni mpya kila siku, Yeye ni mvumilivu na mwenye kusamehe, na hutuongoza katika njia ya wokovu. Siwezi kukupeleka kwenye safari hii bila kwanza kumtaja mke wangu wa ajabu, Drenda. Ni moyo wake, upendo na subira ya Mungu ndani yake iliyonipa ujasiri wa kukabiliana na udhaifu wangu na kumtafuta Mungu ili kupata majibu niliyohitaji sana. Nina furaha kuu kushirikiana nawe:

Mapinduzi Yako ya Kifedha  
*Nguvu ya kuwa Mwaminifu*





# UTANGULIZI

*Nimenyimwa amani; Nimesahau ustawi ni nini.*  
– Maombolezo 3:17

Niliamka na ufahamu kwamba mambo yote hayakuwa sawa! Hofu kuu ilijaa moyoni mwangu nilipoamka. Sikuwa na uwezo wa kuhisi ulimi wangu. Mikono, miguu, na upande mmoja wa uso wangu ulikuwa umekufa ganzi. Nilimwamsha Drenda na nikawa na ugumu kumweleza kilichokuwa kikiendelea huku uso na ulimi wangu wote ukikataa kushirikiana. Kisha nikagundua kuwa moyo wangu ulikuwa unapiga kwa kasi na nilikuwa na shida ya kupumua nilipomshirikisha hali yangu. Aliamka na mara moja akaanza kuniombea. Polepole, hisia hizo zisizoleweka na za kutisha zilipungua kidogo. Nilijilaza tena kitandani huku Drenda akijitolea kuniletea chakula. Nilichanganyikiwa na kuogopa kile kilichokuwa kinatokea mwilini mwangu huku nikiwa nimelala pale nikiomba. Mawimbi ya wasiwasi yalipita juu yangu; hofu ambayo sijawahi kuhisi hapo awali katika maisha yangu ilishambulia akili yangu.

Deni nililokuwa nalo na hitaji lililodumu la pesa lilifanya woga kuwa sehemu ya kawaida maishani mwangu kila siku. Nilikuwa na fadhaba kuu katika miaka michache iliyopita kuhusiana na kuzorota kwa hali yangu ya kifedha. Kazi yangu ilikuwa ya kuuza vitu na kulipwa kamisheni lakini sikuwa nikifua dafu. Tulikuwa tukikodisha nyumba ndogo mashambani ya miaka ya 1800 ilioonekana kana kwamba haikuwa imefanyiwa marekebisho tangu ilipojengwa. Nafikiri natia chumvi hapa kidogo, lakini nyumba haikuwa katika hali nzuri. Viunzi vya dirisha vilikuwa na mapengo ndani yake ambapo mimea ilikua kupitia kwao hadi kwenye sebule yetu. Vidirisha vingi vilikuwa vimevnjika, na tulikuwa tumevisfunga kwa bamba na mkanda. Ingawa nyumba hiyo ilikuwa imechakaa, Drenda aliweza kuifanya kuwa makao yetu. Lakini hata kwa ustadi wake wa ajabu, hatukuweza kufunkika ukweli kwamba kulikuwa na shida nydingi na nyumba hiyo.

Kila kitu tulichokuwa nacho kilikuwa katika hali ileile—ya kuvunjika! Magari yetu yote mawili yalikuwa ya kale, yalikuwa yametumika zaidi ya maili 200,000, na haikuwa rahisi kuanzisha injini. Wavulana wetu wawili walilala kwenye magodoro yaliyokuwa yakitupwa na makao ya kuwatunzia

wazee, zulia kwenye sakafu ya chumba chao cha kulala lilipatikana kando ya barabara kwenye takataka. Maduka ya ukopeshaji yalikuwa kawaida kwetu, na tulimwomba yejote tuliyefikiri angeweza kutusaidia. Kila siku tulikuwa na pesa za kutosha tu bila za ziada, tulitafuta kitu cha kuuza, kisha tungetafuta jinsi ya kuishi, na kutumaini kwamba kesho itakuwa bora.

Kwa sababu ya kukopa kupita kiasi, kadi zangu kumi za mkopo zilikuwa zimeghairiwa miezi kadhaa iliyopita, na watoza deni walikuwa wametumwa kuchukua fedha hizo za kampuni tatu, ambazo sasa zilikuwa zimeongezeka kwa asilimia 28. Malipo ya gari langu (naam, bado nilikuwa na deni la magari yangu yaliyokuwa yamechakaa) lilikuwa limechelewa kwa siku 120 na katika hathihi ya kupokonywa. Kila bili niliyokuwa nayo ilikuwa imechelewa. Hukumu na kuchukuliwa kwa haki ya kuwa mmiliki zilikuwa zimeanzishwa dhidi yangu, na simu za kupokonywa mali yangu ziliniamsha kila asubuhi. Nilidaiwa pesa na shirika la ushuru wa serikali, na wao pia walikuwa wameanzisha shtaka dhidi yangu kwa kuchelewa kulipa ushuru. Mimi na Drenda tulikuwa na deni la wazazi wetu dola 26,000, na walikuwa wamechoka kutusaidia. Jokofu letu mara nyingi halikuwa na chochote. Wakati mwingine kila mwezi, umeme wetu ulikuwa ukitishiwa kuzimwa na kampuni ya umeme. Na nilikuwa nimefikia mwisho kihisias.

Sasa msongo wa mawazo ulikuwa ukifanyia mwili wangu kitu ambacho sikukielewa. Baada ya kuwaona madaktari kadhaa, walisema nimepata mshtuko wa hofu na wakanipa dawa za kupunguza huzuni. Kwa bahati mbaya, mashambulizi haya ya hofu yaliendelea kuongezeka mara kwa mara hadi nikawa na hofu kuondoka nyumbani kwangu. Katika nyakati hizi za hofu, nilipokuwa nikitafuta majibu, nilianza kugundua kwamba vyakula fulani, vyenye sukari, wanga, au kafeini, vilisababisha mashambulio mengine ya hofu. Kwa hiyo sasa niliogopa kula chakula na nilikuwa na ufahamu wa kila kitu nilichokula. Maisha yangu yakawa ya utumwa hadi sasa singeweza kufanya kazi, jambo ambalo bila shaka lilifanya hali ya kifedha kuzorota zaidi.

Mke wangu alifikiri angempoteza mume wake, na aliniambia baadaye baada ya kuponywa kwamba alikuwa akipanga kihalisi kile ambacho angepaswa kufanya ili kuwatunza watoto wetu. Nilimlilia Mungu anijibu kwani sikuwa na uzoefu wala ujuzi wa kile nilichokuwa nikikabiliana nacho. Madaktari walikuwa na majina makubwa kwa tatizo langu, wakisema haliwezi kuponywa na kwamba ningetumia madawa milele. Madaktari wengine walisema kwamba nilikuwa karibu kuwa na ugonjwa wa kisukari, wakisema kwamba ningekuwa wa kufaa katika kufanyiwa uchunguzi kadri

ugonjwa unavyoendelea kadri ninavyozeeka.

Ingawa nilikuwa Mkristo, sikuwa na uzoefu katika vita vya kiroho au jinsi ya kusimama dhidi ya adui. Kwa kweli, wakati huu sikuwa nimetambua kwamba nilikuwa nikipambana na roho ya kishetani. Nilifikiri nilikuwa na tatizo la mwili wangu tu na nilikuwa nikimwomba Mungu aniponye. Mimi kama Mkristo, nilijua kwamba Mungu ndiye jibu langu, lakini wakati huo nilihisi kwamba Mungu alikuwa mbali sana. Madaktari walinipa majina mbalimbali ya hali niliyokuwa nayo, yote yalihusiana na matatizo ya akili yanayotibika kwa kutumia dawa mbalimbali. Kama nilivyosema awali, hakukuwa na tiba, bali tu matibabu yaliyosaidia kukabili hali yangu ya akili. Nilikuwa na athari za madawa, hata hivyo, na hayakunisaidia hata kidogo. Kwa kweli, naamini yaliongeza dalili zingine mwilini. Yalinifanya nihisi kana kwamba nilikuwa nikiishi katika ukungu, huku nikiteswa kila mara na mawazo ya woga ambayo nisingeweza kuyadhibiti. Sikuwa na majibu, na hakuna chochote kilichonisaidia. Jambo hili liliendelea kwa wiki chache, na kukata tamaa kwangu kuliongezeka wakati dalili na hofu zilipoonekana kuyatawala maisha yangu.

Lakini usiku mmoja, nilipata mafanikio makubwa nilipomtafuta Mungu ili kupata majibu. Niligundua jambo muhimu katika kupata uhuru wangu. Nilikuwa kanisani nikihudhuria ibada ya Jumatano jioni. Wakati wa sifa na kuabudu, nilishikwa na hofu kubwa. Sikujua la kufanya. Nilikuwa nimekata tamaa, na nilifahamu nilihitaji maombi, kwa hiyo nilienda mbele ya kanisa. Ingawa nilikuwa nikikatiza ibada kabisa, sikujali. Nilikuwa mshirika wa kanisa kubwa sana na mchungaji hakunijua mimi binafsi, lakini mmoja wa wafanyakazi wa timu ya sifa na kuabudu alinifahamu. Nilipokuwa nikitambaa hadi kwenye jukwaa na moyo huo wa kukata tamaa, kila kitu kilikoma na macho yote yakanigeukia. Mfanyikazi aliyenifahamu aliitikia haraka alipoona maafisa wa usalama wakielekea mbele ili kunizua.

Alipomweleza mchungaji hali yangu, niliona uso wa mchungaji ukibadilika na kuwa mwororo. Alikuja kwangu na kuniombea. Rafiki yangu alimwambia mchungaji kwamba nilikuwa mgonjwa. Mchungaji alinitazama na kusema, "Ana roho ya udhaifu." Kwa hayo, aliweka mikono yake juu ya kichwa changu na kuamuru roho hiyo kuondoka. Papo hapo, jambo la ajabu lilitokea—niliwekwa huru. Kwa mara ya kwanza baada ya miezi kadhaa nilihisi kuwa mzima, hakukuwa na mateso mawazoni, wala woga, ila amani tele tu. Kusema nilishukuru ni kupuuza. Kusema kwamba nilichangamka hakuelezi kikamilifu jinsi nilivyohisi pia. Nilihisi kizunguzungu, mwepesi kama unyoya, na nikajawa furaha.

Baada ya ibada, mimi na Drenda tulienda kwenye hoteli na marafiki wengine kushereheke. Nilipokuwa nimeketi pale nikila, nakumbuka wimbo ulikuja kwenye redio, na ghafla, ile hisia ya kuhuzunisha ya hofu ikanifunika kama blanketi—ilikuwa imerudi. Tena, wakati huo nilielewa hiyo ilikuwa roho. Mchungaji alikuwa amesema ni roho ya udhaifu, lakini sikujua hiyo ilimaanisha nini hasa, na nilichanganyikiwa kidogo. Nilifikiri nilikuwa nimeponywa katika ibada, lakini inaonekana sikuponywa. Siku iliyofuata nilikuwa nikipambana na mashambulizi ya hofu tena, lakini sikuweza kuacha kufikiria juu ya kile kilichotokea kanisani jioni iliyopita. Mchungaji aliponiombea, hakuomba nipone. Alikuwa amechukua mamlaka juu ya roho. Jinsi hali yangu ilivyoitikia mchungaji wangu ilionyesha kwamba labda ilikuwa ni roho badala ya ugonjwa. (Tena, unaweza kuona jinsi nilivyokuwa mchanga ndani ya Kristo kutotambua hili.) Wakati huo, sikujua mengi kuhusu vita vya kiroho, lakini nilijua kwamba pepo walikuwa halisi. Nilikuwa nimemuona mmoja.

Katika ujana wangu, nilikuwa nimesimamia mojawapo ya maduka mawili ya vyakula ambayo wazazi wangu walikuwa wakimiliki. Usiku mmoja, mwanamume alikuja ambaye aliniambia alikuwa akifanya mikutano ya uamsho mtaani katika kanisa la mtaa la Methodisti. Alinialika nihudhurie. Alimalizia mwaliko wake kwa maneno haya, “Yesu angali anafanya yale yale aliyoyafanya katika Biblia.” Sasa, hilo lilivutia umakini wangu. Nililelewa kanisani. Nilitoa moyo wangu kwa Bwana wakati wa Shule ya Biblia ya Likizo nilipokuwa katika darasa la tano. Lakini sikuwahi kuona nguvu za Mungu zikimponya mtu katika miaka hiyo yote, hakuna kitu kilichovutia umakini wangu ambapo nilijua ni Mungu. Kwa hivyo maisha yangu yalielea kutoka kwa Bwana wakati wa miaka yangu ya shule. Mara kwa mara katika miaka hiyo, ningejitoa upya kuhudhuria kanisa, lakini sikupendezwa kudumu huko. Lakini mtu huyu alikuwa tofauti. Yesu alikuwa bado anafanya mambo yale yale aliyoyafanya katika Biblia? Nilivutiwa kwenda kuona alichokuwa akizungumzia. Wafanyakazi wangu kadhaa walikuwa washirika katika kanisa hilo, na walinitia moyo nihudhurie, kwa hiyo niliamua kwenda.

Jioni ya kwanza nilipokuwa pale, nilihisi uwepo wa Mungu kwa njia ambayo sikuwahi kuhisi hapo awali. Ilionekana kana kwamba ningeweza kugusa uwepo wa Mungu; ulikuwa dhahiri sana. Ujumbe alioutoa mtu huyo ulikuwa wa nguvu, na alipouliza kama kuna kuna mtu ye yote aliyetaka kujitoa au kukabidhi maisha yake tena kwa Yesu, niliinua mkono wangu. Lo! Ajabu gani. Nilisisimka sana. Nilitaka kumwambia kila mtu jinsi

Mungu alivyo mkuu.

Siku hizo, hakukuwa na mtandao, wala CD au kaseti, na tulikuwa na chaneli tatu kwenye televisheni yetu. Mji wetu ulikuwa mdogo pia, kwa hiyo hakukuwa na mengi ya kufanya jioni baada ya kazi. Kwa hivyo vijana kwa kawaida walikaa karibu na duka letu cha chakula ili kujiburudisha hadi usiku wa manane. Kwa kawaida Ijumaa na Jumamosi tulifunga saa saba ya usiku, na sehemu yetu ya kuegesha magari ilikuwa inajaa vijana. Mara nyingi nililazimika kuwafukuza, kwa kuwa walifanya iwe vigumu kwa wateja wangu kupata mahali pa kuegesha magari yao. Kulikuwa na zaidi ya usiku mmoja wa vita kati yao, ilibidi vikomeshwe na polisi na watoto kurudishwa nyumbani. Lakini sasa nilikuwa na wazo. Vijana hao walihitaji kusikia kumhusu Yesu. Kwa hiyo nilitoka na kuwaambia kwamba ikiwa ye yote kati yao angetaka kubaki, ningekuwa na mafunzo ya Biblia pale dukani mwetu baada ya kufunga kazi. Kumbuka, hii ingekuwa kama saa saba na nusu ya usiku, kwa sababu tulifanya usafi na kufunga kwanzia saa saba hadi saa saba na nusu. Sikujua kama ye yote kati yao angekuja, lakini wajua nini, baadhi yao walikuja, na wafanyakazi wangu wachache walibaki pia. Usiku wa kwanza nilipofanya mkutano, mmoja wa vijana pale alisema alitaka kumtumikia Kristo na akaniuliza afanye nini. Sasa, hii ililetia shida ya kipekee kwangu kwa sababu bado sikuwa nimefikiria sehemu hiyo. Kumbuka, sikujua chochote kuhusu Biblia, lakini nilikuwa nimesoma andiko lililoonekana kwamba lingejibu mahangaiko yangu.

*Na itakuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataoolewa.*

– Matendo 2:21

Ilionekana kuwa rahisi vyatatosha, kwa hivyo ndivyo nilivyoamua kufanya. Kikundi cha vijana kilikuwa kimeondoka wakati mmoja wao alinijia na swali, nikamwambia aketi kwenye kiti na kutaja jina la Yesu. Nilifikiri ni jambo rahisi kufanya, lakini nilikaa pale kwa takriban dakika mbili, na hakusema chochote. Kwa hiyo nilirudia maagizo yangu, huku nikifikiri kwamba hakunisikia. Bado hakusema kitu. Kisha niliona kwamba alikuwa akitetemeka. Pia niliweza kuona kutokana na mwonekano wake kwamba alikuwa na matatizo ya kutamka jina hilo kutoka kwa kinywa chake. Ghafla, kama bwawa linalopasuka, alitamka jina la Yesu, na amani ikaja juu ya uso wake. Naam, mpango wangu ulifua dafu! Kwa hiyo huo ulifanyika mfumo wangu kila wakati mtu alipotaka kutoa moyo wake kwa Bwana. Niliwataka wakae kwenye kiti na kutamka jina la Yesu. Karibu

kila wakati, hawakuweza kutamka jina hilo moja kwa moja. Walianza kutetemeka, kisha ilionekana kuwa shida kwao, ndipo ghafla wangelitamka, na kupata amani mara moja.

Siku moja nilipokuwa kwenye chumba pemberi nikichanganya unga, nilisikia mlango wa nyuma ukibishwa. Nilipofungua mlango, nilipata vijana wawili ambao hapo awali nilikuwa nimezungumza nao kuhusu Kristo. Niliwakaribisha chumbani, na mmoja wao akasema alitaka kutoa moyo wake kwa Mungu. Basi nilimketisha kwenye kiti; na, kama kawaida, alianza kutetemeka na hatimaye kutamka jina la Yesu. Nilipotazama juu, niliona kwamba yule kijana mwingine alikuwa amesonga nyuma kutoka kwangu na alikuwa upande mwingine wa chumba huku akiwa amejifinilia kwa kona kama mnyama aliyefungiwa. Alikuwa anajaribu kuchimba ukuta kana kwamba anajaribu kwenda mbali zaidi kutoka kwangu. Hili lilikuwa jambo la kushangaza sana, na sikulielewa.

Niliposimama pale nikimtzama, ghafla nilipata wazo, "Sijui kama huyu ni pepo." Sasa, sikuwa na uzoefu na mapepo, lakini nilikuwa nimesoma juu yao katika Biblia. Kwa kweli sikufikiria maelezo mengine yoyote kuhusu matendo yake ambayo hayakuwa ya kawaida. Kwa hiyo nikasema, "Yesu, huyu ni pepo?" Papo hapo, kama pazia linalovutwa nyuma, niliweza kuona pepo akining'inia upande mmoja wa kijana huyo. Pepo huyo alikuwa na urefu wa karibu futi tatu, na alikuwa amemshikilia kijana huyo huku akiwa amechuchumaa. Watu huniuliza kila wakati, "Alionekanaje?" Alifanana tumbili lakini tofauti kidogo. Alikuwa na nywele na mikono mirefu kama ya tumbili, lakini alikuwa na macho mekundu yaliyong'aa, na umbo lake lilikuwa limebondeka-bondeka. Mara tu nilipoyaona macho hayo, kwa kweli nilipiga kelele kwa sauti kubwa. Singeweza kustahimili chuki niliyoiona katika macho yale. Njia bora ninayoweza kueleza kile nilichokiona katika macho hayo ni chuki tupu, chuki iliyoenea kote kiasi cha kuhisika. Nilijua mara moja kwamba kitu hicho hakikunichukia tu bali pia kilikuwa na hasira nydingi dhidi yangu.

Sasa nini? Sikujuu nifanye nini baada ya kuona kitu hiki. Lakini nikawaza ikiwa jina la Yesu lilituingiza katika Ufalme, basi lazima liwe na mamlaka juu ya pepo huyu, kwa hiyo nikasema kwa sauti, "Katika jina la Yesu." Mara moja, pazia likafungwa. Ikiwa unakumbuka runinga za zamani za rangi nyeusi na nyeupe, ulipoizima, kungekuwa na kivuli kidogo cha kile ulichokuwa ukitazama kilichoffia polepole kutoka kwenye skrini. Naam, hivyo ndiyvo kitu hicho kilivyonekana. Singeweza kukiona vyema, lakini niliona kivuli chake kikififia. Mara pazia lilipofungwa, mvulana huyo

alikimbia ghafla nje ya jengo.

Kwa hiyo, ndio, nilijua kwamba pepo walikuwa kitu halisi. Laiti ningeweza kusema kwamba mara nilipoelewa kwamba tatizo langu lilikuwa pepo, nililishughulikia na kuwa huru tangu wakati huo kwenda mbele. Lakini hilo halikutokea mara moja. Inasikitisha kwamba baada ya kuwa kanisani miaka hiyo yote, sikuwa nimejifunza mimi ni nani katika Kristo na jinsi ya kutwaa kwa lazima haki zangu za kisheria dhidi ya adui. Lakini sasa kwa kuwa nilitambua au angalau kufikiri kwamba labda nilikuwa ninakabiliana na pepo fulani, nilitwa moyo kwamba ningeweza kujifunza jinsi ya kumshinda. Nilifahamu vya kutosha kujua kwamba pepo alitakiwa kuitikia mamlaka yangu, lakini nilichanganyikiwa kwa sababu hakufanya hivyo. Baada ya siku chache, kulikuwa na tukio lingine nzuri lillothibitisha kwamba shida yangu ilikuwa ni pepo.

Nilikuwa chumbani mwangu nikiomba katika roho na nilikuwa nimedhamiria kutumia muda wa kutosha kuomba ili nipate jibu kuhusu kilichokuwa kinaendelea. Wakati wa kipindi hicho cha maombi, ghafla nilihisi kuachiliwa na kuwekwa huru tena, kama wakati ule mchungaji aliponiombea. Nilikuwa huru kwa muda wa masaa mawili usiku huo kabla ya pepo huyo kurudi, lakini sasa nilikuwa na hakika kabisa kwamba nilikuwa nikabiliana na pepo kwa sababu alitiikia maombi. Nilijaribu kuomba tena lakini sikufua dafu. Kwa hivyo nilianza kusoma chochote nilichoweza kuhusu vita vya kiroho na nikatumia muda kujizoeza mimi ni nani katika Kristo. Lakini bado pepo huyo hakuondoka. Ni wakati mmoja tu nilipokuwa nikiomba nilipoona pepo huyo akiitikia mamlaka yangu mwenyewe. Nilichanganyikiwa na nikaanza kumuuliza Bwana nifanye nini kwa moyo wa dhati. Ingawa sikuwa huru kabisa, mshtuko wa hofu na kupooza kulikuwa kumepotelea mbali. Kwa hivyo kulikuwa na ushindi mkubwa tayari. Bado nilikuwa nikipambana na mawazo ya kutesa na kushusha moyo, lakini nilikuwa na uhakika nguvu yangu ilikuwa inaongezeka. Nilitumia muda kila siku kuchunguza kile Biblia inachosema kuhusu mamlaka yetu katika Kristo.

Alasiri moja nilikuwa nikipambana na hisia ya kawaida ya mshtuko na woga nilipokuwa nikifanya kazi katika ofisi yangu. Nilikuwa nimejaribu kuomba na kuamuru roho ya woga iondoke lakini sikufua dafu, kama kawaida. Ghafla, nilisikia sauti ya Bwana. Aliniambia niamuru pepo huyo aondoke, kwa sauti kubwa na kwa mamlaka. Kisha akaniambia jambo ambalo libadilisha mtazamo wangu kuhusu mamlaka ya kiroho. Alisema nisizingatie hisia zangu nilipoamuru kitu hicho kuondoka, bali

nisimame kwenye Neno Lake, si juu ya kile nilichoona au kuhisi. Nilikuwa nafanya kazi ofisini kwangu, hivyo singenyanuka na kuanza kumfokea shetani pale pale kwa sababu wafanyakazi wangu walikuwepo pia. Kwa hiyo niliinuka na kwenda chooni na kusema kwa sauti kubwa, "Katika jina la Yesu, ninakufunga, wewe roho ya woga. Unachofanya si halali, na ninakuamuru uondoke sasa, kwa jina la Yesu. Sikuhisi mabadiliko yoyote. Lakini nilikumbuka kile Bwana alichoniambia, "Usijali hisia zako." Kwa hiyo nilimshukuru Bwana kwa mamlaka aliyonipa juu ya roho hiyo, na nikaanza kumsifu Mungu kwamba nilikuwa huru. Nilirudi kazini katika ofisi yangu. Nilipokuwa nimeketi pale kwenye meza yangu, ingawa sikuhisi mabadiliko yoyote, nilimshukuru Bwana tu kwamba nilikuwa huru kila wakati hofu iliposhambulia akili yangu. Nilipokuwa nikishughulikia faili ya mteja, ghafla nilihisi uwepo wa Mungu ukinijia, na nikaona wingu jeusi, jembamba likinitoka na kutoweka haraka kupitia dari la ofisi yangu.

Nilikuwa huru!

Pepo huyo wa kishetani wa woga alitokomea, na ikiwa angerudi, nilijua jinsi ya kukabiliana naye. Nilisisimka sana! Nilimpigia simu Drenda na kumweleza yaliyotokea. Alisema atakuja mara moja, na tukasherehekeea kwa kula chakula cha mchana siku hiyo kwenye mkahawa wa Kichina (niupendao). Ilibidi nirudie msimamo wangu dhidi ya pepo huyo wa woga mara nydingi baada ya siku hiyo maana mapepo hayakati tamaa haraka. Na ingawa pepo alikuwa ameondoka, matatizo ya kifedha maishani mwangu hayakuondoka. Kwa hiyo woga kuhusu fedha ulijaribu tena kujirudisha mawazoni mwangu, na ilinibidi nijifunze jinsi ya kushughulikia akili yangu na kudumu katika amani.

Kumekuwa na vita vingine ambavyo nimelazimika kupigana na kujifunza kupitia kwavyo maishani mwangu, kukiwamo masomo mengi ya kiroho kuhusu Ufalme ambayo bado sijajifunza, lakini sababu ya kutaka kukwambia hadithi hii ni kukujulisha kwamba ninalewa jinsi shinikizo la ukosefu wa fedha linavyoathiri watu na maisha yao na kufungulia ukandamizaji wa pepo wa hofu.

Nataka kuhakikisha unajua kwamba nimepitia jambo hili.

Kwa hivyo haijalishi ni matatizo aina gani unayokabiliwa nayo leo, kuna tumaini. Laiti ningalijua kuhusu Ufalme wa Mungu mapema maishani mwangu kwa uhakika. Inasikitisha kufikiria kwamba mimi na Drenda tulishi katika matatizo ya kifedha kwa miaka hiyo tisa wakati haikuwa lazima!

Kwa bahati mbaya, tatizo letu la kifedha halikuwa tone la maji

baharini; lilikuwa bahari yenyewe. Ilikuwa kawaida ya maisha yetu. Miaka tisa ya maisha ya kuomba-omba, kumbukumbu za matukio na hali zilizofedhehesha. Matukio ambayo nilisahau mara moja. Mke wangu ubarikiwe! Alivumilia mengi katika miaka hiyo. Ndiyo maana siku hizi mimi hujaribu kumbariki kila ninapoweza.

Kama vile Bwana alivyofundisha jinsi ya kukabiliana na pepo huyo wa kishetani wa woga, alianza kunifundisha jinsi ya kushughulikia fedha zangu kupitia kwa mtazamo wa kiroho. Yale Mungu aliyotufundisha mimi na Drenda, na yale ambayo ametuonyesha kuhusu fedha zetu, yalikuwa ya ajabu na yalibadilisha maisha yetu sana kiasi kwamba tumejitolea kutumia maisha yetu yote kusaidia watu kugundua kanuni zile zile.

Mimi na Drenda tulitoka katika hali mbovu ya kifedha tukalipia magari yetu pesa taslimu, tulijenga nyumba yetu ya ndoto bila deni, tumeanzisha kampuni kadhaa, na kuzindua kipindi chetu cha runinga cha kila siku kinachoitwa *Fixing the Money Thing* katika kila eneo duniani. Drenda pia alizindua kipindi cha runinga cha kila wiki kinachoitwa *Drenda* kwenye mtandao wa *ABC Family* ili kusaidia familia kujua jinsi ya kuishi na kuwatia moyo wanawake. Tulihisi Mungu akituongoza kuanzisha Kanisa la *Faith Life*, ambapo tunafundisha maelfu ya watu kuhusu Ufalme wa Mungu kila wiki. Sasa inatugharimu mamilioni kwa mwaka kufanya kile tunachofanya, zaidi ya \$200,000 kwa vipindi vyta runinga tu kufikia wakati wa kuandika kitabu hiki. Bila shaka, hakuna lolote kati ya haya ambalo lingewezekana ikiwa Mungu hangetufundisha yale tunayotaka kukufundisha katika mfululizo huu wa vitabu. Sitaki uone kitabu hiki kama kitabu chochote kingine kuhusu fedha. Sio kitabu kingine cha jinsi unavyohitaji kuandaa bajeti, ingawa hilo labda linahitajika na kupendekezwa. Sio kikao cha mafundisho kama yale ya zamani yasemayo, “mapato hayatoshi,” kwa hivyo tunaweza kuondoa nini.

La, hiki ni kitabu kuhusu mapinduzi, vita dhidi ya Ufalme wa giza na umaskini wake unaokandamiza. Ni kitabu kinachohusu kutupilia mbali vizuizi vyta mamlaka mabovu na kuchukua njia mpya ya maisha. Jibu langu halikuwa ushauri wa jumla wa kifedha. Niligundua kuwa nilihitaji marekebisho kamili ya kifedha:

## MAPINDUZI YA KIFEDHA!



# SURA YA 1

# UFALME

Nilikuambia katika utangulizi jinsi maisha yangu yalivyokuwa yametawaliwa na kusetwa na hofu. Kwa hiyo naamini ni muhimu nianze safari yetu pamoja na kauli hii moja ambayo kwa kweli unahitaji kuelewa: USIWE NA UZOEFU WA KUISHI KATIKA HOFU! Hofu hufungua mlango kwa kila aina ya ushawishi wa kipepo, kuchanganyikiwa, na fadhaha, kama tulivyoona hapo awali katika maisha yangu na maisha ya mamilioni ya watu wengine. Naamini kiwewe cha kifedha hufungua mlango mkubwa wa hofu katika maisha ya watu. Mimi binafsi nimesaidia watu katika masuala yao ya kifedha kwa miaka 34 kuititia kampuni yangu ya kupanga fedha, na nimegundua kwamba si mimi tu niliyepambana au ninayepambana na hali yao ya kifedha.

Hakika, kulingana na utafiti wangu, niligundua kwamba asilimia 23 ya wakazi wa Marekani hawalipii mikopo yao hata kidogo na polepole wanaingia katika maangamizo ya kifedha. Hii ni robo ya nchi! Watu milioni arobaini na saba, asilimia kumi na sita, wanapatiwa msaada wa vyakula na serikali, na familia nane kati ya kumi wanaishi mshahara hadi mshahara. Sitazungumzia deni la dola trilioni 18 ambalo taifa letu linalo na haliwezi kulipa. Pia sitataja wajibu wa kifedha wa thamani ya dola trilioni 120 amba nchi yetu imejitwika bila utaratibu wa kulipia gharama. Tunaishi katika taifa lenye masuala mazito ya kifedha! Nilichogundua maishani mwangu ni kwamba maswala ya kifedha ambayo hayajatatuliwa na fadhaha za kifedha hufanya kuishi katika hofu jambo la kawaida maishani.

Lakini kuna majibu! Unaweza kuwa huru! Biblia iko wazi kuhusu jambo hili: Yesu alikuja kuhubiri habari njema kwa maskini!

*Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu; kwa sababu BWANA amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu (maskini) habari njema;*  
– Isaya 61:1

Ni habari gani njema kwa mtu maskini? Kwamba anaweza kuwa huru! Leo, huenda usijue jinsi hilo litakavyotokea. Wakati mmoja katika maisha yangu, nilikosa tumaini kabisa. Wazo la kuwa na dola 100 ambazo hazikuwa deni la mtu fulani lilikuwa wazo geni kwangu kiasi kwamba ningecheka wazo hilo ikiwa halingekuwa la kuogofya na kuhuzunisha sana. Miaka

## **“ROHO YA BWANA MUNGU I JUU YANGU; KWA SABABU BWANA AMENITIA MAFUTA NIWAHUBIRI (MASKINI) HABARI NJEMA.”**

**- ISAYA 61:1**

wakipiga kelele, “Shikamoo, Baba!” Kwenye video sikuwajibu wala hata kuwatazama.

Nilikuwa na dhiki na kukata tamaa sana kiasi kwamba sikujua ni kitu gani kilichokuwa muhimu.

Mtazamo wangu wakati huo unanikumbusha kitu nilichoifunza wakati mmoja katika mafunzo ya kuogelea. Ikiwa mtu anazama na anapiga kelele akiomba msaada, kuwa mwangalifu ikiwa unakwenda kumsaidia. Kwa nini? Kwa sababu mtu anayezama anataka sana kuishi kiasi kwamba anaweza kukuvuta kwenda chini bila kumaanisha. Hivyo ndivyo nilivyokuwa, kama maiti asiye na ufahamu kuhusu maisha, mwenye uzoefu bila hisia. Kama mume, baba, na mpaji-riziki nilikuwa nimefeli jaribu hilo. Maisha yangu yalikuwa yale yale ya kawaida yenyе picha isiyo na hisia, maono, wala furaha.

Jiji letu la Columbus, kule Ohio, lilikuwa na ongezeko la haraka la nyumba katika nyakati hizo. Nyumba zilikuwa zikijengwa kila mahali, na kwa sababu hiyo, jiji letu liliandaa Gwaride la Nyumba kwa miaka mingi mfululizo. Ikiwa hujui hiyo ni nini, hebu nifafanue. Gwaride la Nyumba ni maonyesho yanayoandaliiwa na wajenzi mbalimbali wa nyumba tofauti zenyе mitindo maalum na vifaa vyę kisasa. Kwa kila mtu katika eneo

hilo, hili lilikuwa jambo kubwa na lilifurahiwa na maelfu ya watu. Lakini niliogopa Gwaride la Nyumba. Kwa sababu ya kuishi katika umasikini, sikutaka Drenda aende kuangalia nyumba hizo. Tayari nilihisi vibaya vyatukosha kuhusu kutofaulu kwangu kifedha; kwa kweli sikutaka mke wangu ajue jinsi alivyoishi katika hali mbaya. Sasa najua kwamba mtazamo wangu huo ulikuwa wa kijinga, lakini wakati huo, huo ndio uliokuwa mtazamo wangu. Nilijua kwamba angeenda huko, angetaka nyumba moja. Kwa hiyo mwaka hadi mwaka, nilisema, “La! Lakini mwishowe, mwaka mmoja nilikubali na nikaamua kwenda.

Nyumba hizo, kama unavyoweza kufikiria, zilikuwa za ajabu kupindukia. Zilifanya nyumba yetu ndogo ya shambani ya miaka ya 1800 ioneckane kama nyumba iliyohukumiwa inayosubiri kubomolewa. Baada ya kupita katika nyumba chache za kwanza na tulipokuwa tukitembea kando ya barabara, ghafla niligundua kwamba Drenda hakuwa kando yangu. Niligeuka nyuma ili nimuone alipo, nilisikitika sana kumuona akiwa amesimama nje ya nyumba tuliyotoka. Machozi yalikuwa yakimtoka. Nilirudi kwake na nikamuuliza swali la kijinga, “Kuna shida gani?” Kana kwamba sikujua jibu la hilo. Alinitazama na kuniuliza, “Nitapata nyumba lini?” Mawazo yangu yalinisokota, “Nyumba? Kama hizi? Hizi zote ni nyumba za \$500,000 hadi \$700,000.” Bado nilikuwa nikijaribu kutafuta njia ya kulipa malipo ya kodi ya \$300 ya kila mwezi yaliyodaiwa kwenye ile nyumba nzee ya shambani. Najua inahuzunisha, lakini sikuwa na suluhu, na sikumpa tumaini mke wangu mpendwa wa kupendeza. Hofu na kutofaulu vilidhoofisha akili na mtazamo wangu. Huyu hakuwa mimi; ni kitu gani kilichofanyikia msisimko na furaha yangu? Singeweza kuona zaidi ya shinikizo la kifedha.

Ilikuwa saa nane au saa tisa usiku na singeweza kulala. Uchungu ulipita kwa taya na uso wangu kama sindano, na nilihitaji nafuu haraka. Masaa thelathini na sita awali nilikuwa nimetibiwa na daktari wa meno kuzuia ugonjwa ambao ulisababisha uso wangu kuvimba kama puto. Maumivu na usumbufu ulikuwa wa ajabu. Nilikuwa nikitumia dawa kali ya kutuliza maumivu kila baada ya masaa manne, lakini haikuonekana kusaidia sana. Nilipokuwa nimeketi sebuleni kwangu, kwa kukosa usingizi huku nikinywa dawa tena, ghafla nilitazama kijisanduku cha ile dawa na kusoma maagizo. Sio kwamba sikujua jinsi ya kunywa dawa hiyo lakini kwa sababu ya kutokuwa na shauku, kama vile sisi sote tunavyosoma kijisanduku cha kiamsha kinywa tunapokila asubuhi. Sio kwamba tunapenda sana kukisoma lakini kwa sababu kiko hapo. Naam, naam, vidonge 2 kila masaa

4, lakini maagizo yalisema nini? Hakuna zaidi ya vidonge 10 katika kipindi cha masaa 24? Akili yangu ilijumlisha haraka idadi ya vidonge ambavyo mtu angetumia ikiwa angevinywa kila baada ya masaa 4, kama nilivyokuwa nimefanya katika siku 2 zilizopita—vidonge 12 kwa siku, vidonge 2 zaidi ya kipimo cha juu zaidi. Ghaffa, tumbo likanibana na hofu ikanishika.

Miaka tisa ya kuishi katika umasikini, kushindwa kama mume, kushindwa kama baba, na kushindwa kama mpaji-riziki kulinifanya niwe ovyo kabisa kihisia. Madaktari walikuwa wamenipa dawa za kupunguza dhiki ili kujaribu kunisaidia. Lakini hakuna kilichosaidia. Nilipokuwa nimeketi pale usiku ule na maumivu kwa meno, sikuwa nimelala siku mbili, na maumivu yalikuwa makali sana singeweza kulala tena. Sasa niliposoma kijisanduku cha dawa, niligundua nilikuwa na jambo moja zaidi la kuwa na wasiwasi kuhusu, uwezekano wa kupitisha kipimo cha dawa. Sikujua matumizi ya kupita kiasi ya dawa hiyo yangenifanya nini, lakini nilikuwa na uhakika haikuwa dawa mbaya kwa sababu mtu yejote angeweza kuinunua bila kuandikiwa na daktari. Niliona kwamba waliweka maonyo kwa kijisanduku hivyo ili kuwatuliza mawakili wao na kubaki ndani ya matakwa yao ya kisheria. Sikufikiri kwamba kupitisha kipimo kwa vidonge 2 kungeweza kusababisha shida kubwa. Lakini roho ya woga ilikamata mawazo yangu, ikachukua ukweli huo, na kuanza kunifyatulia maswali mengi. Kwa hivyo ili kutuliza mawazo yangu, nilifikiri kupiga simu kwa Kituo cha Kudhibiti Sumu ili kupata ufahamu. Nilikuwa na hakika wangesema hilo halikuwa jambo kubwa.

Mwanamke aliyejibu simu upande ule mwingine alisikika kuwa mtaalamu. Aliniuliza jinsi ya kunisaidia, na nikamweleza kwamba nilikuwa nimekunywa ile dawa baada ya masaa 4 kwa kipindi cha masaa 36 zilizopita, na hivyo kumeza vidonge 12 kwa siku badala ya 10. Nilimwambia nilikuwa nikipiga simu ili kuthibitisha kwamba kunywa vidonge 2 vya ziada hakungesababisha madhara yoyote makubwa. Kulikuwa na unyamavu, na nikasikia vitufe vya kompyuta vikitoa sauti. Kisha nikasikia maneno haya, na nikanukuu kile alichonimbilia, “Bwana, hatujawahi kuwa na mtu aliyetumia kipimo hicho ambaye aliishi.” Je, nilimsikia vyema? La hasha! Kwa hiyo nikamweleza tena kwamba nilipitisha kipimo kwa vidonge 2 kwa muda wa masaa 24 na nilifanya hivyo kwa siku 2.

Wakati huu alijibu kwa sauti ya ukali, “Bwana, kama nilivyosema, hatujawahi kuwa na mtu aliyetumia kipimo hicho ambaye hakufa. Nakuhitaji hospitalini SASA! hivi.” Nilipojaribu kumweleza tena kilichotokea, maana nilikuwa na uhakika kwamba hakuwa akinisikia vyema, alinikatiza na

kusema, "Jipeleke hospitalini au nitakutumia gari la wagonjwa." Nilipigwa na mshtuko! "Nitajipeleka mwenyewe," nikasema kwa kigugumizi. "Unaenda hospitali gani?" Akauliza. Nilipomwambia alikata simu.

Nilisimama pale nikiwa nimeduwazwa. Nilikuwa na mukutano muhimu sana saa tatu asubuhi hiyo, na sasa ilikuwa yapata saa 3:30 usiku. Nilipiga hatua kuelekea chumbani mwangu nikamwamsha Drenda na kumweleza kilichotokea. Alinitazama na macho ya huzuni na fadhaa. Mume wake alikuwa anafanya na kwa miezi kadhaa sasa alikuwa amefanya mambo ya ajabu ajabu, na alikuwa amechoka kushikilia kila kitu pamoja, na sasa hili? "Gary, ulipitisha kwa vidonge viwili tu. Hakika, unajua vyema zaidi kwamba havitakuua. Wapigie simu tena," akasema. Lakini hofu haina busara na inasononesha. "Yule mwanamke alisema vinaweza kuniua; nahitaji kwenda hospitalini." Nilipogeuka kutoka chumbani niliona maneno, "Lazima iwe unafanya mzaha" machoni mwa mke wangu.

Nilipokuwa nikiendesha gari kuelekea hospitali, watu wawili waliovalia makoti meupe walikuwa wameningojea nje ya mlango wa lango la dharura. Nilipowasili, walinijia wakaniliza, "Je, wewe ni Gary Keesee?" Haraka wakanipeleka kwa chumba cha matibabu. Nilipopita kwenye ubao wa chumba cha dharura, niliona jina langu tayari limeandikwa. "Gary Keesee—amepitisha kipimo cha dawa." Sikuamini. Ili kufupisha hadithi ndefu, daktari alipochunguza sampuli ya damu yangu, alirudi na kusema, "Kwa nini uko hapa? Kiwango cha dawa kwa damu yako hakitoshi kuponya maumivu ya kichwa. Nilipomwambia hadithi yangu kuhusu Kituo cha Kudhibiti Sumu, alianza kucheka. Sikufikiri lilikuwa jambo la kuchekesha, na hakika sikufikiri hivyo wakati walinitumia bili ya \$2,000. Ibilisi alikuwa amenitega na kuniibia tena.

Ninakusimulia hadithi hizi, pamoja na utangulizi, ili kukusaidia kuona maisha yangu yalikuwa wapi kabla sijagundua Ufalme wa Mungu. Naam, nilikuwa Mkristo. Naam, nilitoa zaka. Naam, niliongoza ibada katika kanisa langu kwa muda. Naam, nilimpenda Mungu. Lakini jambo halikuwa sawa, halikuwa sawa kabisa! Nilikuambia jinsi Mungu alivyofundisha jinsi ya kupigana na roho ya woga na jinsi nilivyojiweka huru kutokana na dawa za dhiki na mashambulizi ya hofu. Lakini bado sikuwa huru kutokana na hali zilizosababisha vita vyangu na woga mwanzoni, yaani hali yangu mbovu ya kifedha! Bado nilikuwa na shinikizo kubwa kila siku la kutafuta pesa na kulipa bili zangu, pamoja na kwamba nilikuwa na kadi kumi za mkopo ambazo nilikuwa nimetumia mkopo wote na zikaghairiwa, mikopo ya kampuni tatu za kifedha, deni la watoza ushuru, pesa zilizodaiwa na

wanafamilia, hukumu, na mali yangu nyingi kumilikiwa na wengine hadi nitakapolipa deni. Kama nilivyosema awali, maisha yetu yalikuwa mabovu kifedha. Shinikizo na msukosuko wa kihisia vilikuwa kawaida

**“NA MUNGU WANGU  
ATAWAJAZENI KILA  
MNACHOKIHITAJI KWA  
KADIRI YA UTAJIRI WA  
UTUKUFU WAKE NDANI YA  
KRISTO YESU.**

- WAFILIPI 4:19

kwangu nilipofanya kazi yangu. Ingawa tulikuwa Wakristo, tulikuwa tunaangamia kifedha, kadi zangu za mkopo zilighairiwa moja baada ya nyingine. Wamiliki wa mali yangu waliongezeka, mikopo ilikataliwa, na wadai kunipigia simu. Katika kilele cha shida yetu ya fedha, na biashara yetu kutozaa faida nyingi, hatukuweza hata kununua chakula. Familia yangu ilizunguka

jiko la kuni katika chumba chetu cha familia ili kupata joto kwa sababu hatungeweza kumudu mafuta. Tulikuwa takitafuta sarafu ambazo labda zilikuwa zimeanguka ndani ya viti huku tukitumaini kupata pesa za kutosha kuwagawanyia watoto wetu mlo mtamu kwa mkahawa unaoitwa McDonald.

Nilikuwa mzuri sana katika kuwakatisha moyo wadai waliponipigia simu, lakini siku moja kampuni moja iliajiri wakili kufuatilia deni langu. Mtu huyo alipiga simu na hakuwa na utu. Alisema, “Ninahitaji pesa kabla ya siku tatu kuisha au nitafungua kesi dhidi yako kwa niaba ya mteja wangu.” Nilikuwa nimekwisha. Sikuwa na la kufanya, sikuwa na pesa, tayari nilikuwa nimeomba marafiki wangu wote, na sasa kufikia hapo nilijua kwamba nimekwisha. Nilijikokota hadi chumbani kwangu nikaanguka kwenye kitanda changu na kumlilia Mungu. Ghafula, nilisikia sauti ya Bwana. Andiko ambalo nilikuwa nimesikia mara nyingi lilielea akilini mwangu.

*Na Mungu wangu atawajzeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wa utukufu Wake ndani ya Kristo Yesu.*

- Wafili 4:19

Nilimjibu Bwana kwamba nilijua andiko hilo lakini mahitaji yangu hayakuwa yakinimizwa! Akajibu swalii langu mara moja, “Ndio, lakini hilo si kosa Langu. Hujatafuta fursa ya kujifunza jinsi Ufalme wangu unavyofanya kazi. Kwa kweli, wengi walio katika kanisa langu wanaishi vile Israeli walivoishi katika Agano la Kale—kama watumwa. Wanaishi maisha

ya madeni na utumwa wa kifedha. Nataka watu wangu wawe huru.”

Nilikimbia haraka chini na kumshika Drenda na kumwambia kile ambacho Bwana aliniambia. Nilitubu kwake kwa kutomtafuta Mungu na kujifunza jinsi Ufalme Wake unavyofanya kazi. Kwa kweli, wakati huo, hatukujua Mungu alimaanisha nini aliposema hatukujua jinsi Ufalme unavyofanya kazi. Hata hivyo, tulikuwa kanisani, tulitoa zaka kutoka kwa mapato yetu mara nyingi, na tulimpenda Mungu. Tulifikiri tayari tulikuwa na mtazamo wa Ufalme wa Mungu. Suala, hata hivyo, ambalo nilikuwa karibu kutambua ni kwamba ndio, nilikuwa naelekea mbinguni, lakini sikuwa najua jinsi ya kuleta nguvu na mamlaka ya mbinguni katika maisha yangu na kubadili hali yangu ya asili. Kwa hiyo tulianza kujifunza Biblia, na Mungu akaanza kuzungumza nasi na kutusaidia kujua alichomaanisha aliposema Ufalme. Tulichojifunza kilitushangaza! Ilikuwa ni kama kuwasha taa kwenye chumba chenye giza. Kwa mara ya kwanza katika maisha yetu, tulipata majibu kuhusu maisha yetu ya kifedha!

### **Mungu, Unamaanisha Nini Unaposema Ufalme?**

Mungu aliponiambia kwamba sikuwa nimejifunza jinsi Ufalme Wake unavyofanya kazi, nilichanganyikiwa, kusema kweli. Ufalme? Mimi na Drenda hatukujua chochote. Tulisali tukamwomba Mungu atufundishe kile alichomaanisha: “Bwana, tufundishe maana ya Ufalme!” Kwa hiyo, jambo la kwanza nililopaswa kujifunza ni Ufalme ni nini. Nafikiri dhana hii ni ngumu kwa akili zetu za Magharibi, maana tunaishi katika mfumo wa mawazo ya Kimarekani wa kidemokrasia na uhuru wa kujieleza wazi. Ufalme wa Mungu hautumii mfumo wa kidemokrasia; ni Ufalme ulio na Mfalme. Mamlaka ya Mfalme hutiririka katika Ufalme kuititia kwa mamlaka yaliyokabidhiwa kwa ofisi mbalimbali za serikali na watu wanaofanya kazi chini ya mamlaka hayo. Kuwa na kundi kubwa la watu sio ufalme. Unaweza kuwa na watu milioni katika kundi la watu na usiwe na ufalme. Ufalme ni kundi la watu wanaoshikiliwa pamoja na sheria au serikali. Ufafanuzi wa ufalme katika kamusi ni: “ufalme: jimbo au serikali iliyo na mfalme au malkia kama mkuu wake.”

Ingawa tunasherehekea kuja kwa Yesu duniani wakati wa Krismasi, huwa tunashindwa kuelewa kwamba alikuwa akileta serikali. Biblia inazungumza juu ya serikali hii katika Isaya 9:6-7:

*Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto wa kiume, na serikali itakuwa mabegani Mwake. Naye ataitwa Mshauri wa Ajabu, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele, Mfalme wa Amani.*

*Kuongezeka kwa serikali Yake na amani hakutakuwa na mwisho. Atatawala katika kitu cha enzi cha Daudi na juu ya Ufalme Wake, akiuthibitisha na kuutegemeza kwa haki na uadilifu tangu wakati huo na hata milele. Wivu wa Bwana Mwenye Nguvu Zote utatimiza hili.*

Yesu ndiye kichwa cha serikali hii, na tunapomkubali Yesu kuwa Mwokozi wetu binafsi tunakuwa sehemu ya serikali hii; tunafanyika raia. Hatufanyiki raia tu bali pia sehemu ya nyumba ya Mungu kama wana na binti za Mungu.

*Bali wote waliompokea, ndio wale waliaminio jina lake, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu—watoto waliozaliwa si kwa jinsi ya asili, wala si kwa maamuzi ya kibinadamu, wala kwa mapenzi ya mume, bali ya Mungu.*

– Yohana 1:12-13

*Kwa hiyo, ninyi si wageni tena, bali ni raia pamoja na watu wa Mungu na pia washiriki wa nyumba Yake.*

– Waefeso 2:19

Sisi kama jamaa ya nyumba ya Mungu, tunafanyika sehemu ya familia Yake na hivyo kumiliki au kuwa sehemu ya kila kitu ambacho Mungu anamiliki. Lakini pia tunafanyika raia wa serikali Yake kuu. Hii ina maana kwamba tuna haki na manufaa ya kisheria ndani ya serikali hiyo. Ili kuelewa vyema kile ninachozungumzia, acha nizungumzie kuhusu kuwa raia wa asili nchini Marekani. Kama raia wa Marekani, una haki za kisheria. Haki zako za kisheria zimeandikwa katika katiba yetu na katika sheria ambazo zimepitishwa ndani ya serikali yetu. Sheria na manufaa hutiririka chini hadi kwa kila raia, bila kujali wao ni nani. Haki hizo hazifanyi kazi kulingana na hisia zetu au jinsi tulivyo werevu. La, zimeimarishwa na sheria, zinapatikana kisheria kwa kila raia anayeta Amerika kwao. Inawezekana raia asijue haki zake za kisheria, lakini hata hivyo, anazo kwa kuwa raia wa Marekani.

Sasa hapa kuna jambo la kutafakari, na ninatumai litabadilisha mtazamo wako kuhusu Mungu na jinsi unavyopokea kutoka kwa Mungu. Hapa Marekani tukigundua kwamba kitu au mtu fulani anajaribu kutunyang'anya haki zetu za kisheria au kwamba tumetendewa isivyo haki, tuna njia ya kupata haki (haki maana yake ni utekelezaji au usimamiaji wa sheria), mchakato ambaa unatekeleza haki zetu za kisheria. Tunaenda

mahakamani, na hakimu hajali mwonekano wetu, au jinsi tulivyo tajiri au maskini. Anafuata sheria. Anapaswa kukata kauli kulingana na sheria kila wakati. Huu ndio usalama wetu: kwamba tuna haki za kisheria, na serikali yetu itatekeleza haki zetu za kisheria kupitia kwa mchakato wa haki ndani ya Amerika. Ukiwa na hilo akilini, chunguza kwa makini Isaya 9 inapozungumza kuhusu serikali hii mpya ambayo Yesu analeta duniani.

*Yeye (Yesu) atatawala katika kiti cha enzi cha Daudi na juu ya Ufalme Wake, akiuthibitisha na kuutegemeza kwa haki na uadilifu....*  
– Isaya 9:7b

Andiko hili linasema kwamba Ufalme wa Mungu umeimarishwa na kudumishwa kupitia kwa haki, utekelezaji wa sheria ya Mungu. Usimamiaji unamaanisha mchakato wa kutekeleza au kulazimisha haki zako za kisheria. Haki zako za kisheria ni kile Mungu anachokiita uadilifu au kile anachosema ni sahihi, yaani sheria Yake. Ili kuhakikisha kuwa una kile Mungu anachosema ni sahihi katika Ufalme Wake, kile kilicho chako kisheria kama raia katika Ufalme, Mungu amekupa njia ya kupata haki, mchakato au dhamana ya kwamba utapata kile alichokuahidi. Mungu ametujulisha mapenzi Yake kwa Neno Lake, Biblia, ili tujue haki zetu katika Ufalme Wake. Hii ni habari njema! Kila kitu unachosoma katika Biblia kuhusu kile Mungu amekuahidi ni chako tayari kisheria kama raia wa Ufalme Wake!

2 Wakorintho 2:20 inasema wazi kwamba kila ahadi—KILA AHADI—ni “Ndio” na “Amina.” Tayari uamuzi umefanywa; ni yako kisheria.

*Kwa maana hajalishi ni ahadi ngapi ambazo Mungu ametoa, zote ni “Ndio” katika Kristo. Na hivyo kupitia Yeye “Amina” inasemwa na sisi kwa utukufu wa Mungu.*

– 2 Wakorintho 2:20

Msingi hasa wa Ufalme wa Mungu ni haki na uadilifu—hauwezi kuyumba-yumba. Kwa hivyo lifikirie jambo hili hivi: “Ikiwa ninaijua sheria ya Ufalme wa Mungu (mapenzi Yake), na ninajua kwamba ninaweza kupata haki kupitia kwa mchakato taratibu wa utekelezaji unaonihakikishia kile ambacho sheria inasema, basi nina uhakika na sina woga.

*Huu ndio ujasiri tulio nao katika kumkaribia Mungu, ya kwamba, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi Yake, atusikia. Na ikiwa tunajua*

*kwamba anatusikia—chochote tunachoomba—tunajua kwamba tunayo tuliyomwomba.*

— 1 Yohana 5:14-15

Aya hii inaposema anatusikia, haizungumzi juu ya kutusikia kwa sauti kama vile kusikia maneno tunayosema na vinywa vyetu; inazungumzia Yeye kushughulikia kesi zetu. Fikiria hakimu anavyosikiliza kesi ili kuhakikisha

## FALME HUTENDA KAZI KUPITIA KWA SHERIA NA SHERIA HAZIBADILIKI.

haki inatendeka. Chumba cha mahakama na hakimu wapo kuhakikisha kuwa haki inapatikana kwa kila mtu, kiti Chake cha enzi (mahali pa mamlaka) na uwezo Wake upo kuhakikisha haki (kutekelezwa kwa

mapenzi Yake) kwa watu wote wanaokuja kwa Yesu na Ufalme Wake.

Tafadhalii soma kauli hiyo tena polepole sana na iache iwe changamoto kwenye mtazamo wako kumhusu Mungu. Watu wengi huhisi kwamba Mungu hufanya maamuzi Yake kwa msingi wa kesi hadi kesi, lakini hiyo si kweli. Yeye ni Mfalme wa Ufalme wenye sheria zisizobadilika. Hafanyi na hatafanya maamuzi nje ya sheria Yake. Hivyo tunaweza kujua jibu Lake ni nini kabla ya kuuliza, na tunaweza kuwa na uhakika kwamba tuna kile ambacho sheria Yake inasema kabla hatujakiona kwa sababu Yeye ana uwezo wa kutekeleza sheria Yake.

Mimi na Drenda tulipoanza kujifunza kuhusu haki zetu za kisheria katika Ufalme, jambo hilo lilibadili sana maoni yetu kumhusu Mungu na Biblia. Matokeo ya ufahamu wetu mpya ni maisha yaliyobadilishwa. Hatukuomba-omba tena. Hatukumsihi yeoyote tena. Tulijifunza yale Mungu alisema tayari tulikuwa tumepewa sisi wenyewe kisheria kama raia wa Ufalme Wake. Kile tu tulichohitaji ni kuendelea kujifunza jinsi ya kuweka madai ya kisheria kwa yale yaliyokuwa yetu kisheria na kuyaachilia katika ulimwengu. Fikiria unapoenda kwenye benki kutoa pesa. Ingawa unaweza kuwa na pesa nydingi katika akaunti yako, kuna mchakato wa kisheria unaohitaji kufuata ili kudai na kutoa pesa. Kuna mchakato katika mfumo wowote wa kisheria wa kudai kitu, hata kama tayari ni chetu.

*Uweza Wake wa Uungu umetupatia kila kitu tunachohitaji kwa ajili ya uzima na utauwa kwa kumjua Yeye aliyetuita kwa utukufu Wake na wema Wake.*

— 2 Petro 1:3

Ni ufalme! Wale ambao ni raia wa Ufalme huo wana haki sawa na mtu mwingine yeote ambaye ni raia wa Ufalme huo. Ni muhimu tuelewe jambo hili: Falme hutenda kazi kupitia kwa sheria na sheria hazibadiliki. Kwa nini jambo hili ni muhimu? Ni muhimu kwa sababu inamaanisha kwamba ikiwa Ufalme unatenda kazi kwa kutegemea sheria zisizobadilika, basi hakuna upendeleo katika Ufalme huo. Kila mtu katika Ufalme ana haki ileile ya kufurahia utendaji wa sheria ya Ufalme kwa niaba yao kama mtu yeote mwingine katika Ufalme.

Hapa ndipo kanisa huchanganyikiwa kidogo. Wakristo wengi hufikiri kwamba Mungu huamua kiholela kile anachotaka kufanya katika maisha ya mtu. Kwa maneno mengine, wanafikiri Mungu anachagua kubariki mtu fulani na si mtu mwingine. Wanafikiri Mungu huruhusu mambo wasiyoweza kudhibiti yawatokee. Wanafikiri atamponya mtu mmoja na si mwingine. Wakristo wengi humwomba Mungu awasaidie wakati tayari amefanya yote awezayo kuwasaidia. Amewapa Ufalme, Ufalme wote!

Mungu alipoanza kunena nami kuhusu fedha zangu na kwamba nilihitaji kujifunza zaidi kuhusu Ufalme Wake, alinipa andiko hili.

*Heri ninyi mlio maskini, kwa maana Ufalme wa Mungu ni wenu.*  
– Luka 6:20b

Mungu alikuwa akiniambia kwamba jibu langu kuhusu fedha zangu lilikuwa katika Ufalme Wake na kuongeza kwa hilo, kujua jinsi ya kudai sheria za Ufalme hapa duniani kama Yesu alivyofanya. Nakubali sikujua hayo yote yalimaanisha nini mwanzoni. Lakini nilipotafakari kuhusu yale Mungu aliyoniambia, nilitambua kwamba kweli falme hufanya kazi kupitia kwa sheria. Kazi na athari ya sheria fulani inaweza kujulikana na kuhesabiwa kufanya kazi sawa kila wakati kwa sababu sheria hazibadiliki. Sikuwahi kufikiria jambo hilo kwa mtazamo wa kiroho hapo awali. Lakini, ikiwa ndivyo ilivyo, na Ufalme wa Mungu hutenda kazi hivyo, basi najua naweza kujifunza sheria hizo, kuzitumia, na kupata manufaa yao maishani mwangu.

Nilitambua kwamba sheria zinazotawala dunia hii hazibadiliki. Kwa kweli, kazi yao ya kudumu na isiyobadilika inaweza kutegemewa kutuma mtu mwezini au kusababisha ndege kupaa angani. Lakini Wakristo wengi hawamwendei Mungu wakiwa na ufahamu huo. Badala yake, wao huomba na kulia wanapohitaji kitu, huku wakijaribu kumsadikisha Mungu kuhusu kile wanachohitaji kana kwamba Mungu hulazimika kuchagua kuwatunza.

Kwa mfano, ikiwa ningekuwa mnenaji katika kongamano la kanisa fulani, je, watu wote wa kanisa hilo wangeanza kuomba kwamba taa zisizime kwa mkutano huo? Je, wangefunga na kuomba wakimsihi Mungu, “Mungu, unajua jinsi mkutano huu ulivyo muhimu na jinsi tunavyohitaji taa hizo zisizime,” huku wakilia na kuomboleza katika sala? Sidhani. Hakika, sifikiri kwamba waliingiwa na wasiwasi wowote kuhusu taa kuzimika walipokuwa wakiandaa mkutano huo. Ikiwa kwa sababu moja au nyingine wangekuja jioni kwa kongamano na kupata taa zimezimwa, je, unafikiri wangeita kampuni ya umeme kuwasihii wawashe taa? La. Iwapo wangefanya hivyo, nina hakika mwakilishi wa kampuni angeskiliza kwa sekunde moja, amgeukie mfanyakazi mwenzake na kusema, “Nina kichaa hapa.” Kisha angesema, “Mama, umeme upo; tatizo liko upande wako.”

Ninapowaambia watu maneno haya katika mikutano yangu, kila mtu hucheka. Unajua kwa nini? Kwa sababu wanajua kuita kampuni ya umeme, kwa kilio kikubwa, kuwaambia wawashe taa ni ujinga; watu wengi wangejua cha kufanya. Wangebonyeza kibonyezi cha taa tu. Ni rahisi hivyo! Bila dhiki wala mafadhaiko. Je! unataka kujua ni kwa nini hawangesisitiza kwamba taa ziwashwe? Ni kwa sababu ya KUTARAJIA kwamba taa zingekuwa zimewashwa. Wangetarajia taa ziwashwe kwa sababu wanajua jinsi umeme unavyofanya kazi. Wanaelewa SHERIA ya umeme, na wanajua haibadiliki kamwe.

Lakini ukirudi nyuma miaka 1,000 iliyopita na kumwambia mtu kwamba ungewasha jiji zima kwa kutumia balbu ndogo za kioo, angefikiri wewe ni kichaa. Na kama wangeona jengo la jiji likiwashwa na balbu ndogo za vioo, wangesema ni muujiza. Kitu chochote watu wasichoweza kueleza, huwa wanakiita muujiza. Lakini sio muujiza bali ni sheria ya umeme inayofanya kazi kama inavyoweza kuwa kwa ye yeyote atakayechukua fursa ya kujifunza jinsi umeme unavyofanya kazi.

Tumejifunza jinsi umeme unavyofanya kazi, au unaweza kusema tumefanya upya akili zetu kuhusu sheria za umeme. Kwa hivyo tunatarajia umeme ufanye kazi na hatushangai tunapoona taa zimewaka. Tunashangaa zisipowaka. Kwa kuelewa sheria za umeme na kuziandika, tunaweza kuwasha taa kote ulimwenguni. Vipi? Kwa kuwafundisha wengine jinsi sheria hizi zinavyofanya kazi na kuwapa fursa ya kufurahia manufaa ya kuwa na taa pia. Haya yote yanawezekana kwa kuelewa sheria zinazosimamia umeme. Ndivyo ilivyo pia kuhusu sheria za kiroho. Ikiwa hatuzielewi, hatutakuwa na uwezo wa kufurahia manufaa yao au kuzitumia katika hali zingine tunapozihitaji.

Tunapoona ndege ikipaa angani, hatusemi, "Ajabu, huo ni muujiza." La, tunatarajia ndege kupaa kwa sababu, tena, tunaelewa jinsi ndege inavyopaa na ni kwa nini inapaa. Na tena, kama tungerudi nyuma miaka 1,000 na moja ya ndege mpya zenyenye ghorofa mbili aina ya Airbus 380 ikapaa juu ya miti, watu wangesema nini? Wangesema huo ni muujiza! Ninakubali ndege aina hii ni ya kuvutia sana, ina uzani wa pauni milioni 1.2, inabeba zaidi ya watu 800, inasafiri kwa mwendo wa maili 570 kwa saa moja kwa umbali wa maili 9,000. Inashangaza sana kiasi kwamba unaweza kufikiria ni muujiza. Lakini sivyo. Tunaweza kuwaauliza wahandisi waliounda ndege hii jinsi inavyopaa, na watatuambia kila sheria ya fizikia na vifaa walivyotumia ili ndege hiyo iweze kupaa. Wahandisi hawakuwa kwenye uwanja wa ndege mara yake ya kwanza ya kupaa wakisema, "Ajabu, tazama; siamini kwamba kitu hicho kinapaa." Tena, tuna uhakika tunapopanda ndege kwa sababu tunajua uwezo wake wa kupaa unategemea sheria za kiasili zisizobadilika. Mradi tukae ndani ya mipaka ya sheria hizo, ndege hiyo itapaa. Kumbuka hili: Sheria hazibadiliki!

Hatungepanda ndege ikiwa sheria yake haikuwa thabitii. Ikiwa tungenunu tikiti ya ndege inayosema, "Ilani - Safiri kwa ndege hii kwa hatari yako mwenyewe kwa sababu sheria ya mvuto hufanya kazi mara kwa mara. Siku moja sheria inafanya kazi na nyingine haifanyi kazi. Hakuna mtu anayejua kwa hakika—unajihisi kuwa na bahati? Safiri salama." Ni lini mara ya mwisho uliogopa kwamba utaalea kutoka kwa kiti chako? Kamwe? Kwa nini? Kwa sababu unajua sheria ya mvuto haibadiliki.

Mambo haya ambayo nimetaja ni sheria za asili za ulimwengu ambaao Mungu aliumba. Lakini wajua nini? Sheria za kiroho za Ufalme Wake hufanya kazi vivyo hivyo—hazibadiliki! Kabla ya Mungu kunena nami kuhusu Ufalme Wake, nilifahamu vyema sana jinsi sheria za asili za dunia zinavyofanya kazi, lakini nilifikiri Ufalme wa Mungu ulikuwa tofauti. Nilifikiri kwamba Mungu alifanya chochote alichotaka wakati wowote. Lakini niligundua kwamba huo haukuwa kweli. Nilipoona kwamba sheria za Ufalme wa kiroho wa Mungu hazibadiliki na zinaweza kusomwa, kueleweka, na kutumiwa, ndipo nilipolewa kwa nini Yesu alisema mara kwa mara, "Hivi ndivyo Ufalme wa Mungu ulivyo." Kisha angehusianisha Ufalme na kitu fulani katika ulimwengu wa asili ili watu waelewe jinsi ulivyofanya kazi. Ghafla, ni kama taa iliwaka akilini mwangu. Nilikuwa na wazo hili, "Ikiwa Mungu alitupa Ufalme, na kweli ametupa, na Ufalme unatenda kazi kulingana na sheria zisizobadilika, basi naweza kujifunza sheria hizo na kuzitumia maishani mwangu."

*Msiogope, enyi kundi dogo, kwa maana Baba yenu ameona vyema  
kuwapa ninyi Ufalme.*

– Luka 12:32

Hiyo ndiyo siku nilipata kuwa mwanasayansi wa mambo ya kiroho! Niliiona Biblia kwa njia tofauti kabisa. Nilianza kuuliza maswali niliposoma Biblia: “Kwa nini samaki hao waliongezeka? Kwa nini mtu huyo aliponywa? Kwa nini mkate huo uliongezeka?” na kadhalika. Nilipoisoma Biblia na mtazamo huo, wa kumwomba Mungu anionyeshe sheria zilizokuwa humo—AJABU!

Bwana aliponena nami ile siku ambayo wakili alinipgia simu na kuniambia shida yangu ni kwa sababu sikuwa nimejifunza jinsi Ufalme Wake unavyofanya kazi, mara moja nielienda nikatubu kwa mke wangu kwa kutomtafuta Bwana na kutuacha tuingie katika dhiki hii, kama nilivyosema hapo awali. Lakini hatukujua ilimaanisha nini hasa kutumaini Ufalme wa Mungu ili kupata majibu yetu. Tayari tulikuwa washirika kanisani, waliokuwa wakielekea mbinguni, na tulimpenda Mungu. Wakati huo hatukuwa na dhana ya kile Mungu alichomaanisha aliposema “Ufalme.” Tulikuwa na tatizo kubwa mikononi mwetu, na hatukujua jinsi ya kupata pesa wakili alizosema tuna siku tatu za kupata au jinsi ya kushughulikia kesi ambayo sasa ingeanzishwa dhidi yetu ikiwa hatungepata pesa hizo kabla ya siku tatu kuisha.

Kwa hiyo, hili lilikuwa jaribio nzuri. Ilikuwa mara yangu ya kwanza kuwa na tatizo la pesa, na nilitaka Bwana anionyeshe kile alichomaanisha aliposema “Ufalme.” Hebu nikwambie kilichotokea. Kumbuka, wakili alisema nilikuwa na siku tatu za kumletea pesa, ambazo sikuwa nazo! Kukata tamaa kwangu ndiko kulikonifanya niende chumbani mwangu na kumlilia Bwana; nilikuwa matatani! Hapo ndipo aliponena nami kuhusu Ufalme kuwa jibu langu; na tena, sikujua alichomaanisha, lakini hakika nilikuwa tayari kujifunza.

Baada ya siku mbili, jioni, nilielekea kukutana na mteja kuhusu bima yake ya maisha. Katika siku hizo nilikuwa nikiigesha gari langu pembeni mbali na nyumba ya mteja wangu, wala sio mbele ya nyumba yake. Gari dogo nililokuwa nikiendesha lilikuwa na tatizo kidogo. Nilipoliwasha, lilijaza barabara na moshi mwingi mweupe. Nilihisi kila wakati kwamba haingesaidia biashara ikiwa ningegesha gari mbele ya nyumba ya mteja wangu, kisha, baada ya kuondoka, nikajaza moshi kwa barabara yake. Niliwaza kwamba uaminifu wangu katika eneo la fedha ungeathiriwa

kidogo ikiwa hilo lingetokea kwa sababu nilikuwa nikiwataka wawekeze mamia ya maelfu ya dola kwa kampuni yangu. Ikiwa nilikuwa meneja mkuu wa fedha, kwa nini nilikuwa nikiendesha gari lililokuwa na hitilafu? Jioni hiyo haikuwa tofauti.

Nilipokuwa nikitoka nyumbani kwa mteja wangu, nilijawa na hofu kuona kwamba mteja wangu alikuwa akinifuata barabarani kwenda kwa gari langu. Hakumaanisha chochote kwa hilo; tulikuwa tukiongea tu. Lakini nilikuwa na wasiwasi kidogo kwamba angekaa hapo hadi nilipowasha gari. Tuliendelea kuongea huku nikiingia kwenye gari langu. Niliendelea kuzungumza naye huku nikiwa nimefungua dirisha la gari, nikitumaini kwamba angeniaga kwa kusema “usiku mwema” na ningejifanya kana kwamba ninafanya kitu kwa dakika moja alipokuwa akiondoka, lakini hakufanya hivyo. Hatimaye, alisema “usiku mwema,” kisha akarudi nyuma kutoka kwa gari tu na kusimama pale. Nilijua nilikuwa nimepatikana. Niliwasha gari, nikitumaini kwamba labda mara hii moja haitafuka moshi mweupe, lakini haikuwa hivyo. Mara moja, hewa ilijaa moshi ambao ulichoma macho.

Mteja wangu alinipungia mkono kwa haraka, nizime gari. Alirudi kwa dirisha na kuniuliza kama ningeweza kufungua sehemu ya mbele ya gari. Kisha akaendelea kunieleza kwamba alifanya kazi ya kando kama fundi wa magari, na alitaka kuangalia jambo fulani. Baada ya dakika moja, alirudi na kusema, “Ni vile nilivyoshuku; kifaa kinachozuia maji ya injini kumwagika na hivyo kupunguza nguvu ya gari kimepasuka. Peleka gari nyumbani na urekebishe hilo mara moja.” Nilimshukuru huku nikiondoka na gari, lakini tathmini yake haikuwa na maana yoyote kwangu. Sikuwa na pesa za kukarabati gari.

Ofisi yangu ilikuwa kama maili sita tu kutoka nyumbani kwa mteja wangu, na nilipoelekea ofisini mwangu, uzito wa kushusha moyo ulinifunika. Lakini nilipokuwa nikiendesha gari, nilikumbuka kile ambacho Bwana alikuwa ameniambia, na nikaanza kuzungumza naye kuhusu gari langu. “Bwana,” nikasema, “sina pesa za kukarabati gari hili. Bado nina deni lake, na siwezi kuliiza likiwa na hitilafu. Sijui la kufanya. Labda itakuwa bora liungue. Hivyo kampuni ya bima italilipia na litaniondokea.”

Takriban maili tatu kutoka kwa ofisi yangu, niliona tone kwa sehemu ya mbele ya gari kana kwamba ilikuwa ikichemka, jambo sikuwa nimeona awali. Nilipotazama, tone hilo lilizidi kuwa kubwa zaidi na zaidi, na nilipoingia kwenye sehemu ya kuegesha magari katika ofisi yangu, tone hilo lilipasuka likawa kama duara la moto. Nilipigwa na mshtuko; sehemu

nzima ya mbele ilikuwa imefunikwa na moto uliokuwa na urefu wa futi sita. Nilikimbia haraka ndani ya ofisi na kupiga simu kwa wazima moto. Siku

**PAPO HAPO, TULIKUWA  
TUMEJITHIBITISHIA  
WENYEWE KWAMBA  
MFUMO WA MUNGU  
UNAFANYA KAZI, NASI  
TUKAJITOlea KUENDELEA  
KUJIFUNZA NA KUTUMIA  
MFUMO WA UFALME WAKE  
KUANZIA WAKATI HUO  
NA KUENDELEA.**

iliyofuata, kampuni ya bima ilijumlisha hesabu ya gari, kisha wakanilipa pesa ambazo zilitosha kuilipia na kutumia yule wakili aliyenipigia simu siku tatu awali. Mimi na Drenda tulishangaa. Hatukujua la kufikiria. Tulijua kwamba Mungu alikuwa akifanya kazi kwa ajili yetu na kwamba jambo lilikuwa linabadilika. Lakini kujitoa kwetu katika Ufalme kulikuwa karibu kujaribiwa kwa njia mpya ambayo ingefanyika mwongozo wetu kwa miaka mingi baadaye.

Baada ya gari hilo kuungua, bila shaka tulisisimka, lakini ghafla tuligundua kwamba hatukuwa na gari. Ingawa gari lilikuwa limelipiwa na wakili wa kadi ya mkopo alikuwa amelipwa, hatukuwa na pesa za kununua gari jipya. Babangu aliposikia kuhusu kuteketeta kwa gari letu, alitupigia simu akatuambia kwamba alitaka kutusaidia kununua gari jipya. Tulifurahi tuliposikia habari hizo. Kwa hiyo mimi na baba tulienda kwenye eneo la kuuza magari na kupata gari ambalo mimi na Drenda tulipenda. Baba yangu alisema kwamba angetupa \$5,000 ili kuongezea kwa jumla ya bei yake, ambayo ilikuwa karibu \$17,000. Hilo lingetuachia \$12,000 za kulipia sisi wenyeve. Nilijaza fomu la mkopo bila kupenda na babangu akatia saini yake. Walisema wangewasiliana nami asubuhi iliyofuata.

Usiku huo hatukuweza kulala. Tulifahamu kwamba haingefaa tuchukue mkopo huo. Bwana alikuwa amenena nami kuhusu kutofanya jambo kama hilo. Lakini kwa kuwa sikuwa na gari, shinikizo lilikuwepo kwamba nikubali nichukue mkopo. Baada ya usingizi mzito sana, mimi na Drenda tulikubaliana tusitie sahihi kwenye fomu hiyo ya mkopo. Nilimpigia baba yangu simu na nikamshukuru kwa toleo lake zuri lakini nikamwambia kwamba hatukulikubali. Kisha nikapiga simu kwa wauzaji na kuwaambia jambo lile lile. Walikatishwa tamaa kwa sababu mkopo ulikuwa umeidhinishwa asubuhi hiyo na gari lilikuwa tayari kuchukuliwa. Ingawa hatukujua jinsi Mungu angelivyotusaidia na gari letu, tulihisi amani kuhusu hilo.

Katika kipindi hicho, Drenda alikuwa akiuza vitu vichache nya kale alivyopata kweneye mnada. Alikuwa amemwachia mtu fulani ujumbe kuhusu kununua samani alizokuwa akiuza mwezi mmoja kabla ya gari letu kuteketeta, lakini hakuweza kuwasiliana naye. Siku mbili baada ya gari letu kuungua, mtu huyo alimpigia Drenda simu na kukubali kumuuzia samani hizo zilizoja kwa vyumba vitatu kwa chini ya \$1,000. Drenda alifanya makubaliano na kampuni ya mnada kumuuzia samani hizo na kuweza kujadiliana nao kwamba kama kamisheni ya kuziua wampe gari la kampuni lililotumika badala ya pesa taslimu. Kwa hivyo sasa tulikuwa na gari nzuri bila deni, kadi ya mkopo na mkopo wa gari zote zilikuwa zimelipiwa.

Ajabu! Hivyo ndivyo Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi. Papo hapo, tulikuwa tumejithibitishia wenyewe kwamba mfumo wa Mungu unafanya kazi, nasi tukajitolea kuendelea kujifunza na kutumia mfumo wa Ufalme Wake kuanzia wakati huo na kuendelea. Unaweza kuuliza, “Tulifuata kanuni gani?” Muhimu kabisa ilikuwa kutoamini madeni bali kumwomba Mungu kile tulichohitaji na kumwachia atuonyeshe jinsi ya kukipata.

Tukio hilo la gari lilinishangaza na kutia nguvu kisa kingine kilichotukia miezi michache awali, lakini wakati huo, sikuelewa Mungu alikuwa akinionyesha nini. Nukta hizo bado hazikuwa zimeunganishwa akilini mwangu kama kanuni ya Ufalme.

Napenda kuwinda kulungu lakini sikuwa napata kitu kwa miaka mingi. Nilikuwa ninatoka nje, ninakaa kwa baridi siku hadi siku bila bahati. Sio tu kwamba nilikuwa ninapenda kuwinda; bali nilikuwa na watoto wa kulisha na hakika nilihitaji mawindo. Ingawa nilifanikiwa kidogo hapo awali, miaka kadhaa ilikuwa imepita tangu niwe na msimu mzuri wa kuleta nyama ya kulungu nyumbani. Siku moja nilipokuwa nikifirkiria kuhusu msimu wa uwindaji wa kulungu uliokuwa ukija, nilisikia sauti ya Bwana. Alisema, “Kwa nini usiniruhusu nikuonyeshe jinsi ya kupata kulungu wako mwaka huu?” Hilo lilinishangaza. “Anionyeshe jinsi ya kupata kulungu wangu mwaka huu?” Hiyo ina maana gani? Nilipoomba kuhusu maneno hayo, nilihisi kutoa fedha kama mbegu au kipaji kwa kusudi hasa la kumwinda kulungu huyo. Nilihisi Bwana akiniambia kwamba nilipotoa mbegu yangu, nilipaswa kuamini kwamba tayari nilikuwa nimempokea kulungu kabla ya kumpata, kulingana na Marko 11:24:

*Kwa hiyo nawaambia, Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.*

Ingawa kama Mkristo sikuzote nilitoa na kusaidia kanisa letu, kutoa kama huku kwenye mtazamo uliozingatia na kuamini kwamba nitapokea nitakaposali ulikuwa mpya. Nilichukua hundi nikaandika katika sehemu ya kumbukumbu, "Kwa ajili ya kulungu wangu wa 1987." Niliwekelea mikono na kuituma kwa huduma niliyokuwa na imani nayo na nikatangaza kwamba nilipokea kulungu wangu wakati niliituma. Maana nilikuwa ninaishi katika mipaka ya jiji la Tulsa, Oklahoma wakati huo, kweli sikuwa na mahali pa kuwinda, lakini rafiki yangu kutoka kanisani alinalialika twende nyumbani kwa nyanyake mashambani kwa ajili ya Siku ya Kutoa Shukrani. Alisema kulikuwa na kulungu wachache karibu na shamba hilo. Kwa hivyo familia yangu ilielekea asubuhi mapema ili kufurahia siku hiyo kuu ya chakula na ushirika na sasa kumkamata kulungu wangu.

Rafiki yangu hakujuuani ambie niende wapi hasa, lakini kulikuwa na malisho ya wanyama yaliyokuwa yamepakanana msitu, akapendekeza niende huko na nikae karibu na mti mkubwa uliokuwa pale. Sasa, nataka upate picha hii. Niliketi sehemu ambayo nyasi ilikuwa imekatwa na mti mkubwa ulikuwa katikati. Kwa hiyo niliketi na kuegemeza mgongo wangu kwenye mti huo na kuangalia upande wa msitu, amba labda ulikuwa na umbali wa karibu mita 120 kutoka kwangu. Sasa ninapotazama nyuma, nilikuwa nimeketi kando ya mti pale nje uwanjani, sio hali unayoweza kuiita bora.

Asubuhi hiyo, baada ya takriban dakika 30 au 40, bila mimi kujua, kulungu dume aliokuwa akikimbia kwenye uwanja nyuma yangu kuelekea kwenye msitu uliokuwa mbele yangu. Mti ulizua kulungu kuniona wala mimi kumwona. Kulungu alikimbia moja kwa moja kuelekea kwenye mti ule huku akielekea porini, bila kuona kwamba nilikuwa nimeketi pale. Alipokaribia mti ule, alisikia harufu yangu na akasimama huku akishangaa nilikuwa wapi. Alizunguka mti ule, na macho yetu yakaangaliana papo hapo tukiwa na umbali wa karibu mita tano tu. Sina hakika ni nani aliyeshangaa zaidi, lakini dume huyo hakupoteza wakati katika kutoroka haraka sana. Alikoroma vikali huku akinyanyuka kwa kasi kuelekea msituni. Bado nilikuwa nimeketi pale, huku akikimbia kwa kasi, nami nikijaribu kuinyanya bunduki yangu ili nimpate akiwa karibu.

Sasa, kujaribu kumlenga kikamilifu kulungu huyo mwenye mkia mweupe mwenye mbio za kasi na kufyatua risasi haikuwa rahisi. Kusema kweli, sikuwa nimewahi kumpiga risasi kulungu aliye kuwa anakimbia. Nakumbuka kwamba ilikuwa vigumu kumfikia kulungu huyo kwa sababu alikuwa akiruka juu angani, kama vile kulungu wenye mikia mieupe

wanavyofanya wanapokimbia kwa kasi. Lakini nilipofyatua risasi, alianguka wala hakusonga. Nilishtuka! Yote yalifanyika kwa sekunde moja. Nilimpiga risasi nikiwa katika umbali wa karibu mita tisini maana nilimkimbiza.

Rafiki yangu aliposikia sauti ya bunduki, alitoka nje na kunipongeza kwa kumuua kulungu kwa kuwa alimwona akiwa amelala hapo chini. Sikuwa nimemwambia rafiki yangu kile ambacho Bwana alikuwa ameniambia kuhusu jinsi ya kumpokea kulungu wangu, lakini sasa nilimtzama na kusema, "Sidhani nilimuua kulungu huyu kwa sababu ya uwezo wangu mkubwa wa kuwinda." Kisha nikachomoa kutoka kwa koti langu la kuwinda kipande cha karatasi, ambacho nilikuwa nimeandika siku nilipotuma hundi ile. Nilikuwa nimeandika, "Naamini nimempokea kulungu wangu wa 1987, kwa jina la Yesu." Kilikuwa na tarehe na saa niliyoomba sala hiyo pia. Niliinua kikaratasi hicho ili rafiki yangu akione kisha nikaanza kumwambia kuhusu kile Bwana alichoniambia nifanye.

Tukio hili lilivutia umakini wangu. Najua bila shaka kwamba Mungu ndiye aliyesababisha tukio hilo. Lakini kwa sababu moja au nyine, sikuelewa kwamba nilikuwa natumia sheria ya Ufalme. Kwa kweli, bado sikuwa nimefikiria neno "Ufalme." Kumpata kulungu huyo nilikuwa jambo la kushangaza, lakini je, lingetokea tena? Bila dhana ya sheria ya Ufalme, singejua jinsi au ni sheria gani zilizosababisha kulungu huyo kujitoneza. Kwa hivyo niliweka hilo akilini mwangu kama kitendo cha kiungu na nikatarajia kujaribu tena katika msimu mwingine wa kulungu. Lakini kabla ya msimu huo kuja, gari letu liliteketea. Mara baada ya hilo na gari lingine kutokea bila deni, Mungu alikuwa na usikivu wangu kamili. Sasa nilikuwa na furaha sana kwenda kuwinda kulungu katika msimu uliokuwa ukija. Nilitaka kujaribu nadharia yangu na kujifunza zaidi kuhusu Ufalme wa Mungu. Msimu mwingine wa kulungu haukuwa mbali sana!

Nilimuua kulungu huyo wa kwanza huko Oklahoma katika msimu wa vuli wa 1987. Lakini mnamo Julai 1988, tulihamia Ohio ambako nililelewa. Ingawa nilikuwa nimekulua huko, ilikuwa imepita miaka 12 tangu niishi huko. Nilipokuwa nikikulia huko, sikupata mafanikio yoyote katika kuwinda kulungu huko. Ingawa nilikuwa nimejaribu mara kadhaa, sikuwa nimempiga risasi hata kulungu mmoja. Mara tu tulipopata nyumba mjini ambapo tulikuwa tukikodisha huko, nilitambua kwamba sikuja mahali pa kwenda kuwinda. Nikiwa mvulana, nilikuwa nimewinda sungura kando ya barabara ya nyumba ya baba yangu karibu na kijito kilichokuwa hapo. Niliweka mitego kwa miaka kadhaa nilipokuwa nikikua, lakini kamwe sikuona hata kulungu mmoja au ishara yoyote kwamba kulungu walikuwa

katika eneo hilo. Siku moja nikiwa chuoni, kaka yangu alinipigia simu kwa furaha. Alisema alikuwa amemwona kulungu akipita kando ya kijito karibu na nyumba ya baba yangu. Sote tulishtuka.

Nilipokumbuka mazungumzo hayo, niliamua kwamba ningelekeea chini kwa kijito hicho katika siku ya kwanza ya msimu wa kulungu. Nilimpigia simu kaka yangu na kumwomba ushauri kuhusu sehemu ya kwenda katika kile kijito. Ingawa miaka michache ilikuwa imepita tangu arudi huko, alikumbuka mti mkubwa wa mchongoma uliokuwa ukipakana na kijito nyuma ya msitu na akafikiri kwamba huenda palikuwa mahali pazuri. Kwa kuwa nilikuwa nimeenda juu na chini ya kijito kile katika miaka yangu yote ya kukua, nilijua kila sehemu ya kijito hicho na nilijua ni wapi alikuwa akinielekeza.

Drenda nami tulirudia kile Bwana alichotuonyesha mwaka uliopita huko Oklahoma—toa toleo kama mbegu, liandike, na kuamini kwamba tumepokea tunapoomba, kulingana na Marko 11:24. Wakati huo, Ohio haikuruhusu uwindaji wa zaidi ya kulungu wawili iwe wa kike au dume, lakini tulifikiri kutoa toleo la kulungu mmoja kisha baadaye tungeenda kumwinda wa pili. Mimi na Drenda tulitoa toleo la kulungu mmoja na tukaamini kwamba tulimpokea tulipoomba. Cha kushangaza ni kwamba, asubuhi ya mwanzo wa msimu wa kulungu, katika dakika 40, sikuwa na kulungu mmoja tu bali wawili. Ajabu, hakika tulikuwa na jambo hapa!

Baada ya mwezi mmoja, nilikuwa na ndoto kuhusu wazo la biashara. Biashara ilihuisha ujuzi wote wa kifedha niliopata kutoka kwa biashara ya bima, lakini ilikuwa na madhumuni tofauti katika ndoto. Sikuelewa kabisa, lakini nilikuwa na hakika kwamba Mungu alikuwa akiniongoza kuanzisha biashara yangu mwenyewe na kuacha kampuni niliyokuwa nayo kwa miaka minane. Wakati wa ndoto hii, nilikuwa bado nikifanya kazi ya kuuza bima ya maisha na dhamana.

Wiki niliyoota ndoto hiyo, nilikuwa na mpango wa kutembelea familia fulani ili kuzungumza juu ya bima, na ingawa tulizungumza juu yake, nilifahamu kwamba kumiliki bima ya maisha haikuwa hitaji lao au shida yao halisi. Walikuwa katika hali mbaya kwa bajeti yao ya kila mwezi na katika madeni. Mojawapo ya kazi yangu ya kawaiida kwa wateja ilikuwa kuwapa fomu ya kujaza taarifa zao zote za kifedha. Hii ilinipa fursa ya kujua ni kiwango gani cha bima ya maisha ambacho wangehitaji. Usiku huo, nilikasirishwa na familia hiyo. Nilitaka kuwasaidia, lakini sikujua kwa jinsi gani. Niliketi na fomu yao na nikaanza kuichunguza ili kufanya uamuzi kuhusu aina tofauti ya bima iliyowafaa. Nilipofanya kazi na kikokotoo

changu cha fedha, niliachana na bima ya maisha na nikaanza kuchunguza kama ningeweza kutenga pesa zozote katika bajeti yao ya kila mwezi. Kwa kupanga upya mambo machache na kwa kutumia kikokotoo, nilishangaa

kwamba familia hiyo ingeweza kutoka kwa madeni chini ya miaka 7, ikiwa ni pamoja na rehani yao, bila kubadilisha mapato yao.

Kufikia wakati huo, nilikuwa nimefanya kazi katika nyanja ya fedha kwa miaka 8, na sikuwa nimewahi kusikia mtu akisema hilo lingewezekana. Nilirudia hesabu tena

na tena na nikapata jibu sawa: miaka 6.2 tu na wangetoka kwa madeni. Kisha nikaenda kwenye kabati langu la faili na kuanza kuchunguza fomu za taarifa za wateja wengine. Nilifanya hesabu ile ile na nikapata jibu sawa: chini ya miaka 7 wangetoka kwa madeni. Kwa kweli, nilishtushwa na habari hizi.

Niliwaza kwamba mteja wangu angetiwa moyo kuona hili, kwa hiyo nikaamua kuchapa kipande cha karatasi vyema na nikawasilisha nilichopata nilipokutana nao kujadiliana kuhusu mahitaji yao ya bima ya maisha. Nilihisi vibaya sana kuhusu familia hii. Nilijua jinsi shinikizo la kifedha linavyoathiri kila eneo la maisha na nilitaka wasikate tamaa. Kwa hiyo niliwaonyesha karatasi yangu ndogo iliyochapwa, na nilipowaelezea ile hesabu wakiwa wameketi pale, walipigwa na butwaa. Baada ya kuwaonyesha jinsi wangelyoyeza kumaliza deni haraka, yule mume alirukaruka huku machozi yakimdondoka na kuanza kunishukuru. Kwa kweli, ilikuwa kama tunavyoona kwenye runinga familia inaposhinda bahati nasibu au zawadi kuu kwenye kipindi cha mchezo. Walishindwa kuamini nilichokuwa nikiwaambia. Kwa kweli lilikuwa jambo la kusisimua kwao, lakini pia kwangu.

Nilipotafakari jioni hiyo, singeweza kuondoa wazo akilini mwangu kwamba kwa kupanga upya mali na fedha za mteja huyo niliweza kuwaonyesha jinsi ya kutoka kwa madeni katika muda usiozidi miaka 7. Niliona jinsi jambo hili lilivyowagusa na kuwapa tumaini. Nilirudi kwa faili nyingi za wateja wangu na nikashangaa kuona kwamba asilimia 85 yao walikuwa katika kikundi hicho cha “kuwa huru kutoka kwa madeni katika muda usiozidi miaka 7.” Lakini ni nani aliquwa akiwafunza watu hivi? Baada ya kuwa na mteja wangu usiku ule na baada ya kuchunguza

faili nyingi za wateja wangu wa zamani, niligundua kwamba ningeweza kuanzisha biashara ya kuwaonyesha watu jinsi ya kujiondoa kwa madeni kwa kutumia mpango wangu.

Sasa, wakati huo sikuwa na deni, lakini kweli nilihurumia watu waliokuwa chini ya shinikizo la kifedha, na kazi hii ilinivutia zaidi kuliko kuuza bima ya maisha. Nilianza kuwaonyesha wateja wangu wote wa bima mpango wangu nilioupiga chapa, na kila mmoja wao alishtuka.

Katika mfumo wangu wa biashara, nilikuwa na shida kadhaa za kutatua. Kwanza ilinichukua muda mrefu kufanya mahesabu kwa mkono na kisha kuyachapisha kwa mkono kwa muundo uliofaa. Pili, ningepataje pesa kwa kufanya biashara hii? Hatimaye, nilifanya mapatano na mbuni wa programu za kompyuta naye akaandaa programu ambayo ningeweza kutumia kutayarisha mpangilio huo haraka zaidi. Kuhusu tatizo langu la pili, niliuja kwamba kweli singeweza kuwatoza watu pesa ili watoke kwa madeni wakati hawakuwa na pesa. Nilianza kusali kuhusu hili.

Siku moja nilipata wazo la ajabu. Nilihisi kwamba Mungu alinipa wazo la jinsi ya kuendesha biashara ya kampuni yangu, kusaidia watu bila kuwalipisha na wakati huohuo, kupata pesa. Katika mpango wangu, ningetafuta nilichoita pesa iliyopotea, pesa ambayo mteja alikuwa nayo lakini hakuiona. Kwa mfano, ningelinganisha viwango vya bima ya magari, nyumba, maisha na afya, huku nikitatufa kuokoa pesa. Ningelinganisha viwango vya rehani ili kuona ikiwa kukopa tena kulikuwa na maana yoyote. Ningegangalia mambo mengi kama hayo, ingawa sikushughulikia kibinasi kila eneo nililotafiti. Nilipokuwa nikiwatembalea wateja wangu, ningewaonyesha pesa zilizookolewa kwa bajeti yao kisha ningewatuma kutafuta kampuni ambayo ingeweza kutekeleza mfumo wangu au kutafuta mwakilishi ambaye alishughulikia kampuni niliyokuwa nimepata ambayo haikuwa na gharama kubwa kwao. Ghafla, niliwaza kwamba ningelipisha makampuni hayo ada ya rufaa kwa kuwapa wateja.

Tayari nilikuwa nimefanya kazi yote ya kuwajulisha wateja kuhusu makampuni hayo na kuwauzia bidhaa zao. Walichotakiwa kufanya ni kuwasajili tu. Kwa hivyo nilianza kuwasiliana na wachuuzi, wawakilishi, na wataalamu ambao nilipendekeza kwa wateja wangu na kuwaambia nilichokuwa nikifanya na kuwaauliza ikiwa walifikiri nilistahili kulipisha ada ya rufaa. Wote walisema, "Ndio." Hivyo ndivyo nilivyofanya. Niliacha kampuni yangu ya zamani na kuanzisha kampuni yangu ya kusaidia watu kutoka kwenye madeni. Biashara ilishamiri na, katika mchakato huo, ilizalisha pesa za kutosha kwangu na Drenda kutoka kwa madeni katika

kipindi cha miaka miwili na nusu! Tulifurahi sana! (Ikiwa una nia ya kutayarishiwa mpango bila malipo, piga 1-800-815-0818. Bado tunafanya hivyo leo, baada ya miaka 28!)

Kila siku ilikuwa siku mpya maana Mungu aliendelea katuonyesha zaidi na zaidi jinsi Ufalme Wake unavyofanya kazi. Nilipokuwa nikitembelea mteja mwingine, Mungu alinena nami kuhusu kuajiri watu na kujenga biashara yangu ndogo iwe biashara halisi. Nilipoajiri watu wa kufanya kazi nasi, biashara yetu ilianza kufanikiwa kwa viwango vikubwa zaidi. Nilikuambia katika utangulizi jinsi tulivyoanza kulipa pesa taslimu tuliponunua magari yetu na jinsi tulivyojenga nyumba ya ndoto yetu. Wakati wa mikutano yangu ya biashara ya kila mwezi na wafanyakazi wangu wapya, nilishiriki kuhusu Ufalme wa Mungu, na watu walivutwa kwenye kampuni yangu ili kusikia zaidi kuhusu Ufalme na jinsi ya kuutumia maishani mwao wenyewe ingawa walikuwa wamekuja kwa ajili ya fursa ya biashara yenyewe.

Masomo ambayo Mungu alikuwa akinionyesha yalikuwa ya ajabu na, bila shaka, nilijifunza mengi yao nilipokuwa nikiwinda kila mwaka. Mambo niliyoyaona katika uwindaji yalikuwa ya kushangaza, kusema kweli. Nisingeyaamini isipokuwa niliyaona yakinende mbele ya macho yangu. Kila hadithi ilinifundisha jambo jipya ambalo sikuwa nimewahi kuona kuhusu Ufalme. Niliwaza nishiriki nawe mambo machache katika kitabu hiki, lakini ikiwa kweli ungependa kusoma hadithi zangu za uwindaji, unaweza kupata nakala ya kitabu changu, *Faith Hunt*, kutoka kwenye tovuti yangu.

Tukio hili lilitokea miaka kadhaa baada ya kugundua jinsi ya kuwinda kulungu kwa kutumia ujuzi wangu mpya wa Ufalme. Kama nilivyoshiriki nawe tayari, Mungu alinifundisha jinsi ya kutoa matoleo kama mbegu kwa ajili ya kulungu wangu na kuamini nimepokea nilipoomba—na bila kukosa, kila mwaka nilimuua kulungu wangu kati ya dakika 30 hadi 45. Hilo limejirudia kwa miaka 28. Walakini, kuna mwaka mmoja nilitoka kama kawaida, nikiwa na hakika kabisa kwamba kulungu angetokea. Hakika, katika dakika chache, niliona dume akitembea kutoka kwangu na kukaribia shamba la jirani yangu umbali wa karibu mita 180. Nilijua kwamba mara tu kulungu huyo angeingia msituni atakuwa ameponyoka, na bado nilijua kwamba alikuwa wangu. Hii ilikuwa mwanzoni kabla ya kujuachochote kuhusu jinsi ya kutumia mishale, kukoroma, au kutoa sauti zinazoita kulungu dume. Nilijua kwamba dume huyo alikuwa mavuno yangu, lakini nilitazama bila tumaini yule dume akiwa karibu kuingia kwenye shamba la jirani yangu. Lakini ghafla nikasikia rohoni mwangu, “Mwambie aje

kwako.” “Eti nini? Nimwambie aje kwangu; maana yake nini?” Sikuwa na hakika, kwa hivyo nikasema kwa sauti kubwa, ingawa haikuwa kubwa vya kutosha ambapo kulungu angenisikia, “Kulungu, ninakuamuru ukome kutembea, ugeuke, na uje usimame hapa chini ya mti wangu.” Niliongeza sehemu ya mwisho ya kusimama chini ya mti maana nilikuwa ninatumia mshale siku hiyo na nilitaka kulungu awe karibu kabisa. Niliwaza kwamba ikiwa imani ingeniletea dume huyo, basi ingekuwa afadhali aje chini ya mti wangu ambapo ningeweza kuipiga mshale rahisi.

Cha kushangaza ni kwamba, niliposema maneno hayo, dume yule alikoma kutembea mara moja, akageuka na kuanza kuelekea moja kwa moja kwa mti wangu. Nilikuwa na mshtuko wakati yule dume alipotembea zile mita 180 na kuja moja kwa moja chini ya mti wangu na, naam, alisimama tuli chini ya mti wangu, uliokuwa na umbali wa futi 12 juu yake. Sikuwa nimevaa nguo za kujisitiri, wala kutumia harufu, au milio ya kukoroma, bali ilikuwa mimi na Mungu tu, na kulungu huyo sasa alikuwa amesimama moja kwa moja chini yangu. Katika umbali huo sidhani kuna mtu yejote ambaye angekosa kumuua. Nilimpeleka dume huyo nyumbani kwa furaha kubwa, lakini singeweza kusahau nilichokuwa nimeona. Je! kweli kulungu huyo alinijia kwa sababu nilitamka na kumwamuru? Hakika ilionekana hivyo.

Shamba tulilokuwa tukikodisha huko Ohio lilikuwa kwenye ekari 89 na lilikuwa na miti, vichaka kwenye sehemu za chini za kijito, na mashamba. Wakati wa miezi ya baridi, na hasa kulipokuwa na theluji ardhini, tulipenda kwenda kuwinda sungura. Ohio ilikuwa na msimu wa ndege zenye mviringo kama pete kwa shingo ulioambatana na msimu wa sungura, lakini kwa kawaida hatukuona ndege hao kwenye shamba letu.

Siku moja tulikuwa tumetoka kuwinda sungura kwenye sehemu ya chini ya kijito wakati tulimwona ndege mmoja jogoo akipita. Haraka nilimrukia yule ndege na kumpiga risasi. Nilijua dakika nilipofyatua risasi kwamba nilikuwa nimekata bawa lake tu. Yule ndege alianguka; lakini, alipofika ardhini, aliruka na kukimbia haraka. Aliweza kukimbia mwendo wa maili 35 kwa saa moja, na alifanya kila awezalo kuhakikisha hilo. Ardhi ilikuwa imefunikwa na theluji mpya, na ndege alikuwa akikimbia kwenye uwanja wazi kwa sehemu iliyokuwa imeinuka kidogo, kwa hivyo niliweza kuona kwa urahisi kila hatua aliyoipiga alipokuwa akitoroka.

Nilisimama pale kwa muda nikiwa nimekata tamaa nikidhani ndege angeondoka, lakini ghafla nilihisi kitu rohoni. Nilijua kilichotokea nilipomwamuru yule kulungu dume kusimama na kuja upande wangu.

Nilihisi nilipaswa kujaribu hilo sasa, kwa hiyo nikasema kwa sauti kubwa, "Ndege, katika jina la Yesu, SIMAMA!" Mara moja, sikuona tena ndege akienda mbele au juu. Niliona dhahiri uwanja mzima, na ndege alikuwa amesimama wakati ule ule nilipoamuru kwa sauti kubwa. Mwanangu Tim ambaye alikuwa nami alisema, "Baba, ndege alisimama dakika tu ulipopaza sauti." Lakini alikuwa wapi? Tim na mimi tulimfuata hadi uwanjani, na tukampata hapo juu ya theluji. Karibu nusu ya kichwa chake kilikuwa kimezikwa ndani ya theluji, lakini mwili wake wote ulikuwa nje, kwenye theluji. Alikuwa amefichwa kidogo na nyasi, ndiyo sababu hatukumwona awali. Je, alikuwa amekufa? Nilimnyanya yule ndege, ambaye mara moja alipeperusha mabawa yake na kupiga kelele. Ndege alikuwa hai kabisa! Nilipomchunguza yule ndege wakati tulipomchinja, niliona kwamba nilikuwa nimempiga kidogo tu kwa bawa lake la kulia. Mimi na Tim tulitazamana kwa mshangao. Hakuna hata mtu mmoja ambaye angeamini kile tulichokuwa tumeona, la hasha!

Kama niliviyotaja hapo awali, kule Ohio hawakuruhusu uwindaji wa zaidi ya kulungu wawili wa jinsia yoyote, lakini dume mmoja tu ndiye aliyekubaliwa kuwindwa kwa mwaka. Jimbo la Ohio lilikuwa linajaribu kupunguza idadi ya kulungu kwa kulenga kulungu wa kike zaidi. Kwa hiyo ningetoa matoleo yangu ili kuua jinsia zote, kisha siku ya kwanza kila mara, dume angetokea baada ya dakika 30 hadi 40; halafu mara ya pili nilipoenda kuwinda kulungu wa kike angetokea. Siku moja ufahamu ulinijia, "Subiri kidogo; kulungu wanakuja kwa utaratibu ambao niliwaandika nilipotoa matoleo yangu." Je, hiyo ni kweli? Ni kitu gani kingetokea kama ningebadilisha utaratibu huo? Kawaida nilitoa matoleo ya kulungu dume kisha wa kike, na hivyo ndiyo walivyojitekeza. Kwa hivyo mara hii, nilitoa matoleo ya kulungu wa kike kisha ya dume badala ya kulungu dume kisha ya kike; na tena kulungu walikuja, lakini wakati huu kulungu wa kike alikuja kwanza kisha dume. Nilibadilisha utaratibu huu kwa miaka michache, huku nikijaribu kuthibitisha ikiwa nadharia yangu ilifanya kazi, na ilifua dafu kila wakati. Nilipoona mambo hayo yakitendeka, nilistaajabu sana Ufalme na jinsi nilivyojua mambo machache kuuhusu. Jambo moja lilikuwa hakika, Bwana alikuwa akinionyesha kwamba nilikuwa na mamlaka mengi zaidi kuhusiana na jinsi maisha yangu yalivyokuwa yanaenda kuliko nilivywahi kufikiria.

Neno la ziada, huu ni msimu wa kulungu wa mwaka wa 2015. Nilitoa matoleo ya kulungu dume mwenye pembe nne (uzani wa karibu kilo sabini) au zaidi, kulungu mchanga wa kike, na dume mchanga, kama chakula

cha familia yangu. Kama ilivyo kawaida, kulungu mwenye pembe sita alikuja moja kwa moja kwa mti wangu; kisha wakati mwingine nilipoenda kuwinda, akaja kwa mti wangu kulungu mchanga wa kike mmoja tu. Najua wakati mwingine nitakapokwenda kuwinda dume mchanga atatokea. Nafahamu haya yote yanaskika kana kwamba ni mzaha; lakini nakuambia kile ninachoona kikitokea.

Lakini kulikuwa na uwindaji mmoja wa kulungu uliofanya haya yote kuwa dhahiri sana kiasi cha kuniogopesha. Nilikuwa nimetoa matoleo yangu ya kulungu dume mwenye pembe nne au zaidi na pia ya kulungu dume mchanga mwenye pembe ndogo sana (kulungu dume mchanga huhesabiwa kama kulungu wa kike kwa sababu pembe zake ziko chini ya manyoya na ni ndogo sana). Nilienda kuwinda kama kawaida na kulungu wangu dume mwenye pembe nane alitokea baada ya dakika 15 wakati wa msimu wa kuwinda na mshale na upinde. Nilipoenda kuwinda wakati uliofuata, nilikuwa na hakika kwamba kulungu wangu dume mwenye pembe ndogo angekuwa pale.

Baada ya majuma mawili nilienda kuwinda tena, na nilipokuwa nimeketi chini ya mti wangu, niliona kulungu dume mzuri mwenye pembe nane akivuka shamba yapata mita karibu 270 kutoka kwangu. Alikuwa akielekeea moja kwa moja kwenye mti wangu. Hakubadili mwelekeo wake, bali alivuka uwanja ule moja kwa moja na akaja chini ya mti wangu kisha akasimama pale kwa takriban sekunde 20. Baada ya hilo aligeuka na kurudi moja kwa moja katika uwanja ule akitumia njia ile ile aliyoitumia kufika kwangu. Kumbuka, Ohio iliruhusu uwindaji wa kulungu dume mmoja tu, na tayari nilikuwa nimechukua mwenye pembe nane, kwa hivyo ilinibidi kuketi tu na kutazama dume huyo na kutompiga risasi. Sasa nilichanganyikiwa kabisa. Hii ilikuwa mara ya kwanza kwangu kuwinda na kulungu kuja karibu nami ambaye hakuwa kulungu haswa ambaye nilikuwa nimetolea matoleo yangu. Jinsi dume huyo alivyotenda, kuja moja kwa moja kwenye shamba lile na kisha kusimama moja kwa moja chini ya mti wangu, kisha kurudi uwanjani akitumia njia ile ile aliyojuu nayo ilikuwa ajabu sana. Ilikuwa kana kwamba kulungu huyo alikuwa na kazi fulani. Nilisubiri asubuhi nzima, lakini dume yule hakurudi tena.

Usiku huo nikiwa ofisini kwangu nilisumbuliwa na haya yote. Jambo halikuwa sawa; dume mchanga alipaswa kutokea. Na ni kwa nini huyo mwenye pembe nane alitokea hivyo? Nikiwa nimekaa pale nilianza kusali rohoni nikimwomba Mungu anionyeshe kilichotokea. Nilisikia sauti Yake ikiniambia, “Tazama matoleo yako.” Nitazame matoleo yangu? Nilifahamu

nilichotoa. Benki yangu hutengeneza nakala za hundi zangu, hivyo nikatoa taarifa yangu na kuangalia hundi niliyokuwa nimeandika nilipotoa matoleo ya kulungu wangu. Nilifikiri kwamba nilikuwa nimetoa matoleo ya dume wawili, dume mmoja mwenye pembe nne au zaidi na dume mchanga mwenye pembe ndogo, ambaye anahesabiwa kama kulungu wa kike, kama nilivyosema awali. Lakini hundi yangu ilikuwa imeandikwa ifuatavyo, "dume wawili, wenyе pembe nne au zaidi, na dume mchanga mwenye pembe ndogo." Nilimaanisha kusema dume wawili, mmoja mwenye pembe nne au zaidi na mwingine mchanga mwenye pembe ndogo, lakini haikuwa hivyo. Niliandika, "dume wawili wenyе pembe nne au zaidi na dume mmoja mchanga mwenye pembe ndogo." Ni kulungu wangapi hao? Watatu, na wa pili alikuwa mwenye pembe nne au zaidi kama wa kwanza. Nilipoona hivyo niliketi hapо nikiwa nimeduwa. Yule dume mwenye pembe nane alikuwa ametumwa. Alipaswa kuwa pale kwa sababu ya sheria ya Ufalme. Niliruka juu na nikaanza kupiga kelele na kukimbia ndani ya nyumba. AJABU!!!!

Nilichoona kiliniogopesha pia. Ikiwa nilichoona kilikuwa jinsi Ufalme unavyofanya kazi kwa ukamilifu na umahususi, basi nilihitaji kuwa mwangalifu zaidi. Nilikuwa nimesababisha mambo bila kukusudia ambayo kwa kweli sikutaka yatokee, lakini yalitokea kwa sababu niliyaachilia kulingana na sheria ya kiroho. Sasa nilitambua kwamba watu wengi, nikiwemo pia, hupitia mambo ambayo hawakutaka kabisa kuona yakinukia, lakini wao wenyewe ndio waliyoyaanzisha. Kumbuka, kwa maneno Yake, Yesu aliukausha mtini na vile vile wakati mwingine kumwita Lazaro kutoka kaburini. Matukio yote mawili yalitumia sheria sawa kwa madhumuni tofauti. Wakati mwingine nilipoenda kuwinda, yule kulungu dume mchanga mwenye pembe ndogo alitokea kulingana na matoleo yangu.

Mfululizo huu wote wa matukio ulinishangaza na ulibadili sana mtazamo wangu kuhusu Ufalme. Sasa nilifahamu, bila kuchanganyikiwa kwamba Ufalme ulikuwa mahususi sana. Hata hivyo tunapaswa kushangazwa na hilo? Kila sheria ya kiasili duniani ni mahususi. Nafikiri sikujua kwamba sheria za kiroho hufanya kazi kama sheria za kiasili ambazo zililetwa na zile za kiroho. Nilipaswa kujua hilo lakini sikujua. Lakini sasa najua Ufalme ni mahususi, mahususi sana.

Sawa, uliuliza, kwa hivyo nitakupa hadithi nyingine moja ya uwindaji. (Napenda mafunzo haya niliyojifunza nilipokuwa nikiwinda, kwa hiyo tafadhalii nivumilie.) Nilipoona jinsi Ufalme ulivyo mahususi, niliamua kujaribu jambo kwa umahususi zaidi. Mwaka huo, niliamua kutoa matoleo ya kulungu dume mwenye pembe saba. Kwa kawaida, kulungu huwa na

idadi sawa ya pembe kila upande. Mwenye pembe nne ana pembe mbili kila upande; mwenye pembe nane ana nne kila upande, nk. Lakini mara nyingi, idadi ya pembe za dume zinaweza kukosa kuwa sawa na hivyo kuwa tofauti kila upande. Lakini, kama nilivyosema, kawaida, huwa wana idadi sawa kila upande.

Nilipokuwa nikijaribu jambo hili nilitaka kuachilia imani yangu kwa kitu mahususi wala sio cha kawaida. Tayari nilikuwa nimejifunza kwamba umahususi wako utaamua muda wako wa kusubiri jibu, na umaalum wa maelekezo yako kutoka kwa Roho Mtakatifu ili kulitimiza. Kwa hiyo siku ya kwanza ya msimu wa kuwinda na mshale na upinde, nilijua sikuhitaji kwenda kuwinda; nilifahamu kulungu hakuwepo. Kwa kweli, nilingoja Oktoba nzima, huku nikiwa na ufahamu moyoni mwangu, “La, bado kulungu wangu hajaja.” Lilikuwa jambo la kukatisha tamaa; rangi za majira ya vuli, misitu, nilitaka sana kwenda. Lakini bado nilisubiri.

Kisha ikatokea. Usiku mmoja nilipokuwa nimeketi sebuleni nikizungumza na wazazi wa mke wangu, waliokuja kututembelea kutoka Georgia, nilihisi ndani yangu. Asubuhi iliyofuata ndiyo siku niliyohitaji kwenda. Dume mwenye pembe saba angekuwepo! Niliwaambia wanafamilia wote kwamba keshoye ningepata dume wangu. Ukiwa umeketi karibu na kinamasi, panya wakubwa, na hata nguchiro huonekana wakizunguka ukingoni mwake. Kinamasi hicho kimezungukwa na nyasi, na ni mojawapo ya maeneo kulungu wanapenda kulala katika shamba langu. Nilipongoja mahali pangu pa kawaida, hakuna kilichotokea. Nilisubiri kwa dakika 45, kisha saa moja, na hakukuwa na chochote.

Nilisikia milango ya gari ikifunguliwa na kufungwa kutoka kwa shamba langu, na nikajua ni wazazi wa Drenda waliokuwa wakirudi Georgia. Nilikuwa nimeahidi kula kifungua kinywa nao kabla yao kuondoka, nami ndiye niliyekuwa mpishi. Mpango wangu wa awali ulikuwa ni kumuua kulungu wangu mapema kisha kurudi nyumbani kuandaa kifungua kinywa. Lakini kulungu dume hakuwa ametokea, kwa hivyo nilitoka mahali pangu na kuelekea nyumbani huku nikiwa na kusita kwingi. Nilifahamu kutokana na uzoefu wangu kwa shamba langu kwamba kulungu walikuja katika eneo la kinamasi baada ya asubuhi kufika, maana kama nilivytaja, lilikuwa eneo lao walilopenda kulala. Hata hivyo, nilijua dume angetokea dakika yoyote, lakini singeweza kuendelea kukaa hapo. Ilinibidi nirudi asubuhi nyingine.

Niliwasalimu watu wote pale nyumbani na kuanza kupika kifungua

kinywa. Mimi ndiye hupika kifungua kinywa nyumbani kwangu kila wakati na nimefanya hivyo kwa muda mrefu. Nina mapishi yangu maalum ya keki ndogo ya rojo ya unga ambayo inashangaza kabisa, ikiwa nasema hivyo mwényewe. Mayai, soseji na vipande-vipande vya jibini, lakini kitu kinachofanya kifungua kinywa changu kuwa kizuri sana ni sharubati halisi ya mwaramoni. Ohio ina sharubati nyingi ya mwaramoni, na watu wanaoishi karibu nami katika eneo langu hutengeneza na kuuza sharubati ya mwaramoni. Siruhusu sharubati yoyote bandia ndani ya nyumba yangu, napenda ile halisi tu. Kwa hiyo, nilikuwa ninapika kifungua kinywa, na dirisha la jikoni letu liko upande unaotazamana na msitu na kinamasi. Ghafla, niliona kulungu dume akituwa shamba akielekea kwenye kinamasi. Nikapiga kelele, “Dume wangu ndiye yule!” Nikaambia genge langu wachukue usukani katika upishi ili niende kumfuatilia!

Nilijua kutokana na kuwatazama kulungu wakivuka shamba hilo katika siku za nyuma haswa alikokuwa akielekea; na ili kufika huko, alihitaji kupita moja kwa moja chini ya mti wangu. Nilifikiria kwamba ikiwa ningeweza kuingia mahali pangu pa kusimama kutoka upande wa nyuma na labda nipande ule mti kabla ya huyo dume kufika hapo, huenda ningempiga risasi. Kutoka nyumbani na kupanda juu ya mti kabla ya dume kufika ingekuwa vigumu, kwa hivyo ilinilazimu kuondoka MARA MOJA! Nilikimbia nje ya mlango, huku nikinyanya upinde wangu wakati wa kutoka. Nilikimbia nikizunguka shamba, kisha kwa utulivu kadri ya uwezo wangu, nilipanda mti polepole. Kufikia hapo kila kitu kilikuwa sawa kabisa, sikuona dalili yoyote ya kulungu dume.

Nilipanda pale kwa mti na kuketi palepale wakati nilimwona kulungu dume akipita kwenye kinamasi akielekea moja kwa moja kwa upande nilikokuwa nimeketi. Dume hakuwa makini na chochote isipokuwa yule kulungu wa kike aliyekuwa akimfuata wala hakuniona au kulinusa. Kulungu wa kike alipita chini ya mti wangu na kuingia kwenye kinamasi, na dume huyo alikuwa akielekea kwenye njia ile ile. Singeomba kupata hali nyingine bora kuliko hiyo. Sasa dume akiwa na umbali wa mita karibu ishirini, nililenga kwa uangalifu upinde wangu na kuuachilia mshale. Niligundua mara tu mshale ulipofyatuka kwamba nilikuwa nimeurusha vibaya. Acha tukubaliane; nilikuwa karibu kuishiwa na pumzi kutokana na kukimbia nilipokuwa nikizunguka upande wa nyuma wa shamba na kinamasi ili kujaribu kufika hapo kabla ya dume.

Nilikatishwa tamaa kuona mshale ukipiga sehemu za chini sana, na kwamba nilikuwa nimekosa kupiga sehemu yoyote muhimu. Alipopigwa na

mshale, yule dume aliruka kwenye nyasi kubwa iliyokuwa kwa kinamasi na kutembea polepole wala sikumwona tena. Kile nilichoona katika uwindaji uliopita ni kwamba unapotumia upinde, wakati mwingine kulungu hawajui kilichotokea wakati wanapogongwa. Mara nyingi, wao huondoka tu, mradi hawajakuona au kukunusa. Pia nilijua kwamba kwa kawaida kulungu aliyejeruhiwa hulala chini kwa nyasi na hatembe i mbali sana. Kwa sababu kulungu huyu hakuwa ameniona, hivyo ndivyo alivyokuwa akifanya. Nilishuka kwa utulivu sana kutoka kwa mti na kuelekea upande wa nyumba kwa ile njia ndefu niliyoipita ili kufika huko bila kumshtua kulungu.

Nilipofika nyumbani kila mtu alianza kuniuliza ni nini kilichotokea na ikiwa nilimpata yule kulungu. Niliwaambia kilichotokea na kuwaambia wanangu waje kunisaidia kumfukuza yule dume kwenye nyasi, nikiwa na tumaini kwamba ningempiga risasi. Tulizunguka eneo hilo lenye nyasi nyingi na polepole tukapita humo. Ghafla, nikaona kwamba mmoja wa wanangu alikuwa amemshtua huyo dume, na alikuwa akikimbia haraka kwenye nyasi ndefu. Alikuwa karibu mita sitini mbele yangu, huku akivuka kutoka upande wangu wa kulia kwelekea upande wa kushoto.

Ghafla, dume alimuona mwanangu mwingine katika ukingo wa shamba. Alipogundua kwamba huyu si yule mtu aliymshua na kwamba hakujua ni njia ipi ya kukimbilia usalama, alisimama ili kutathmini haraka kile ambacho angefanya. Nilijua hiyo ndiyo iliyokuwa fursa yangu pekee ikiwa nilitaka kumchukua. Bado hakuwa ameniona. Sasa alisimama kwa umbali wa karibu mita sitini kutoka kwangu huku akimtazama mwanangu. Upinde una nguvu nyingi za kuua kulungu kwa umbali huo, lakini mshale unaweza kupita chini inchi au futi nyingi. Sikuwa nimewahi kutumia upinde wangu kwa ukaribu huo hapo awali, na huu haukuwa upinde mpya mwenye uzito wa kilo 90 ambaa unaweza kurusha mshale kwa zaidi ya futi 400 kwa sekunde. Usahihi wake ulikuwa kati ya mita 30 hadi 35 hivi.

Kwa kuwa kulungu alikuwa amesimama tuli, niliamua kufyatua mshale. Niliinua upinde, huku nikuelekeza juu ya kulungu bila kuwa makini sana, kisha nikauachilia mshale. Niliutazama ule mshale ukiruka kwenda kwa kulungu na, kwa mshangao, niliona mshale ukimpiga kulungu shingoni. Mshale uliokua umepita katikati ya shingo lake (samahani kwa kutoa maelezo yote), sasa ilitoboa pande zote mbili za shingo alipokuwa akijinyanyua. Sikuona alikokwenda alipoingia kwenye nyasi. Nilianza kutembea polepole kuelekea kwenye nyasi ambapo kulungu alikuwa ametoweka. Alikuwa hapo! Mshale ulikuwa umefanya kazi, na nilikuwa

nimempata kulungu wangu.

Mwanangu Tim alipojiunga nami, kile nilichojali kujua tu ni kuhusu idadi ya pembe wala sio kitu kingine chochote. Sikuwa nimepata fursa ya kuzihesabu, lakini tulipozihesabu zilikuwa saba. Tulipomchunguza dume huyo kwa ukaribu, tuliona kwamba alikuwa na pembe nane awali lakini moja ilikuwa imevunjika, na hivyo kumfanya awe na saba. Tim na mimi tulisimama pale tukiwa tumestaajabu na kumsifu Bwana. Ufalme ni wa ajabu kabisa! Tulipokuwa tumesimama hapo mimi na Tim tulitambua pia, “Ni nani angewahi kutuamini? Je, kuna yejote anayejua kwamba Ufalme hufanya kazi kwa njia hii?”

Nafikiri unaelewa. Ufalme wa Mungu hutumia sheria hususa ambazo zimewekwa na zinaweza kutegemewa kufanya kazi kwa njia ile ile kila wakati. Ilisisimua sana hapo mwanzoni nilipogundua kwamba sheria hizi zinafaa kwa kitu chochote, hata fedha. Labda ningefanyika mwanasayansi wa mambo ya kiroho, anayefahamu jinsi Ufalme unavyofanya kazi kwa kujifunza sheria hizi. Mungu angenisaidia.



SURYA 2

# UKUNGU WA RANGI YA SAMAWATI

Mimi na Drenda tulipoanza kuona Ufalme ukitenda kazi maishani mwetu, tulitoka kwa madeni kabisa, na tulitaka kumwambia kila mtu tuliyeutana naye yale tuliyojifunza. Tulikuwa tukimwambia mtu yejote ambaye angetusikiliza tulipokuwa tukianzisha kanisa letu huku nikiendelea na biashara zangu. Lakini nilihisi rohoni mwangu kulikuwa na kitu cha ziada; wala sikujua ni nini, lakini nilijua kwamba kuna mengi zaidi ambayo Mungu alikuwa akiniongoza nifanye ili nishiriki Ufalme pamoja na watu.

Mwaka wote wa 2005 nilikuwa na msukumo katika roho yangu wa kuwa na kile ambacho ningekiita kongamano la mapinduzi ya kifedha, mfululizo wa mikutano mitano ambapo nilihisi ningekuwa na wakati wa kuweka wazi baadhi ya kanuni za kifedha za Ufalme ambazo zilikuwa zimebadilisha maisha yangu. Nililelewa katika kanisa la Methodisti, ambapo wakati mwingine tulikuwa na mikutano ya uamsho ya wiki nzima. Huo ndio mfano nilioona rohoni mwangu, vikao vitano ambapo ningekuwa na muda wa kuwafunza watu dhana na kanuni ambazo Mungu alikuwa amenifundisha katika ulimwengu wa kifedha. Hadi wakati huo, sikuwa nimewahi kuandika kanuni hizi pamoja katika utaratibu wowote. Lakini rohoni mwangu niliendelea kujiona nikifundisha katika mkutano wa vikao vitano kuhusu masuala ya fedha.

Nilipokuwa nikisali kuhusu jambo hilo nilikutana na Larry, rafiki yangu ambaye sikuwa nimemwona kwa muda mrefu. Aliniambia kuhusu kongamano alilokuwa akiongoza kule Albania, na akanialika niwe mmoja

wa wanenaji. Larry alikuwa amefanya kazi ya umishenari huko Albania kwa karibu miaka 12 na alikuwa na matokeo makubwa katika nchi hiyo. Wazo la kusafiri umbali huo lilikuwa geni kidogo kwangu. Sikuwa nimesafiri sana wala kufika Albania, na sikuwa na uhakika kama nilifahamu Albania ilikuwa wapi. Larry alinitia moyo, akaniambia alikuwa akifanya mkutano wa nchi nzima ambao ungekuwa na wachungaji wengi wa taifa hilo, na alifikiri ufahamu wangu kuhusu suala la fedha katika Ufalme ungewasaidia watu. Larry alisema ningekuwa na vikao viwili au vitatu kwenye mkutano ili kushiriki. Ingawa havikuwa vikao vitano, bado nilikuwa na hamu ya kufundisha juu ya mada hiyo kwa vikao kadhaa alivyonipa. Kwa hivyo nilikubali mwaliko wake.

Niliposhuka kutoka kwa ndege huko Albania, Larry alinisalimu huku akiniambia maneno ya kushangaza. "Gary," akasema, "mmoja wa wanenaji wangu alighairi dakika ya mwisho, kwa hivyo utafanya vikao vitano." Moyo wangu uliruka. Ndilo hili! Nilijua kwamba huu ulikuwa mpango wa Mungu na sasa ningeona jinsi yale niliyoyaona rohoni mwangu yangefanyika. Nilikuwa na maandishi yangu lakini sikuwa nimeyapangilia ili kutosha vikao vitano. Kwa hiyo kila siku nilifundisha, kisha ningerudi na kuomba katika roho, na kuandika maandishi yangu ya kipindi kijacho. Kila kikao kilijawa na upako wa ajabu sana.

Kabla sijaenda mbali zaidi, ninahitaji kukuambia kwamba nilipoenda Albania ilikuwa nchi maskini sana. Wastani wa mshahara ulikuwa dola 500 kwa mwezi, na hongo ilikuwa kawaida kwa watu. Nilipokuwa nikitafakari jinsi nitakavyowafundisha watu katika masuala ya fedha, sikuwa na uhakika jinsi wangelivyoyapokea. Nilifahamu Neno lilitenda kazi kwa mtu yejote, lakini hii ilikuwa hali mpya kwangu. Nilipofundisha somo la kwanza, nilihisi watu walikuwa wameweka vizuizi lakini kufikia kipindi cha pili, niliweza kuhisi njaa ya kiroho ya watu ikivuta mafundisho, na niliweza kuona imani ikiongezeka katika nyuso zao waliposikia habari njema ya Ufalme. Kila siku nilipokuwa nikifundisha watu walipata furaha na furaha zaidi, na niliona kwamba walisisimka kuhusu Ufalme.

Jioni kabla ya kikao cha mwisho nilichopaswa kufundisha, Bwana alinena nami nipokee sadaka kwa ajili ya makanisa ya mtaa. Sikuwa na hakika na hili kwa sababu, kwanza kabisa, halikuwa kongamano langu; na pili, sikuwa na uhakika jinsi watu wangelivyoitikia. Mimi na Larry tulilazimika kulipia wachungaji wenyeji gharama nyingi za usafiri na hoteli ili kuwaleta kwenye mkutano. Nilizungumza na Larry kuhusu jambo hilo, naye akakubali nipokee matoleo.

Kwa hiyo wakati wa kikao cha mwisho nilipokea matoleo ya kongamano, na upako ulikuwa mwingi sana nilikuwa na shida kusimama. Kila mtu alikuwa akicheza na kupiga kelele huku akileta sadaka yake mbele. Mashemasi walikuwa wakilia na kushindwa kusimama huku wakiwa wameshikilia vikapu vya kupokea matoleo. Kamwe sikuwa nimeona kitu kama hicho hapo awali, hasa wakati wa kutoa matoleo. Sasa nilipokuwa nikitazama watu wakicheza na kupiga kelele za furaha huku wakitoa, niliguswa sana na upako na pia imani ya kweli ya wale waliokuwa wakitoa matoleo hayo ya thamani.

Baada ya ibada, ni wazi Larry aliguswa moyo na kile alichokiona. Pia alishangazwa na mifuko miwili ya sadaka tuliyokuwa tukirudi nayo nyumbani kwake kutoka kwa ibada ya jioni. Larry aliniambia kwamba kwa kawaida mfuko mmoja tu wa matoleo ungejaa kwa kiasi baada ya mkutano ambapo alikuwa amepokea matoleo. Tulitembea haraka kwa barabara ilijoja watu huku tukificha mifuko ya matoleo tulipokuwa tukielekea kwa chumba cha Larry.

Tulipofika kwa chumba cha Larry, tuliketi sebuleni mwake na kufungua mifuko ya matoleo ili kuhesabu matoleo. Larry alipokuwa akimwaga juu ya meza yale matoleo yaliyokuwa kwenye mifuko, kuna jambo lililotokea ambalo hadi leo ni gumu kulieleza. Ghafla, ukungu mwepesi wa rangi ya samawati ulijaa chumbani na uwepo wa Mungu ukatushinda nguvu. Tuliketi chini ya upako huo uliojaa mahali pale. Haukuwa kama upako niliowahi kuhisi nilipokuwa nikihubiri au kuombea watu, bali upako huu ulikuwa na uwepo fulani. Ulikuwa mtakatifu na ulinifanya nijisikie kama nilikuwa katika uwepo wa Mungu, Mwenyewe. Tukiwa tumeketi pale, upako ulizidi kuongezeka ndani ya chumba kile. Tulichoweza kufanya ni kuketi na kulia tu. Kisha nikaona pete ya harusi ya mtu, katikati ya rundo la fedha ambalo sasa lilikuwa juu ya meza ndogo. Nilishangaa kwamba mtu pale ambaye hakuwa na pesa alitoa kitu pekee kilichokuwa cha thamani kwake. Bwana alinena nami papo hapo akasema:

*“Ninawaita kwa mataifa ili kuwafundisha kanuni hizi nilizowafundisha kuhusu Ufalme na fedha. Pete hii iliwekwa katika sadaka jioni ya leo kwa imani kubwa. Lakini nataka uichukue na kuiweka kama ukumbusho. Pia fahamu kwamba kama vile pete ya arusi inavyohusu agano, unatangaza agano Langu la riziki kwa watu Wang’u. Na fahamu kwamba popote nitakapokutuma, nitatoa pesa za kulipia gharama ya matumizi.”*

Nilikaa katika chumba cha Larry usiku huo na sikuweza kulala usiku kucha, maana upako ulidumu hapo. Vile vile katika safari yangu yote ya kurudi nyumbani na ndege ambayo ilipaa juu ya Bahari ya Atlantiki sikuweza kulala. Kile nilichoweza kufanya ni kutazama nje ya dirisha na kulia kwa muda wote wa masaa 8 wa usafari wa ndege. Sikuweza kulala kwa masaa 46 baada ya Bwana kunena nami usiku ule. Kwa miezi kadhaa baada ya usiku ule, kila nilipotafakari tukio lile, nilihisi uwepo uleule na kuanza kulia.

Sikumwambia Larry kile Bwana alikuwa ameniambia kuhusu ile pete. Matoleo yalikuwa ya makanisa ya Albania, na nilijua pia kwamba pete hiyo ingeweza kuuzwa ili kupata pesa za ziada—lakinilifahamu kile ambacho Bwana aliniambia kuihusu. Kwa hiyo nilifurahi sana wakati Larry alinipigia simu akasema kwamba Bwana alimwambia anipe ile pete. Niliiandalia mahali pazuri, na sasa iko ofisini kwangu. Tangu wakati huo kuna nyakati nyingi ambapo nimeitazama ile pete na ikabidi nikumbuke maneno ya Bwana kwangu usiku ule, wakati ninapokabiliwa na kile kinachoonekana kama changamoto kubwa ya kifedha. Bila shaka, Mungu alikuwa mwaminifu kunipa kila kitu nilichohitaji ili kutekeleza mwelekeo Wake kwangu usiku ule. Usiku ule huko Albania ulibadili maisha yangu, lakini kulikuwa na mengi zaidi ambayo Mungu alitaka kunionyesha katika siku za usoni.

Nilipofika nyumbani kutoka Albania, nilitamani sana kupeleka ujumbe huu wa Ufalme kila mahali. Nilikuwa na shauku kubwa sana ya kueneza habari hii, na nilikuwa na hamu ya kufundisha tena vikao vile vitano na kuona kama jambo lile lile lingetokea. Sikungoja kwa muda mrefu. Nilialikwa na mchungaji kule Utah kufundisha vikao hivyo hivyo vitano. Alikuwa amesikia kutoka kwa Larry kwamba mafundisho yalikuwa ya ajabu na alitaka niende huko pia. Alikuwa mchungaji wa kanisa dogo la Kihindi ambalo lilikuwa maskini sana. Walihitaji msaada wa kifedha, na ikiwa yale ambayo Larry alimwambia yalikuwa ya kweli, alihisi kwamba ningeweza kuwasaidia.

Kwa hiyo nilisafiri kwa ndege na kufanya mikutano Jumapili asubuhi na jioni hadi Jumatano jioni. Kulikuwa na vikao vitano kwa jumla kama huko Albania, na nilikuwa na mwitikio uleule. Watu walipiga kelele na kucheza usiku wa mwisho wa kongamano hilo, chini ya upako mkuu sana, walipokuwa wakitoa sadaka zao. Sikuona ukungu wa rangi ya samawati wakati huu, lakini nilihisi upako mkuu katika vikao vyote vitano. Baada ya kikao cha mwisho, nilishtuka kama vile Larry alivyoshtuka huko Albania,

kwa sababu ya ukubwa wa matoleo ambayo waume 17 na wake wao pekee walikuwa wametoa. Nilifungia matoleo kwenye begi la sadaka na kuipeleka ofisini kwangu ili iweze kushughulikiwa siku iliyofuata.

Baadaye asubuhi keshoye, nilipigwa simu kutoka ofisini kwangu. Katibu wangu alikuwa kwa simu, na niliweza kutambua kwamba kulikuwa na jambo lililokuwa limetokea. Sauti yake ilikuwa ikitetemeka, na ilionekana kana kwamba alikuwa akilia. Maneno yake ya kwanza yalikuwa, “Mchungaji, kuna kitu kuhusu hizo pesa ulizorudi nazo.” “Unamaanisha nini Tracy?” Nikauliza. Kisha akaniambia kwamba alikuwa amefungua begi la matoleo ili kuyahesabu na kuyaweka kwenye benki, lakini dakika ile alipofanya hivyo, upako ulimjia sana ofisini, na ukamwangusha chini. Katibu wangu mwingine aliposikia vurugu hiyo, alikuja pembeni naye pia akaanza kutetemeka chini ya upako. Tracy aliuliza, “Ni kitu gani kilichofanyikia fedha hizi huko Utah?” Nami nikamjibu kwamba sikuju.

## **LAKINI YESU HAKULIPIA HAKI YETU YA KWENDA MBINGUNI TU, BALI PIA ALIFANYA IWEZEKANE KUISHI KAMA WANA AU BINTI ZA MUNGU NA KUFURAHIA MANUFAA ZA UFALME WA MUNGU HAPA DUNIANI.**

Baada ya majuma machache, nilikuwa nikifundisha kanuni hizo hizo katika kanisa dogo kusini mwa Ohio. Katika kanisa hili, tulikuwa tumewatumia vipindi vinne vyta kwanza kwa DVD, na walikuwa wamevitazama kwa majuma manne. Kisha nikasafiri huko Jumapili jioni ili kumaliza kikao cha mwisho. Upako ulikuwa karibu kutuangusha tena. Nilipopokea sadaka jioni hiyo, nilikuwa na mwitikio uleule niliokuwa nao katika mikutano mingine.

Watu walifurahi sana kutoa. Wakati wa sadaka, kanisa liliweka kikapu kimoja mbele ili watu waweze kuweka matoleo yao. Mara hii, ukungu ule wa rangi ya samawati ulikuwepo tena. Kulikuwa na mviringo mwenye upana wa futi tano uliozunguka kikapu cha sadaka watu walipokuwa wakitoa. Upako ulikuwa mwingi sana kiasi kwamba nililazimika kusaidiwa kwenda kwa gari baada ya mkutano kwa sababu sikuweza kutembea mwenyewe.

Mambo haya yalipokuwa yikitokea, sikuju ni nini kilichokwu kikiendelea, na sijasikia kikitokea mahali pengine popote. Niliendelea kufanya makongamano, na upako uliendelea kuwa na nguvu sana. Na ndio, ukungu ule ulionekana tena katika kongamano kadhaa. Lakini jambo lililonishangaza zaidi ni kwamba upako ulikuwa juu ya pesa yenye. Baada

ya kongamano, wafanyakazi wangu walikuwa na wakati mgumu kuhesabu matoleo. Je! unakumbuka kwamba upako ulikuja katika nyumba ya Larry huko Albania alipomwaga matoleo juu ya meza? Mtu yejote aliposhika mkononi pesa yoyote iliyotolewa katika matoleo haya, mara moja alihisi upako na kuanza kutetemeka. Najua inasikika kana kwamba ninafanya mzaha, lakini haya ndiyo niliyoyaona.

Kama mwanasayansi wa kiroho, nilistaajabishwa na haya yote na nikamuuliza Bwana kuyahusu. Alinena nami na kuniambia kwa nini upako huu wenyewe nguvu ulionekana kwenye sadaka. Aliniambia kwamba watu wengi hutoa kwa sababu ya wajibu au kufuata sheria. Wengine hutoa kwa sababu ya fomyula fulani, lakini hawana imani ya kweli wanapotoa. Wengi hutoa kwa sababu wanafikiri Mungu atawakasirikia wasipofanya hivyo. Wengine hutoa kana kwamba ni bili wanadaiwa. Aliniambia kwamba ninapofundisha Ufalme Wake na kufunua kanuni za kifedha za Ufalme zilizofichwa, imani huinuka katika mioyo ya watu. Kisha wanapotoa wanakuwa kweli katika imani, na uhusiano wa Ufalme unaimarishwa, na utiririko wa upako kuachiliwa.

Tangu safari hiyo ya kwenda Albania mwaka wa 2005, maisha yangu yamebadilika sana. Shauku yangu ya kuwahubiria watu habari njema ya Ufalme imetufanya mimi na Drenda kutumia runinga ili kufikia mataifa na habari hii njema. Sasa tunatumia mamilioni ya dola kila mwaka kuwaambia watu kuhusu Ufalme huu tuliovumbua miaka mingi iliyopita. Lakini labda bado hujasikia habari njema ya Ufalme. Tulikuwa hivyo—waumini walio katika safari ya kwenda mbinguni wasiofahamu jinsi ya kuleta yaliyo mbinguni hapa duniani. Lakini Yesu hakulipia haki yetu ya kwenda mbinguni tu, bali pia alifanya iwezekane kuishi kama wana au binti za Mungu na kufurahia manufaa za Ufalme wa Mungu hapa duniani. Lakini muhimu zaidi, kuna mamilioni ya watu tunaopaswa kufikia na habari njema za Injili, na inagharimu fedha kufanya hivyo. Watu wanatazama. Maisha yetu yanapaswa kuwa na mwonekano tofauti!

Ni kitu gani nilichofundisha huko Albania kilichoachilia upako ule? Mungu aliniambia nihubiri nini kwa mataifa? Naam, hilo ndilo kusudi la kitabu hiki, na ninaamini kitabadilisha maisha yako jinsi kilivyobadili yangu.

## SURA YA 3

# TAFADHALI MUNGU, UTUREHEMU!

Jerry alinipigia simu ofisini kwangu na kuniuliza ikiwa angeweza kunitembelea na kula chakula cha mchana nami nilipokuwa katika eneo lake. Nilikuwa nikifanya mahojiano katika kituo cha televisheni katika mji uliokuwa karibu naye, na alitaka kuniambia jinsi maisha yake yalivyokuwa yamebadilika kutokana na mafundisho yangu na vipindi vyangu vya runinga. Sikuwa nimewahi kukutana na Jerry awali lakini nilikuwa nimezungumza naye kwenye simu mara moja au mbili. Nikasema, “Bila shaka.” Hata hivyo tungekula chakula cha mchana, na niliwaza kwamba nikiwa huko, ingekuwa vyema kukutana naye ili kusikia hadithi yake.

Wakati wa chakula cha mchana nilikutana na Jerry na mwanawe, kisha akaanza kunisimulia hadithi yake. Jerry alikuwa mchungaji kwa miaka 30, lakini ilimbidi aache huduma kwa sababu ya kiharusi ambacho kilikuwa kimemlemaza. Baada ya kiharusi, maisha yake yalidhoofika sana. Kwa sababu hakuweza kufanya kazi, alichelewa kufanya malipo ya nyumba yake na hilo lilifanya wakopeshaji wake waamue kuiuza. Kulipa bili na kununua chakula vikawa changamoto pia. Jerry alisema mambo kweli yalikuwa mabaya sana kiasi kwamba aliketi siku moja akiwa na bunduki katika mkono mmoja na Biblia katika mkono mwininge, akifikiria kujiua.

Ilikuwa katikati ya hali hii ya kukata tamaa ambapo Jerry aliona kipindi chetu cha televisheni na kuagiza baadhi ya rasilimali za mafundisho yangu. Aliendelea kueleza kwamba alipopokea mafundisho hayo mara ya

kwanza, alikuwa na hitaji kubwa la takriban dola 2,000 ili kulipia mahitaji ya kimsingi na chakula. Alisikiliza mafundisho tena na tena hadi imani ilipoanza kuongezeka moyoni mwake. Aliamua kumwamini Mungu ampe dola hizo 2,000 alizohitaji. Kwa hiyo akafanya vile mimi na Drenda tulivyofanya wakati wa yule kulungu wa kwanza niliyempokea. Alitoa matoleo kama mbegu kwa ajili ya ombi lake hilo. Aliandika kwenye karatasi tarehe na wakati alipoamini kwamba alipokea pesa hizo, kulingana na Marko 11:24, kisha akatuma hundi hiyo kwa huduma yetu.

Sikujua hili lilikuwa limetokea kwa sababu sikuwa nimezungumza na Jerry. Alisema kwamba katika muda wa juma moja na nusu hivi mwanamume mmoja alikuja kwa mlango wake na kuomba kuzungumza naye. Jerry alimjua mtu huyo tangu zamani, lakini akasema walikuwa hawajazungumza kwa muda mrefu. Waliendelea na mazungumzo kidogo, kisha mtu huyo akasema kwamba alikuwa amepitia kumpa Jerry hundi ya \$2,000. Aliendelea kueleza kwamba wiki moja na nusu awali, alihisi msukumo wa Roho Mtakatifu kumletea Jerry pesa hizo.

Jerry alisimama pale akiwa ameduwaa. Haraka alichukua mkwiji wake ambapo alikuwa ameweke kikaratasi kilichoeleza siku na saa ambayo aliamini kwamba alipokea dola 2,000 alizohitaji. Tarehe na saa ilioandikwa kwenye karatasi ya Jerry iliambatana na wakati uleule amba mtu huyo alihisi msukumo wa kumpa Jerry \$2,000. Jerry alijua hii haikuwa bahati nzuri tu; alijua kwamba lilikuwa jibu la moja kwa moja kutoka kwa Ufalme wa Mungu, hasa sheria za Ufalme.

Aliendelea na hadithi yake na kuniambia kwamba alikuwa na watoto saba, wote walikuwa wameolewa isipokuwa mtoto wa kiume wa miaka 16 (yule aliyeju naye kwa chakula cha mchana), ambaye alikuwa amemwacha Mungu alipoona mapitio yote ya babake. Mwana huyo alimkasirikia Mungu kwa sababu babake alikuwa mwaminifu kwa miaka 30, na alihisi kwamba Mungu alikuwa amemwacha.

Jerry alitaka kutafuta njia ya kumfikia mwanae, na akapata wazo. Huwa ninahubiri sana kuhusu uwindaji wa kulungu na kueleza jinsi Mungu alivyonifundisha kuwinda kwa imani katika mafundisho yangu. Mwanae alipenda sana kuwinda kulungu, kwa hivyo Jerry akamweleza jinsi ya kupata dume wake katika msimu wa vuli, akitumia mfumo wa Ufalme wa Mungu. Mwanae alitafakari jambo hilo na hatimaye akakubali, kisha ye ye na Jerry wakatumia imani yao, kama vile Jerry alivyo fanya kwa zile \$2,000 zake. Kijana huyo alipata dume wake katika dakika nane. Jerry na mwanawe walipokuwa wakimpeleka kulungu kwenye duka la nyama,

alikuwa anasikiliza CD yangu kwa gari. Alipotoka kwa gari ili kumbeba kulungu kwenda dukani, kijana huyo alisema alitaka kubaki ndani ya gari ili aweze kusikiliza zaidi. Jerry aliporudi, mtoto wake alisema, "Baba, nafikiri tumekuwa tukikosa kitu miaka hii yote. Najua kwamba kulungu huyu ni matokeo ya Ufalme wa Mungu."

Mwanawe basi aliyatoa tena maisha yake kwa Bwana na akamwambia babake kwamba ikiwa Mungu angeweza kuleta dola 2,000 na kulungu basi angeweza kuleta \$17,000 walizohitaji ili kuzuia kuuzwa kwa nyumba yao. Huu ndio wakati nilikuwa nikikutana na Jerry mara ya kwanza. Nakumbuka Jerry alinitumia barua pamoja na matoleo ya mwanawe ya kuzuia nyumba yao kuuzwa. Barua ilikuwa fupi lakini iliweka wazi kile walichohitaji. Hawakutaja kitu kingine chochote. Pia nakumbuka iliweka mkono wangu juu ya barua hiyo na kukubaliana nao. Naweza kukumbuka muda na wakati haswa nilipofanya hivyo.

Kufikia hapo, Jerry aliniambia kwamba katika muda wa wiki mbili hivi mwanamume mwingine alikuja kwa mlango wake nyumbani. Tena, huyu alikuwa mtu ambaye Jerry alimjua hapo zamani. Mtu huyo alimwambia aliona kwamba nyumba yake ilikuwa imewekwa katika orodha ya kuuzwa na akamuuliza Jerry ni kiasi gani cha fedha zilizohitajika ili kuiondoa kwenye orodha hiyo. Jerry alimwambia kiasi kilichohitajika, zaidi ya \$17,000. Mtu huyo alimwandikia hundi ya kiasi chote na kuondoka. Jerry alitazama hundi kwa mshangao. Akiwa ameketi kando yangu mezani kwa mkahawa ule, alianza kulia huku akinishukuru kwa kuwafundisha watu kuhusu

Ufalme wa Mungu. Jerry alisema alifurahi sana kwamba watoto wake wote waliona mkono wa Mungu, na hilo lilimpa nafasi ya kushiriki Ufalme wa Mungu pamoja nao. Napenda hilo! Huu ndio uhalisi wa Ufalme wa Mungu, na nimebarikiwa sana kuweza kushiriki na watu na kisha kusikia hadithi zao. Wajua, Jerry hakuhitaji huruma. Alihitaji majibu, na aliyapata katika Ufalme.

Sasa, ninahisi kwamba ninahitaji kuongeza kitu hapa kuhusu hadithi ya Jerry. Hata ingawa inaonekana kwamba watu walikuja kwa mlango

**"KWA MAANA, AMIN,  
NAWAAMBIA, MKIWA NA  
IMANI KIASI CHA PUNJE  
YA HARADALI MTAUAMBIA  
MLIMA HUU, 'ONDOKA  
HAPA UENDE KULE,'  
NAO UTAONDOKA; WALA  
HALITAKUWAKO NENO  
LISILOWEZEKANA KWENU."**

**— MATHAYO 17:20B**

wake na kumpa pesa, sitaki upate wazo lisilofaa kwamba jibu lako la kifedha litakuja ukiwa umeketi na kunywa soda. La, utakuwa na sehemu yako ya kutimiza katika uvunaji wa kile unachohitaji. Katika kisa cha Jerry, alikuwa mchungaji kwa miaka 30. Alikuwa amehudumia watu kwa muda mrefu sana. Na pili, Jerry hakuwa na uwezo wa kuondoka nyumbani kwake kwa sababu ya kiharusi. Jerry alivuna kutoka pale alipokuwa amepanda, kupertia kwa watu wa kanisa lake ambapo alikuwa amehudumu kwa miaka hiyo yote.

Pia nataka kukuambia kwamba Jerry alikuwa mzima kabisa kutokana na kiharusi, na alikuwa amepunguza uzani zaidi ya pauni 70 nilipokutana naye siku ile katika chakula cha mchana. Mungu asifiwe, aliupata Ufalme. Labda unaweza kusema, “Vema, Jerry alikuwa mchungaji; bila shaka, alijua yote kuhusu Ufalme.” Sidhani ni hivyo, na nina hakika hayuko peke yake kwa sababu ya yale ambayo nimeona. Inasikitisha kwamba, watu wengi kanisani hawajui jinsi ya kuingia katika Ufalme wa Mungu na kupokea majibu yao pia. Hadithi katika Mathayo inaonyesha jinsi wengi wanavyofikiri.

*Nao walipoufika mkutano, mtu mmoja akamjia akampigia magoti akisema, “Bwana, umrehemu mwanangu, kwa kuwa ana kifafa, na kuteswa vibaya; maana mara nydingi huanguka motoni, na mara nydingi majini. Nikamleta kwa wanafunzi Wako, wasiweze kumponya.”*

*Yesu akajibu, akasema, “Enyi kizazi kisichoamini, kilichopotoka, nitakaa pamoja nanyi hata lini? Nitachukuliana nanyi hata lini? Mleteni huku Kwangu.” Yesu akamkemea pepo, naye akamtoka; yule kijana akapona tangu saa ile.*

*Kisha wale wanafunzi wakamwendea Yesu kwa faragha wakasema, “Mbona sisi hatukuweza kumtoa?” Yesu akawaambia, “Kwa sababu ya upungufu wa imani yenu. Kwa maana, amin, nawamibia, mkiwa na imani kiasi cha punje ya haradali, mtauamibia mlima huu, ‘Ondoka hapa uende kule,’ nao utaondoka; wala halitakuwako neno lisilowezekana kwenu.”*

– Mathayo 17:14-20

Katika hadithi hii, tunaona mtu aliykata tamaa pamoja na mwanawewe aliyesewa na pepo wachafu, karibu hata kufa. Aliposikia kuhusu huduma ya Yesu na kwamba Yesu alikuwa na uwezo wa kutoa pepo, alifanya mipango ya

kumpeleka mwanawe kwa Yesu ili aweze kumponya. Hata hivyo, alipofika huko, aligundua kwamba Yesu hakuwepo bali alikuwa amewachukua wanafunzi Wake watatu juu ya mlima ili kusali. Wanafunzi waliokuwa wamebaki pale walisema hilo halikuwa tatizo kwao; kwamba walikuwa wametoa pepo tangu Yesu alipowapa mamlaka ya kufanya hivyo, katika jina Lake, na wangeweza kumshughulikia kijana huyo. Lakini walipokuwa wakimwombea, yule pepo hakuondoka. Kwa vyovyote walivyajaribu, pepo huyo hakuondoka. Babake kijana alikasirika na umati uliomfuata Yesu ukachanganyikiwa.

Lakini papo hapo, Yesu na wale wanafunzi watatu walirudi kutoka mlimani. Yesu alipoona vurugu hiyo, aliuliza ni nini kilichokuwa kinaendelea. Baba wa kijana alieleza jinsi alivyomleta yule kijana kwa wanafunzi, lakini hawakuweza kumtoa pepo. Baba basi akafanya kile kinachowafaa wengi wanapokabiliwa na shida wakati hawaoni majibu yao. Alimlilia Yesu amrehemu. Ingawa kuomba rehema kunasikika kama jambo zuri kufanya unapokata tamaa, hilo halikuwa jibu la mtu huyu, wala sio lako pia. Baba huyo, katika kutaka kuchochea huruma ya Yesu, aliendelea kumweleza Yesu jinsi pepo huyo alivyokuwa akimtesa mwana wake, huku akimtupa motoni, na kujaribu kumwua. Yesu alimnyamazisha baba yule. Hakuhitaji kusikia zaidi kuhusu mateso ambayo mwana wake alikuwa akiyastahimili. Yesu alikerwa na kupaza sauti, *"Enyi kizazi kisichoamini, kilichopotoka, nitakaa pamoa nanyi hata lini?"* Mleteni huku Kwangu." Yesu alieleza wazi katika sentensi Yake moja kwa nini pepo hakutoka.

Lakini kabla hatujachunguza kwa undani maana ya yale Yesu aliyoyasema, tunahitaji kuthibitisha tena msingi tunaoegemea, ambao ni kwamba Mungu hasemi na hawezi kusema uwongo. Kile asemacho ni kweli. Tukiwa tumeshughulikia hilo, tunaweza kutathmini hali hii tukitumia kauli hii, "Pepo WANAPASWA kutoka! Wasipofanya hivyo, basi kuna kitu ambacho si sawa, na sio upande wa Mungu bali ni wetu. Kumbuka hili, tatizo la kupokea kutoka kwa Mungu daima liko upande wetu. Yesu anatuambia waziwazi sababu pepo hakutoka—mawazo potovu na kutoamini. Tutashughulikia sababu hizi mbili baada ya muda mfupi. Lakini sasa katika mjadala wetu, nataka tuzingatie baba na mwana katika hadithi hii.

Ni wazi baba alikuwa na shauku kuu kuhusu uponyaji wa mwanawe. Wakati hakuna kitu kilichotokea wanafunzi walipomwombea, hakukuwa na kitu kilichosalia. Hakukuwa na jibu la hakika. Jibu pekee alilofikiri lingesaidia halikufua dafu. Kulikuwa na jambo moja tu lililosalia, nalo

lilikuwa ni kuomba rehema. Maneno “kuomba rehema” yanadokeza kwamba mtu fulani ana uwezo au mamlaka ya kuwa msaada lakini ameamua kutofanya hivyo. Hivyo, jambo pekee lililobakia kufanya ni kutoa maelezo marefu juu ya mateso ya kutisha ambayo kijana huyo alikuwa akistahimili, akijaribu kumtia Yesu huruma kuhusu hali yake.

Kwa kweli kabisa, hivi ndivyo watu wengi huomba, wakijua kwamba Mungu ana uwezo wa kuwasaidia lakini kwa kutokuwa na uhakika kuhusu jibu Lake, wanaomba rehema. Kwa maombi marefu na maneno mengi, wao hueleza kwa undani maumivu na hali yao. “Baba, unajua nahitaji hiyo pesa ifikapo Ijumaa; tafadhali, Mungu nisaidie.” Au “Mungu, tafadhali, ukimponya mtoto wangu, nitakutumikia siku zote za maisha yangu. Tafadhali, Mungu.” Sipuuzi hali zinazowakabili watu, lakini tafadhali kumbuka jinsi Yesu alivyoachilia nguvu za Mungu katika hali hiyo haraka na kumweka huru kijana huyo. Huu ndio moyo wa Mungu, na nia Yake. Hana uhaba wa huruma, nguvu, au mamlaka. Hilo halikuwa tatizo katika hadithi. Yesu aliweka wazi tatizo kama fikra potofu na kutoamini. Kwa maneno mengine, fikra zisizo sahihi na ukosefu wa imani vilizuia mamlaka ya Ufalme katika tukio hili.

Basi kuna mengi ya kuzungumza hapa, mambo mengi muhimu kuhusu Ufalme na jinsi unavyofanya kazi. Sitaki kuzungumzia kwa kina baadhi ya mambo unayopaswa kujua hapa, bali sasa nitayataja tu, halafu baadaye tutajifunza sheria tunazoziona zikifanya kazi hapa.

Ili kuelewa msingi wa sheria ya Ufalme, ni lazima tuelewe jambo hili muhimu na la kimsingi: Mungu alimpa Adamu mamlaka kamili juu ya ulimwengu. Alipaswa kuutawala.

*Mungu akasema, na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu;  
wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na  
nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi.*

– Mwanzo 1:26

Nafikiri Waebirania 2:7-8 inaweka wazi sana:

*Umemfanya mdogo punde kuliko malaika, Umemvika taji ya  
utukufu na heshima, umeweka vitu vyote chini ya nyayo Zake. Kwa  
maana katika kuweka vitu vyote chini Yake hakusaza kitu kisichowekwa  
chini Yake.*

Kwa sasa, elewa kwamba Mungu hawezi kutumia mamlaka Yake katika

ulimwengu (katika Ufalme wa wanadamu) isipokuwa mwanamume au mwanamke aliye na mamlaka ya kisheria aachilie mamlaka ya mbinguni hapa.

Ndiyo maana Yesu aliwaambia wanafunzi Wake katika Mathayo 18:18:

*“Amin, nawaambieni, yoyote mtakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yoyote mtakayoyafungua duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni.”*

Kwa mara nyingine tena, mbingu haina mamlaka ulimwenguni isipokuwa ni kupitia kwa mwanamume au mwanamke ambaye anayaachilia hapa. Ndiyo maana Yesu alisema hapa kwamba ikiwa mwanamume au mwanamke ataachilia mamlaka ya mbinguni hapa, mbingu itamuunga mkono. Tusipofanya hivyo, mbingu haiwezi. Ikiwa wazo hili linaonekana kuwa geni kwako, tafadhalii usikome hapa. Nitashughulikia kwa undani zaidi baadaye. Lakini kwa sasa kubali ukweli huo kama sababu ya pepo huyo kutomwondokea kijana yule –

## **LAKINI HUYU SI WEWE, RAFIKI YANGU; UNAWEZA KUPATA HAKI KATIKA UFALME. KUNA MAJIBU YA SHIDA ZAKO.**

**haikumpasa!** Alikuwa na haki kisheria

kukaa ndani yake. Tena, Yesu alisema sababu iliyomfanya pepo huyo asipaswe kuondoka ni kwa sababu ya ukosefu wa imani, au ukosefu wa mamlaka. Mungu alipoteza mamlaka Yake katika masuala ya wanadamu Adamu alipomtenga Mungu kupitia kwa uasi wake. Hapa ndipo Shetani anapata mamlaka yake juu ya wanadamu.

*Akampandisha (Yesu) juu, akamwonyesha milki zote za ulimwengu kwa dakika moja. Ibilisi akamwambia, “Nitakupa wewe enzi hii yote, na fahari yake, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa ye yote kama nipendavyo. Basi, wewe ukisujudu mbele yangu yote yatakuwa yako.”*

– Luka 4:5-7

Mungu alipoteza uhalali Wake duniani alipompoteza mtu aliyeubeba–yaani Adamu. Kama nilivyosema awali, nitazungumzia zaidi kuhusu sheria hizi mahususi baadaye, lakini sababu yangu kuu ya kuangazia hadithi hii ni kuonyesha nia na kukata tamaa kwa baba na jinsi alivyoegemea kuomba

rehemza. Tafadhali soma sentensi hizi chache zifuatazo kwa makini sana.

Ikiwa hakuna mamlaka au sheria na mfumo wa kuleta haki na suluhisho kwa mtu mwenye hitaji, basi kuomba rehemza ndilo suluhisho lililosalia. Acha niseme kwa njia nyingine. Ikiwa mtu hana suluhisho la kisheria kwa tatizo wala kuwa na njia ya kupata haki, basi hakuna uhakika wa kupata majibu. Kilichobaki kufanya ni kusihi pekee.

Lakini huyu si wewe, rafiki yangu; unaweza kupata haki katika Ufalme. Kuna majibu ya shida zako. Kumbuka, ufalme ni serikali, na unafanya kazi kwa sheria zisizo na upendeleo na zinapatikana kwa raia yejote anayeishi chini ya mamlaka ya ufalme huo. Kama nilivyosema awali katika kitabu hiki, Ufalme wa Mungu umejengwa juu ya haki (mchakato wa kisheria unaotumia mamlaka ya Mungu kutekeleza kile ambacho sheria Yake inasema ni sawa) na ni chema. Kulikuwa na sababu huyo pepo hakutoka, na haikuwa udhaifu wa Mungu wala mabadiliko katika mapenzi Yake. Yesu alituonyesha jambo hili kwa jinsi alivyowakemea upesi wanafunzi kisha akamtoa pepo.

Wakristo wengi, wasipoona utendaji wa Ufalme, wao hubadili imani yao, wakisema, "Pepo wote hawatoki." Wanajua Mungu ana nguvu zote, kwa hiyo wanafikiri kwamba anaweza kufanya chochote anachotaka ulimwenguni, kwa hivyo ikiwa pepo huyo hakutoka, basi lazima iwe kwamba Mungu aliamua kutomwondo. Rafiki yangu, mtazamo huu si sahihi kabisa. Yesu alisema fikira ZAO potovu na kutoamini kwao ndiko kulikopunguza mamlaka ya mbinguni katika tukio hili. Hebu niliseme hivi. Sababu yule pepo hakutoka ilikuwa suala la kisheria—tosha. Haikumpasa kutoka kwa sababu hakuna mtu hapo aliyeleta mamlaka ya mbinguni na ya kisheria katika hali hiyo. "Lakini, Gary, walikuwa wakijaribu kumwondo." Ndio, lakini kama nilivyosema awali, kisheria, haikumpasa kutoka. Kwa nini? Tena, mbingu hazikuwa na mamlaka ya kumfanya pepo huyo atoke.

## **KWA KUWA MWANADAMU ANA UHALALI ULIMWENGGUNI, SERIKALI YA MUNGU NA MAMLAKA YAKE HAYAWEZI KUFANYA KAZI HADI MTU, ALIYE NA MAMLAKA DUNIANI, ATAKAPOSADIKI KIKAMILIFU KUHUSU KILE AMBACHO MBINGU INASEMA, KISHA AKIACHILIE HAPA.**

Acha nifafanue kile ambacho nimesema. Walikuwa na mawazo potovu, wakiita kitu kibaya chema au kinachokubalika, au kufikiri kinyume

na kile ambacho Mungu angesema kuhusu suala fulani. Kutokuamini pia kulikuwa suala kuu kwa sababu imani inahitajika kabla ya mamlaka ya mbingu kutenda kazi ulimwenguni. Wanafunzi hawakusadiki, wala kushawishika kabisa, kwamba pepo huyo angetoka. Waliogopa.

Kwa kuwa mwanadamu ana uhalali ulimwenguni, serikali ya Mungu na mamlaka Yake hayawezi kufanya kazi hadi mtu, aliye na mamlaka duniani atakaposadiki kikamilifu kuhusu kile ambacho mbingu inasema, kisha akiachilie hapa. Kuwa na miyo iliyoshawishika kikamilifu kuhusu kile ambacho mbingu zinasema kunaitwa imani, na hakuna mtu aliye kuwa na imani siku hiyo. Walikuwa na nia mbili na kujawa na kutoamini, na hivyo kuzuia mamlaka ya mbinguni katika tukio hili. Lakini Yesu alikuwa na imani na alifahamu kwamba pepo huyo angetoka! Yesu alichukua mamlaka dhidi yake naye akatoweka. “Lakini, Gary, sababu ya pepo kumtoka wakati Yesu alimkemea ni kwa sababu alikuwa Yesu.” Kweli? Hebu tuangalie Marko 6:5 wakati Yesu alihudumu kwao mjini.

*Wala hakuweza kufanya mwujiza wo wote huko, isipokuwa aliweka mikono Yake juu ya wagonjwa wachache, akawaponya.*

Unakubali kwamba Yesu alikuwa na nguvu za kuponya, sivyo? Basi lazima ujibu kwa nini hakuweza kufanya yote ambayo alitaka kufanya katika tukio hili. Hitaji lilikuwepo, lakini kuna kitu kilichomzuia. Alijibu jambo hili katika mstari wa 6, “*Akastaajabu kwa kutokuamini kwao.*” Imani (kukubaliana na mbingu) huipa mbingu uhalali katika ulimwengu. Kwa mfano, unaweza kuona kanuni hii kwa urahisi katika jinsi ulivyookolewa na kuja kwa Kristo.

*Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*

– Warumi 10:10

Unaamini moyoni mwako (yale ambayo mbingu inasema), kisha unahesabiwa haki. Ni neno la kisheria, linalomaanisha utendaji wa sheria na linadokeza kwamba mbingu sasa ina uhalali katika ulimwengu. Kwa mtazamo rahisi wa kanuni hii, tukumbuke kwamba Adamu alipewa mamlaka ya kisheria hapa duniani, na wanadamu bado wana nafasi hiyo. Hili halipaswi kuchanganywa na kutokuwa na uwezo wa kutawala kiroho kwa mwanadamu, ambako alipoteza kwa Shetani katika bustani

ya Edeni. Mungu hawezi kukiuka nafasi ya kisheria ambayo mwanadamu anashikilia sasa katika ulimwengu. Hivyo, ni lazima Mungu atafute mtu ambaye atakubaliana na mbingu ili kupata kiingilio halali na kujidhihirisha ulimwenguni.

Katika Warumi 10:10, utaona kwamba kuna mambo mawili ambayo lazima yatendeke kabla ya mamlaka na nguvu za mbinguni kuachiliwa hapa duniani. La kwanza nimeshalitaja: Ni lazima tushawishike kikamilifu na tukubaliane miyoni mwetu na yale mbingu inasema; hii inaitwa imani. Pili, tunahitaji kuelewa kwamba kuwa na imani pekee hakutaachilia mamlaka ya mbinguni hapa. Umeshangaa? Hebu nifafanue. Fikiria kibonyezi cha taa. Nguvu ya umeme ipo, lakini bado lazima ubonyeze kibonyezi ili kuwashaa taa. Tunapoamini miyoni mwetu kile ambacho mbingu inasema, hilo linafanya uhusiano na mbingu kuwa halali au kuhesabiwa haki. Lakini inabidi basi tuyachilie mamlaka hayo hapa. Kama katika mfano wangu, tunahitaji kubonyeza kibonyezi. Tunafanya hivyo tunapokiri na kutenda kulingana na mamlaka ya Ufalme.

Najua kuwa ninajrudia, lakini kuielewa sheria hii ya Ufalme ni MUHIMU kwako katika kuwa na uwezo wa kupokea kilicho chako kutoka mbinguni. Utapokea kila kitu utakachopokea kutoka mbinguni jinsi ulivyookoka—kwa kuamini kile ambacho mbingu inasema moyoni mwako na kisha kukinena au kikitenda.

Ufalme, kama Yesu alivyofundisha na kuudhihirisha, haukuwa wa kawaida kabisa kwa wanafunzi. Mara nyingi, wanafunzi walichanganyikiwa na yale waliyoyaona. Katika andiko tulilosoma awali, naamini kwamba wanafunzi walitishwa na udhihirisho wa pepo na wakawa na nia mbili, na hivyo kubatilisha imani yao. Nafikiri kwamba walipoenda kumtoa pepo huyo, alijidhihirisha sana, na labda kumwangusha kijana huyo chini. Hili labda liliwatia hofu. Ninakisia tu hapa, lakini jambo moja nina uhakika nalo. Jambo lilitokea kutoa miyo yao kwa makubaliano na mbingu na kuwafanya wasiamini.

Kwa upande mwagine, Yesu alikuwa na hakika kabisa kile mbingu ilichosema kuhusu hali kama hiyo na akaamuru pepo huyo aondoke. Kwa hiyo, kama tunavyoona, tatizo la yule pepo kutotoka lilikuwa ulimwenguni, wala si mbinguni.

Ikiwa ningechagua andiko moja bora zaidi kuliko mengine yote yanayodhihirisha kazi ya Ufalme ulimwenguni, ningepaswa kusema kwamba ni Marko 11:22–24. Ili kuweka msingi, tunahitaji kurudi nyuma aya chache, na tutaona kwamba Yesu alinenea mti kisha ukafa. Baada ya

# “KWA SABABU HIYO NAWAAMBIA, YOYOTE MYAOMBAYO MKISALI, AMININI YA KWAMBA MNAYAPOKEA, NAYO YATAKUWA YENU.”

— MARKO 11:24

‘Ng’oka ukatupwe baharini,’ wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake. Kwa sababu hiyo nawaambia, Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.’

— Marko 11:22-24

Tazama kwamba Petro alishangazwa na kile kilichotokea. Jambo hilo lilifanyikaje? Yesu aliunenea mti huo tu. Bila shaka mti uliitikia maneno ya Yesu na ukafa. Kisha Yesu akamwambia Petro “kweli” fulani, ambayo ni sheria katika Ufalme wa Mungu. Maelezo ya Yesu yanatupa ufahamu zaidi wa jinsi Ufalme wa Mungu unavyotenda kazi katika ulimwengu. Tena katika mfano huu tunaona sheria hiyo hiyo ambayo tumekuwa tukizungumzia ikifanya kazi; mtu duniani, aliyesadiki kikamilifu kile mbingu inasema (anahesabiwa haki) kisha ananena au kuachilia mamlaka ya mbinguni. Bila shaka, mtu katika hadithi hii ni Yesu, Mwenyewe, lakini aliweka wazi katika maelezo Yake kwa wanafunzi Wake kwamba “mtu ye yoyote” angeweza kufanya kile alichokifanya.

Nina hakika utakubali kwamba ikiwa watu kweli wangejua hili na kuelewa sheria ambayo Yesu alikuwa akiwafundisha, ingekuwa na matokeo makubwa katika maisha yao. Niliona matokeo ya Ufalme katika maisha ya familia yangu, lakini pia ilistaajabisha kuona matokeo katika familia zingine tulipowafundisha yale tuliojifunza. Niruhusu nisimulie tukio katika kanisa langu mwenyewe ambapo sheria hii ilidhihirika. Mara nyingi, ujuzi wa Ufalme na utendaji wake ni muhimu kama kitu kinachokutoa kwa kifo na kukupa uhai. Jambo hili liko dhahiri katika hadithi hii.

Jennifer alianza kuhudhuria kanisa langu na kusikia kuhusu imani na Ufalme. Alifurahia kujua kuhusu mamlaka na haki zake katika Ufalme maana alikuwa na mimba ya mtoto wake wa pili, na alitamani kuzaa akiwa

kutopata matunda kwenye mti huo, Yesu aliulaani. Siku iliyofuata wanafunzi walipopita karibu na mti ule tena, waliona kwamba umekufa. Petro alishangazwa na kile alichokiona na kumlilia Yesu akiwa na mshtuko.

Yesu akajibu, akamwambia,  
*“Mwaminini Mungu. Amin, nawaambia,  
Ye yote atakayeumibia mlima huu,*

nyumbani. Kwa hiyo, alianza kujifunza yale ambayo Neno la Mungu linasema kuhusu kuzaa mtoto na ahadi za Ufalme ambazo zingehusu mtoto wake. Alikuwa amesadiki kwamba angezalia nyumbani vyema. Alitafuta mkunga, kisha akamwomba mwanamke mmoja wa kanisa letu, ambaye amezalia watoto kadhaa nyumbani, ikiwa angekuwa mkufunzi wake wakati wa kujifungua.

Kabla ya kujifungua, alikuwa katika kila ibada akijifunza kuhusu kanuni za Ufalme. Dhana hizi zilikuwa mpya kwa Jennifer, naye alipenda kujifunza kwamba kulikuwa na majibu ya kweli katika Ufalme wa Mungu. Kwa bahati mbaya, wakati huo, mume wake alipaswa kufanya kazi siku ya Jumapili na mara nyingi hakuweza kuhudhuria kanisa pamoja naye. Naam, hatimaye wakati wa mtoto kuzaliwa ulifika. Mkunga na mkufunzi waliitwa.

Ilikuwa yapata saa nane au saa tisa usiku wakati simu iliyokuwa kando ya kitanda changu ililia. Nilisikia mkufunzi wa Jennifer akipiga mayowe kwa simu, "Mchungaji, tafadhali omba; mtoto amezaliwa akiwa amekufa!" Habari hizo zilinizindua kutoka kwa usingizi. Kisha mkufunzi akasema kwamba mtoto alikuwa amechukuliwa na gari la wagonjwa kwenda hospitalini. Aliniambia kwamba, timu ya wauguzi ilipowasili ilitangaza kwamba mtoto amekufa.

Mimi na Drenda tuliruka na kuvaa mara moja. Nilianza kuomba katika Roho, huku nikisikiliza kile nilichopaswa kufanya. Nilijua kwamba shetani angependa kukashifu kanisa letu kwa sababu ya tukio hilo. Niliwaza nikiona vichwa vya majorida vikitangaza, "Mtoto Afa kwa sababu ya Kanisa la Uongo Linalohimiza Kuzalia Nyumbani." Kwa kweli hatukuchukua msimamo juu ya suala la jinsi mtoto anavyopaswa kuzaliwa, iwe nyumbani au la, lakini wanawake wengi walichagua kuzalia nyumbani. Mimi na Drenda tuliendelea kuomba katika Roho huku tukiendesha gari kuelekea hospitali, mwendo wa dakika 20 kwa gari. Karibu nusu ya safari, ghafla nilihisi Roho wa Mungu akija juu yangu, na nikafahamu kwamba mtoto atanusurika. Wakati huo huo, mke wangu alinigeukia akasema kwamba Bwana amemwambia mtoto atakuwa sawa.

Nilijua kile Bwana alikuwa ameniambia pamoja na mke wangu, kwa hivyo nilipoingia kwenye chumba cha dharura hospitalini, nilikuwa na hamu ya kujua ni hali gani ambayo ningepata. Niliona kikundi cha wauguzi saba au wanane waliokuwa wamemzunguka mtoto aliyekuwa mzima, mwenye rangi nzuri ya ngozi ambaye alikuwa akilia. Nilichunguza nyuso zao kwa makini. Katika hali nyingi ambapo mtoto amebebwa na kundi la wanawake, utaona tabasamu. Lakini wakati huu, tabasamu hazikuwepo.

Badala yake, kulikuwa na mshtuko kwa nyuso zote.

Tulikutana na yule mwanamke aliyetupigia simu. Alitufahamisha tena kwamba walitangaza mtoto amekufa walipokuwa nyumbani, ambayo ni umbali wa dakika 20. Walitangaza pia kwamba mtoto alikuwa amekufa walipowasili hospitalini lakini ghafla, akaamka. Bwana asifiwe! Drenda na mimi tulifurahi kumuona mtoto akiwa hai na mzima kama vile Roho Mtakatifu alivyokuwa ametuambia.

Wakati huohuo, gari nyingine ya wagonjwa ilikuwa imemsafirisha mama ya mtoto, Jennifer, hadi kwenye hospitali ya mama wajawazito. Kwa hivyo, hakujua kuhusu hali ya binti yake. Mke wangu, Drenda, alienda hadi kwenye ghorofa ya uzazi ili kumtazama. Drenda alipoingia kwenye chumba alichokuwa amepumzika Jennifer, alisema, “Jennifer, mtoto wako yuko sawa, na ni mrembo kupindukia.” Muuguzi aliyekuwa karibu na Jennifer aliingilia kati na kupinga, “La, huyo mtoto yuko kwenye begi la miili!” Mke wangu alimsahihisha muuguzi kwa ukali mwangi kuhusu kosa lake. Leo, kwa utukufu wa Mungu, mtoto huyo wa kike, ambaye jina lake ni Haley, ni msichana mrembo asiye na majeraha kwa ubongo au masuala ya kiafya ya aina yoyote. Kwa kuelewa kwamba Ufalme wa Mungu unafanya kazi kwa kutegemea sheria ya kiroho, nilijua matokeo haya hayakuwa ya kubahatisha. Kwa hiyo, kwa kuwa mimi ni mwanasayansi wa mambo ya kiroho (sio dini ya Sayansi ya Kikristo, bali mtu anayesoma jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi), nilitaka kujuwa ni nini hasa kilichotokea.

Nilifahamu wauguzi wenyewe gari la wagonjwa lililokuja nyumbani walitangaza rasmi kwamba mtoto Haley alikuwa “amekufa walipowasili.” Nilifahamu pia kwamba hospitali ilitangaza mtoto alikuwa amekufa alipofikishwa hospitalini. Kwa hivyo ni kitu gani kilitokea? Nilizungumza na yule mkufunzi wa uzazi, na nikamwomba anieleze kila kitu kwa undani kuhusu kile kilichotokea. Nilikuwa nikitatufuta vidokezo. Alisema kila kitu kilikuwa sawa hadi mtoto alipozaliwa. Hakuwa na dalili za kuwa hai na alikuwa na rangi ya samawati. Mkunga alijaribu kumfufua mtoto lakini hakuweza. Kisha mkufunzi akasema kwamba Jennifer alikuwa na wanafamilia wake wengi hapo ambao walianza kuingiwa na hofu. Lakini Jennifer aliwaambia kwa utulivu wanyamaze, kisha akaweka kidole chake usoni mwa mume wake, na kusema, “Usiseme neno lolote—mtoto huyu atakuwa sawa!”

Nilikatisha hadithi ya mkufunzi hapo hapo na kumwuliza ikiwa angeweza kurudia yale ambayo Jennifer alikuwa amemwambia mume wake tena. Aliniambia jambo lile lile alilokua ameniambia, kwamba Jennifer

aliweka kidole chake usoni mwa mume wake na kusema, “Usiseme neno lolote—mtoto huyu atakuwa sawa!” Ajabu! Hiyo ndiyo sababu! Hayo ndiyo matamshi yaliyookoa maisha ya mtoto Haley. Nilihisi kama mpelelezi ambaye alikuwa ametatua kesi kubwa! Nilifurahi sana. Lilikuwa jambo rahisi sana, lakini la kina pia. Jennifer alikuwa ametumia sheria ya kiroho katika hali hiyo, na ilikuwa imeokoa maisha ya mtoto wake! Nilipotafakari juu ya yale nilikuwa nimejifunza, kila kitu kilieleweka.

Jennifer alijua kwamba mume wake kwa sababu ya ratiba yake ya kazi hakuwa amejengwa katika imani jinsi alivyokuwa amejengeta kwa miezi kadhaa kabla ya kujifungua. Alijua pia kwamba, kama kichwa cha nyumba yao, makubaliano yake na matukio ya kutisha yaliyotokea alipokuwa akimzaa mtoto wao yangefunga hatima yake. Ndio maana mwitikio wake wa kwanza ulikuwa ni kuzungumza na mumewe na kutomruhusu akubaliane na kifo cha mtoto wao. Badala yake Jennifer alikuwa na hakika kwamba mtoto angeishi na kuwa sawa, na alitangaza jambo hilo kwa ujasiri na imani.

Mara tu aliporuhusiwa kutoka hospitali, Jennifer alienda kwa timu ya wauguzi waliombeba mtoto kwa gari la wagonjwa na kuwaauliza ni nini walichomfanya mtoto walipokuwa wakielekea hospitalini usiku ule. Walimtazama wakiwa na nyuso zenyehaya kidogo.

“Hakuna kitu,” hatimaye mmoja wao akasema.

“Unamaanisha nini unaposema, hakuna kitu?” Jennifer aliuliza, “Je, mlajaribu kumfufua?”

“Hapana,” wakasema.

“Mlimfanya mtoto chochote?”

“La,” wakasema tena.

Walimwambia mtoto alikuwa amekufa, na hawakuwa na tumaini kwamba angepata nafuu. Hata hivyo, mtoto “aliamka” walipofika hospitalini! Timu hiyo ya gari la wagonjwa ilipokea tuzo inayotolewa kila mwaka kutoka kwa hospitali na idara ya wazima moto kwa mwitikio mzuri katika hali ngumu. Lakini walikiri hawakuwa wamefanya chochote.

Hivi majuzi tulikuwa na Hailey kwenye kipindi chetu cha televisheni pamoja na mamake, Jennifer; na sisi sote, tukiwa na machozi machoni mwetu, tuliadhimisha tena Ufalme wa Mungu. Tulisherehekeea kwamba kulikuwa na mtu katika tukio hili aliyefahamu jinsi ya kutumia sheria ya kiroho na mamlaka ya Ufalme.

Katika tukio hili, Jennifer akiwa amesadiki kikamilifu kile ambacho mbingu inasema, aliachilia mamlaka hayo kwa maneno yake mwenywewe.

## Sheria ilifanya kazi!

Tukio kama hili lenye sheria ya Ufalme wa Mungu lilifanyikia familia nyingine katika kanisa langu. Dada wawili waliamua kula chakula cha mchana pamoja, jambo ambalo halikuwa rahisi, kwa sababu kati yao wawili huenda walikuwa na watoto 12 au 13. Walipokuwa wakila chakula cha mchana, walitambua kwamba Joel, mtoto wa miaka minne, hakuwepo. Walitafuta nyumba nzima na hawakumpata. Kwa hiyo walidhani huenda amejificha, lakini tena baada ya kumtafuta kabisa, hawakumpata. Ghafula mamake, Tina, akawa na wazo baya sana. Je, bwawa la maji lililo nyuma ya nyumba? Alikimbia nje kupitia mlango wa nyuma na mpwa wake, Courtney, mwenye umri wa miaka 13. Tina alijawa na hofu baada ya kumkuta Joel chini ya bwawa akiwa kama mtu aliyekufa. Hakuna aliyejua ni muda gani alikuwa amekaa hapo. Tina alipiga mayowe waite 911 huku akiruka ndani ya bwawa na kumtoa Joel nje. Mwili wake ulikuwa rangi ya kijivu, hakuwa anapumua wala kusongea.

Mtoto wa umri wa miaka 13, ambaye alilelewa katika huduma yetu ya watoto, alimwambia shangazi yake, "La, Shangazi Tina, hatuhitaji kuita 911; tuna mamlaka hapa. Tunahitaji kuomba." Kwa hiyo wote wawili walianza kuomba, lakini hakuna kilichotokea. Tina alisema kwa sauti tena, "Piga 911!" Kisha Courtney akamwambia shangazi yake, "Shangazi Tina, tunahitaji kumtangazia uzima." Kwa hivyo Courtney akasema, "Joel, kwa jina la Yesu, amka!" Ghafla Joel alikohoa, akatema maji, akapata fahamu, kisha akawa mzima kabisa.

Ninapokumbuka hadithi hii, huwa nashangaa, sistaajabu kwamba mtoto alikuwa sawa, bali kwamba mtoto wa miaka 13 alikuwa na akili kama hiyo. Katika hali yenyе fadhaha kubwa na kifo, aliweza kutathmini kile kilichohitajika kufanya bila kuogopa. Courtney alithibitisha tena kwamba kujua jinsi Ufalme unavyofanya kazi si mahubiri mazuri tu; ni uzima au kifo!

Kwa mara nyingine tena, tazama jinsi sheria ya Ufalme ilivyofanya kazi. Mwanzoni Courtney alisema kwamba walihitaji kuomba, jambo ambalo walifanya, lakini hakuna kilichotokea. Hiyo ni kwa sababu tunapoomba hatuachilii mamlaka na nguvu za Mungu. Tunaomba ili kupata mwongozo. Hilo ndilo hasa walilohitaji wakati huo. Kisha Courtney alisema kwamba walihitaji kumtangazia uzima. Walipofanya hivyo, aliamka akiwa sawa kabisa na yuko mzima kama kigongo hadi leo. Tena, tunaona moyo uliosadiki kabisa kile mbingu inachosema, lakini hakuna kilichotokea hadi mamlaka hayo yalipoachiliwa ulimwenguni na mtu mwenye imani.

Acha nikupe hadithi nyingine moja, ambayo ilituhusu mimi na mke wangu, Drenda. Kaka ya Drenda alikuwa amempeleka Candy, mke wake, hospitalini ili kujifungua mtoto wao wa tano. Drenda na mimi tulipitia hospitalini asubuhi Candy alipokuwa na uchungu wa kuzaa ili kuona nyongeza mpya katika familia. Tulifikiri alikuwa amejifungua muda mrefu kabla yetu kufika huko. Lakini tuligundua, kwa sababu ya kuchelewa kidogo, alikuwa amejifungua saa hiyohiyo. Mtoto Holland alikuwa analetwa kwenye chumba cha watoto tulipokuwa tukiingia kwenye wodi ya uzazi. Labda umetambua kwamba chumba cha watoto wachanga katika wodi ya uzazi huwa kimejaa madirisha tupu, ili kukuruhusu kuona watoto wanapoletwa.

Walipomleta Holland, mara moja niliona kwamba alionekana kuwa mweupe zaidi. Watoto wote wa Johnny wana nywele zenye weupe wa rangi ya dhahabu; na mwanzoni, nilifikiri kwamba ukosefu wa rangi ulikuwa kawaida kwa watoto wake wakati wa kuzaliwa. Lakini bado hakuonekana kuwa sawa. Ghafla, madaktari wote walianza kukimbia huku na kule. Wauguzi walifunga pazia haraka ili nisiweze kuona ndani ya chumba cha watoto, na nilijua hiyo haikuwa dalili nzuri. Japo pazia lilifungwa, kulikuwa na ufa katika pazia ambao nilitumia kutazama kila kitu kilichokuwa kikiendelea. Wauguzi walianza kutoa vifaa, na daktari akaanza kujaribu kumfufua Holland. Nilizunguka nikaenda kwenye mlango mwingine wa chumba cha watoto wachanga ambapo niliweza kusikia vyema kile ambacho madaktari walikuwa wakisema. Nilipokuwa nasikiliza nilishtuka kusikia wakisema moyo wa mtoto haupigi na hawakuwa na uwezo wa kuufanya uanze kupiga. Nilipoendelea kusikiliza, nilisikia ukipiga-piga kidogo baada ya muda fulani. Nilisikia ukipiga mara moja kisha baada ya sekunde 15 au 20, ungepiga tena. Moyo wa Holland haukuwa unapiga!

Daktari alitoka chumbani na kumsogelea Johnny, “Mambo si mema,

## **KUMBUKA KWAMBA SHERIA ZA UFALME HUFANYA KAZI KILA WAKATI, KWA MTU YEYOTE!**

Johnny; samahani, lakini bado tunajaribu.” Hatukuruhusiwa kuingia katika chumba cha watoto, kwa hiyo Drenda na Johnny waliwekelea mikono yao kwenye mlango uliokuwa upande mmoja, nami niliweka mikono yangu kwenye mlango uliokuwa upande mwingine wa chumba hicho. Kisha tukaanza kuomba na kutangaza kwamba

Holland angeishi na hangekufa na kwamba angekuwa sawa. Tuliamuru moyo wake upige, kwa jina la Yesu.

Ghafla, daktari aliyejekwa akizungumza na Johnny alitoka nje ya chumba cha watoto kwa haraka sana. Alipita haraka karibu nasi bila kusema chochote. Baada ya dakika chache alirudi haraka akiwa na mwuguzi nyuma yake akisema kwa sauti ya juu, "Daktari hatuwezi kufanya hivyo. Hatuna idhini ya kutumia njia hiyo katika hospitali hii. Sitakuruhusu uchukue hiyo damu." Hakumsikiliza huku akirudi ndani ya chumba cha watoto. Alichukua kitabu cha maelezo, na niliweza kuona kwamba alikuwa akisoma kwa uangalifu jinsi ya kutumia utaratibu fulani wa matibabu. Nilitazama kupitia kwa ufa wa mapazia huku akinyanyuka na kuanza kuingiza bomba ndefu ndani ya mtoto. Nikatambua kwamba alikuwa akimwekeea damu.

Ghafula moyo uliana kupiga. Uliongeza kasi kisha ukasawazishwa na mapigo ya kawaida ya moyo wa mtoto mchanga. Baada ya muda mfupi daktari alitoka na kusema, "Kulikuwa na malaika mle ndani; Mungu alinisaidia kumtibu mtoto huyu!" Tuliweza kuona kwamba alikuwa ametikiswa na jambo hili. Baadaye tuligundua kwamba haikuwa zamu yake kuwa kazini na hakuwa amehusika katika kuzaliwa kwa Holland. Alikuwa amepitia hospitalini kuangalia mgongwa mwingine wakati haya yote yalipotokea. Niliweza kuona kwamba daktari bado alikuwa ameshangazwa na kile kilichotokea maana alituambia kwamba Holland hakuwa na mapigo ya moyo kwa dakika 36!

Leo Holland ni mtoto wa kupendeza wa kawaida mwenye umri wa miaka minne. Ninaamini kwamba ni ufahamu wetu wa sheria ya Ufalme ambao uliletu majibu katika hali hiyo. Bado nakumbuka, nilipoweka mikono yangu kwenye mlango ule wa chumba cha watoto, nikijiwazia, "Hatutafanya mazishi ya mpwa mdogo wa Drenda! Sio ikiwa tungali tupo!"

Tunapotulia ili kutafakari jinsi Ufalme ulivyofanya kazi katika kila moja ya hadithi hizi nilizoshiriki, ningependa ukumbuke kwamba sheria za Ufalme hufanya kazi kila wakati, kwa mtu yeoyote! Kama nilivyosema mwanzoni mwa kitabu hiki, sheria za asili za ulimwengu hufanya kazi na kuwa na matokeo sawa kila wakati. Hazina upendeleo na zitafanya kazi kwa yeoyote atakayetenga wakati wa kujifunza na kuzitumia. Umeme hufanya kazi sawa Marekani kama unavyofanya Afrika; hakuna tofauti.

Nilipoanza kutambua kwamba Ufalme wa Mungu ulikuwa ni Ufalme wenye sheria halisi ingawa zimefichwa, nilijua nimepata jibu kwa matatizo yangu. Nilitambua kwamba Mungu hakuwa akikataa kunibariki au kunisaidia katika wakati wangu wa shida. La, sasa nilitambua kwamba Mungu alikuwa amenipa kila kitu ninachohitaji maishani kupitia kwa Yesu Kristo, ambaye kupitia kwa dhabihu Yake alinipa uwezo wa kupata vyote

vilivyo mbinguni. Nilipata ufahamu kwamba Ufalme unaongozwa na sheria zilizowekwa ambazo ningeweza kujifunza na kutumia maishani mwangu.

Nilianza kusoma kila hadithi katika Biblia nikiwa na mtazamo tofauti, huku nikitafuta vidokezo ambavyo vingenifunulia sheria zingine za Ufalme. Nilijitolea kuwa mwanasayansi wa kiroho ili kujifunza kwa nini mambo yalitokea katika hadithi za Biblia nilizosoma mara nydingi. Andiko hili katika 1 Yohana linasikika kuwa la kuchekesha na lisilo la kawaida kwa watu wengi. Najua tulilisoma awali, lakini tulisome tena kwa sababu ndani yake kuna ukweli ambaao ni jibu lako.

*Na huu ndio ujasiri tulio nao Kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi Yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia (anashughulikia tatizo)—tuombacho chote—TWAJUA kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.*

—1 Yohana 5:14-15

Napenda andiko hili kwa sababu linazungumzia sheria, na sheria inatupa ujasiri kwamba tutapata haki. Huu ndio ujasiri tulio nao—tukiomba kitu sawasawa na mapenzi ya Mungu (sheria, kile Mungu anachokiita chema), Yeye hutusikia. Tena, neno hili “atusikia” halizungumzii kuhusu Mungu kusikia maneno yetu, ingawa Yeye huyasikia. Lakini, linazungumzia Mungu kushughulikia tatizo letu. Ukitaka kuelewa andiko hili vyema, tafakari kuhusu hakimu anayefanya uamuzi wa kesi kwa mujibu wa sheria, wala sio kulingana na hisia zake mwenyewe (hivyo ndivyo inavyotakiwa kuwa). Yeye hutusikiliza—anashughulikia au kusikia tatizo letu, kwa hivyo tuna hakika kwamba tutapata haki, ambayo ni yetu kisheria.

Rafiki yangu, nafikiri unahitaji kukoma hapa kidogo na kusoma maneno haya tena, polepole. Ikiwa ulichosoma ni kweli, na ni kweli, basi maisha yako karibu kujawa na furaha! Watu wanaoomba bila ujuzi huu hawana ujasiri; wanaporokwa tu wanapoomba. Yesu alizungumzia jambo hili katika Mathayo 6:7–13.

*“Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi.”*

— Mathayo 6:7

Neno “kupayuka” linamaanisha kutamka mchanganyiko wa maneno

au kutoa sauti isiyo na maana. Hivi ndivyo watu wengi huomba. Hawajui kwamba wana haki ya kupata haki au hata yale ambayo Mungu amewapa tayari kisheria katika Ufalme. Huhitaji kumsihi Mungu au kulia kuhusu kitu ambacho tayari unacho!

Hebu tuseme kwa mfano afisa wa polisi amesimama barabarani na ameambia lori lisimame, kisha aanze kulia na kulisihii lori lisimame. "Tafadhali lori, simama. Nihurumie. Tafadhali, tafadhali lori nzuri, simama." Hilo lingekuwa tusi la kusikitisha na la fedheha zaidi kwa taifa la Marekani na mfumo wake wa kisheria. La hasha, afisa huyo wa polisi atasimama kidete na kulambia lori hilo waziwazi lisimame, nalo litasimama kwa kuzingatia sheria ya nchi na cheo chake kama afisa anayewakilisha serikali ya taifa.

Watu wanaomsihi Mungu hawajui sheria ya nchi wala vyeo vyao. Sababu afisa wa polisi kusihii lori lisimame ni tusi kwa taifa ni kwamba inaonyesha taifa lisilo na sheria wala mamlaka. Yale utakayokuwa nayo katika nchi aina hiyo ni machafuko. Wakristo wanapomsihi Mungu na kuendelea kufanya hivyo, inaonyesha kwamba Ufalme wa Mungu ni dhaifu, na hauna majibu. Linawafanya watu watilie shaka nia ya Mungu au uwezo Wake wa kuwasaidia, wakati muda huo wote, wana haki ya kupata kile wanachoomba. Yesu anatupatia jibu wazi kuhusu maombi haya hafifu ya kumsihi—"KOMA!"

*Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi. Basi msifanane na hao; maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba. Basi ninyi salini hivi;*

*'Baba yetu uliye mbinguni, Jina Lako litukuzwe, Ufalme Wako uje, mapenzi Yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majoribuni, lakini utuokoe na yule mwovu.'"*

— Mathayo 6:7-13

Kumbuka, Yesu anatufundisha jinsi ya kuomba katika mstari huu. Cha kusikitisha ni kwamba, watu wengi wameweka aya hizi katika vibao vya mapambo manyumbani mwao ilhali hawaelewi maana yake. Kifungu hiki kinaitwa Sala ya Bwana, lakini alikuwa akiyatumbia maneno haya kuwfundisha wanafunzi Wake jinsi ya kuomba. Hakuwa akiyatumbia

kihalisi kama tunavyofanya katika ibada zetu za kanisa. Maneno haya ni mwongozo, ukipenda, ya jinsi ya kuomba na kupata matokeo, sio mstari wa kumbukumbu wa kunukuu.

*“Ufalme Wako uje, mapenzi Yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni,”* ni maagizo kuhusu jinsi ya kusali. Tunapaswa kuomba, ambako ni kuleta mapenzi ya Mungu yaliyo mbinguni katika ulimwengu na katika hali zetu. Kwa hivyo jibu lako ni nini? Amini kile ambacho Mungu anasema ni chako, na tumia mamlaka yako katika Ufalme wa mbinguni kuleta yaliyo mbinguni hapa duniani kisha mahitaji yako na ya wale walio karibu nawe yatatimizwa.

Kwa hivyo koma kidogo na utafakari juu ya hili. Ikiwa ungejua bila shaka kwamba maombi yako yanafaa na mbingu yote inakuunga mkono, je, hilo lingekufanya uwe na ujasiri unapoomba? NDIO!!! Kwa kujua haki zako za kisheria ni zipi kama raia wa mbinguni, kujua kile ambacho tayari kimetolewa kwako bila malipo na kuelewa mchakato wa kupokea, na kufurahia manufaa ya sheria hizo, unaweza kuishi kwa njia mpya kabisa—njia ya Ufalme. Ni nini kitafanyikia hofu? Ni nini kitafanyikia kutokuwa na uhakika? Je, ujuzi huu utachochaje ujasiri katika siku zako za usoni na katikati ya dhoruba? Haya ndiyo mabadiliko ambayo Ufalme uliletwa kwangu mimi na Drenda tulipoanza kuufahamu. Mara nyingi tulishangazwa na yale tuliyoyaona. La, acha niseme kwa njia nyingine. Tulishangazwa na kustaajabishwa mara kwa mara! Zaidi ya hili, tulishangazwa na mamlaka ambayo Mungu ametoa kwa kanisa kufanya kazi kwa niaba na kupitia kwa serikali Yake hapa duniani.

*Kwa sababu SHERIA ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na SHERIA ya dhambi na mauti.*

– Warumi 8:2

Kugundua kwamba tuliwekwa huru kutoka kwa “sheria ya dhambi na mauti” na kupewa Ufalme wenye “sheria ya roho wa uzima” lilikuwa jambo la ajabu sana. Ajabu zaidi ilikuwa kutazama sheria hiyo ikizaa uadilifu wa Ufalme maishani mwetu.

Ufalme ulinipa fursa ya kuponywa kimwili, kihisia, kupata tumaini jipya, na kuwa huru kutokana na dawa za kupunguza huzuni. Ulinitoa kwa umaskini wa kujitahidi kulipia nyumba nzee ya mashambani ya mwaka wa 1800 kodi ya \$300 kila mwezi na kuniwezesha kujenga na kuilipia kikamilifu nyumba ya futi za mraba 7,700 kwa shamba nzuri la ekari 59. Mke wangu

alinipenda zaidi sana, pia! Lilikuwa jambo la thamani kuendesha magari ya kifahari yasiyoharibika kila siku. Miaka michache iliyopita kutoa mamia ya maelfu ya dola kwa Injili lilikuwa jambo lisilowezekana. Giza lilikuwa likimezwa na uzima na nuru ya Ufalme, kama vile Mungu alipotazama uumbaji Wake ulipokamilika katika kitabu cha Mwanzo na kusema, "Ni chema!" Mimi pia, nilisimama nyuma kwa mshangao na kusema, "Hili ni jambo jema, jema sana."

Mimi na Drenda tulifurahia sana kiasi kwamba tulimwambia yeote ambaye angesikiliza kuhusu Ufalme na kumsimulia hadithi yetu. Watu katika kanisa letu walianza kuelewa na kupata matokeo sawa na yetu, na mmoja wa watu hao alikuwa binti yetu mwenye umri wa miaka 12. Alikuwa amemwona Mungu akifanya mengi sana na alikuwa ameshuhudia mara kwa mara sheria halisi za Ufalme zikizaa katika maisha yetu. Nilijua alikuwa akitazama na kujifunza kuhusu sheria hizi, lakini tukio moja lilinionyesha hakika ni kiasi gani alikuwa akijifunza.

Siku moja nilikwenda chumbani mwake kumtakia usiku mwema na jambo lilikuwa tofauti. Kwenye ukuta wake kulikuwa na picha ya mbwa mdogo aina ya Pomerani yenyе manyoya mengi. Sasa, kwa mtu yeote ambaye amekuwa mzazi kwa muda, picha kama hiyo ilikuwa ishara ya hakika kwamba hivi karibuni wangeombwa kununua mbwa. Niliamua kushughulikia ishara hiyo kwa sababu sikutaka mbwa mwingine wa kukaa ndani ya nyumba. Dada ya Kirsten, Polly tayari alikuwa na mbwa wa kukaa ndani ya nyumba, na alilala kwa chumba chao, kwa hiyo mbwa wa Polly alikuwa pamoja na Polly na Kirsten kila wakati.

Nilimwambia Kirsten kwa upole jinsi nilivopendezwa na picha yake lakini sikutaka mbwa mwingine wa kukaa ndani ya nyumba. Kwamba ikiwa alitaka kumfuga mbwa, alipaswa kutumia muda zaidi kumpapasa mbwa wa dadake. Kirsten hakusema lolote usiku huo, alikubali tu nilichosema. Nilifikiri jambo hilo lilikuwa limekamilika, lakini lilitajwa mara chache baada ya hapo katika matamshi kama, "Je, si ingekuwa vyema kuwa na mbwa wa kipomerani?" au "Wana manyoya mengi na ya kupendeza sana." Kisha Kirsten angenionyesha haraka picha yao moja aliyokuwa amepata mtandaoni. Tena, ningesema, "Hapana." Mimi ndiye niliyekuwa na mamlaka kwetu, na kamwe hatungenunu mbwa mwingine wa kukaa ndani ya nyumba.

Tena nilifikiri kwamba jambo hilo lilikuwa limekamilika hadi siku moja baada ya karibu mwezi mmoja tuliporudi nyumbani kutoka kanisani, Kirsten alinijia kwa ujasiri na, akiwa na tabasamu usoni mwake akasema,

“Baba, leo nilipokea mbwa wa kipomerani kwa imani kama unavyofundisha.” Nilimkumbusha tena kauli zangu za awali kuhusu kuwa na mbwa mwininge. Bila kubadili tabasamu lake, alisema, “Lakini Baba, Mama husema kwamba Mungu anaweza kubadilisha moyo wa mfalme.” Maneno yake kwangu hayakuwa ya uasi. Alikubaliana na mamake na kuomba kwamba Mungu abadilishe moyo wangu. Nilikuwa nimepatikana. Sasa nilifahamu kwamba mamake naye walikuwa wamezungumza, na mamake akamtia moyo kwamba kweli Mungu angeweza kubadili mawazo yangu.

Kulingana na kitiamoyo hicho, alikuwa ameachilia imani yake kanisani asubuhi hiyo, na kutoa matoleo huku akikiri kwamba amempokea mbwa huyo kwa imani. Nilikataa na kumhakikishia kwamba ninampenda na kumwambia kauli yangu tena, “Hatutakuwa na mbwa mwininge ndani ya nyumba.” Nilimwomba radhi na nikamwambia hilo halitatokea. Aliondoka akitabasamu; haikuonekana kama alijali nilichosema. Tena, nilidhani suala hilo hatimaye lilikuwa limekamilika.

Lakini baada ya karibu mwezi mmoja, nilialikwa kwenda kufundisha katika kanisa dogo huko Mississippi. Lilikuwa kanisa dogo sana la mashambani lililozungukwa na maili za ardhi iliyokuwa wazi. Mwishoni mwa jioni ya kwanza, mchungaji alinijia na kusema Bwana alikuwa amenena naye katika ibada. Alisema, “Sijui kama unajua hili au la, lakini ninakuza mbwa wa kipomerani kama jambo la ziada, na Bwana ameniambia nikupe mmoja wa watoto wa mbwa ambao sasa wana wiki sita na wako tayari kupata makao mapya.” Nilisimama na mdomo wazi. Bado sikuwa nataka kumchukua huyo mbwa, kwa hiyo nikasema, “nitakujulisha.” Sikujua kwamba alifuga mbwa wa aina yoyote na hakika sikumwambia hapo awali chochote kuhusu Kirsten kutamani mtoto wa mbwa.

Hatimaye nilivunjika moyo na kumweleza Drenda kilichotokea na kwamba sikutaka kumleta mbwa nyumbani. Alinitazama na kusema, “Je, utaikana imani ya binti yetu?” Drenda kwa kweli hakutaka mbwa wa pili ndani ya nyumba pia, lakini alimpenda Kirsten kuliko usumbufu wowote ambao mbwa mwininge angetuletea. Na sasa kwa kuwa Mungu alikuwa amemleta mbwa kama matokeo ya imani ya Kirsten, tungewezaje kumkana? Kwa hiyo nilimwambia mchungaji kwamba ningemchukua mbwa.

Hatukumwambia Kirsten bali tulimwambia dadake ahakikishe kwamba amemleta Kirsten kwenye uwanja wa ndege watakapokuja kunichukua. Kirsten alikuja kwenye uwanja wa ndege, na tukatembea na kumpa kifurushi kidogo cha kusafiri tulichomnunulia mbwa. Kirsten alipomwona yule mtoto mdogo wa mbwa, aliangua kilio. Kila kitu kilisimama. Kila mtu

aliyekuwa karibu nasi alisimama ili kutazama tukio lililokuwa mbele yao. Muda si muda, umati ulikuwa umetuzunguka Kirsten alipokuwa akilia huku akiwa amemshika mtoto huyo mdogo. Drenda alikuwa akiwaambia watu wote jinsi tulivyopewa mbwa huyo na jinsi Kirsten alivyomwamini Mungu kumpata.

Hapo ndipo nilipogundua kwamba unaweza kuwa na mkutano wa uamsho katika uwanja wa ndege ikiwa tu umembeba mbwa mkononi mwako. Watu wote walitaka kumwona mtoto huyo wa mbwa, na umati kwenye uwanja wa ndege ulikuwa ukilia na Kirsten, hata maafisa wa usalama. Papo hapo, nilihisi kama baba mbaya. Nilipoona shangwe ambayo mbwa huyo ailetta kwa binti yangu na jinsi Mungu alivyompletea mbwa huyo kwa sababu ya imani yake, nilijiuliza kwa nini nilipinga kitu chenye thamani hivi kwake. Shakespeare, jina ambalo alimpa, alikuwa mzuri ajabu. Alifanyika sehemu halisi ya familia. Ingawa alikuwa mbwa mdogo wa kiume aliyejitegemea, alimfuata Kirsten kila mahali alipoenda mchana na usiku.

Ingawa hii ni hadithi ya kugusa moyo, ninataka kuuliza swalii ambalo linahitaji kujibiwa na hakika ndilo kusudi la kitabu hiki. **Mbwa huyo alikujaje?** Sikuwa nimewahi kupewa mbwa hapo awali. Na alikuwaje yule haswa ambaye binti yangu alikuwa ameachilia imani yake kupokea? Je, ilikuwa kibahati tu? La, sivyo. Lilikuwa tokeo la moja kwa moja la Ufalme na sheria zake kuleta mazao katika familia yangu. Ulileta mazao kama vile unavyoweza kufanya wakati wowote ambapo mtu ye yeyote mwenye imani atakapoachilia mamlaka ya Ufalme hapa ulimwenguni. Tunawenza kukiri kwamba ni Ufalme wa Mungu uliomzaa mbwa huyu. Lakini Ufalme ulisababishaje hili? Je, ni sheria gani zilizofanya kazi ili kusababisha hili kutokea? Ninatumai unaposoma kitabu hiki, kutakuwa na majibu yaliyo wazi ambayo yatakusa idia kujua jinsi ya kufurahia Ufalme wa Mungu. Hata hivyo, wewe ni raia wa Ufalme huo na una haki na manufaa za kisheria! Lakini hebu kwanza nikupe mfano mwengine wa Ufalme kutoka kwa maisha ya familia yetu.



## SURA YA 4

# SAMAKI MKUBWA

Drenda na mimi tulipojifunza kuhusu Ufalme wa Mungu na mamlaka tuliyokuwa nayo ulimwenguni, tulifahamu zaidi na zaidi kwamba hakika sisi ndio tunaaoamua jinsi tunavyoishi. Ufalme wa Mungu hugusa kila eneo la maisha yetu, lakini sisi ndio tunaopaswa kuachilia riziki tunayohitaji au kutaka maishani mwetu. Haitokei yenewe tu. Kama yule mbwa mdogo wa binti yetu, hakuna jambo lolote lililo dogo sana au lisilo la maana sana kuleta chini ya utawala wa Ufalme. Tulipogundua hilo, hakika hakukuwa na jambo ambalo halikuwezekana au kuwa nje ya uwezo wetu. Muda mrefu maishani mwangu, sikuelewa hakika kwamba Mungu alitupa Ufalme MZIMA ili tuufurahie. Kwa hiyo tulifurahi kuona Ufalme ukileta matokeo katika kila eneo la maisha yetu, hata maeneo madogo yasiyo muhimu. Mfano mmoja wa jambo hili uko katika hadithi ifuatayo. Ninaiita hadithi ya samaki mkubwa.

Ilitokea wakati familia yetu ilikuwa Alaska katika likizo. Kwamba tuliweza kwenda huko ilikuwa ndoto kwangu. Tulisafiri kwa ndege hadi Anchorage kisha tukakodisha gari kwa wiki tatu halafu tukazunguka sehemu kubwa ya pwani ya magharibi. Ilikuwa nzuri ajabu! Siku moja tulipokuwa tukiendesha gari katika kisiwa cha Kenai, tuliona samaki mkubwa juu ya rafu iliyoning'inia nje ya mashua ya kukodisha. Mashua nyingi kama hii zilikuwa zimeingia; na juu na chini kwa bandari, zote zilikuwa na samaki hawa wakubwa. Ilionekana kama samaki mkubwa aina ya *flounder* (kwa lugha ya Kimombo). Kabla ya wakati huo sikuwa nimewahi kuona samaki aina ya *halibut* (kwa lugha ya Kimombo), na sikujua walionekanaje, lakini walikuwa kubwa. Tulishangaa tulipopita kampuni moja ya kukodisha mashua hadi nyingine, na wote walikuwa na matangazo ya uvuvi wa

siku moja wa samaki aina ya *halibut*. Ghafla, mke wangu alinigeukia na kusema, “Ningependa kumkamata *halibut*, na ningependa kufanya hivyo pamoja na nahodha huyo pale pale.” Alinionyesha ofisi iliyokuwa na kibao cha matangazo ya uvuvi wa *halibut*, na kibao hicho kilikuwa na ishara ya Kikristo ya samaki.

Kwanza nilishtuka! “Unataka kumkamata *halibut*?” Hakuwa anapenda kuvua samaki tangu zamani. Lakini hakubadili mawazo, kwa hiyo tuliingia ofisini humo. Wafanyikazi walikuwa wakimshughulikia mteja mwagine, kwa hiyo tulitazama hapa na pale, tukisoma mambo ambayo watu walikuwa wameweke kwenye ubao wa matangazo. Tuliona matangazo ya mashindano ya kumkamata *halibut* ambayo yalikuwa yakiendelea, lakini yalikuwa karibu kuisha. Kwa kuwa hatukujua ni nini, huenda wewe pia usijue, kwa hivyo hebu nikueleze. Hilo lilikuwa shindano la yeote ambaye angemkamata *halibut* mkubwa zaidi katika mwezi mzima kati ya manahodha wote wenye mashua za kukodisha. Mshindi angepewa hundi na picha yake ingechapishwa kwa gazeti. Mimi na Drenda tulizungumzia kuingia mashindano hayo kwa kuwa tulikuwa tumeamua kuenda kumkamata *halibut*. Walilipisha dola chache tu kuingia mashindano; na hapo ndipo lilipotokea.

Drenda, mke wangu wa kupendeza sana alinigeukia na kusema kwamba alikuwa ameamua kuwa ataibuka mshindi ili biashara ya nahodha huyo ipate kutambuliwa kati ya zingine zote kwa sababu yeye ni Mkristo na Mungu angepata utukufu. Kwa hivyo ilipofika zamu yetu ya kujiandikisha kwenye dawati, Drenda alitamka kwa ujasiri kwamba angeibuka mshindi ili Mungu apate utukufu na biashara yao itambulike kwa sababu ilikuwa biashara ya Kikristo. Bila shaka, kwa nahodha wa mashua, unaweza kufikiria alichofikiria. Kila mtu angependa kuwa mshindi; na nina hakika kwamba alisikia hilo kutoka kwa watalii wengi aliowachukua kuvua. Lakini, sina uhakika kama alikuwa na watu wengi waliotangaza kwamba wangeshinda kwa utukufu wa Mungu.

Hakusema mengi juu ya maneno ya Drenda kuhusu mashindano. Tulipotoka na kuanza kuvua samaki, tulianza kuwakamata *halibut*, na Drenda aliendelea kumuuliza nahodha, ambaye pia alikuwa mwenye mashua hiyo, ukubwa wa *halibut* uliohitajika ili kuweza kushinda. Kila mara alisema kwamba samaki alihitaji kuwa mkubwa kuliko yule ambaye alikuwa amemkamata, jambo ambalo lilimfanya arudie swali hilo hilo kila alipomkamata samaki mmoja. Kwa hiyo Drenda alipomshika samaki mwenye uzani wa kilo 18, nahodha alisema hakuwa mkubwa vyta kutosha. Alipomkamata mwenye uzani wa kilo 31, hakuwa mkubwa vyta kutosha.

Bila shaka, kila mtu anajua jinsi *halibut* alivyo samaki mtamu kula, kwa hiyo tulipanga kumpeleka nyumbani yule tuliyemkamata. Kila mtu aliruhuswi kukamata samaki wawili tu, kwa hivyo tulimchukua yule mwenye uzani wa kilo 31.

Siku iliendelea na sasa jioni ilikuwa imefika. Mwanangu Tom, binti yangu Polly, pamoja na mimi, kila mmoja wetu tulikuwa na *halibut* wawili. Watoto wangu wengine wawili, Amy na Tim, walilazimika kusafiri nyumbani mapema ili kuhudhuria mkutano na hawakuwa nasi. Drenda, alikuwa na samaki wake wa kilo 31, lakini hakuna samaki tuliyekuwa naye ndani ya mashua ambaye angeshinda mashindano. Walakini Drenda alikuwa na imani kwamba angemshika samaki mkubwa. Jioni ilipokuwa ikikaribia, nahodha alituambia sote tuvute nguzo zetu kwa kuwa wakati wa kurudi bandarini ulikuwa umefika. Drenda alipuuza hilo kwa kuwa nahodha alikuwa ameanza kutusaidia kuweka vifaa vyetu. Aliomba dakika chache za ziada huku akitangaza tena kwamba angemkamata *Halibut* ambaye angeshinda mashindano hayo. Nahodha alingoja dakika chache kisha mwishowe akaanza kumsogelea huku akisema, “Samahani, lakini tunahitaji kwenda.”

Kabla tu ya kufikia nguzo yake, ghafla ilivutwa kwenda chini kwa maji. Ni wazi alikuwa samaki mkubwa maana nguzo iliinama na kifaa cha kuvuta kamba ya kuvua kilianza kutoa sauti. Nahodha aliinua nguzo ili kuhisi ukubwa wa samaki na alikubali alikuwa samaki mkubwa lakini alikuwa papa. Alisema alijua kwa sababu ya jinsi samaki alivyovuta nguzo. Naam, Drenda alichukua muda mrefu kumtoa samaki huyo. Alitumia nguvu zake zote kumwinua maana alikuwa futi 300 chini ya maji. Samaki huyo alipotokezea juu ya maji, kila mtu aliona kwamba alikuwa *Halibut* mkubwa sana, mkubwa hata kuliko Drenda mwenyewe.

Samaki alipokuwa akivutwa karibu na mashua, nahodha alisema alikuwa mkubwa sana hangedungwa mkuki tu na kuvutwa ndani ya mashua akiwa bado hai kwa vile angerukaruka; na maana alikuwa mkubwa, angeweza kumjeruhi mtu au kuharibu mashua. Alikuwa na kifaa maalum kilichotengenezewa samaki wakubwa kama hao. Kifaa hicho kilikuwa na sehemu ndogo ambayo, iliposhinikizwa kwenye kichwa cha samaki, ingelipuka na kumuua samaki. Nahodha alipokuwa akisukuma kifaa hicho kichwani mwa samaki na kikalipuka, samaki alishtuka na hilo lilifanya akose kupigwa na mlipuko huo.

Aliposikia sauti ya mlipuko, samaki alijitumbukiza tena moja kwa moja hadi chini kwa nguvu zake zote. Hadi futi 300 kule chini, kifaa cha kuvuta

kamba kwa nguzo kilipiga kelele. Tulihofu kwamba kamba haingeweza kumbeba samaki au kigingi kingetoka kwa samaki wakati alikuwa akipiga mbio kwenda chini. Kwa hivyo ilimbidi Drenda amvute samaki huyo mkubwa juu tena. Alikuwa akipambana kufanya hivyo maana tayari alikuwa ameshindana naye mara moja; kwa hivyo nilimkumbatia, nikashika kamba pamoja naye, na sote wawili tukamrudisha juu polepole. Safari hii nahodha aliweza kuiweka ndani ya mashua ambapo sote tulistaajabia ukubwa wake.

Tulimpeleka samaki mjini ambapo walikuwa na mizani kubwa vya kutosha kumpima. Samaki huyo alikuwa na uzito wa kilo 55 na alikuwa mrefu kuliko Drenda. Mtu aliyempima alisema kwamba, kwa wakati huo, huyo ndiye aliyekuwa samaki mkubwa zaidi kwene mashindano kuisha; lakini wiki mbili zilikuwa zimesalia kabla ya mashindano, kwa hivyo hatungejua kwa uhakika kama samaki wetu angeshinda au la. Lakini hakika siku moja hundi yenye jina la Drenda na nakala ya makala ya gazeti yenye picha yake ilitumwa kwetu. Tulifurahi sana.

Ufalme ulifanya kazi tena! Na tena ninahitaji kuuliza swalii, “Alimkamataje samaki huyo?” Amevua samaki mara mbili tu katika ndoa yetu, na uvuvi sio jambo alipendalo. Bado nilishangaa kwamba alitaka kumkamata *Halibut*. Lakini alikuwa na sababu; alikuwa anataka kumkamata mshindi wa mashindano yale! Na alifua dafu. Tulipokuwa tukimuaga yule nahodha huko Alaska, tulishiriki naye kuhusu Ufalme wa Mungu na jinsi tulivyomkamata yule samaki. Ingawa samaki wetu hakuwa mshindi rasmi siku ile tulipoondoka, alikuwa mkubwa vya kutosha kuvutia watu. Na hata hivyo alilibuka mshindi mwishowe.

Unaweza kufikiri kwamba hadithi yetu, au niseme ya samaki mkubwa wa Drenda inaishia hapo. Najua watu wanafikiri kwamba alikuwa na bahati tu, lakini viyi kuhusu mara mbili? Vema, yapata miaka mitano baadaye, mimi na Drenda tulikuwa tumemwalika rafiki yetu mchungaji kwenda kuvua samaki huko Alaska ili kumkamata samaki aina ya samoni. Hatukuwa tumerudi tangu tulipokuwa huko kwenye safari na familia na tulikuwa tukijaribu kutafuta kisingizio cha kurudi tangu wakati huo. Tulikodisha gari tena na tukapanga kuvua samoni kwa sababu walikuwa wameanza kuelea baharini maana ulikuwa msimu wa kuzaana. Tulipokuwa tukivua, mazungumzo yalikwenda kwenye uvuvi wa *Halibut* na samaki wa Drenda. Rafiki yetu hakuwa amewahi kuvua *Halibut*, kwa hiyo tulisema, “Vema, twende.” Tuliamua kurudi kwa eneo lile lile na nahodha yule yule ikiwa bado alikuwa akifanya biashara.

Tulipokuwa tukielekeea mahali alipokuwa, tuliona hakuwepo tena na

tukafikiri kumtumia nahodha mwingine. Kabla ya kufanya hivyo, tuliamua kuangalia kwa mtandao ili kuona kama tungeweza kupata jina lake, kwa kuwa hatukukumbuka jina la mashua au kampuni yake. Baada ya kutafuta, tuliweza kupata nakala ya makala ya gazeti iliyosimulia kuhusu samaki wa Drenda, pamoja na picha yake ya miaka mitano awali. Ilitaja mashua na jina la kampuni, kwa hivyo tulipiga simu haraka na kupanga mambo. Kampuni ilikuwa bado inafanya biashara lakini ilikuwa imehamisha biashara kama maili tano kutoka mahali ilipokuwa awali.

Tulipokuwa tukiingia ofisini mwao, mwanamke aliyekuwa kwa dawati la kupokea wateja, ambaye ni mke wa nahodha mwenye biashara hiyo, alitazama juu na kusema, “Mshindi wa *Halibut!*” Tulifurahia kuzungumza kwa dakika chache kuhusu yule *Halibut* wetu mkubwa na kuhusu mambo yaliyokuwa yametokea katika miaka ile mitano. Huu ulikuwa wakati wa uchumi kuzorota na biashara haikuwa nzuri. Alisema kwamba watu hawakusafiri na kutumia pesa zao katika uvuvi kama awali, na hilo lilimkatisha tamaa mumewe. Tulimkumbusha kuhusu Ufalme, naye akasema kwamba mume wake hakutamani kumtumikia Mungu.

Tulipokuwa tukiingia kwa mashua, ye ye pia alimkumbuka Drenda na yule samaki mkubwa. Drenda alimwendea na kumuuliza jinsi uvuvi ulivyokuwa, akasema walikuwa wakivua samaki wadogo unapolinganisha na yule waliyempata katika mashindano. Lakini alisema kwamba samaki wakubwa hawakuishi katika eneo alilokuwa sasa kwa sababu lilikuwa na kina kifupi. Alisema alihamisha biashara yake kutoka mahali alipokuwa awali ambapo Drenda alimkamata samaki yule mkubwa kwa sababu naam palikuwa pa kina kirefu lakini palikuwa pamejaa papa. Papa walikula chambo kabla hakijafika chini ndani ya maji, na hilo lilimgharimu sana na alitumia wakati mwingi.

Kwa hiyo tuliuliza walikuwa wakivua samaki wa ukubwa gani katika eneo hilo jipy, naye akasema kwamba hakuwa ameona samaki mkubwa zaidi ya kilo 9 hadi 13 kwa mwezi. Kwa hiyo Drenda alimtzama na kusema, “Sawa, nitakamata mkubwa leo, mkubwa kuliko yule uliyemwona kwa muda mrefu, ili ujue kwamba Mungu ni mwaminifu.” Lakini alimtania tu. Siku nzima tulikamata samaki wa kilo 9 kama nahodha alivyosema, naye aliendelea kumtania Drenda kuhusu “samaki mkubwa” ambaye angevua. Ilikuwa ni marudio ya wakati ule mwingine.

Jioni ilipofika nahodha alituambia tuvute na kurejesha kamba zetu zote kwa nguzo, lakini Drenda hakujali hilo, alisema alihitaji dakika moja au mbili ili kukamata samaki mkubwa. Tena, nahodha alingoja kwa dakika

moja lakini akamwambia kwamba alihitaji kuondoka. Ghafula nguzo ya Drenda ilizama, na ili kufupisha hadithi ndefu, alimshika samaki wa kilo 31. Nahodha alishangaa tena.

Tulipoenda kwenye mkahawa baada ya kuvua samaki, tulizungumza na nahodha mwininge aliyekuwa akila chakula cha jioni huko. Aliposikia kwamba Drenda alimshika samaki wa kilo 31, hakuamini. Ulikuwa katika eneo lipi na umbali gani ndani ya maji? Alitaka kujua tulimkamata samaki huyo mkubwa wapi. Baada ya kuondoka kwenye mkahawa, tulipaswa kurudi kwa ofisi ya yule nahodha wetu wa kwanza ili kutia saini kwa hati ya kusafirisha samaki kwenda nyumbani kwetu.

Kabla ya kuondoka kwa ofisi hiyo, tulipata nafasi nyingine ya kushiriki kuhusu Ufalme wa Mungu. Nilimtazama nahodha na kusema, "Kwa kweli unahitaji kujua jinsi alivyokamata samaki hawa wawili. Sheria za Ufalme hufanya kazi kwa pesa pia." Hapo ndipo tulipokamata usikivu wake, na angalau alivutiwa kidogo. Tulimwachia kitabu changu, *Fixing the Money Thing* kisha tukaondoka.

Je, samaki hawa wawili walitokana na bahati nasibu au yalikuwa matokeo ya sheria ya Ufalme? Wewe amua mwenyewe, lakini mimi na Drenda tayari tuliamua zamani. Kwanzia safari za kwenda kuvua, kutoka kwa madeni, au kuponywa, Ufalme wa Mungu ulikuwa wa kufurahisha na maisha yetu yalibadilika. Wengine wanapata matokeo kama yetu pia. Hapa kuna barua kutoka kwa mwanamke mmoja aliyesikia kuhusu hadithi ya Drenda.

Salamu Gary na Drenda,

Niliwaza kwamba baada ya kusoma kitabu chenu ambapo Drenda alimkamata samaki mkubwa, inanibidi mimi pia nishiriki nanyi Hadithi yangu ya Samaki. Hivi majuzi tulienda likizo na familia hadi Cocoa Beach/ Cape Canaveral, kule Florida. Mume wangu, Robert, alitaka kwenda kwenye mashua ya kuvua kwa bahari kuu akiwa na matumaini ya kurudi kwetu nyumbani Colorado na samaki. Tulikuwa tumepanga safari hiyo kwa miezi kadhaa, kwa hivyo aliponiambia alitaka kwenda kuvua samaki, nilisisimka na kusema, "Twende! Na tumwamini Mungu atuwezeshe kukamata samaki wengi!" Nilimuuliza Bob ni samaki aina gani waliokuwa wakipatikana huko Florida. Kati ya samaki wote alioniambia, nilichagua kuomba na kuamini kumkamata snappa mkubwa mwekundu.

Siku ilifika na tulikuwa tukingoja kupata maagizo kutoka kwa nahodha na wafanyakazi wa mashua. Nilikuwa nikikiri kwamba ningekamata snappa mkubwa mwekundu, kwa hiyo msisimko wangu uliongezeka nahodha

alipokuwa akizungumza. Nilikatishwa tamaa kusikia nahodha akisema kwamba kwa wakati huo samaki pekee ambao hatukuruhusiwa kushika ni aina ya *bass, flounder*, na snappa mwekundu! Doh! Jamani tungeamini kumkamata samaki yupi?

Kwa kweli, sikuacha nafasi hii ya kutumia imani yangu. Nilisema, "Bwana, nimekuwa nikiamini kumkamata snappa mkubwa mwekundu, na iwe hivyo, nitamshika na nitarudi nyumbani na samaki aina moja au nyingine!"

Kwa hiyo tulipokuwa ndani ya mashua, nilimgeukia binti yangu Rachel, mwenye umri wa miaka 8, na kusema, "Kumbuka kwamba unaweza kuomba na kumwamini Mungu kwamba utavua samaki leo. Unaamini?" Alitabasamu na kutikisa kichwa kuafiki. Nilitamka maneno yaleyale ya kutia moyo kwa binti yangu Jordan mwenye umri wa miaka 21. Alinitazama kwa mshangao lakini akakubali. Nilimtazama Bob kisha nikasema, "Jamani tuamini kumshika samaki mkubwa!"

Masaa machache yalipita na hakuna kilichotokea. Kisha ghafla, nguzo ya Rachel ulivutwa chini naye alisisimka sana. Alimwita baba yake amsaidie. Baada ya dakika chache, walipata ni papa wa Atlantiki! Ajabu, Rachel alikuwa ameewela suala la kuwa na imani! Kwa hiyo tulimpongeza. Alikuwa mwanatimu bora zaidi!

Nakumbuka nilianza kufikiria kuwa labda singepata chochote, lakini nilikataa wazo hilo na nikakiri kwamba tayari nilikuwa na samaki wangu. Niliketi na kustarehe kisha nikamsikia Mungu akisema, "Ukistarehe na kuniruhusu nikuletee samaki, utampata." Kweli nilijua sikuwa mvuvi mtaalam, kwa hivyo singweza kutegemea ujuzi wangu mwenyewe. Niliketi chini na kuvuta pumzi ya ujasiri wa Mungu kisha nikasubiri. Baada ya takriban dakika 20-30, kamba ya nguzo yangu iliguswa kidogo; sikufikiri ni jambo kubwa, lakini niligundua ni samaki.

Mume wangu alianza kunifundisha, kisha nahodha akaja kufanya vivyo hivyo. Nilipokuwa nikivuta kamba ya nguzo yangu, aliniambia labda nilikuwa nimemshika snappa mkubwa. Nilishangaa sana kwamba alijua ni samaki aina gani kabla ya kumtoa majini! Na hakika, nilipoendelea kuvuta kamba, samaki wangu mkubwa mwekundu mwenye uzito wa kilo 9 alitokezea! Nilimshukuru Mungu kwa furaha na msisimko mwangi. Nilijua nilikuwa nimepata upenyo katika mfumo wangu wa imani. Sikusahau ujasiri wa Drenda na niliwaza kwamba nilikuwa na uwezo wa kuamini na kuwa na imani kama yake. Niliyahimili kisha nikapata mavuno mazuri.

Asanteni kwa huduma yenu na kwa kuandika vitabu, kikiwemo kile

kiitwacho *The Faith Hunt*. Nina shukrani na ninamshukuru Mungu na huduma yenu ambayo imenisaidia kupata baraka nyingi sana. Ninatazamia siku zijazo kwa imani na furaha zaidi. Ninajua jinsi tukio hili lilivyohudumia familia yetu pia!

Kwa dhati,  
S.T.

## SURA YA 5

# ULIKUWA UAMUZI WA NANI?

Katika hadithi nilizosimulia awali, tuliona Ufalme wa Mungu ukizalisha hapa duniani, mbwa, samaki, pesa za kulipia rehani na kulipia magari na nyumba tulizohitaji, kuokoa maisha ya watoto watatu, na zaidi. Hadithi hizi zote zilikuwa matokeo ya Ufalme wa Mungu, au niruhusu nilifanye zaidi jambo la kibinasi, Ufalme wa Mungu WETU! Hatupaswi kushangaa kwani Ufalme Wake ni mkuu kupita kipimo.

2 Petro 1:3a inasema:

*Kwa kuwa uweza Wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote  
vipasavyo uzima na utauwa.*

Katika hadithi zote tulizozungumzia, nataka kuuliza swali muhimu sana, “Uamuzi ulikuwa wa nani?” Ninachomaanisha ni hiki: je, Mungu aliamua ghafla tu kumleta mbwa huyo kwa Kirsten, au samaki huyo kwa mke wangu, Drenda? Je, haya yalikuwa matukio ambayo Mungu katika ukuu Wake aliamua kutufanya? Au kulikuwa na sababu nyingine ya mambo haya kutokea? Nafikiri jibu litawash tua watu wengi. Najua liliinishhtua.

Ili kujibu swali hili, hebu tuangalie hadithi ya Biblia katika Luka 8.

*Na alipokuwa akienda makutano walimsonga. Na mwanamke  
mmoja, ambaye ametokwa na damu muda wa miaka kumi na miwili,  
[aliyekuwa amegharimiwa mali zake zote kwa kuwapa waganga] asipate  
kuponywa na mtu ye yote, alikwenda nyuma Yake, akaugusa upindo wa*

*vazi Lake; na mara hiyo kutoka damu kwake kulikoma.*

*Yesu akasema, "Ni nani aliyenigusa?" Basi, watu wote walipokana, Petro alimwambia, "Bwana mkubwa, makutano haya wanakuzunguka na kukusonga." Yesu akasema, "Mtu alinigusa, maana naona ya kuwa nguvu zimenitoka."*

*Yule mwanamke, alipoona ya kwamba hawezi kusitirika akaja akitetemeka, akaanguka mbele Yake, akamweleza mbele ya watu wote sababu yake ya kumgusa, na jinsi alivyoponywa mara.*

*Akamwambia Binti, "imani yako imekuponya; enenda zako na amani."*

– Luka 8:42-48

Biblia iko wazi sana kwamba Yesu alikuwa amesongwa kila upande, na hata Petro alishangazwa na swalii la Yesu, "Ni nani aliyenigusa?" Mimi kama mwanasayansi wa kiroho, nilitaka kujua, nilihitaji kujua, kwa nini hakuponywa mtu mwengine ilaa mwanamke huyu. Kwa nini upako ultiririka kwake tu na haukuwa ukitiririka kwa kila mtu mwengine aliyemgusa wakati huo? Jibu liko hapa, lakini kabla sijajibu swalii hilo, tuulize lingine. Je, Yesu alikuwa akimhudumia kimakusudi? Je! Alikuwa ameweuka mikono Yake juu yake? Jibu ni la; hakika, Yesu hakujuwa kwamba mwanamke huyu alikuwa hapo. Ilibidi aulize ni nani aliyevuta upako kwa sababu hakuwa amemwona. Kwa hivyo uamuza ulikuwa wa nani kwamba aponywe siku hiyo?

Subiri nikuulize kwa njia nyingine. Je, ni Mungu aliyeamua kumponya wakati huo au ulikuwa uamuza wake kupokea kutoka kwa Mungu? Hili ni swalii muhimu kwa sababu watu wengi "humngoea" Mungu afanye jambo fulani maishani mwao. Ninaamini kwa sababu Yesu hakujuwa kwamba alikuwa hapo inathibitisha kwamba ulikuwa uamuza wake kupokea wala sio uamuza wa Yesu kumponya.

Sasa, jambo hili linafungua ufunuo muhimu sana, na ndio huu—Mungu haamui kumponya kwa nasibu mtu fulani na si mtu mwengine. Tayari ametupa uponyaji kupitia kwa mahali petu kisheria katika Ufalme Wake. Kwa hivyo ukweli ni kwamba sisi ndio waamuza. Lakini nataka kujua, yule mwanamke alipataje nguvu hizo? "Aliamuaje" kupokea? Yesu alituambia hasa jinsi alivyojingiza katika mamlaka na nguvu za Ufalme. Alimwambia, "Binti, imani yako imekuponya. Enenda zako kwa amani." Sentensi hii

inatuambia kila kitu tunachohitaji kujua na kujibu swalı letu la kwa nini alipokea wala sio mtu mwıngine katika wakati huo. Kama wanasyansi wa kiroho, hebu tuanze kuchunguza hadithi hii kwa ukaribu ili tuone ikiwa tunaweza kupata dalili za jambo hili.

Kwanza kabisa, Yesu alimwita “binti,” kumaanisha kwamba alikuwa raia wa taifa la Israeli. Hiyo ina maana alikuwa na agano na Mungu. Au unaweza kusema, alikuwa na uhalali mbele ya mbingu kama raia wa taifa la Israeli kupokea kutoka kwa Mungu. Ukweli huu hauwezi kuwa sababu pekee ya kumfanya apokee kwa sababu kila mtu pale siku hiyo ambaye alikuwa akimsonga Yesu alikuwa na uhalali huo huo. Lazima kuwe na kitu kingine kilichosababisha nguvu kuachiliwa. Kisha Yesu alitaja sababu moja nyininge. Yesu alisema hiyo ndiyo sababu halisi iliyomfanya apokee binafsi. Alisema imani yake ilikuwa imemponya.

Kwa hiyo sasa tunajua sababu iliyomfanya aweze kupokea. Kwanza, ilikuwa ni haki yake kisheria kupokea kwa vile alikuwa binti wa Ibrahim; na pili, imani yake ilikuwa kibonyezi kilichoachilia nguvu hiyo kutiririka ndani ya mwili wake papo hapo. Kuwa binti wa Ibrahim kulimaanisha kwamba alisimama mbele ya mbingu chini ya agano Mungu alilompa Ibrahim, na inaweza kulinganishwa na kampuni ya umeme iliyowasha umeme na waya zake zimeingia nyumbani kwako, lakini taa zako haziwaki. Lazima ubonyeze kibonyezi pia ili taa ziwake. Kwa hivyo sasa tunachohitaji kujua ni mahali kibonyezi kiko au kibonyezi ni nini. Yesu alitaja imani yake, lakini imani ni nini na nitaiwashaje? Hili ni swalı muhimu linalopaswa kujibiwa.

## **Imani Ni Nini?**

Imani ni neno Wakristo wanaloatumia kiholela. Na ninasadiki kwamba wengi hawajui imani ni nini, kwa nini inahitajika, jinsi ya kujua ikiwa wana imani, na jinsi ya kuipata. Ikiwa imani ndiyo kibonyezi kilichomponya mwanamke huyu, basi tunahitaji kuichunguza imani kwa ukaribu! Tunapata ufanuzi wetu wa imani katika Warumi 4:18–21. Lo, najua unachofikiria, “La, Gary. Waebrania 11:1 ndiyo ufanuzi wetu ya imani.”

*Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.*

—Waebrania 11:1

Naam, hilo ndilo jibu la kawaida, lakini ukichunguza Waebrania 11:1, inatuambia faida za imani, si imani hasa ni nini. Naamini maandiko katika Warumi yatatupa pitcha dhahiri ya maana ya imani.

*Naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate kuwa baba wa mataifa mengi, kama ilivyonenwa, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako. Yeye asiyekuwa dhaifu wa imani, alifikiri hali ya mwili wake uliokuwa umekwisha kufa, (akiwa amekwisha kupata umri wa kama miaka mia), na hali ya kufa ya tumbo lake Sara. Lakini akiiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu kwa imani, akimtukuza Mungu; huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi.*

– Warumi 4:18-21

Hebu tuelewe hali ilivyokuwa katika hadithi hii. Abramu na Sara hawakuwa na uwezo wa kupata watoto. Sisemi walikuwa na shida ya kupata mtoto na walikuwa wakijaribu kupata. Nasema walikuwa karibu miaka 100, na kamwe haingewezekana! Miili yao haingeweza kupata watoto. Lakini Mungu alimwahidi Abramu mtoto ingawa kwa asili haingewezekana

## **“BASI IMANI NI KUWA NA HAKIKA YA MAMBO YATARAJIWAYO, NI BAYANA YA MAMBO YASIYOONEKANA.”**

– **WAEBRANIA 11:1** ikiwa imetulia na kuwa na hakika kabisa kuhusu yale Mungu amesema, ijapokuwa ulimwengu wa asili unaonyesha jambo lingine.

kabisa. Biblia inasema kwamba Abramu alijua hakika kwamba Mungu alikuwa na uwezo wa kufanya yale aliyosema, licha ya mambo ya asili yaliyosema jambo tofauti. Huu hapa basi ndio ufanuzi wetu wa neno imani: “kuwa na hakika kabisa kwamba Mungu anao uwezo wa kufanya kile alichoahidi.” Ninafanua hivi: **Kukubaliana na mbingu**, si kiakili tu bali kusadiki kikamilifu, huku mioyo yetu

### **Ufanuzi Wetu wa Maana ya Imani:**

Imani ni kusadiki kikamilifu kile anachosema Mungu! Ni mioyo yetu na akili kuwa katika makubaliano na mbingu, huku mioyo yetu ikiwa na hakika kabisa, bila mashaka na kutulia.

## Kwa Nini Imani Inahitajika?

Kwa nini Mungu hamponyi kila mtu hospitalini anapotaka? Mbona hakomeshi vita? Kwa nini hatumi malaika watuhubirie Injili? Nina hakika umesikia maswali haya yote hapo awali. Jibu ni kwamba hawez. Sio kwamba Mungu hana uwezo wa kufanya hivyo lakini hana mamlaka kisheria kufanya hivyo. “Gary, unasema kwamba Mungu hawez kufanya chochote anachotaka?” Najua hili linasikika kuwa geni kwako sasa hivi, lakini hebu tuangalie Biblia ili kupata jibu letu kwa hilo.

*Ila mtu mmoja ameshuhudia hivi mahali fulani, akisema,*

*“Mwanadamu ni nini hata umkumbuke, ama mwana wa binadamu, hata umwangalie? Umefanya mdogo punde kuliko malaika, umemvika taji ya utukufu na heshima, umemtawaza juu ya kazi za mikono Yako; umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake.”*

*Kwa maana katika kuweka vitu vyote chini yake hakusaza kitu kisichowekwa chini yake. Lakini sasa bado hatujaona vitu vyote kutiwa chini yake.*

– Waebrania 2:5b-8

Tunaweza kuona katika andiko hili kwamba Mungu alimpa mwanadamu mamlaka kamili ya kisheria juu ya ulimwengu wote alipomweka hapa. Hakuna kitu ambacho hakikuwa chini ya mamlaka yake. Alitawala ulimwengu kwa mamlaka kamili kisheria. Uwezo wake wa kutawala kwa mamlaka uliungwa mkono na serikali iliyomweka hapa. Kimsingi, alitawala na mamlaka aliyokabidhiwa na Ufalme wa Mungu. Alivaa taji la serikali hiyo, ambalo liliwakilisha utukufu wa Mungu, upako, na cheo cha heshima alichobeba.

Ili kupata picha nzuri kuhusu hili, fikiria mfalme wa kiasili. Ingawa yeye ni mtu wa kawaida na hana nguvu halisi katika utu wake, yeye huvaat taji ambayo inaashiria kwamba anawakilisha ufalme mzima na serikali. Maneno yake yana mamlaka kwa sababu yanaungwa mkono na mamlaka na maliasili zote za serikali na ufalme anaowakilisha.

Ukifikiria askari anayeelekeza magari, yeye husimamisha lori kubwa kwa amri, “Simama katika jina la sheria.” Naam, lori ni kubwa zaidi kumliko, na mtu hawez kulinganishwa na lori, lakini lori husimama. Halisimami

kwa sababu yake bali kwa sababu ya beji aliyoivaa, inayowakilisha serikali.

**HII NDIYO SABABU  
MUNGU ANAPASWA  
KUTUMIA WATU  
WALIOJAZWA NA ROHO  
ILI KUTIMIZA MAPENZI  
YAKE KATIKA MAISHA  
YA WANADAMU.**

Katika hali hii, serikali ni kubwa zaidi kuliko mtu mwenye kuvala beji. Dereva wa lori hana hofu ya mtu huyo, lakini ana hofu ya serikali ambayo mtu huyo anaiwakilisha, na hilo linasababisha lori kusimama. Vile vile ni kweli hapa. Adamu alitawala kila kitu kilichoumbwa katika ulimwengu. Nguvu na utawala wa Mungu, uliowakilishwa na taji ya utukufu na heshima, ulimpa mwanadamu uhakikisho wa kwamba maneno yake

yalitawala kwa niaba ya Ufalme wa Mungu.

Ni muhimu sana kutambua kwamba Adamu alipopoteza uwezo wake wa kutawala dunia kwa kufanya uhaini dhidi ya serikali ya Mungu, alipoteza taji lake. Dunia ilichafuliwa na kubadilika. Kifo kiliingia ulimwenguni, na sasa Shetani alikuwa na dai la kisheria la mamlaka na ushawishi katika mambo ya wanadamu. Ni muhimu pia kuelewa kwamba mwanadamu bado ndiye mtawala wa kisheria juu ya ulimwengu, kama Mungu alivyokuwa ameweka, lakini sasa hana mamlaka ya kutawala kiroho kama alivyokuwa hapo awali. Hata katika hali yake ya kutenda dhambi, angali anaisimamia dunia. Naam, hana taji lake la serikali ya Mungu la kumuunga mkono. Hana mamlaka ya kutawala kwa nguvu na utukufu wa Mungu; amepoteza nafasi yake ya heshima. Lakini bado ye ye ndiye mlango pekee wa kisheria katika ulimwengu. Hii ndiyo sababu Mungu anapaswa kutumia watu waliojazwa na Roho ili kutimiza mapenzi Yake katika maisha ya wanadamu. Vivyo hivyo, Shetani hutumia watu waliopuliziwa na roho waovu kuathiri ulimwengu ili kutimiza mpango wake dhidi ya mwanadamu. Kanuni hii ya utawala wa mwanadamu duniani ni muhimu katika ufaamu wako kuhusu sheria ya Ufalme, na mara tu utakapoilewa, itajibu maswali mengi utakayokuwa nayo katika siku zijazo kuhusu kwa nini mambo fulani hutokeea, au kwa nini mambo fulani yalifanyika au hayafanyiki kiroho.

Unaweza kusema, "Lakini nilifikiri kwamba Mungu anamiliki dunia na vyote vilivyomo? Kweli, ndivyo ilivyo. Natumai mfano huu utakusaidia kuelewa ninachosema. Iwapo umekodisha nyumba yangu, ingawa ninamiliki nyumba hiyo kisheria, sina haki ya kuitembelea wakati wowote ninapotaka. Kuna kifungu katika ukodishaji kinachobainisha wakati wenyewe nyumba wanawenza kuingia kihalali katika nyumba lililokodishwa—kwa mfano, kushughulikia hali ya dharura au kufanya matengenezo—na kiasi cha notisi

kinachohitajika. Nikijaribu kuingia nyumbani nje ya mkataba huo, itaonwa kama kuvunja na kuingia, hata kama mali ni yangu. Ikiwa nimekiuka sheria iliyoainishwa katika mkataba wa ukodishaji, basi ninaweza kulazimishwa kisheria kuondoka hata ingawa mimi ndiye mmiliki. Hii inaonyesha sababu Shetani alipaswa kupitia kwa Adamu ili kuingia ulimwenguni. Adamu pekee ndiye aliyekuwa na ufunguo! Shetani alilazimika kupitia kwa mlango na Adamu ndiye aliyekuwa mlango. Ikiwa Shetani angejaribu kutumia njia nyingine ila Adamu, angelazimika kutoka kisheria.

*Akampandisha juu, akamwonyesha milki zote za ulimwengu kwa dakika moja. Ibilisi akamwambia, “Nitakupa wewe enzi hii yote, na fahari yake, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa ye yote kama nipendavyo. Basi, wewe ukisujudu mbele yangu yote yatakuwa yako.”*

– Luka 4:5-7

Unaweza kuona katika mstari huu kwamba Shetani anadai kwamba mamlaka na fahari (utajiri) wa falme za wanadamu amepewa yeye. Nani alimpa mamlaka haya? Yule aliyekuwa nayo, Adamu! Hivyo Mungu hawesi kuingia katika mambo ya wanadamu bila kupitia mlango wa kisheria. Akifanya hivyo, Shetani atadai kufanyiwa hila. La, ilimbidi Mungu apitie mlango uleule amba Shetani alitumia kuleta serikali na mamlaka yake duniani, na mlango huo ni mwanadamu. Lakini kulikuwa na mwanadamu?

*Bwana akamwambia Abramu, “Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha; 2 nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka; nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa.”*

– Mwanzo 12:1-3

Ibrahimu anaitwa baba wa imani yetu kwa sababu yeye ndiye mtu aliyemfungulia Mungu mlango wa ulimwengu ambapo mataifa yote duniani yangebarikiwa. Bila shaka, mstari huu unapozungumza juu ya mataifa kubarikiwa, unazungumza juu ya Yesu Kristo, ambaye baadaye angetengeneza njia kwa serikali ya Mungu kupata kiingilio tena kisheria katika ulimwengu kupitia kwa imani ya Ibrahimu. Imani ya Ibrahimu

## **BASI IMANI, CHANZO CHAKE NI KUSIKIA; NA KUSIKIA HUJA KWA NENO LA KRISTO.**

### **— WARUMI 10:17**

ilifungua mlingo wa kisheria wa mbinguni, ambao Mungu aliufungua wazi kabisa kwa kufanya mapatano ya kisheria (agano) na Ibrahimu na uzao au warithi wake.

Niruhusu nifafanue ninachosema. Serikali ya mbinguni inaweza kuingia ulimwenguni kupitia kwa wanadamu tu kwa sababu wao ndio walio na mamlaka ya kisheria hapa. Sheria hiyo inaweza kutimizwa ikiwa mtu ameshawishika kabisa moyoni mwake kuhusu kile ambacho Mungu anasema (imani).

Njia nyininge ya kufafanua ni kwamba mbingu zinaweza tu kufanya kazi kisheria katika maisha ya mwanadamu ulimwenguni ambaye anatamani na kuchagua kuwa chini ya utawala na mamlaka ya Mungu. Hii ndio kanuni ileile ambayo Shetani alitumia kuingia duniani, akimtumia Adamu kufanya hivyo. Alimsadikisha Adamu kwamba Mungu hangeweza kutegemewa na akautoa moyo wa Adamu katika mapatano na Mungu. Kwa hiyo, Adamu alichagua kumwamini Shetani na kukataa mamlaka ya Mungu.

Hii ndio kanuni ileile ambayo Mungu alitumia kurudisha serikali na mamlaka Yake katika ulimwengu kupitia kwa Ibrahimu. Ibrahimu alimwamini Mungu na mapatano yake yalihesabiwa na Mungu kuwa haki, jambo lilolomaanisha kwamba makubaliano ya kisheria yaliyotakiwa yalikuwepo. Makubaliano haya kati ya Mungu na Ibrahimu, yaliyruhusu Mungu kuweka mkataba wa kisheria (agano) uliohakikisha mbingu zilipata kiingilio ulimwenguni, LAKINI ni muhimu kutambua kwamba mapatano haya yaliathiri Ibrahimu na warithi wake pekee. Ishara ya agano hili ilitolewa kwa warithi wote wa Ibrahimu, ambayo ilikuwa tohara. Tohara ilikuwa ni kukatwa kwa govi kutoka kwa mboo ya kiume. Mwanamume alipopanda mbegu yake ndani ya mwanamke, mbegu yake ilipita katika uume ule uliotahiriwa, ambalo lilikuwa tangazo kwa Shetani na baba na mama wenye kwamba mtoto huyu alisimama mbele ya mbingu kama mrithi wa agano la kisheria ambalo Mungu na Ibrahimu waliratibisha.

Hata hivyo, kama tulivyosoma hapo awali, ingawa kila mtu alikuwa na mapatano hayo ya kisheria, bado alipaswa kutimiza matakwa ya kisheria ya moyo wake kwa kusadiki kabisa yale ambayo Mungu alisema ili kufurahia faida za kibinagsi za mapatano hayo ambayo Mungu na Ibrahimu walifanya. Kimsingi, agano lilipeleka waya hadi nyumbani, lakini bado iliwabidi wabonyeze kibonyezi kwa kuamini kibinagsi na kutenda kulingana na Neno

la Mungu.

Naam, sasa tunajua imani ni nini na kwa nini imani inahitajika kisheria. Sasa ni muhimu kwamba tujue jinsi ya kupata imani na jinsi ya kujua kama tuko na imani.

## **Je, Tunapataje Imani?**

Hapa kuna kidokezo: Huwezi kuomba kupata imani. Umeshangaa? Nilifkiri hivyo.

*Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.*

– Warumi 10:17

Imani huja kwa kusikia Neno la Mungu? Je, hilo tu ndilo linalohitajika? Ni mchakato upi unaohitajika? Je, kusikia Neno ndilo jambo pekee linalohitajika ili imani isitawishwe katika roho ya mwanadamu? Ili kuelewa jinsi imani inavyokuja na kile ambacho Warumi 10:17 inazungumzia, tunaweza kutazama Marko sura ya 4. Ukirusha Biblia yako hewani, inapaswa kutua kwenye Marko sura ya 4; andiko hili ni muhimu hivyo! Yesu alisema katika Marko 4:13 kwamba ikiwa huelewi kile alichokuwa akifundisha katika sura hii, hutaweza kuelewa mfano mwininge wowote katika Biblia. Nasema hilo ni muhimu sana!

Kwa nini sura hii ni muhimu sana? Ni kwa sababu inatuambia jinsi mbingu inavyoingiliana na ulimwengu, jinsi inavyopata uhalali, na mahali hilo linafanyika. Hakuna kitu muhimu zaidi maishani mwako kuliko kujua sura hii yote inazungumzia nini. Unaweza kuuliza, “Ufalme wa Mungu unatendaje kazi?” Soma Marko sura ya 4! Katika sura hii, Yesu alitoa mifano mitatu kuhusu jinsi imani inavyokuja katika roho ya mtu, ambayo kama unavyojua tayari, inahitajika ili kuwezesha mbingu kuingilia dunia kihalali.

Hadithi tatu katika sura hii ni mfano wa mpanzi, mfano wa mtu aliyetawanya mbegu, na hadithi ya mbegu ya haradali.

Hebu tuanze kwa kutazama hadithi ya pili ambayo Yesu alisimulia katika Marko sura ya 4, kuhusu yule mtu alietyawanya mbegu.

*Akasema, “Ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi; akawa akilala na kuondoka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua, asivyojua yeye. Maana nchi*

*huzaa yenye; kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke.  
Hata matunda yakiiva, mara atapeleka mundu, kwa kuwa mavuno  
yamefika.”*

– Marko 4:26-29

Kabla hatujaingia katika kifungu hiki, hebu kwanza tufafanue maneno kadhaa. Yesu alizungumza kuhusu mbegu gani, na nchi ni nini? Yesu alifafanua maneno haya katika mfano uliotangulia wa mpanzi katika sura hiyohiyo. Mbegu ni Neno la Mungu, na nchi ni moyo au roho ya mwanadamu. Kwa hivyo katika mfano huu, kwa kutumia ufanuzi wa Yesu mwenyewe wa maneno haya mawili, tunaweza kusema kwamba Yesu alisema mtu hutawanya Neno la Mungu ndani ya moyo wake mwenyewe. Kisha udongo au moyo wa mwanadamu huanza kuzaa imani (kukubaliana na mbingu) duniani.

Kabla sijaenda mbele, ni muhimu ukumbuke ufanuzi wetu wa imani ni nini: ni moyo wa mtu kusadiki kabisa kile mbingu inasema. Kifungu hiki kinasema kwamba ingawa mwanadamu hajui jinsi mchakato huo unavyofanya kazi, Neno liliopandwa moyoni mwake huanza kukua na kuleta mapatano peke yake. Hii hutokea iwe amelala au yuko macho; haijalishi, mchakato huendelea. Mtu anapoweka Neno moyoni mwake, polepole moyo wake huanza kukubaliana na yale ambayo mbingu inasema, na imani inazalishwa.

Andiko letu katika Marko sura ya 4 linatuambia kwamba moyo huanza kukubali kuitia mchakato fulani. Hadithi inatuambia kwamba mwanzoni wakati mioyo yetu inapokea Neno, imani huanza kukua. Yesu alilinganisha hilo na kukua kwa majani. Kisha majani yakawa suke. Hatimaye, kichwa kikamea kwenye suke, lakini hata hapa hakukuwa na matunda, makubaliano, au mabadiliko katika ulimwengu wa asili. Kisha Yesu alisema mchakato huo uliendelea huku kichwa kikiendelea kukomaa mpaka kikatokeza ngano pevu. Mchakato unapofikia hatua hii ambayo mbegu iliyokomaa iko kichwani, na mapatano na imani zipo, basi mtu anavuna duniani kile ambacho mbingu ilikuwa imepanda ndani ya moyo wake.

Sasa sikiliza kwa makini sana. Tuangalie kile kinachotokea. Mbingu hupanda Neno la Mungu duniani ndani ya moyo wa mtu ambapo makubaliano yanahitajika. Wakati huo, moyo wa mtu huyo bado haujakubaliana na mbingu, lakini mchakato unaofanya moyo kupatana na kile kilichopandwa huanza. Yesu alitumia mfano mzuri kutuonyesha mchakato huu. Yesu alitupa picha ya jinsi mchakato huu wa imani ulivyo

kwa kutumia mfano wa mkulima anayepanda mbegu na jinsi mmea unavyokomaa. Katika ulimwengu wa asili, mbegu iliyo kwa kichwa cha mmea inapokomaa huwa **INAFANANA** kabisa na ile mbegu iliyopandwa ardhini. Hebu nirudie tena.

**Mbegu iliyo kwenye kichwa cha mmea inapokomaa, huwa INAFANANA kabisa na ile iliyopandwa ardhini.**

Ukipanda mahindi, mbegu iliyokomaa katika kichwa cha mmea wa mahindi itafanana ile uliyopanda. Itafanana kwa kila njia, na ladha yake ni ileile. Huwezi kutofautisha mbegu hizo mbili; zinafanana.

Hebu nitumie maneno mengine kufafanua kile Yesu alichosema. Tunaposikia Neno (Warumi 10:17), tunamwaga Neno la Mungu ndani ya mtu wetu wa kiroho au mioyo yetu. Tukiliweka Neno hilo miyoni mwetu, litakomaa na kusababisha picha zilizo katika miyoni yetu (milki ya ulimwengu) kulingana na kile mbingu inachosema. Kwa maneno mengine, tunaweza kusema kwamba unapopanda ahadi kutoka mbinguni ndani ya moyo wako, polepole peke yake itazalisha ujasiri wa kile ambacho Mungu amesema. Hatimaye, moyo wako utashawishika kikamilifu kuhusu kile mbingu ilichosema, na kutakuwa na makubaliano. Kwa mfano, ikiwa unakabiliwa na ugonjwa, mwili wako unazungumza nawe kwamba wewe ni mgonjwa. Unapopanda Neno la Mungu linalosema kwamba Mungu tayari amelipa gharama ya uponyaji wako kuititia yale aliyoyafanya Yesu, moyo wako unaanza polepole kukubaliana peke yake na kile ambacho Mungu amesema.

Neno hilo linapokomaa moyoni mwako, unapata ujasiri wa kuamini na kutangaza kwamba umeponywa. Hutamki bure kile mbingu inachosema bali moyo wako sasa umeshawishika kikamilifu. Unapotangaza, “Nimepona,” sio mfumo fulani unaonukuu; bali hilo ndilo unaloamini na kufahamu kuwa ukweli. Kile mbingu inachosema sasa kinakuwa mtazamo wako mwenyewe wa jinsi mambo yalivyo.

Ndiyo maana Waebrania 11:1 inasema:

*Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.*

Kukiwa na imani, kuna uhakikisho usio wa kawaida wa kile mbingu inachosema, lakini bado kuna hatua nyingine katika mchakato huo.

Sasa lazima mtu atumie mundu wake kuvuna, ili kuleta katika mazingira yake kile hakika alicho nacho moyoni mwake.

*Hata matunda yakiiva, mara atapeleka mundu, kwa kuwa mavuno yamefika.*

– Marko 4:29

Tazama kwamba ingawa moyo umekubaliana na mbingu, na uhalisi wa mbinguni umefanyika uhalisi wa mtu, bado hakujatokea mabadiliko dhahiri ulimwenguni. Kwa sababu mwanadamu ndiye ambaye kwa asili ana mamlaka hapa duniani, ye ye ndiye anayepaswa kuachilia mamlaka hayo ya mbinguni katika ulimwengu huu. Mungu hawezi kufanya hivyo bila mwanadamu. Ninaweza kukuonyesha hilo katika andiko tunalolijua sana ambalo tulizungumzia awali.

*Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa bukiri hata kupata wokovu.*

– Warumi 10:10

Kwa moyo mtu huamini Neno linalozaa imani, kisha anahesabiwa haki. Kupata haki kisheria inamaanisha utendaji kazi wa sheria. Kwa hiyo moyo wa mtu unapokubaliana na mbingu, na kusadiki kabisa kile mbingu inachosema, anahesabiwa haki. Inakuwa halali sasa kwa mbingu kutiririka katika maisha yake ulimwenguni. Lakini kuahesabiwa haki pekee hakuachilii nguvu za Mungu. Kama nyumba iliyvo na umeme unaotoka kwa kituo cha umeme, kuna hatua moja zaidi—kubonyeza kibonyezi ili kuachilia nguvu za umeme kisha taa zinawaka. Kwa nini? Kwa sababu kama Warumi 10:10 inavyosema, kuna hatua moja zaidi baada ya kuahesabiwa haki.

Mtu anayesimama mbele ya mbingu na dunia akiwa amehesabiwa haki lazima basi akiri au achukue hatua kulingana na makubaliano hayo ili kuachilia nguvu na upako wa Mungu katika ulimwengu. Tafadhali soma andiko hilo tena na tena mpaka uelewe kabisa ninachosema. Hivi ndivyo inavyofanya kazi! Hivi ndivyo mbingu inavyopata uhalali katika ulimwengu, moyo ukiwa kiingilio cha mbingu katika ulimwengu, na maneno na matendo yetu yakiwa kibonyezi kinachoachilia nguvu za mbinguni. Tafadhali zingatia kwa makini sehemu ya pili ya mstari huo tena: Sisi ndio tunaopaswa kuachilia mamlaka ya mbinguni hapa.

Wazo la mbingu kumngaja mtu ili kwanza kabisa atoe uhalali, na pili, aachilie mamlaka katika ulimwengu, liko dhahiri katika kile Yesu alichofundisha katika Mathayo 16 na 18.

*Amin, nawaambieni, yoyote mtakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yoyote mtakayoyafungua duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni.*

– Mathayo 18:18

Yesu alisema hapa kwamba angelipa kanisa funguo (mamlaka) za

**HIVI NDIVYO MBINGU  
INAVYOPATA UHALALI  
KATIKA ULIMWENGU,  
MOYO UKIWA KIINGILIO  
CHA MBINGU KATIKA  
ULIMWENGU, NA MANENO  
NA MATENDO YETU  
YAKIWA KIBONYEZI  
KINACHOACHILIA  
NGUVU ZA MBINGUNI.**

Ufalme wa mbinguni katika ulimwengu. Alisema chochote utakachofunga au kufungua duniani mbingu zitaunga mkono. Tena tafakari afisa wa polisi; ye ye ana mamlaka, lakini serikali ina nguvu. Afisa wa polisi ndiye anayeshikilia ufunguo au mamlaka ya serikali, maana aliapishwa kuwa mwakilishi wa serikali hiyo. Serikali inaunga mkono anachosema. Kumbuka ni mwanadamtu aliye na mamlaka ya kisheria hapa, na hivyo ndiye pekee anayeweza kuipa mbingu mamlaka ya kisheria hapa.

Kuna suala lingine muhimu zaidi unalohitaji kufahamu kuhusu imani. Hebu nirejelee andiko letu katika Marko sura ya 4 kwa muda mfupi.

*Maana nchi buzaa yenyeze; kwanza jani, tena suke, kisha ngano peru katika suke.*

– Marko 4:28

Kumbuka, Yesu alifafanua udongo unaotajwa katika mfano huu kama moyo au roho ya mwanadamtu, kama nilivyotaja hapo awali. Tazama mahali ambapo imani huzalishwa; hilo linakushangaza? Imani haitoki mbinguni, kama watu wengi wanavyoamini, bali ni zao la moyo wako hapa duniani. Huwezi kumwomba Mungu akupe. Imani haihitajiki mbinguni maana hatuhitaji makubaliano huko. La, inahitajika hapa ulimwenguni tu, na inapaswa kuzaliwa katika mioyo ya wanadamtu duniani. Kama mfano katika Marko 4 unavyofundisha, kuna njia moja tu ya kuipata, kwa kuweka Neno la Mungu moyoni mwako na kuruhusu mchakato wa makubaliano ufanyike. Kwa hivyo ikiwa ninahitaji imani, ninapaswa kufanya nini? Kutawanya Neno la Mungu moyoni mwangu na kuliacha likue mpaka

imani ikuwepo. Hiyo ndiyo njia pekee imani huja.

Kabla sijatoka kwa Marko 4, nataka kuzungumzia tena mundu uliotajwa hapo.

*Hata matunda yakiiva, mara **atapeleka mundu**, kwa kuwa mavuno yamefika.*

—Marko 4:29

Ninaamini waumini wengi duniani hawajafundishwa jinsi ya kutumia mundu, kumaanisha kwamba hawajafundishwa jinsi ya kuvuna kile wanachohitaji. Kanisa kwa ujumla limefundishwa jinsi ya kutoa matoleo lakini sio jinsi ya kupalilia na kuvuna kutoka kwa mbegu waliyoipanda. Yesu alisema wazi katika mstari huu kwamba mavuno ya imani yetu yanapopatikana, ni lazima tutumie mundu. Hata iwe tumefanya kazi nzuri ya kuachilia mbegu zetu kwa imani, tusipojua kutumia mundu, hakutakuwa na mavuno. Kusema kweli, sikujua lolote kuhusu hili hadi Bwana alipoanza kunifundisha jinsi Ufalme unavyofanya kazi. Niruhusu nikupe mifano michache ya jambo hili.

Nilialikwa kuhubiri katika kanisa fulani huko Atlanta. Ilikuwa ibada ya Jumatano jioni na kanisa halikuwa kubwa vile, lakini hilo lilikuwa sawa kwangu. Nilipenda sana kufundisha watu kuhusu Ufalme. Nilipofika kanisani, nilistaajabu kwamba milango ilikuwa imefungwa na hakukuwa na mtu pale. Ilikuwa dakika kumi kabla ya ibada kuanza. Kisha nikasikia mlion wa gari kubwa sana nyuma yangu; ilionekana kana kwamba haikuwa na kifaa cha kupunguza sauti hata kidogo. Nilipotazama nyuma, niliona gari kuukuu, bovu, likiingia kwa kichochoro kilichoolekea kanisani. Sikufikiria chochote kuhusu hilo maana nilikuwa jijini. Nilipokuwa nikingoja, mwanamume mmoja alikuja kutoka nyuma ya jengo na kujitambulisha kuwa yechelewa kwa sababu gari lake kuukuu lilikataa kuwaka. Aliniambia ilimbidi aanzishe gari kwa mteremko kwa sababu kibonyezi cha kuwasha gari kilikuwa kimeharibika. Alisema mara nyangi gari lilikataa kuwaka kabisa, na ilimlazimu atembee maili tano hadi kanisani.

Alipoendelea kunieleza kuhusu kanisa lake, aliniambia kwamba ingawa alikuwa mchungaji wa kanisa hilo, kazi kuu ya kanisa ilikuwa kulisha maskini jijini. Walilisha zaidi ya watu 10,000 kwa mwezi mahali hapo. Mchungaji alipokuwa akizungumza, nilijawa na fadhaha. Huyu ni mtu wa Mungu anayelisha watu 10,000 kwa mwezi, lakini hana hata gari la

kutegemewa? Alikuwa picha pekee ya Mungu ambayo wengi wa watu hao aliowalisha wangewahi kuona. Ikiwa walimwona akisongwa na shida, huku akilazimika kutembea maili tano katika siku ya kiangazi yenyе digrii 37 kwenda kanisani, wangekuwa na uhakika gani kwamba Mungu angeweza kuwasaidia? Niliamua kushughulikia hitaji hilo. Nilikuwa na gari mpya nyumbani iliyokuwa imesafiri maili 20,000 pekee ambayo ningempa. Nilimweleza kuhusu mpango wangu na kwamba ningemtuma mmoja wa wafanyakazi wangu Atlanta ili amletee gari. Yeye, bila shaka, alifurahia sana. Jioni hiyo nilimfundisha pamoja na kanisa lake dogo kuhusu Ufalme wa Mungu na jinsi unavyofanya kazi inapohusu fedha.

Niliporudi nyumbani, nilipanga gari liendeshwe hadi Atlanta. Wakati mfanyakazi wangu alikuja nyumbani kwangu kuchukua gari, nilifahamu nilikuwa ninafanya shughuli ya kiroho mbinguni. Nilijua kwamba nilipoachilia gari hilo katika Ufalme wa Mungu, ningeweza kumwamini Mungu kupata gari nililohitaji pia. Mimi sio mtu wa magari, maana yake sipendi magari sana. Kuna watu wanaopenda magari sana, lakini si mimi. Gari ni chombo tu kwangu. Bila shaka napenda kuwa na gari zuri, lakini huwa ninaziendesha hadi zitakapohitaji kubadilishwa.

Mfanyikazi wangu alipopitia, nilienda kwenye karakana yangu, na kuwekelea gari hilo mikono yangu na kusema, “Baba, ninaachilia gari hili lifanye kazi ya huduma Yako, na ninapoliachilia, ninapokea gari...” Nilisita. Ninajua jinsi Ufalme wa Mungu ulivyo mahususi, na nilijua kusema neno “gari” tu haingefua dafu. Pia nilifahamu nilipaswa kuwa mahususi na kwamba mimi na Drenda tulihitaji kukubaliana kuhusu jibu hususa ambalo tungepokea. Nilipokuwa katikati ya mazungumzo yangu, niligundua pia kwamba sikujua ni aina gani ya gari nililotaka. Kwa hiyo nilianza tena, “Bwana, leo ninaachilia gari hili kwenye huduma Yako, na ninaamini nitapokea gari zuri sana ninapotoa hili, lakini itabidi nirudi kwako kuhusu aina ninayotaka nitakapojuwa hilo.” Tosha gari; gari liliondoka. Kwa kweli sikuwa na aina yoyote ya gari akilini ambayo ningeweza kusema, “Naam, nataka gari FULANI.”

Miezi michache ilipita. Drenda alikubaliana nami kuhusu kutoa gari na, kama mimi, hakujua ni aina gani ya gari alilotaka. Kwa kipindi cha miezi miwili iliyofuata tulizungumza kuhusu magari, na hatimaye siku moja alisema, “Wajua nini, nafikiri ningefurahia kuwa na gari ambalo linawenza kuendeshwa sehemu ya juu ikiwa wazi.” Nilimwambia nilikubaliana na hilo, na nikasema nilifikiri hilo likuwa jambo la kufurahisha, lakini gari aina gani? Tena, hatukujua ni gari aina gani tulivoitaka hasa. Lakini siku

moja tulipokuwa tukienda kula chakula cha mchana, mke wangu alisema ghafula, "Ndio ile!" "Ni nini?" Nikasema. "Ndio ile," alisema huku akiashiria kwa kidole sehemu ya maegesho ya mkahawa amba tulikuwa tumeingia. "Ni nini?" Nikasema. "Hilo ndilo gari ninalotaka!" Kisha nikaona gari hiyo kwenye eneo la maegesho. "Twende tuone ni aina gani," nikasema. Kwa hiyo tulienthesha gari hadi kwenye gari hilo na kusimama nyuma yake.

Naam, si ajabu tulilipenda. Lilikuwa gari aina ya BMW 645Ci, la kifahari, na bei kubwa sana. Kusema kweli, nilipoona lile gari, niliwaza, "Sawa, Bwana, tuonyeshe cha kufanya." Nilijua singelipa \$115,000 ili kununua BMW mpya, lakini pia nilijua kwamba Mungu anaweza kufanya mambo ya ajabu. Mimi na Drenda hatukumwambia mtu yejote kuhusu gari hilo wala kumtajia mtu yejote kuwa tunatafuta gari.

Baada ya karibu wiki mbili, kaka ya Drenda alitupigia simu na kusema, "Nimepata gari la Drenda!" "Unamaanisha nini umepata gari la Drenda?" Nikasema. "Niliona gari likiuzwa, na ghafla, nikahisi kwamba linapaswa kuwa gari la Drenda; na ilinibidi nikwambie kulihusu," Akasema. "Ni gari aina gani?" Nikauliza. "Ni BMW 645Ci, na liko katika hali nzuri kabisa. Lina umri wa miaka miwili, halijasafiri sana, wala halina mkwaruzo juu yake. Ni kamilifu kabisa. Zaidi ya hayo, unamjua mtu anayeliuza." "Kweli?" Nikasema. "Ndio," akajibu; "Na unapaswa kumpigia simu mtu huyo." Aliponiambia muundo na aina ya gari hilo, huku nikiwa na ufahamu kwamba hilo ndilo gari tulilipenda mimi na Drenda wiki chache awali, nilijua kwamba Mungu alikuwa na kusudi fulani.

Nilimpigia simu mwenye gari. Ndio, nilimfahamu, na tulizungumza kidogo juu ya gari, na alikuwa akiniambia jinsi gari hilo liliyokuwa katika hali nzuri. Kisha akaniambia maneno haya. "Wajua, tangu tuanze kuzungumza kwa simu kuhusu gari hili, nahisi kama linapaswa kuwa gari la Drenda." Sikuwa nimemtajia hata kidogo kwamba nilikuwa ninatafutia Drenda gari. Kisha mtu huyo akasema, "Nitakwambia nitakachofanya, nitakuuzia kwa dola 28,000." Masikio yangu hayakuamini kile nilichokuwa nimesikia. Gari lilikuwa na thamani kubwa kuliko hiyo. Nilipomwambia Drenda kuhusu hilo, alifurahi sana. Tulilipia gari hilo pesa taslimu na bado tuko nalo hadi leo. Bado linaenda sawa na linaonekana vizuri. Bado halina mkwaruzo juu yake, na tumeliendesa mara nyingi sehemu ya juu ikiwa wazi, huku radio yake ikicheza muziki kwa sauti kubwa, na jua likiwaka juu yetu kuondoa uchovu wa siku.

Safari tulioipenda zaidi kwa gari hilo la kifahari ilikuwa katika milima ya Colorado, huku tukiwa na vifaa vyetu vyaa kupiga kambi kwenye

lori. Binti yetu Kirsten alikuwa nasi katika safari hiyo, na ninakumbuka nikiendesha gari kuptia jimbo la Kansas kwenye barabara kuu ya I-70 usiku huku sehemu ya paa ya gari ikiwa imetolewa. Kirsten alikuwa amelala kwenye kiti cha nyuma huku nikiendesha gari. Nyota ziling'aa sana juu ya vichwa vyetu, na barabara ilikuwa wazi isipokuwa lori moja au mbili mara kwa mara. Ulikuwa mojawapo wa usiku mwema ambapo hewa ilikuwa safi na kila kitu ulimwenguni kilikuwa ajabu. Tulitumia wiki mbili zilizofuata kuendesha gari milimani, na nikatambua jinsi lilivyokuwa gari la ajabu. Ni maneno machache tu yanayoweza kueleza wakati wetu huko—Ajabu kupita fahamu!

Lakini swalii muhimu ni hili. Gari hili lilikujaje kwetu? Kwa nini lilikuwa gari haswa ambalo Drenda alisema, “Ndilo hilo!” Nilifahamu kwamba Ufalme wa Mungu ulileta gari hilo maishani mwetu. Nilijua kwamba nilipotoa gari langu kwa mchungaji yule, nilikuwa nimetumia sheria ya kiroho. Nakumbuka sikutaja muundo wa gari ambaa ningependa kupokea bali nilisema ningepata gari kubwa na nzuri. Lakini ilitubidi mimi na Drenda tutumie mundu. Gari hili halingkuja ikiwa hatukusema, “Ndilo hilo!” Ingawa nilikuwa na imani nilipoachilia gari langu, hatukuwa tumetumia mundu hadi Drenda aliposema, “Ndilo hilo.”

Tukio lingine lilitokea ambalo lilidhihirisha kanuni hii kwa njia kubwa zaidi. Kama unavyojuu, napenda kuwinda. Ninaishi katika eneo zuri sana la uwindaji, na nimebarikiwa kumiliki ardhi yangu ya kuwinda. Katika ekari zangu 60, nina takriban ekari 19 za msitu na 10 zenye kinamasi. Mimi huwa na mafanikio makubwa katika uwindaji wa kulungu na kindi kila mwaka. Kila wakati huwa kuna bata na bata bukini wanaorukaruka hapo, lakini kwa sababu moja au nyingine, sikuwa nimewahi kufikiria kuwawinda hata kidogo. Mara moja au mbili katika miaka mingi, mimi na vijana wangu tumeenda kwenye bwawa na kupiga risasi bata bukini wachache ili kuwala jioni. Lakini hatukuwa tumewahi kuwinda bata kweli.

Sasa miaka michache iliyopita, nilipokuwa nikitazama bata kadha wa kadha wakiruka na kuingia kwenye kinamasi, niliwaza kujaribu kuwawinda. Ajabu, ilisisimua sana! Nilipata uraibu wa kuwawinda. Katika msimu huo wa vuli wa kuwinda bata, nilitambua kwamba nilihitaji mazoezi mengi ya kuwapiga bata risasi. Nilifanikiwa kubeba kadhaa na kupata kwamba walikuwa watamu sana kula. Niligundua kwamba mara nyingi sikuwa nawaua kwa sababu walikuwa mbali au bunduki yangu haikuweza kuwafikia. Nilikuwa nikitumia bunduki yangu ya kawaida aina ya Remington 11-87, ambayo nilitumia kuua kila kitu iwe sungura au kulungu. Usielewe vibaya,

ninaipenda bunduki hiyo, na ni bunduki nzuri sana. Lakini nilikuwa nimesikia kulikuwa na aina mpya za bunduki zilizotengenezwa kwa ajili ya kuwinda bata pekee. Haikuwa rahisi kuzipata lakini zilikuwa na nafasi ya kubeba risasi zenye urefu wa inchi tatu na nusu, jambo ambalo nilijua lingesaidia nilipohitaji kufyatua risasi mbali. Niliamua kutafuta moja ya hizo kabla ya msimu mwingine wa kuwinda bata kuanza.

Msimu wa bata ulikuwa umekwisha, sasa ilikuwa Januari, na nilikuwa nikipitia duka linaloitwa Cabela's ambalo linauza vifaa mbalimbali na nikafikiri kuptia sehemu yenye bunduki ili kuona jinsi bunduki hizo zilivyoonekana. Nilipoingia kwenye sehemu yenye bunduki, niliona kwamba walikuwa na sehemu nzima iliyotengwa kwa ajili ya bunduki za kuwinda bata pekee. Nilichunguza chache na nikataka kununua ile niliyopenda, lakini ilikuwa \$2,000 na msimu wa kuwinda bata ulikuwa umesalia miezi kadhaa. "Nitasubiri," nilijiwazia. Lakini nilifanya jambo lisilo la kawaida nilipokuwa karibu kuondoka. Kwa kweli sikutambua nilichokuwa nikifanya wakati nilipokifanya. Nilikifanya bila kufikiria. Nilielekeza kidole kwa bunduki niliyoitaka kisha nikasema kwa sauti. "Nitakuwa na bunduki hii, katika jina la Yesu." Sikufikiria jambo hilo sana; nilikuwa nikitangaza tu kwamba ningekuwa na bunduki hiyo. Moyo wangu ulikuwa na picha dhahiri ya bunduki ya bata niliyoitaka.

Baada ya majuma machache nilialikwa kuhubiri katika kongamano la biashara, na jambo fulani lilitokea huko ambalo lilivutia umakini wangu. Baada ya kuhubiri, mwenye kampuni alinijia na kusema walitaka kunipa zawadi ili kunishukuru kwa kuja. Alisema, "Tulijua unapenda kuwinda, kwa hivyo tulikununulia bunduki hii." Nilipigwa na butwaa walipotoa bunduki mpya aina ya Benelli ya kuwinda bata, kama ile niliyoona pale dukani, na kuielekezea kidole! Je, unaona hili?

**...MUNGU ALITAKA  
TU KUNIONYESHA  
KWAMBA ANANIPENDA.  
ALINIONYESHA  
ANANIPENDA  
ALIPOMTUMA YESU KWA  
AJILI YANGU NA KUNIPA  
UFALME!**

Je, bunduki hiyo haswa ilikujaje? Nilikuwa nimetoa bunduki nyingi kwa miaka mingi lakini sikuwa nimewahi kutumia mundu. Kwa maneno mengine, nilikuwa nimetoa bunduki hizo kwa imani na ukarimu lakini sikuwahi kutumia mundu. Sikuwa nimewahi kusema, "Bwana, ndiyo hiyo! Hiyo ndiyo ninayoitaka." Lakini mara tu nilipofanya hivyo, mavuno yalitokea!

Nilikuwa nikimsimulia rafiki yangu

mhudumu kuhusu hadithi hii ya bunduki. Alisema, "Naam, nafikiri Mungu hufanya hivyo wakati mwingine. Yeye hutubariki na zawadi ndogo maalum ya kutuambia anatupenda." Nilipotafakari kile alichosema, nilitambua, "La, hilo halikuwa sahihi. Ndio, Mungu ananipenda, lakini hataki tu kunishangaza na zawadi ndogo." Mbwa, samaki, kulungu waliokuja kwa mpangilio huo, magari, na yote yaliyokuwa yamekuja haikuwa kwa sababu Mungu alitaka tu kunionyesha kwamba ananipenda. Alinionyesha ananipenda alipomtuma Yesu kwa ajili yangu na kunipa Ufalme!

Nataka kukusimulia hadithi moja nydingine kuhusu mavuno. Kama nilivyokuambia, mimi si mtu wa magari. Tunaziendesha hadi zinapohitaji kubadilishwa. Mfano ni gari letu aina ya Honda Pilot lenye umri wa miaka minane. Tunapenda gari hilo, ni muhimu, linafanya kazi vyema, linaonekana jipy, na hivyo tunakaa nalo. Lakini mara nyigi tulifirkiria kununua gari kubwa zaidi ya kubeba abiria na wageni. Hivi karibuni, tulikodisha gari aina ya Cadillac Escalade katika moja ya kongamano tulizoandaa kwa jengo letu, na mimi na Drenda tuliliendesha kila mahali. Tulilipenda.

Tulipenda rangi yake, na muundo wake mfupi kama ile tulikuwa tukiendesha badala ya Escalade ndefu. Tulisema, "Hili ndilo gari tunalolitaka, Cadillac Escalade, lenye rangi hii, na muundo mfupi. Tunahitaji kununua gari kama hili." Maisha yalikuwa na shughuli nyigi na kwa kweli bado hatukuwa na wakati wa kutafuta na kufikiria kununua.

Baada ya karibu mwezi mmoja, nilikuwa nimetoka nje ya mlango wangu wa mbele nyumbani ili kuchukua gazeti langu la asubuhi, kisha simu yangu ya rununu ikalia. Mtu akasema, "Habari Mchungaji, nataka kukununulia Cadillac Escalade; unataka rangi gani? Nilipigwa na mshtuko, nikasema, "Ajibu, hilo ni jambo nzuri. Mimi na Drenda tunapenda gari lenye rangi nyeupe ya lulu." "Sawa," akasema, "acha nitafute nione lile nitakaloweza kupata." Katika msisimko wangu, nilisau kumwambia kwamba tulipenda zaidi muundo mfupi. Kusudi lake lilikuwa ni kutafuta gari lenye umri wa mwaka mmoja au miwili lenye muundo mkamilifu na lenye maili ya chini sana.

Hatukusikia kutoka kwa mtu huyu kwa karibu mwezi mmoja kisha hatimaye alipiga simu na kusema, "Nina gari lako aina ya Escalade; njoo tukutane wakati fulani mahali fulani, na unaweza kwenda nyumbani nalo." Kwa hivyo tulikutana naye na alikuwa na gari aina ya Escalade yenye muundo mfupi na rangi nyeupe ya lulu. Jamani lilipendeza! "Samahani ilichukua muda mrefu kurejea kwako," alisema. "Nilijaribu sana kupata muundo mrefu lakini zinahitajika sana hawakuwa nazo. Nilipata muundo

mfupi tu. Natumai hiyo ni sawa.” Sawa? Hilo ndilo tulilotaka na ndivyo tulivyosema!

Tena, ninauliza swali: Je, gari aina ya Escalade ambalo tulitaka haswa lilitujaje? Kwanza kabisa, nimetoa magari nane mbali na gari nililompa mchungaji niliyetaja hapo awali. Lakini sikuwa nimewahi kusema, “Ndilo hili!” kuhusu gari awali hadi Drenda alipofanya hivyo na ile BMW. Sasa, tena, mimi na Drenda tuliafikiana na kusema kwa sauti, “Ndilo hili!” Nimesema kwa miaka mingi kwamba kanisa limefanya kazi nzuri sana ya kufundisha juu ya kutoa lakini kazi mbovu kuhusu jinsi ya kuvuna. Kwa hiyo unaweza kutambua mundu ni nini kutoka kwa hadithi nilizosimulia awali? Natumaini ni dhahiri! Nilikuwa nimetoa magari mengi kwa imani huku nikitarajia kupata mengine, lakini mimi na Drenda hatukuwa tumekubaliana kuhusu gari jipy. Tena, tulipenda kuendesha magari yetu kwa muda mrefu. Lakini mara tu tuliposema, “Ndilo hili!” lilijitokeza. Mundu ni maneno yetu!

*Mauti na uzima huwa katika uwezo wa ulimi; na wao waupendao watakula matunda yake.*

– Mithali 18:21

Kulikuwa na msimu ambao kanisa lilionekana kufundisha sana kuhusu maneno yetu. Nimekuwa pamoja na watu, na labda wewe pia, ambao wanasema jambo fulani kisha wanafunika midomo yao na kusema, “Ninahitaji kuchunga maneno yangu.” Hiyo inaonekana kama kazi nzuri, na ninakubali kwamba itasaidia kuweka Neno moyoni mwako. Walakini, kuchunga maneno yako kwa kweli hakuna uhusiano wowote na mundu. Eti nini? Lakini nilifikiri umesema mundu ni maneno yetu. Ndio, lakini kujua jinsi ya kutamka maneno sahihi pekee sio jambo muhimu.

*Amin, nawaambia, Yeyote atakayeuambia mlima huu, Ng’oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake.*

–Marko 11:23

Tena, mundu katika Marko sura ya 4 ni maneno yako! Marko sura ya 4 inapozungumzia mundu, tayari imezungumzia mchakato wa imani na jinsi ya kuipata. Inasema mbegu inapokomaa unatumia mundu kwa kuwa mavuno yamekuja. Mavuno yamekuja kwa sababu uko na imani kwa

kukubaliana na mbingu moyoni mwako. Aya hii ya Marko 11 inadhihirisha kanuni hiyo hiyo. Moyo wako unaamini Neno, kisha unatamka na kuachilia mamlaka ya mbinguni. Lakini tazama maneno haya, “*aamini kwamba hayo asemayo yametukia.*” Kujaribiwa katika imani kunadhihirisha ikiwa unaamini unachosema. Kutamka au kukiri Neno la Mungu pekee sio imani. Moyo wako usipokubaliana na mbingu, unaweza kukiri mpaka uchoke wala hakuna kitakachotokea. Kwa hiyo je, tunapaswa kuchunga maneno yetu au miyo yetu?

*Mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake hutoa yaliyo mema, na mtu mwovu katika hazina mbovu ya moyo wake hutoa yaliyo maovu; kwa kuwa mtu, kinywa chake hunena yale yaujazayo moyo wake.*

– Luka 6:45

*Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo; maana ndiko zitokako chemchemi za uzima. Kinywa cha ukaidi ukitenye nawe, na midomo ya upotovu uiweke mbali nawe.*

– Mithali 4:23-24

Tunaweza kuona wazi kwamba yale tunayosema yanatoka moyoni mwetu na yale tunayoamini. Kwa kufuata mchakato katika Marko sura ya 4, tutajua jinsi ya kubadili kile ambacho miyo yetu inaamini na kukifanya kipatane na mbinguni katika imani. Kisha tutakaposhawishika kabisa, itatubidi tutumie mundu ya maneno na matendo yetu. Umeelewa? Vema, tuendelee.

Tunapoendelea na mjadala wetu juu ya imani, nataka kuuliza swalı ambalo lazima uweze kujibu.

## Nitajuaje Kama Kweli Niko Na Imani?

Hili ni swalı zuri ambalo unapaswa kufahamu kwa sababu haiwezekani kuomba maombi ya imani bila kuwa na imani kwanza. Kuna njia nyingi za kujua ikiwa uko na imani au la, na dalili nyingi unazohitaji kujua na kutafuta. Wakati hauna imani unaweza kufanya maamuzi mengi yasiyofaa kwa sababu ya hofu. Maamuzi yanayotokana na hofu kila mara yatakufanya uwe mateka chini ya laana ya dunia na kukufanya ukose kile Mungu anachokutakia. Kwa hivyo ishara ya kuwa na imani ni nini? Ya kwanza ni rahisi; unaweza kutazama nyuma katika ufanuzi wetu wa imani na

kuelewa kwamba kusadiki kikamilifu moyoni mwako ni jambo muhimu. Lakini mara nyingi huwa tunafikiri kwamba tumeshawishika lakini tunakubaliana tu katika akili zetu na Neno wala sio mioyo yetu. Unahitaji kuwa na uwezo wa kutofautisha. Unaposadiki kikamilifu, bila shaka kuna mapatano ya kiakili na yale ambayo Neno linasema lakini pia ufahamu wa hakika, na ujasiri unaoleta amani na matarajio.

*Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.*

– Waebrania 11:1

Ikiwa una ushahidi kwamba una kitu fulani, je, bado unahitaji kuhakikishiwa kwamba unacho? La hasha. Ukiwa na imani, kuna ufahamu, amani, na ujasiri kwamba una kile ambacho Neno la Mungu linasema, hata ingawa hujakiona. Watu wengi husema hivi: “Ninajua kwamba ninacho.” Ufahamu huu unatoka ndani yetu na sio kutoka kwa jinsi hali zilivyo. Uko rohoni au moyoni mwako. Hofu inatoweka, hakuna tena mawazo sumbufo ya wasiwasi yanayoshambulia akili yako; unajua yote yamekamilika.

Kipengele kingine cha kuwa na imani ni furaha na matarajio. Jibu lako limekuja. Unalo! Imani ni zaidi ya hisia ya amani au ujasiri, ingawa utakuwa na yote mawili. Unapaswa pia kuwa na uwezo wa kutetea msimamo wako kiroho. Ninaposema hivyo, tafakari mahakama ambapo wewe ni wakili anayemhoji shahidi. Kwa nini unaamini kile unachokiamini kuhusu hali yako? Ungeteteaje msimamo wako? Kuna jibu moja tu, nalo ni Neno la Mungu.

Kwa mfano, mtu akija nyumbani kwako na kusema, “Ondoka nyumbani kwangu,” je, utasema, “Samahani; tupe siku moja, nasi tutaondoka?” La, hutafanya hivyo; labda utacheka. Mtu huyo akisema, “La, hii ni nyumba yangu; toka la sivyo tutaonana mahakamani,” jibu lako litakuwa, “nitafurahi kukuona mahakamani!” Wakati wa kusikilizwa kwa kesi yako, utamwonyesha hakimu hati ya umiliki wako kwa utulivu. Ataiangalia mara moja na kumkamata yule mwingine kwa kukunyanyasa na kumfanya alipe gharama zote za mahakama. Ujasiri wako haukuegemea kwa jinsi ulivyo hisia zako, bali juu ya sheria na ukweli kwamba wewe ni mmiliki halali wa nyumba hiyo.

Linapokuja suala la kuwa na imani, naona kwamba mara nyingi watu ambao hawaelewi imani ni nini huchanganyikiwa kwa urahisi kwa kuweka ujasiri wao katika matendo yao badala ya chanzo chao pekee cha imani,

ambacho ni Neno la Mungu. Ni rahisi kuchanganya kitendo au kanuni ya

**BASI IMANI NI KUWA  
NA HAKIKA YA MAMBO  
YATARAJIWAYO, NI  
BAYANA YA MAMBO  
YASIYOONEKANA.**

**- WAEBRANIA 11:1**

halina nanga ya uhakikisho. Uhakikisho wako uko katika Neno la Mungu pekee.

Siwezi kuhesabu idadi ya watu ambaao wamenitazama bila jibu nilipowauliza kwa nini waliamini wangepokea nilipowaombea. Ninapouliza, ninatafuta imani yao, yaani makubaliano yao na mbingu. Ninataka kuwasikia wakisema, "Najua nitapokea kwa sababu Mungu ameniahidi katika kitabu fulani na fulani na katika mstari fulani kwamba kitu hiki ni changu." Ikiwa hawanipi andiko kuna uwezekano kwamba hawana nanga na hawajui hakika mashua yao inaelekeea wapi.

Kumbuka, imani inaweza kuwepo tu unapojua mapenzi ya Mungu. Kwa nini? Kwa sababu imani inaweza kuwepo tu wakati moyo wako unakubaliana na mapenzi ya Mungu. Ninaamini kwamba watu wengi hufikiri wana imani wakati sivyo. Tena, akili zao zinaweza kukubaliana kwamba Neno la Mungu ni kweli na ni jema, lakini imani huja wakati mioyo yao imesadiki kabisa. Kwa wengi, akili zao zinakubaliana na Neno la Mungu, lakini mioyo yao haina utulivu.

Hapa kuna kielelezo kizuri cha kile ninachokizungumzia, ambacho ninaamini kitaonyesha kuwa wengi hawana imani wanapodhani wanayo. Je, kama ningekuambia niligundua hivi majuzi kwamba anga haikuwa ya rangi ya samawati, kama watu walivyosema, bali ni rangi ya njano? Kwa maneno mengine, ni kusema kwamba maisha yetu yote tulifundishwa kimakosa kuhusu rangi na kwamba rangi ya samawati sio samawati, bali ni njano. Ungefanya nini? Je, ungeshtuka na kunyakua simu yako ya mkononi haraka na kumpigia mwalimu wako wa darasa la kwanza na kumzomea, huku ukimshutumu kwa kuharibu maisha yako, kwa kukufundisha vibaya kuhusu rangi zote? Sidhani. Hautaitikia kwa hofu wala kufanya mambo mengi. Utajua tu kwamba mimi ni mjinga, na useme kwamba maneno

yangu hayana maana, kisha uendelee na shughuli zako. Kwa nini? Kwa sababu una hakika kabisa kwamba rangi ya samawati ni rangi ya samawati!

Sasa, hebu tulinganishe mfano wangu na mjadala wetu kuhusu imani. Je, ikiwa umesadiki kabisa yale anayosema Mungu kuhusu uponyaji, lakini daktari akuambie kwamba utakufa kwa sababu ya ugonjwa wa saratani. Je, utamtazama daktari na kusema yeye ni mjinga maana unafahamu hilo kamwe haliwezi kutokea? Kwa nini? Kwa sababu unasadiki kikamilifu kuhusu uponyaji alioulipia Yesu. Unaona jambo hili? Bila shaka, watu wengi huomba, lakini ninapochunguza, napata maombi yao sio maombi ya imani bali ya tumaini, wala hawana uhakika wa matokeo. Rafiki yangu, hii ndiyo sababu ni muhimu sana tujijenge wenyewe katika Neno la Mungu. Tunahitaji kujua mapenzi ya Mungu ni nini ili tuwe na uhakika katika kile anachosema, na pia tuweze kukataa kile ambacho si mapenzi Yake. Hebu nikupe mfano kutoka kwa maisha yangu binafsi kuhusu jinsi ilivyo muhimu kujilisha na kile Mungu anachosema juu ya maisha.

Nilikuwa na uchovu, kwa sababu ya kuwa na ugumu katika biashara yangu kwa majuma kadhaa (hii ilikuwa kabla ya kuanzisha kanisa). Ratiba yangu ilikuwa imeja simu za wateja wangu, na bila shaka, shinikizo la kifedha la kuishi kwa kulipwa kamisheni. Nilikuwa nimeenda kwa daktari wangu wa meno kwa matibabu ya mara kwa mara. Kila kitu kilikuwa kawaida hadi daktari alipodunga dawa ya kupunguza maumivu. Alipoingiza ile sindano, nilishtuka kisha taya yangu ikakufa ganzi mara moja, badala ya kufa ganzi polepole. Nilishangaa na nikamwambia daktari kilichokuwa kimetokea. Akasema, “Doh! nafikiri niligusa neva.” Nilimuuliza haraka, “Je, hiyo ni kawaida?” Alisema maneno haya, “Kwa kawaida huwa inapona.” Eti nini? Je, nilimsikia kwa usahihii? “Daktari, unamaanisha nini unaposema hivyo?” Akasema, “Huwa inapona kabisa asilimia 80 hadi 85 bila athari mbaya inayodumu.”

Eti nini? Ghafla hofu iliniingia. Sasa nini? Je, itapona? Akili yangu ilianza kuingwiwa na mawazo ya woga. Baada ya kutibiwa na daktari, uso wangu uliendelea kukufa ganzi, jambo lisilo la kawaida maana ganzi huisha polepole. Nilikuwa ninaelekeea kukutana na mteja takriban saa moja kutoka kwa daktari wa meno, kwa hivyo nilikuwa na wakati mwangi wa kufikiria juu ya kile ambacho kilikuwa kimetokea. Lakini safari hiyo yote nilikuwa na uchungu, si kwa maumivu yoyote, bali kwa kukosa amani na kuingwiwa na hofu akilini mwangu.

Njiani kwenda nyumbani mchana baada ya kukutana na mteja wangu, nilipitia kwa nyumba ya rafiki. Uso wangu ulikuwa bado umekufa ganzi, na

nilikuwa nikitafuta uhakikisho fulani kutoka kwa mtu kwamba ningepona. Tazama kosa langu: Sikulitumaini Neno la Mungu bali mtu ambaye hakuwa mwamini mwenye nguvu ili kunipa ujasiri. Nilimwambia rafiki huyo wangu kilichotokea na nilikuwa nikingojea aseme, “Hilo si jambo kubwa, Gary; utapona!” Badala yake, nilisikia yafuatayo. “Doh! Hapana! Nilikuwa na rafiki ambaye jambo hilohilo lilimfanyikia, na uso wake kamwe haukupona bali ulipooza tangu wakati huo.” Sikuamini nilichokisikia! Akili yangu sasa iliingwa na hofu nyingi kupita kiasi. Nilijifanya kana kwamba nilifahamu ingekuwa sawa na nikamshukuru kwa kunipa wakati wake. Kwa moyo uliokata tamaa, nilipitia kwa nyumba ya rafiki yangu mwigine kuuliza swali lile lile, na kwa mshtuko, nilisikia jibu lile lile, “Doh! Hapana,” akasema, “Nilikuwa na rafiki ambaye alipita jambo hilo hilo, na uso wake haukupona kamwe; uso wake bado umepooza leo.”

Baada ya ziara hiyo, nilivunjwa moyo kabisa. Nilifahamu kwamba Mungu huponya (katika mawazo yangu), lakini sikuweza kuondoa woga huo. Moyo wangu kweli haukuwa umeshawishika. Usiku huo, nilikuwa na uchungu mwangi! Akili yangu ilijawa na hofu, na uso wangu ulikuwa bado umekufa ganzi kama ilivyokuwa kwenye ofisi ya daktari wa meno. Nilipokuwa nikijaribu kupata usingizi, nilianza kusikia maumivu kidogo chini ya sikio langu la kulia. Je, ulikuwa ugonjwa wa babangu wa kupooza? Alipambana nao kwa mwaka mmoja au miwili awali, na aliniambia

## **PAPO HAPO, NILITAMBUA KWAMBA TUMAINI LANGU PEKEE LILIKUWA NENO LA MUNGU.**

kwamba ulianza kwa maumivu chini ya sikio lake. Ugonjwa huu hutokeea wakati neva inayodhibiti misuli ya uso na inayopitia tundu dogo la mfupa chini ya sikio, inapobanwa na maambukizi au kuvimba.

Nilipolala pale huku nikijaribu kupata usingizi, nilichowenza kusikia tu ni maneno haya kupitia kwa mawazo yangu, “Utakuwa na ugonjwa wa kupooza kama babako.” Nilipoamka asubuhi, nilikuwa na ugonjwa wa kupooza! Sasa, si tu kwamba taya yangu ilikuwa imekufa ganzi, bali pia uso wangu wote wa upande wa kulia, na sikuweza kufunga macho yangu au mdomo wangu. Nilikuwa katika hali mbaya.

Nilienda kwa daktari aliyekuwa karibu ili kuthibitisha tuhuma zangu. Baada ya uchunguzi, alinitazama na kusema kwamba kwa hakika nilikuwa na ugonjwa wa kupooza. Kisha nikauliza, “Ni nini kitatokea baada ya hili?” Akasema, “Takriban asilimia 80 hadi 85 ya wagonjwa hupona kabisa.” “Je,

alisema kile nilichofikiri alikuwa amesema?"

Papo nilijua kwamba nilikuwa nimeingia shidani. Nilijua kwamba shetani hangemalizia hapo, na sikutaka kuona kile ambacho kingefuata. Nilifahamu vya kutosha kuhusu vita vya kiroho kutambua kwamba nilikuwa nikielekea katika njia potovu. Kumbuka, hii ilikuwa miaka mingi kabla ya kupata ufahamu wa mengi ya mambo haya. Lakini nilijua vya kutosha kutambua kwamba nilipaswa kukabiliana na jambo hili kwa kiroho ikiwa ningefanikiwa kwa njia yoyote kulishinda. Pia niligundua kwamba huu ulikuwa mpango wa kishetani wa kunitega wakati nina uchovu na kutotazamia matatizo yoyote.

Papo hapo nilitambua kwamba tumaini langu pekee lilikuwa Neno la Mungu. Ndani yangu sikuwa na uwezo kabisa wa kuizua hofu iliyokuwa inaishambulia akili yangu. Kwa hivyo niliandika maandiko ya uponyaji kwa kadi ndogo ambazo nilibandika kote nyumbani kwangu. Nilitubu mbele za Bwana na kuanza mchakato wa kukuza imani moyoni mwangu. Nilijua kwamba nilipaswa kupanda Neno moyoni mwangu ili imani ikue, kwa hivyo nilitafakari Neno la Mungu siku nzima.

Mwanzoni hakuna kitu kilichobadilika. Uso wangu ulikufa ganzi, na mara kwa mara nilipambana na roho ya woga. Baada ya wiki moja, nikiwa katika hali hiyo ya kutokuwa na mabadiliko yoyote, ghafula jambo lilitokea! Kama ule mchakato ambao andiko letu katika Marko 4:26 linavyofundisha, nilipotawanya Neno moyoni mwangu, imani ilianza kukuzwa, kwanza jani, suke, kisha ngano pevu kwenye suke.

Katika mchakato huu wote, huwa hakuna makubaliano na hivyo hakuna imani—bado. Walakini, ingawa hatuoni mabadiliko au kufahamu jinsi mchakato huu unavyofanya kazi, kulingana na andiko letu katika Marko 4, mambo yanabadilika kweli. Mabadiliko ninayozungumzia bado hayajadhihirishwa katika ulimwengu wa asili, bali yanatokea miyoni mwetu. Tukilishikilia Neno, linabdalisha polepole mfumo wa imani ya miyo yetu kutoka kwa kutokuamini hadi kukubaliana na mbingu. Kwa hiyo nilishikilia Neno, huku nikijua kwamba hilo ndilo lililokuwa jibu langu pekee.

Ghafla, siku moja, nilipokuwa nikitembea nyumbani mwangu nikiwa na kadi hizo zote zenye maandiko ya uponyaji zikiwa zimebandikwa kila mahali, nilitazama moja ambayo nilikuwa nimeiona mara mia moja. Lakini safari hii nilipoitazama, ghafla, upako ulinijia, hofu ikaondoka mara moja, NIKAJUA kuwa nimepona. Ndio, uso wangu ulikuwa bado umekufa ganzi. Hakukuwa na mabadiliko, lakini nilijua nilikuwa mzima. Baada ya

masaa kadhaa, uso wangu ulikuwa kawaida kabisa, na ganzi yote ilikuwa imekwisha. Bwana asifiwe! Jamani neno linafanya kazi!

Ingawa nilikuwa nimeruhusu maisha yangu ya kiroho kudhoofika kwa sababu ya shughuli nyingi na kupuuza kwangu, hatimaye nilitambua kosa langu na kutubu kutokana na upumbavu wangu. Huu ni wakati nilikuwa nikijifunza kwa mara ya kwanza jinsi imani inavyofanya kazi, na sikuwa na uzoefu mwingi kuihusu. Ilikuwa upumbavu kwangu kuuliza watu kuhusu siku zangu za usoni wakati wa shida badala ya kwenda moja kwa moja kwenye Neno la Mungu. Mara nilipolewa kilichokuwa kikiendelea, niligeukia Neno la Mungu kwa ujasiri. Cha kusikitisha ni kwamba, watu wengi hawana ujasiri katika mchakato huu kwa sababu hawajawahi kufundishwa kuhusu imani na jinsi inavyokuja. Kwa sababu hawajui mchakato huu, wanapokuwa chini ya shinikizo, huwa wanaacha Neno, wakidhani kuwa halifanyi kazi.

### **Elewa Mashambulizi ya Kulipiza Kisasi ya Shetani**

Christine alipokuja kanisani mwetu hakujuu mengi kumhusu Mungu. Aliokoka katika mojawapo ya ibada zetu za Jumapili asubuhi na maisha yake yalibadilika sana. Katika kanisa letu tuna mafundisho ya kuwalishwa waumini wapya kuhusu Ufalme. Moja ya maeneo tunayozungumzia na kufundisha ni haki ya kisheria ya kupokea uponyaji. Christine alikuwa na shida na masikio yake kwa miaka mingi. Alikuwa ametumia kifaa cha kumsaidia kusikia kwa miaka 40 na tayari alikuwa amepoteza zaidi ya asilimia 50 ya uwezo wake wa kusikia. Mamake alikuwa kiziwi, na kakake pia alikuwa na shida hiyohiyo ya kupoteza uwezo wa kusikia. Christine aliposikia kwamba, ye ye kama muumini, alikuwa na haki ya kisheria ya kuponywa, alisisimka sana!

Darasani, mke wangu alimwekelea mikono na kuomba kwamba masikio yake yafunguliwe, na papo hapo, aliweza kusikia kikamilifu. Christine alianza kupiga kelele na kulia na kumsifu Mungu. Mke wangu, Drenda, na Christine walipokuja na kuniambia habari njema, nilihisi msukumo wa kumwonya kuhusu mashambulizi ya kulipiza kisasi ya Shetani. Nilimwambia Drenda amwelekeze Christine kwamba dalili zikianza kumrudia anenee suala hilo kwa ujasiri na atangaze kuwa amepona na kwamba Shetani aondoke. Asubuhi iliyoleta jaribu lilikuja. Kusikia kwake kulikuwa kumedhoofika na hakuweza kusikia vyema. Kwa hivyo alifanya jinsi tulivyosema, "LA! Shetani, ninakataa hili. Niliponywa na

nimepona, kwa jina la Yesu!” Mara moja! Masikio yake yalifunguka na yamekaa wazi tangu wakati huo.

Kumbuka kwamba Shetani hushambulia ili kujaribu kutwaa eneo hilo tena. Usimruhusu afanye hivyo. Simama kwa Neno la Mungu!

Katika sura hii, nimechukua muda kukupa ufahamu wa kimsingi kuhusu maana ya imani, jinsi inavyofanya kazi, jinsi ya kujua kama uko na imani, na mahali pa kupata imani. Ili Ufalme wa Mungu ufanye kazi maishani mwako, unapaswa kujua hili. Kumbuka, Yesu alimwambia yule mwanamke, “Imani yako imekuponya.” Na ndivyo itakavyokuwa kwako: Imani yako, moyo wako ulio na hakika kabisa kuhusu kile mbingu inachosema, na kutumia mundu ndiyo suluhisho lako kwa shida au hitaji lolote utakalokabili maishani.

## SURA YA 6

# BARAKA YA BWANA

Nilikuwa nimekaa kwenye mgahawa na mke wangu na mnenaji mgeni. Ilikuwa karibu saa nne usiku, na tulikuwa tumemaliza ibada ya jioni yenye nguvu. Mhudumu wa hoteli alipokuja kuchukua agizo la chakula chetu tulianza mazungumzo naye. Mgeni wetu alianza kumwambia jinsi ibada ilivyokuwa ya ajabu na kuhusu kanisa letu. Kisha akamuuliza, “Je, unapenda kuwinda?” Alijibu kwamba alipenda kuwinda. Mgeni wetu alifurahia sana hadithi zangu za uwindaji, na nilikuwa nimemwandalia mojawapo ya vitabu vyangu vinavyoitwa *Faith Hunt* jioni ile ili apeleke nyumbani kwa rafiki yake. Kitabu hicho kilikuwa sakafuni karibu nami.

Mhudumu huyu wa hoteli aliendelea kutwambia jinsi alivyokuwa akiwinda tena na tena bila kumpata kulungu. Mimi na mgeni wetu tulianza kumweleza jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi na kwamba angeweza kutazamia kupokea kulungu wake kila mara alipoenda kuwinda. Hakujuu afikirie nini kutuhusu. Lakini nilikumbuka kile kitabu nilichokuwa nacho na nikajitolea kumpa. Nilimwambia mgeni wetu kwamba ningempa nakala nyingine na akakubali. Yule mhudumu alinishukuru na kuahidi kukisoma kile kitabu, lakini nilifikiri labda hiyo ndiyo ingekuwa mara yangu ya mwisho kusikia kutoka kwake. Haikuwa hiyvo.

Baada ya mwaka mmoja, yule mgeni wetu alirudi kanisani mwetu kuhudumu kisha akasema kwamba aliupenda ule mkahawa tulioenda mwaka uliopita na akaomba kwenda huko. Tulifanya hivyo. Tulipoketi, tulishangaa kwamba tulikuwa na mhudumu yule yule wa hoteli aliyetuhudumia mwaka uliopita. Alipokuja kwetu, alitutazama kisha akasema, “Habari zenu? Mlikuwa hapa mwaka mmoja uliopita, na tulizungumza kuhusu kuwinda kulungu.” Tukasema, “Ndio, tulikumbuka.” Naye akasema, “Nilisoma

kile kitabu ulichonipa, na nilifanya kile kilichosema. Nilipata kulungu wawili mwaka jana na ninatarajia kupata kulungu wangu mwaka huu pia.” Tulifurahi kusikia hadithi yake lakini hatukushangaa. Ufalme hufanya kazi kila wakati!

Nilikuwa na kongamano la wachungaji takriban 25, ili kueleza Ufalme wa Mungu na jinsi unavyotenda kazi. Ulikuwa mukutano mzuri sana. Nilipokuwa karibu kuondoka kwenye chumba cha mikutano huku wafanyakazi wetu wakifanya usafi, mmoja wa wachungaji alirudi ndani ya chumba. Yeye na mke wake walikuja kwa mke wangu wakauliza kama wangeweza kuzungumza nasi. Mchungaji alianza kutuambia kwamba kufikia mwisho wa juma nyumba yake ingeuzwa isipokuwa angepata dola 6,900. Alieleza kwamba hakuwa na pesa ila dola 100, ambazo sasa zilikuwa mkononi mwake. “Hizi ndizo nilizo nazo,” akasema, “lakini nataka kuzitoa kama matoleo jinsi ulivyofundisha jioni ya leo, wewe na mke wako mkubaliane nasi tupate fedha tunazohitaji juma hili.” Sote tulishikana mikono na kuomba na kumshukuru Mungu kwa ajili ya pesa hizo.

Baada ya karibu mwezi mmoja, nilimwona mchungaji huyo kwa mukutano mwingine, naye akanikimbilia akiwa amesisimka. “Lazima nikwambie kilichotokea,” akasema. “Sikukuambia hili tulipozungumza hapo awali, lakini mimi na mke wangu tuna biashara ya fulana za hariri ambazo huwa tunatengeneza mara kwa mara katika karakana yetu. Huwa hatuifanyi biashara hiyo sana, lakini kila mara baada ya muda fulani huwa tunapata wateja. Sasa siku moja baada ya maombi yetu nanyi, tulipokea kazi ya jumla ya \$8,900. Ilitubidi tufanye kazi kwa bidii sana juma hilo, lakini kufikia Ijumaa hiyo, tulikuwa na dola 6,900 tulizohitaji ili kulipia nyumba yetu. Asante!”

Nilikuwa kwenye kongamano la wachungaji huko North Carolina na wachungaji wengine wapatao 500. Sikuwa mnenaji, nilihudhuria tu. Mwanaume fulani alinijia na kusema, “Ninahitaji kuzungumza nawe.” Alikuwa mchungaji kutoka Ujeruman, na alisema alikuwa na hadithi ya kuvutia ya kuniambia.

Mwanawawe, ambaye alikuwa tineja, kwa njia moja au nyingine alipata CD zangu. Baada ya kuzisikiliza, aliamua kwamba angepokea *PlayStation 3* kwa imani maana hakuwa na pesa za kuinunua. Naamini kwamba kila mtu anajua *PlayStation 3* ni nini, lakini ikiwa hujui, ni kifaa cha michezo ya kompyuta. Mchungaji aliniambia jinsi mtoto wake alivyoingia ofisini kwake siku moja na kumuuliza kama angekubaliana naye kupata hiyo *PlayStation 3*. Mtoto alimweleza babake kile alichokuwa akijifunza kwenye CD zangu

na jinsi aliviyotaka kutoa matoleo kama mbegu na kuomba pamoja naye kuhusu hilo. Mchungaji aliniambia hakufikiria sana jambo hilo, lakini kwa sababu alikuwa mchungaji wa kanisa, alipokea matoleo kutoka kwa mwanawewe, sadaka ya kifedha aliyoitoa kwa kanisa. Yeye na mwanawewe walisali pamoja na kukubaliana kwamba sasa alikuwa na *PlayStation 3*, na wakasema suala hilo lilikuwa limekamilika.

Siku iliyofuata, mwanamume mmoja wa kanisa lao alimpigia simu kasisi huyo na kumuuliza ikiwa mtoto wake angetaka kupata pesa za ziada maana alikuwa na mradi wa muda mfupi aliohitaji kusaidiwa. Mwana wa mchungaji alifurahia kupata pesa za kutosha kutoka kwa mradi huo wa siku mbili kisha akanunua *PlayStation 3*.

Jambo hilo lilikamata usikivu wa mwana huyo, na baada ya majuma machache, mchungaji huyo alisema kwamba mwanawewe alirudi ofisini mwake na kuuliza ikiwa angeweza kukubaliana naye kuhusu jambo jingine. Mchungaji aliniambia alimjibu, “Ndio,” lakini alishangaa kidogo mwanawewe alipomuuliza ikiwa angekubaliana naye kwamba Mungu angempa misuli mikubwa zaidi. Mchungaji aliniambia hakujua jinsi ya kumjibu mtoto wake kuhusu hilo. Lakini hatimaye, alimwambia mwanawewe kwamba angepaswa kufanya sehemu yake inapohusu misuli na kwamba angekubaliana naye maadamu angelelewa hilo. Mwanawewe alikubali. Kwa hiyo tena mwanawewe alitoa matoleo ya kupata misuli mikubwa zaidi, kisha wakaomba kwa makubaliano kwa ajili ya hilo.

Siku iliyofuata, gari lilikuja likasimama barabarani nyumbani kwa mchungaji. Ilikuwa ni familia kutoka kanisani. Mchungaji alipotoka nje ili kuzungumza nao, walisema kwamba walikuwa wakisafisha karakana yao na walikuwa na kifaa cha mazoezi ya mwili ambacho walifikiri kwamba huenda mwana wa kasisi angetaka. Kama sivyo, walifikiri kwamba mchungaji angejua ni nani mwingine kanisani ambaye angekipenda. Mchungaji aliniambia kwamba hakuna mtu aliyejua chochote kuhusu shauku ya mwanawewe ya kuwa na misuli na kwamba walikuwa wameomba kuhusu jambo hilo usiku. Mchungaji alisema alishtuka! Aliingia ndani ya nyumba na kumwambia mwanawewe, “Hizo CD ziko wapi?”

Hadithi za aina hii ni za kawaida. Huwa ninazisikia kila wakati, na ninataka ziwe za kawaida katika maisha yako pia. Kufikia sasa tumeanzisha na kujadili vipengele kadhaa muhimu vya jinsi sheria za Ufalme wa Mungu zinavyofanya kazi, na pia jinsi makubaliano au imani inavyohitajika ili mbingu ipate uhalali au mamlaka katika ulimwengu. Sasa, hebu tuchunguze kwa undani zaidi jinsi sheria hizi za Ufalme zinavyoweza kusaidia katika

mahitaji yetu ya kifedha.

*Baraka ya Bwana hutajirisha, wala hachanganyi huzuni nayo.*

—Mithali 10:22

Nilipoona andiko hili kwa mara ya kwanza, niliwaza, “Jamani andiko hili halimaanishi kile linachosema, sivyo?” Lakini nimeona kwamba linamaanisha kabisa kile linachosema! Ili kuelewa kifungu hiki kinazungumzia nini, tutahitaji kutazama nyuma mwanzoni, wakati mwanadamu alipoumbwa mara ya kwanza.

Ila mtu mmoja ameshuhudia hivi mahali fulani, akisema,

*“Mwanadamu ni nini hata umkumbuke, ama mwana wa binadamu, hata umwangalie? Umemfanya mdogo punde kuliko malaika, umemvika taji ya utukufu na heshima, umemtawaza juu ya kazi za mikono Yako; umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake.”*

*Kwa maana katika kuweka vitu vyote chini yake hakusaza kitu kisichowekwa chini yake. Lakini sasa bado hatujaona vitu vyote kutiwa chini yake.*

—Waebrania 2:5b-8

Tulisoma kifungu hiki hapo awali, lakini ni muhimu kwa mjadala wetu sasa. Kama tulivyosema awali, mwanadamu alipoumbwa, kila kitu duniani kiliwekwa chini ya utawala wake. Hakukuwa na jambo moja ambalo halikuwa chini yake. Alitawala ulimwengu akiwa katika cheo cha mamlaka iliyokabidhiwa na alivaa taji la serikali aliyoiwakilisha. Alivikwa upako wake na kuheshimiwa kwa nafasi ya mamlaka aliopewa. Shetani, ambaye alikuwa amemwasi Mungu, alikuwa tayari ametupwa duniani kabla ya Adamu kutokea. Shetani alimdhara mwanadamu maana alijikuta akitawaliwa na mtu huyu aliyeavaa taji ya mamlaka ya Mungu. Sasa ilimbidi shetani anyenyekiee kwa kiumbe hiki ambacho katika hali yake ya asili, kilikuwa na umbo dhaifu sana kuliko lake. Walakini kiroho, kila neno alilonena Adamu lilikuwa na mamlaka sawa na ya Mungu. Adamu, mwana wa Mungu, alitawala juu ya dunia akiwa na cheo hiki cha ajabu cha mamlaka na ukuu.

Kwa hiyo Shetani alimchukia mtu huyu na akatamani mamlaka aliyokuwa nayo juu ya nchi. Jibu lake pekee lilikuwa kwa njia moja au

# **“BARAKA YA BWANA HUTAJIRISHA, WALA HACHANGANYI HUZUNI NAYO.”**

**— MITHALI 10:22**

nyingine kuchukua taji yake, na nafasi ambayo mwanadamu alikuwa nayo. Kulikuwa na tatizo moja dogo tu. Shetani hakuwa na uwezo wa kutwaa taji hiyo kutoka kwa Adamu; tumaini lake pekee lilikuwa kwamba kwa njia fulani angeweza kumdanganya Adamu ili avue taji yeye mwenyewe. Kwa kumsadikisha Hawa kwamba Mungu hakupaswa kutegemewa na kwamba maisha yalikuwa na mengi zaidi ya kutoa kuliko yale ambayo Mungu alikuwa akiruhusu, Adamu na Hawa walichagua kumwamini Shetani badala ya Mungu na hivyo kumuasi Mungu. Mwishowe, Adamu na Hawa walipoteza cheo chao cha kisheria cha mamlaka ndani ya Ufalme wa Mungu, na Shetani akafanyika mungu wa ulimwengu huu, kama tunavyoona katika 2 Wakorintho ambapo Paulo anazungumza.

*Ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu.*

— 2 Wakorintho 4:4

Kabla ya Adamu kuasi, alifurahia faida za kuwa mwana. Yote ambayo Mungu alikuwa nayo yalikuwa yake ya kufurahia, na hakuwa na mahitaji yoyote au wazo la hofu hata siku moja ya maisha yake. Kila kitu alichohitaji ili kuishi duniani tayari kilikuwa kimewekwa hapa kabla hajaumbwa.

Tukitafakari nyuma kuhusu siku sita za uumbaji katika kitabu cha Mwanzo, tunapata kwamba mwanadamu aliumbwu mwishoni mwa siku ya sita ya uumbaji, alikuwa sehemu ya mwisho ya mpango wa uumbaji wa Mungu. Hatma yake ilikuwa kuishi katika siku ya saba, ambayo Mungu alitangaza kuwa siku ya mapumziko. Hii haikuwa kwa sababu Mungu alikuwa amechoka bali kwa sababu alikuwa amekamilisha kila kitu. Tafakari kuhusu kile ambacho Mungu alikuwa amekamilisha na mpango mtukufu aliokuwa nao kwa mwanadamu. Cha kusikitisha ni kwamba Adamu alipoteza yote hayo, na kwa hiyo kupoteza cheo chake cha kisheria katika Ufalme.

Mungu alimwendea baada ya uamuzi wake wa kutotii, na kumwambia Adamu:

*Ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako; michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni; kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.*

—Mwanzo 3:17b-19

Jambo la kwanza ninalotaka uone ni kwamba Mungu hakuilaani dunia, Adamu aliilaani. Alikuwa na mamlaka kamili juu yake. Alikuwa mlinzi wake. Adamu alikuwa na mamlaka kamili juu ya dunia, lakini alipoasi serikali ya Mungu, kimsingi alimfukuza Mungu. Uamuzi huo ulikuwa na matokeo makubwa sana si kwa Adamu tu bali pia kwa dunia nzima na kila mwanamume au mwanamke ambaye angeishi duniani kuanzia siku hiyo na kuendelea. Ingawa bado alidumisha mamlaka Mungu aliyoukuwa amempa juu ya dunia, sasa hakuwa na uwezo wa kutawala kadri ya taji na serikali aliyoiwakilisha hapo awali ambayo iliunga mkono utawala wake. Alitenganishwa na uzima wenyewe, na kifo, ambacho kilikuwa dhana geni kwake, sasa kilichukua nafasi hiyo.

Mungu alimkabili Adamu kuhusu yale aliyofanya na kumwambia Adamu kwamba sasa, kwanza, kuitia kwa dhambi yake, alikuwa amepoteza nafasi yake ya kisheria katika serikali ya Mungu. Na kwa sababu Adamu alikuwa mwakilishi wa serikali hiyo duniani, mbingu ilikuwa imepoteza uwakilishi wake wa kisheria duniani ambao ilipata kuitia kwake. Pili, dunia yenye sasa ilikuwa imeathirika na haingetoa tena riziki kama ilivyofanya hapo awali kwenye bustani ya Edeni. Sasa kazi ngumu na jasho la Adamu mwenyewe lingehitajika ili dunia itoe kile alichohitaji na aweze kuendelea kuishi. Miiba na michongoma sasa ilijaa mashambani na maisha yalifanyika kuwa magumu; kuishi katika shida lilifanyika jambo la kawaida maishani.

Ninaita njia hii ya kuishi maisha ya ugumu na yenyе mawazo ya kunusurika, ambayo yamechafuliwa na harufu ya hofu na kifo, na kulemea kila mwanadamu anayekuja baada ya Adamu, mfumo wa laana ya dunia. Ndipo ambapo mimi na wewe tumelelewa na sote tunaujua vyema sana. Daudi aliita bonde la uvuli wa mauti katika Zaburi ya 23.

*Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana Wewe upo pamoja nami.*

—Zaburi 23:4

Ni eneo ambalo hofu ya kifo inaenea hewani. Lakini pia kuna matokeo mengine mabaya. Mwanadamu anapoteza uhusiano wake na Mungu na hivyo basi, hajitambui—anapoteza kusudi la kuumbwa kwake na utambulisho wake. Mwanadamu alipoumbwa, alipewa lengo, yaani kazi fulani. Alipaswa kutawala dunia kwa niaba ya Mungu. Kwa maneno mengine, alikuwa na kazi na kusudi la kiungu maishani mwake. Lakini sasa mtazamo wote wa mwanadamu uligeuzwa kuwa wa kuishi maisha ya kunusurika. Hili limefanyika kusudi na kazi yake mpya.

Sasa, kila uamuza aliofanya mwanadamu ulichujwa kupitia kwa laana hii ya manusuru, ya kujitafutia au kujihifadhia riziki. Hakuna amani; na

kila siku imejaa kazi yenyeye uchungu na jasho. Njia pekee ya kuepuka hili maishani, yaani mbio za panya kama tunavyoziita leo, ni kutafuta njia ya kujihifadhia riziki ya kutosha ili hatimaye tuache kukimbia. Hii ndio ndoto ya kila mtu tangu mwanadamu atende ile dhambi ya asili. Hili ndilo

lengo lao namba moja, kuacha kukimbia. Yeyote anayebahatika kupata riziki ya ziada sasa huihifadhi kwa uangalifu na ulinzi mwingi. Wanaishikilia kwa hofu kubwa ya kuipoteza, maana wakifanya hivyo, watalazimika au watafanya watumwa wanaokimbia hapa na pale katika taabu chungu na jasho tena.

Ndoto ya mwanadamu, lengo lake la kuishi, kama nilivyosema awali, ni kupata riziki ya kutosha ili aweze kuacha mbio za watumwa manusuru na kupata pumziko. Ninataka kuhakikisha kwamba una ufahamu dhahiri wa ukweli huu: Kila mtu amechoka kukimbia hapa na pale kama manusuru katika mfumo wa laana ya dunia.

Nakumbuka niliketi chini kuzungumza na mchungaji fulani asubuhi moja. Aliniambia aliipenda sana huduma kila kukicha anapoamka hadi anapokumbuka hali yake kifedha, madeni, na ukosefu wa pesa. Alisema masuala yake ya kifedha yalikuwa kama blanketi yenyeye unyevunyevu iliyokuwa ikijaribu kuyakaba maisha yake na kumnyang'anya furaha ya yale yote aliyyofanya. Sio wachungaji tu wanaokabiliwa na tatizo kama hili. Ni kawaida ya maisha katika familia nyingi kwa sababu wanaishi maisha ya madeni, na mshahara mmoja hadi mwingine.

Kila mtu anatafuta njia ya kuwa huru, na njia pekee ni utajiri, kuwa na riziki zaidi. Katika mfumo wa laana ya dunia, mtu anajulikana sasa na kile

## **KILA MTU AMECHOKA KUKIMBIA HAPA NA PALE KAMA MANUSURU KATIKA MFUMO WA LAANA YA DUNIA.**

alicho nacho na pesa alizo nazo. Kwanza, mwanadamu alijaribu sana kuficha uchi wake alipopoteza kusudi lake la kweli na utambulisho alioumbwa nao, kisha akanyakua ule wa bandia. Sasa anajaribu kufunika upako na utukufu aliofunikwa nao kwa kutumia utajiri. Pili, anajaribu kubadilisha cheo chake chenye taji ya heshima, ambacho alitumia kutawala katika Ufalme wa Mungu, na kiburi cha maisha na kuwatawala wanadamu wengine. Mwanadamu sasa ametawaliwa na kitu kimoja—kutafuta au kushikilia mali. Utambulisho wake sasa unapatikana katika mali nyingi alizonazo na uwezo mkubwa alionao juu ya wanadamu wengine. Hali na cheo katika jamii ni muhimu sana sasa katika heshima ya mwanadamu aliyeanguka.

Tafakari kuhusu jambo hili. Ni swalí gani la kwanza ambalo mwanamume humuuliza mwingine wanapokutana mara ya kwanza? “Je, unafanya kazi gani?” Kwa nini? Je, tunajali au kufurahia hilo kweli? La hasha, lakini swalí hili linatuwekeea kiwango cha heshima tutakayompa mtu huyo. Kwa maneno mengine, tunajiuliza, “Mtu huyu ni nani? Je, ana cheo au kiwango gani duniani? Je, ninapaswa kumheshimu kiasi gani?” Sasa, akina dada, ninazungumza kwa mtazamo wa wanaume tu hapa. Ninatambua nyinyi wanawakee hutumia mtazamo tofauti kabisa katika kujitambulisha.

Leo mfumo huu wa laana ya dunia bado unafanya kazi! Watu huchuja maamuzi yao yote kupitia kwa kichujio cha kutafuta au kushikilia pesa. Watu huhamia jimbo lingine kuchukua kazi inayolipa pesa zaidi bila kufikiria madhumuni yao ni nini. Kila mtu anataka kuwa mashuhuri. Kwa nini? Ni kwa sababu ya utambulisho (cheo) na utajiri.

Utafiti ulifanywa mionganî mwa maelfu ya wanafunzi wa darasa la tano hadi nane kuhusu kazi ambayo wangependa kufanya wakiwa wakubwa. Asilimia 65 kati yao walisema kwamba lengo lao la kazi lilikuwa kuwa watu maarufu. Maarufu? Ni tangu lini kuwa maarufu kulifanyika kuwa kazi?

Utafiti mwingine ulionyesha kwamba asilimia 30 ya wafanyakazi wanachukia kazi zao, na mwingine kwamba asilimia 40 hawapendi kazi zao. Kwa hivyo tuna wafanyakazi asilimia 70 nchini Amerika wasiopenda kazi zao! Basi wanafanya nini hapo? Ni kwa sababu wao ni watumwa manusuru tu, wanaokimbia juu na chini katika taabu chungu ya kudondoja jasho ili kuendelea kuishi. Kusudi na shauku ya wengi wao si mambo muhimu kwao; motisha yao ni kulipa bili. Kuwa mtumwa wa hitaji la kupata pesa hakuachi nafasi kubwa ya kuwa na chaguo lingine. Anayelipa pesa nyingi hushinda kila wakati. Inaitwa mbio za panya! Hapa ndipo sote tulipo. Pata picha akilini mwako ya mnyama kama panya anayekimbia haraka iwezekanavyo, bila kwenda popote kwenye gurudumu. Tunaweza kucheka

na kufikiria inapendeza. Lakini katika ulimwengu wa asili, sio vyema, sio vyema hata kidogo. Watu hufa kwenye gurudumu hilo na kamwe hawafiki mahali walipotarajia kufika.

*Ninyi msitafute mtakavyokula wala mtakavyokunywa; wala msifanye wasiwasi, kwa maana, hayo yote ndiyo watafutayo mataifa ya duniani, lakini Baba yenu anajua ya kuwa mna haja na hayo. Bali utafuteni ufalme wa Mungu, na hayo mtaongezewa.*

– Luka 12:29-31

Kukimbia hapa na pale kwa taabu chungu na jasho ndio mfumo pekee tunaoujua. Ikiwa ningekuambia kwamba unapaswa kutoka kwa madeni, na ni LAZIMA utoke kwa madeni katika miezi 12 la sivyo familia yako yote itahamishwa kwenda Ncha ya Kaskazini milele (ninatumia mfano mkali kutoa hoja), je, ungefanya nini? Nitakuambia kile utakachofanya. Mara moja utaanza kuunda mpango wa kukimbia haraka hapa na pale kutafuta njia. Utasema, “Labda ninaweza kufanya kazi kadhaa za ziada. Mke anaweza kufanya kazi kadhaa za ziada, na watoto wanaweza kusaidia pia.” Unaona, huu ndio mfumo pekee wa kupata riziki uliojifunza, taabu chungu na kutokwa jasho. Ngoja nikupe picha nyingine ya mfumo huu.

Tuseme ninakimbia mtaani kwenu, kisha nipate mfuko wa karatasi wa rangi ya kahawia upande mmoja wa barabara yenu ulio na dola milioni kumi ndani yake. Ninafurahi sana, lakini najua kwamba ninapaswa kuripoti jambo hilo. Na kwa sababu ninakujua, ninakimbia hadi nyumbani kwako na kuomba kutumia simu yako. Ninapiga simu kwa polisi huku ukiwa umesimama hapo na kunisikiliza. Ninaambia polisi kilichotokea na kile nilichopata. Baada ya kimya kifupi wanapokagua ripoti zao, wananiambia hawana taarifa yoyote ya kupotea kwa pesa hizo na ninaweza kuzimiliki. (Sidhani hivyo ndivyo wanavyoweza kusema, lakini inafaa mfano wangu.) Wanaponiambia hivyo, ninaruka juu na kupiga kelele za shangwe. Kisha ninakwambia yale ambayo wamesema, huku nikiwa na furaha tele.

Unatabasamu kwa upole ninaposhangilia na kukueleza haya yote. Lakini unafikiri utafanya nini mezani usiku huo unapomsimulia mwenzi wako hadithi hiyo? Utatabasamu? Sidhani. Utasema, “HIYO SIYO \_\_\_\_\_!” Umejaza pengo, sivyo? Ulijuaje kwamba neno, “HAKI” ndilo jibu sahihi? Nitakuambia kwa nini, kwa sababu ndivyo ulivyolelewa. Huo ndio mfumo uliokua nao. Taabu chungu na kutokwa jasho ndivyo maisha yalivyokuwa.

Katika mfano wangu, nimepata pesa bila kufanya kazi yoyote, na

hiyo ni kudanganya mfumo. Sio haki. Sio haki kwa sababu sikufanya kazi ili kupata fedha hiso; nimezipata tu. Ukiwa na ufahamu kwamba labda huwezi kuwa na bahati kama hiyo, unajawa na wivu na uchungu, huku ukijua kwamba siku zako bado zitajawa na utumwa wa kunusurika na kulazimishwa.

Kwa kulinganisha, ikiwa ningekuja kanisani siku moja na nguo zangu zote zikiwa zimechanika na chafu na kusimama na kuwaambia watu, “Tumefaulu! Drenda na mimi tulifanya kazi kwa masaa 22 kila siku katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, na hatimaye tumemaliza kulipia nyumba yetu,” kila mtu angeshangilia kwa vifijo. Kwa nini? Kwa sababu kuna mtu ambaye amefaulu, na hilo limewatia moyo. Kuna mtu ambaye amefaulu kwa hivyo kuna njia ya kuwa huru! Labda tunaweza kufunga mkanda, tulipe gharama, na kuwa huru pia. Lakini kwa nini kila mtu hakupiga kelele na makofi nilipopata pesa kando ya barabara? Na kwa nini ilikuwa rahisi kwako kujaza pengo? Kwa sababu hivi ndivyo unavyofikiri; ndivyo unavyoota pia. Kuwa na kazi chungu na ya kudondo jasho ndio mfumo wa haki tuliojifunza. Pesa bila kazi sio haki.

Lakini kutoroka kutoka kwa mfumo wa kazi ngumu ya kudondo jasho ni ndoto ya kila mtu. Kuwa tajiri, kuwa milionea ni wazo la kuvutia kwa watu wengi. Thamani ya dola milioni, sio kama ilivyokuwa hapo awali, lakini hata kama ni nambari tu, ingali inazungumzia utajiri. Utajiri unaleta uwezekano wa kuwa huru ambalo ni jambo lililo kinyume na maisha magumu ya kila siku ya watu wengi. Kila mtu amechoka kukimbia juu na chini, na kuwa na dola milioni kunamaanisha wanaweza kuacha hilo na kufanya kile walichotaka kufanya. Tafakari juu ya hili: Mvuto wa bahati nasibu ni nini? UHURU! Uhuru wa kuchagua, kufanya maamuzi ambayo hayahuju kulipa bili au kutafuta riziki.

Kipindi cha runinga kinachoitwa, *Who wants to be a Millionaire?*, kinapendwa sana. Kinavutia kwa sababu kila mtu anaota kupata uhuru huo. Watu wanapotazama kipindi hicho, huwa wanahusika kihisia, wakimshangilia mshindani huku wakiwa na tumaini kwamba atafanikiwa.

Kubadilisha mada kidogo, kwa ufanuzi rahisi, kuiba pia ni kupata riziki bila kufanya kazi. Kunaleta uhuru kutoka kwa mfumo wa laana ya dunia lakini kwa njia potovu. Tukubaliane basi kwamba kila mtu anataka kuacha kukimbia! Lakini je, kuna njia ya kuacha? Kashfa za wizi wa pesa zipo kwa wingi. Huwa ninapokea barua pepe kumi na zaidi kwa siku kutoka kwa watu walio nje ya nchi yetu wanaonisimulia hadithi zao za kusikitisha kuhusu jinsi walivyorithi dola milioni 20 na wanahitaji mtu wa kuwasaidia

kuziweka mahali salama. Wananiahidi nusu yake ikiwa tu nitajitolea kuchukua pesa zao na kuzihifadhi. Hapo basi bila shaka wanataka anwani yangu ya barua pepe, nilipe ada ndogo ya usindikaji, usafirishaji, bima, na chochote wanachoita ada ili urithi uachiliwe. Kweli? Je, ninaonekana kama mjinga?

Nilikuwa na mteja aliyenipigia simu wakati mmoja, na alitaka ushauri kuhusu uwekezaji. Niliuliza maswali yangu ya kawaida, na nikagundua kwamba alikuwa na takriban dola milioni tano za kuwekeza. Aliniambia kuwa hakuwa na pesa hizo wakati huo, lakini zilikuwa zinatoka kwa urithi. Nilimuuliza ni wakati gani alifikiri angepata pesa hizo, naye akasema baada ya wiki mbili hivi. Kwa hiyo nilimpigia simu baada ya karibu wiki mbili, kisha akasema kwamba ingechukua muda mrefu kidogo zaidi. Alikuwa na shida ya kupata urithi kutoka kwa benki ya Ulaya iliyokuwa inaushikilia. Hilo lilikamata usikivu wangu, kwa hiyo nikaanza kuuliza maswali. Hadithi ilikuwa kwamba alikuwa na mtu aliyedhaniwa kuwa mjomba wake ambaye alikuwa huko Ufaransa. Mjomba huyo ndiye aliyemwachia hizo dola milioni tano. Hata hivyo, kulikuwa na dhima ya kodi ya \$50,000 iliyokuwa inadaiwa juu ya urithi huo ambayo ilihitaji kulipwa kabla ya urithi huo kutumwa kwake. Aliniambia bado alikuwa akijaribu kupata pesa na kwamba alikuwa ametuma barua kwa benki kuomba mkopo wa kununua nyumba.

Nilimuuliza kama alikuwa na wakili, akasema, "Ndio, wakili aliyenipigia simu kutoka Ufaransa ndiye anayeshughulikia jambo hili." "Kwa hivyo, huna wakili wa Marekani anayelishughulikia?" nikauliza. Akasema, "Hapana, ninaye yule aliyenipigia simu kutoka Ufaransa." Aliendelea kueleza kwamba kwa sababu alikuwa na ugumu wa kupata dola hizo 50,000, wakili huyo nchini Ufaransa alisema atalipa nusu yake, na kwamba angeweza kumrejeshea pindi pesa hizo zitakapotolewa. "Hapana," nikasema, "huo ni utapeli!" Ingawa hakuwa amewahi kusikia kuhusu mjomba huyo hapo awali, aliamini kwamba hii ilikuwa kweli. Nilimpigia simu tena baada ya majuma mawili, kisha akasema kwamba alikuwa karibu kupata pesa zote za kutuma kwa benki. Tena, nilimwambia, "Tayari wanazo dola hizo milioni tano. Iwapo wanataka pesa za ushuru, wangekutumia barua pepe au barua ya kawaida uipokee siku iliyofuata kisha utie saini na kuwatumia tena ili kuwaiddhinisha wachukue dola 50,000 kutoka kwa zile pesa ambazo tayari wanazo. Lakini hakuniamini na alisadiki kwamba walikuwa wanasema ukweli.

Jumapili hii iliyopita kanisani, nilikuwa na kesi nyingine kama hiyo. Kijana mmoja alikuwa akiniorba ushauri wa uwekezaji kuhusu pesa ambazo

angepata kutoka ng'ambo kama urithi. Sikumruhusu amalize sentensi yake. Nilisema, "Najua, najua, wanataka uwatumie ada ya aina fulani kisha watoe pesa, sivyo?" "Ndio, ulijuaje?" Nilimwambia jambo lile lile, kwamba ni utapeli. Ingawa hakumjua mtu huyo ambaye walimwambia amekufa, na hakuwa na wakili hapa Marekani, bado alipingana nami kuhusu ukweli wa pesa hizo. Kwa nini watu hawa waliangukia mambo kama haya? Kwa sababu wanataka kuwa huru! Hawawezi kuziachilia kwa sababu, katika akili zao, iwapo ni kweli hata kidogo wanazitaka.

Acha nikupe mfano mwagine. Biashara ya huduma za kifedha ambayo mimi na Drenda tunamiliki inashughulikia Marekani nzima. Ni biashara nzuri! Fursa katika kampuni yangu ni nzuri ajabu; nina watu wanaopata mamia ya maelfu ya dola kwa mwaka. Lakini pia kuna mengi ya kujifunza katika biashara yangu. Unashughulikia pesa za watu. Kuna sheria ambazo lazima ujue na mikakati ya kupanga mali unayojifunza.

Nilikuwa nimeweka matangazo kwa redio katika eneo la Columbus, Ohio, kwenye kituo cha redio cha Kikristo cha mtaa nikiomba wasifu, kwa sababu nilikuwa nikitatufuta mawakala wachache wazuri wa kuuza bima. Tulikuwa na takriban watu 50 waliokuja. Badala ya kuwa na mahojiano moja kwa moja, niliamua kuwa na kikao cha maelekezo kwenye hoteli iliyo karibu ili kunisaidia kuchuja wahojiwa. Mkutano huo ulishughulikia fursa kubwa kampuni yetu iliyonayo kibiashara, kushiriki jinsi fedha zinavyofanya kazi na pia kuweka ushauri huu katika mtazamo wa Kikristo. Pia tuliangazia jinsi kampuni ilivyoshughulikia suala la utaratibu, fidia, mafunzo na mahitaji ya leseni. Nilijua kutokana na uzoefu kwamba watahiniwa wangu wengi wangerudi nyuma walipoona kiasi cha kazi kilichohitajika ili kupata \$200,000 kwa mwaka.

Baada ya mkutano, nilikuwa nikitembea kwenye korido ya hoteli hiyo na nikaona kwamba ukumbi wao mkubwa ulikuwa umejaa watu zaidi ya 1,000. Wote walikuwa wamekuja kwa sababu moja. Kampuni maarufu ya biashara ya ngazi mbalimbali ilikuwa ikifundisha jinsi ya kujiunga na kampuni yao. Lakini kwa nini watu walikuwa wengi pale inapolinganishwa na wale 50 waliokuja katika chumba changu? Jibu ni rahisi—pesa! Cha kusikitisha ni kwamba, na kampuni hiyo haikuwa ikisema hivi, lakini dhana ilikuwa kwamba "Nikijiunga nao, basi naweza kuwaelekeza watu watatu, na ghafula, nitakuwa milionea." Sasa, nimeishi muda wa kutosha kujua kwamba mtu yejote anayepata pesa nyingi katika biashara ya ngazi mbalimbali hufanya kazi kwa bidii! Ndio, kuna uwezekano, lakini tena, mtazamo ni kupata pesa rahisi na "Nikiruhusu fursa hii kutoweka, angalia

watu hawa wote hapa, nitakosa fursa kubwa maishani!” Tafadhali usinielewe vibaya. Nina marafiki wengi wazuri ambao wamepata mamilioni kutoka kwa kampuni kama hizi, na kuna kampuni nzuri. Lakini ninaonyesha mtazamo wa mtu wa kawaida anayejiunga na kampuni hizo. Biashara ya pesa za rahisi ni jambo kubwa katika mfumo wa laana ya dunia ya kunusurika.

Ikiwa utatulia kwa muda mfupi na ujiulize ni mara ngapi huwa unafikiria kuhusu pesa, ama kupata au kulinda zile ulizo nazo, utashangaa. Nitasema hivi tena ili upate uhakika tu: Watu wanataka kuacha kukimbia, na wamechoka kuishi maisha ya kunusurika! Mvutio wa wikendi na likizo ni kuacha kukimbia. Mvutio wa kustaa fu ni kwamba hatimaye tunaweza kuacha kukimbia na kufanya kile tunachotaka kufanya. Usinielewe vibaya.

## **USIPOSULUHISHA SUALA LA PESA, UTAKIMBIA CHINI NA JUU KATIKA MFUMO WA LAANA YA DUNIA WENYE MAWAZO YA KUNUSURIKA MAISHA YAKO YOTE.**

Mtazamo wa watu wengi kuhusu maisha sio kwamba wanataka kukaa tu bila kufanya chochote. Wala sisemi hayo ndio mapenzi ya Mungu kwako. La, tuliumbwa ili tuwe watendaji katika kazi yetu, na kusudi letu lililoundwa kwa njia ya kipekee. Cha kuhuzunisha ni kwamba, watu wengi waliacha ndoto zao zamani na sasa wana shughuli

nyingi za kukimbia juu na chini ili kuweza kunusurika.

Nina hakika umesikia mtu akisema hivi, au labda umesema mwenyewe: “Lazima niende kazini leo.” Kweli, kama ulivyo fikiria tayari, watu hawana hisia nzuri “wanapolazimika” kwenda kazini. Lakini, wao hustawi wanapotaka na kupata fursa ya kwenda kazini kwa shauku na bidii katika kile wanachofanya. Lakini hiyo sio kawaida katika maisha ya watu wengi. Badala yake, wangali wanasesma, “Lazima niende kazini leo.” Kulipwa mshahara tu, siku nyingine ofisini tu, siku nyingine ya kunusurika na kuishi maisha ya kiwango cha chini tu. Wengi huanza maisha yao vyema wakiwa na msisimko mwangi. Kazi waliyoichukua ili kulipa bili inakuwa ya muda tu, hadi watakapopata mambo fulani. Lakini wanachogundua ni kwamba maisha yaliingiwa na giza, na mahali fulani katika umri wa miaka arobaini, wanagundua kuwa hakuna njia ya kutoka. Linaitwa janga la miaka ya kati, na kwa mara ya kwanza, wanagundua wamenaswa.

Rafiki yangu, haya si maisha ambayo Mungu alipanga tuishi. Tayari unajua hili. Lakini kukwepa mustakabali huu wa kusikitisha ndio maana mimi na Drenda tumekuwa tukisema kwa miaka mingi kwamba usiposuluhisha suala la pesa, hautapata kusudi lako, kusudi la kipekee la

maisha yako. Usiposuluhisha suala la pesa, utakimbia chini na juu katika mfumo wa laana ya dunia wenyewe mawazo ya kunusurika maisha yako yote.

### **Usiposuluhisha suala lako la pesa, kamwe hutawahi kugundua kusudi la kuumbwa kwako!**

Kwa kulinganisha, hebu tuzungumzie jinsi maisha yako yanaweza kuonekana. Fikiria kitu unachopenda kufanya. Tuseme labda ni mchezo wa gofu. Je! umewahi kusikia mtu akisema, "Doh, lazima niende kucheza gofu leo?" Au umesikia mtu akisema, "Doh, leo ni Ijumaa usiku; ninachukia Ijumaa usiku. Natamani ingekuwa Jumatatu asubuhi, ili nirudi kazini." Au tuseme kitu unachopenda kufanya ni uvuvi. Je! nitawahi kukusikia ukisema, "Doh, lazima niende kuvua samaki leo?" Hapana, bila shaka siwezi kusikia hilo kwa sababu una shauku ya kufanya hilo. Nini kingetokea ikiwa ungeishi maisha yako na shauku na bidii kama hiyo katika yale unayofanya, kwa kuzingatia shauku yako na kupata mahali pako patamu maishani, sio mahali pako pa jasho? Je, ingekuwaje kama ungekuwa na pesa zinazohitajija ili kutunza familia yako na kuishi maisha yasiyo na shinikizo la kifedha? Je, kuna njia kweli ya kufanya hivyo? Drenda na mimi tuligundua kunayo!

*Baraka ya Bwana hutajirisha, wala hachanganyi buzuni nayo.*

—Mithali 10:22

Tazama andiko hili kwa muda mrefu na polepole. Maana yake halisi katika lugha ya Kiyahudi ni mali haswa na hakuna kazi ngumu inayohitajika. Je, unaona hili? Ufalme wa Mungu unatuepusha na mfumo wa kazi chungu na jasho aliotuachia Adamu. Je, kifungu hiki kinaweza kumaanisha kile kinacho sema? Utakubali kwamba ikiwa ndivyo, basi umesoma habari njema ambayo hujawahi kusikia kwa muda mrefu sana. Haswa! Hii ndiyo sababu Isaya 61, ilizungumzia kinabii kile ambacho Yesu angefanya katika huduma Yake:

*Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu; kwa sababu Bwana amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema.*

—Isaya 61:1

Je, habari njema ni nini kwa mtu aliyesawa katika mfumo wa kuishi maisha ya laana ya dunia ya kunusurika? Bila shaka, uhuru wa kifedha! Yesu

anasema kihalisi kwamba Ufalme wa Mungu huleta riziki nje ya mipaka ya mfumo wa laana ya dunia ya kukimbia hapa na pale kwa taabu chungu na kudondokwa jasho. Tuseme ukweli. Unaweza kukimbia kwa kasi fulani tu, na naam, watu wengi, hukimbia kwa bidii sana lakini si haraka vya kutosha kupata uhuru. Nilikuwa nakimbia haraka niwezavyo kwa miaka hiyo tisa ambayo mimi na Drenda tulikuwa na madeni mengi. Mamia ya maelfu ya wateja ambao kampuni yetu imehudumia kwa miaka 27 iliyopita pia walikuwa wakikimbia haraka iwezekanavyo. Hata hivyo, licha ya bidii yao, bado walikuwa wamenaswa katika maisha ya utumwa wa kifedha. Wote walituita kwa sababu walikuwa na utambuzi wa kutisha kwamba hawakuwa na tumaini kifedha, ndoto zao za uhuru wa kifedha zilionekana kuwa ngumu zaidi na zaidi kufikia, na kuishi maisha ya manusuru kulikuwa kumechukua nafasi ya kuwa na maono. Chunguza maneno kupata riziki pamoja nami kwa muda mfupi.

Kupata riziki kusudi lake ni kutimiza maono.

Bila kupata riziki huwezi kuwa na maono kwa sababu bila riziki, kupata riziki, kunafanyika maono yako. Tena, hivi ndivyo watu wengi wanavyoishi—maisha yasiyo na maono. Hii ni hali ya juu ya utumwa wenye udanganyifu.



## SURA YA 7

# MLANGO

Hebu tujikumbushe kwa muda mfupi yale ambayo tumejifunza kuhusu Ufalme wa Mungu. Kwanza, tumejifunza kwamba mwanadamu aliwekwa duniani katika nafasi ya kuitawala dunia. Tuliona katika Waebrania 2:7-8 kwamba hakukuwa na kitu chochote duniani ambacho hakikuwa chini ya mwanadamu. Kwa sababu hii, tuligundua kwamba mwanadamu alikuwa ufunguo au mlango wa ulimwengu. Shetani alijua hili, ndiyo maana aliwalenga Adamu na Hawa katika mpango wake wa kupata mamlaka juu ya dunia. Adamu na Hawa waliposhindwa kupitia kwa mpango wake wa udanganyifu, walifanya dhambi na kukomesha serikali ya mamlaka ya kisheria ya Mungu juu ya maisha yao. Roho wa Mungu, aliywafunika katika uumbaji, sasa ilibidi aondoke. Wakawa uchi sio kimwili tu bali hata kiroho. Ninaweza kufikiria mshtuko waliokumbana nao wakati Roho wa Mungu alipoondoka kwao. Biblia inasema mara moja walianza kusuka majani ya mtini ili kujifunika, maana waliona walikuwa uchi.

Ingawa mwanadamu bado alikuwa na cheo cha kutawala dunia alichopewa wakati wa uumbaji, sasa alikuwa amepoteza mamlaka na uwezo wake wa kutawala ulimwengu kiroho. Kwa sababu alikuwa amechagua kumwasi Mungu na kuchagua kuamini na kujipatanisha na Shetani badala ya Mungu, mwanadamu alikuja chini ya mamlaka ya Shetani na hivyo kupata hukumu ile ile ambayo Shetani (Lusifa) alikuwa ameipata alipotupwa kutoka mbinguni. Hukumu hiyo ilikuwa mahali panapoitwa kuzimu, mahali pa mateso na kutupwa milele kutoka kwa uwepo wa Mungu. Ni lazima ifahamike kwamba kuzimu haikuumbwa kamwe kwa ajili ya mwanadamu au kwa kumfikiria mwanadamu. Haikuwa nia ya Mungu kamwe kwamba mtu ye yote aende huko.

*Kisha atawaambia na wale walioko mkono Wake wa kushoto,  
Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele,  
aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake.*

– Mathayo 25:41

Ili kumwokoa mwanadamu kutokana na hatma hii, Mungu alihitaji kuimarisha tena mamlaka ya serikali Yake duniani. Alilazimika kutafuta njia ya kurudisha mamlaka ambayo Shetani alikuwa ameyashikilia. Kulikuwa na njia moja tu ya jambo hilo kutokea. Mtu ambaye hakuwa na hatia ya dhambi alilazimika kujitolea badala ya Adamu ili kuchukua adhabu ya kifo. Lakini kulikuwa na shida kidogo kwa mpango huo. Kila mwanadamu aliyekuwa duniani, maana ni mzao wa Adamu, alikuwa ametiwa unajisi na dhambi na hivyo hangeweza kubeba Roho wa Mungu na mamlaka Yake. Lakini Mungu alikuwa na mpango wa kushinda tatizo hili. Mpango huo ulihitaji kwamba matakwa Yake ya haki, yaani sheria Yake, iimarishe na kuandikwa duniani ili mwanadamu aliyeishi duniani angeweza kuhesabiwa kuwa mwenye haki kuitia kwa sheria iyo hiyo, kama ingwezekana. Hapo na ndipo tu mwanadamu huyo angeliweza kujitolea kihalali kusimama mahali pa Adamu, huku akichukua adhabu aliyoistahili Adamu juu yake mwenywewe.

Lakini kulikuwa na utata katika dhana hii kwa sababu mtu aliyepaswa kutekeleza mpango huu wa dhabihu hakufaa kuwa mzao wa Adamu, kwa kuwa ukoo huo ulikuwa umechafuliwa na kuwekwa mbali na uwepo wa Mungu. Kwa hivyo mpango wa uokoaji ungewezezanaje? Ili hilo liwezekane, ilimhitaji Mungu kumweka duniani mtu ambaye hakutoka katika ukoo wa Adamu ambaye alikuwa tayari kujitoa kama dhabihu kwa niaba ya mwanadamu. Lakini ulimwengu ulikuwa umepewa Adamu na wazao wake, kwa hiyo kisheria, jambo hilo pia lilikuwa kinyume na sheria. Kulikuwa na njia moja tu ya kutekeleza hili, njia moja tu. Mtu huyo alipaswa kuzaliwa hapa, lakini asiwe wa ukoo wa Adamu.

Kwa mtazamo wa kawaida, unaweza kukubaliana kwamba hili, tena, haliwezekani. Lakini ukweli ni kwamba, kulikuwa na njia. Mungu angeweza kisheria kuweka mbegu ya kiume ndani ya mwanamke duniani ikiwa angeweza kupata mtu ambaye angemwamini kufanya hivyo, na hivyo kumpa Yeye mamlaka ya kisheria. Kumbuka, mwanadamu alikuwa ufunguo wa ulimwengu. Shetani alikuwa ametumia ufunguo huo huo kupata kiingilio katika ulimwengu na kuiba nafasi ya kiroho ya Adamu ya mamlaka juu yake. Ili mpango wa Mungu ufanye kazi na kumthibitishia shetani uhalali

wa mpango huo, ambaye bila shaka angelia sana kuuhusu, Mungu alihitaji kupata mwanamume na mwanamke ambao wangemwamini kupata mtoto wakati jambo hilo halingewezekana kabisa na milele. Wangepaswa kumwamini Mungu kufanya yasiyowezekana.

Kuzaliwa kwa mtoto huyo kungeambatanishwa na ahadi ya hatma yake, kwamba kupitia ukoo wake mataifa yote yangebarikiwa, kwa sababu kupitia ukoo wake Mungu angepata uhalali na mamlaka ya kumleta Yesu katika dunia. Ikiwa kulikuwa na wanandoa ambao wangeweza kumwamini Mungu kufanya hivyo, kuchukua mimba katika tumbo la uzazi lililokufa, huku wakiamini kwamba kupitia mtoto huyo kila taifa lingebarikiwa na kwamba kuzaliwa kwake kungewapa wazao zaidi kuliko mchanga ulioku pwani, basi Mungu angekuwa na uhalali aliohitaji kuweka uzao Wake kwa Mariamu, mama yake Yesu baadaye. Lakini je, Mungu angeweza kupata mtu kama huyo? Jina lake lilikuwa Ibrahimu, baba wa imani yetu.

*Naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate kuwa baba wa mataifa mengi, kama ilivyonenwa, "Ndivyo utakavyokuwa uzao wako." Yeye asiyekuwa dhaifu wa imani, alifikiri hali ya mwili wake uliokuwa umekwisha kufa, (akiwa amekwisha kupata umri wa kama miaka mia), na hali ya kufa ya tumbo lake Sara. Lakini akiiiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu kwa imani, akimtakuza Mungu; huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi.*

– Warumi 4:18-21

Ibrahimu na Sara walimwamini Mungu na kumzaa Isaka wakiwa wazee sana bila uwezo wa kupata watoto. Kwa sababu Ibrahimu ndiye aliyemwamini Mungu, ahadi ingekuja tu kupitia kwa mlango alioufungua Ibrahimu. Yesu angepaswa kuja kupitia ukoo wa Ibrahimu. Subiri niliweke hili wazi kabisa. Ili Mungu amlete Yesu ulimwenguni, ilimbidi aje kupitia ukoo wa Ibrahimu. Ilimbidi! Kuja kupitia kwa Ibrahimu ndio njia pekee iliyokuwa halali. Hii ndiyo sababu ukiitazama sura ya kwanza ya Mathayo, unapata orodha inayochosha ya fulani na fulani akazaa hivi na vile. Sura hii ina sababu ya kuwa ya kwanza katika Mathayo. Inathibitisha ukweli kwamba hapa duniani Yesu alikuwa mzao wa Ibrahimu. Hili lilipaswa kuandikwa hapa duniani ambapo Shetani anadai utawala na mamlaka yake ya kisheria. Ikiwa orodha hii si sahihi au Yesu hakuja kwa kweli kupitia ukoo wa Ibrahimu, basi Shetani angeweza kudai kwamba kuzaliwa na

maisha ya Yesu vilikuwa ulaghai na hakuwa na haki ya kulipa gharama ya dhambi zetu.

Ikiwa unakumbuka vyema, Israeli walikuwa na sheria nyingi zinazokataza ndoa nje ya taifa lao. Kuoa nje ya kabile lao kulikuwa na adhabu ya kifo. Sasa unajua kwa nini ukoo huo ulipaswa kubaki safi na kwa nini waliuchunga kwa uangalifu sana. Naam, kulikuwa na tofauti ilipohusu wanawake kutoka nje ya taifa la Israeli ambao waliolewa na Waisraeli, kwa mfano Rahabu aliyeishi katika jiji la Yeriko ambaye alificha wapelelezi waliotumwa kuipeleleza nchi. Naam, ameorodheshwa hapo katika sura ya kwanza ya Mathayo kwa kuwa alikuwa ameolewa huko Israeli. Lakini unahitaji kuelewa kwamba katika utamaduni wa Kiyahudi ni mwanamume aliyebeba ukoo.

Sasa hebu nibadilishe mazungumzo kidogo. Kuna majadiliano mengi kuhusu muda ambao mwanadamu amekuwa duniani. Je, kuna njia ya kujua jibu kweli? Ndio! Ninaweza kukuhakikishia kwamba ipo. Orodha hiyo katika sura ya kwanza ya Mathayo lazima iwe sahihi. Hakuna mtu aliyesahaulika au mimi na wewe tusingekuwa tunafurahia wokovu tunaoufurahia sasa. Shetani angedai kwamba sio haki. Orodha hiyo lazima iwe kamilifu! Kwa hivyo kwa kuzingatia hilo, unaweza kuhesabu takriban muda ambao mwanadamu amekuwa duniani. Nilifikiri kusema hilo.

*“Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka; nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa.”*

– Mwanzo 12:2-3

Kama unavyoona katika andiko hili, mlango huu wa kuingia katika ulimwengu ambao Ibrahimu aliimarisha ndio mlango wa kisheria Yesu Kristo angelipitia na kuwabariki watu wote duniani. Ingawa Ibrahimu na

## **SASA WALISHI JUU YA LAANA YA KAZI CHUNGU NA JASHO.**

wazao wake walimpa Mungu uhalali na mamlaka yaliyohitajiwa ili kuleta nguvu na ushawishi wa serikali Yake duniani tena, mwanadamu bado alikuwa amenaswa chini ya uzito wa dhambi na kifo cha kiroho

hadi Mungu alipomleta Yesu ulimwenguni, ambapo angelipa gharama ya dhambi ya Adamu. Lakini kimadhubuti lilipokuja suala la riziki, tunaona kwamba Ibrahimu na warithi wake, na wale waliokuwa na alama ya tohara,

walifanikiwa. Sasa waliishi juu ya laana ya kazi chungu na jasho.

*Naye Abramu alikuwa ni tajiri sana kwa mifugo, kwa fedha, na kwa dhahabu.*

– Mwanzo 13:2

Tunaona katika andiko hili mabadiliko makubwa ambayo agano hili lililetu kuhusu riziki. Je, unaona tofauti kati ya kile Mungu alichomwambia Ibrahimu na kile alichomwambia Adamu katika Mwanzo 3:17? Kumbuka, baada ya Adamu kufanya dhambi, Mungu alimwambia kwamba sasa siku zote za maisha yake angekula mazao ya uchungu na kwa jasho la uso wake angekula chakula. Lakini sasa tunaona tofauti kuhusu Ibrahimu. Mungu alisema, “Nami nitakufanya wewe!” Andiko halisemi kwamba Ibrahimu aliachwa atumie uwezo wake mwenyewe na kukimbia juu na chini kiasi cha kutokwa na jasho kwa taabu chungu. Hii inaonyesha kwamba Mungu sasa aliusika. Mungu alisema, “Nami nitakufanya wewe!” Je, tunamwona Ibrahimu akifanikiwa kupitia kwa shida baada ya haya? La hasha!

Ibrahimu alikuwa tajiri! Watoto wake walikuwa matajiri. Ibrahimu aliishi maisha nje ya mfumo wa laana ya dunia. Alikuwa na wingi wa mali! Haikuchukua muda mrefu kabla ya watu kuona tofauti. Tofauti hii iliendelea katika ukoo wake wote. Vizazi vichache baada ya Ibrahimu, mjukuu wake Yakobo alifanya kazi Labani, ambaye alifanya babamkwe wake baadaye. Labani aliona baraka juu ya Yakobo na akajaribu kumlaghai ili asipate mafanikio yake. Lakini Mungu aligeuza mipango yake ya kuiba baraka kwa madhara yake mwenyewe na akambariki Yakobo kwa mali nyingi. Ninachosema ni kwamba ingawa watu walijaribu kuzuia baraka hiyo, hawakuweza. Kadiri warithi walivyodumu katika agano lao na kumwabudu Mungu, Mungu aliwafanikisha.

**ATAKUFUNULIA BWANA  
HAZINA YAKE NZURI, NAYO  
NI MBINGU, KWA KUTOA  
MVUA YA NCHI YAKO KWA  
WAKATI WAKE, NA KWA  
KUBARIKIA KAZI YOTE YA  
MKONO WAKO.**

**– KUMBUKUMBU 28:8A**

Tafakari maana ya kile ninachosema! Huwa ninapata kila aina ya barua na barua pepe kutoka kwa watu wanaoniambia kuwa ninazungumza sana kuhusu pesa. Wananiambia kwamba ufanisi si mapenzi ya Mungu. Wanasisitiza kwamba sote tunapaswa kuteseka maishani kiasi kikubwa ili

kumtumikia Mungu. Nawea kukubaliana na sehemu ya kauli yao. Yesu alisema kwamba ufanisi wetu utatufanya tupitie maudhiko katika Marko 10:30. Jambo la kusikitisha ni kwamba Wakristo wengi wanaamini kwamba Mungu ni mgumu naye hututwika kazi nzito kwa hivyo tunapaswa kuishi maisha ya mateso kama manusuru, wanaoapa kuwa maskini, na kuteseka kupitia kwa magonjwa. La, sivyo, hiyo ni laana ya dunia wala si baraka! Mungu anataka kukuimarisha kifedha.

### **Mungu Anataka Kukuimarisha!**

Bila fedha zako kuwa salama na kuimarishwa, wewe utalazimika kukimbia hapa na pale katika hali ya manusuru maisha yako yote, usiweze kutimiza utume wako wa kiroho, na hivyo kimsingi kuishi maisha ya utumwa. Angalia kile Mungu alichowaambia wazao wa Ibrahimu katika Kumbukumbu la Torati 28:8-13.

*“Bwana ataiamuru baraka ije juu yako katika ghala zako, na mambo yote utakayotia mkono wako; naye atakubarikia katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako. Bwana atakuweka uwe taifa takatifu kwake, kama alivyokuapia; utakaposhika maagizo ya Bwana, Mungu wako, na kutembea katika njia zake. Na mataifa yote ya duniani watakuona umeitwa kwa jina la Bwana, nao watakuwa na hofu kwako. Bwana atakufanya uwe na wingi wa uheri, katika uzao wa tumbo lako, na uzao wa wanyama wako wa mifugo, na uzao wa nchi yako, katika nchi Bwana aliyowaapia baba zako kwamba atakupa.*

*Atakufunulia Bwana hazina Yake nzuri, nayo ni mbingu, kwa kutoa mvua ya nchi yako kwa wakati wake, na kwa kubarikia kazi yote ya mkono wako; nawe utakopesha mataifa mengi, wala hutakopa wewe. Bwana atakufanya kuwa kichwa, wala si mkia; nawe utakuwa juu tu, wala huwi chini; utakapoyasikiza maagizo ya Bwana, Mungu wako, nikuagizayo hivi leo, kuyaangalia na kufanya.”*

Tambua kwamba katika nchi mpya wana wa Israeli bado hawakuwa wameimarishwa ingawa walikuwa na ahadi. Lakini Musa aliwaambia kwamba Mungu angewaimarisha! Ili kuelewa maana ya jambo hili na kile ambacho Mungu alikuwa akijaribu kuwaambia, tafakari mti wa mwaloni. Ukiwa ungali mche, bado haujaimarishwa. Mtu yeoyote anaweza

kuuhamisha wakati wowote na mahali popote anapotaka. Lakini mti huo wa mwaloni unapokua na kukomaa, hakuna mtu anayeweza kuuhamisha. Umeimarishwa.

*Bwana ataiamuru baraka ije juu yako katika ghala zako, na mambo yote utakayotia mkono wako; naye atakubarikia katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako. Bwana atakuweka (atakuimarisha)....*

– Kumbukumbu la Torati 28:8-9a

Kwa hivyo kuimarishwa kifedha kuna mwonekano gani? Mungu anatuambia hapa katika mstari wa 12b-13a:

*Nawe utakopesha mataifa mengi, wala hutakopa wewe. Bwana atakufanya kuwa kichwa, wala si mkia.*

Mungu alisema kwamba angewabariki sana hata wawe wakopeshaji, na wasiwe wakopaji tena. Wangkuwa kichwa wala si mkia. Mkia hauchagui mahali uendako; unakwenda ambapo kichwa kinauongoza.

*Tajiri humtawala maskini, naye akopaye ni mtumwa wake akopeshaye.*

– Mithali 22:7

Mkopaji hajaimarishwa. Yuko chini ya huruma ya mkopeshaji, akifanya kazi kama mtumwa. Lakini Mungu anasema, “LA! Mimi nitakuimarisha! Hakuna mtu atayekuambia uondoke kwa nyumba yako maana itakuwa imelipiwa. Hakuna mtu atakayechukua gari lako, kwa sababu litakuwa limelipiwa. Jikoni yako itajaa vyakula, na utatembea kwa ardhi yako iliyolipiwa, huku ukitimiza utume wako wa kiungu kwa amani kamilifu kifedha. Utaimarishwa!”

## **Mungu Anataka Ufanikiwe!**



## SURA YA 8

# NGUVU YA KUWA MWAMINIFU

Utakachosoma sasa ni kanuni ya Ufalme yenyeye nguvu, kiasi kwamba nilihisi ilistahili kuwa manukuu ya kitabu hiki. Tunaipata katika hadithi na maisha ya Yusufu, mtukuu wa Ibrahimu. Ili kukupa historia fupi, Yusufu alichukiwa na ndugu zake, na walitaka kummaliza. Hakika walitaka kumuua, lakini ndugu mmoja hakutaka kwenda umbali huo; kwa hiyo, badala yake, walimuza kwa wafanyabiashara waliokuwa wakisafiri, nao walimchukua mpaka Misri ambako aliuzwa kwa Potifa, kapteni wa walinzi wa Farao.

Basi Yusufu akaletwa mpaka Misri naye Potifa, akida wa Farao, mkuu wa askari, mtu wa Misri, akamnunua mkononi mwa hao Waishmaeli waliomleta huko. Bwana akawa pamoja na Yusufu, naye akasitawi; naye alikuwa katika nyumba ya bwana wake, yule Mmisri. Bwana wake akaona ya kwamba Bwana yu pamoja naye, na ya kuwa Bwana anafanikisha mambo yote mkononi mwake. Yusufu akaona neema machoni pake, akamtumikia. Naye akamweka awe msimamizi juu ya nyumba yake, na yote yaliyomo akayaweka mkononi mwake.

*Ikawa tokea wakati alipomweka awe msimamizi juu ya nyumba yake, na vyote vilivymo, Bwana akabariki nyumba ya yule Mmisri kwa ajili ya Yusufu. Mbaraka wa Bwana ukawa juu ya vyote alivyokuwa navyo katika nyumba, na katika shamba. Akayaacha yote aliyokuwa nayo mkononi mwa Yusufu; wala hakujua habari za kitu cho chote chake, ila hicho chakula alichokula tu.*

– Mwanzo 39:1-6

Zingatia mstari wa 2a, “Bwana akawa pamoja na Yusufu, naye akasitawi.”

## **MUNGU HANA UHALALI AU MAMLAKA DUNIANI BILA MAPATANO YA KISHERIA, NA AGANO PAMOJA NA MTU ALIYE DUNIANI.**

Hii ina maana gani? Je, Mungu hayuko pamoja na kila mtu? Katika muktadha wa yale ambayo tumekuwa tukiyajadili katika sura zilizopita kuhusu nasaba, jibu ni la. Kumbuka, imani ya Ibrahimu na agano lililoambatana lilimpa Mungu ruhusa kisheria juu ya Ibrahimu na warithi wake—pekee.

Kwa hiyo tunapozungumzia Mungu kuwa pamoja na kila mtu, isichanganywe na Mungu kumpenda kila mtu; Yeye anapenda watu wote. Lakini kwa wale wasio na mahali pa kisheria mbele za Mungu, mikono Yake imefungwa.

*Kwamba zamani zile mlikuwa hamna Kristo, mmeferakana na jamii ya Israeli, wageni wasio wa maagano ya ahadi ile. Mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani. Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo.*

– Waefeso 2:12-13

Tazama andiko hili linazungumzia kutokuwa na agano, kumaanisha kwamba Mungu na nguvu Zake zimekatiliwa mbali kisheria kutoka kwa mtu. Kwa nini? Kwa sababu Mungu hana uhalali au mamlaka duniani bila mapatano ya kisheria, na agano pamoja na mtu aliye duniani. Mstari huu unaweka jambo hili wazi unaposema kwamba bila agano, watu hawana tumaini wala Mungu duniani. Kumbuka kwamba kwa sababu Yesu aliweka agano jipya kwa ajili yetu, sisi ni washiriki wa nyumba ya Mungu na raia wa Ufalme wake mkuu. (Waefeso 2:19) Kwa hiyo sasa, tunapotazama nyuma kwenye andiko letu katika Mwanzo 39, tunaelewa maneno “*Bwana akawa pamoja na Yusufu*” yalimaanisha kwamba kisheria, Mungu alikuwa na ushawishi katika maisha ya Yusufu kuititia kwa agano ambalo babu yake Ibrahimu alikuwa ameweka. Agano hilo la kisheria, lililoruhusu baraka na ushawishi wa Mungu kuwa juu ya Yusufu, lilihinda taabu na mfumo wa jasho na uchungu wa ulimwengu. Ilikuwa halali kwa Mungu kumbariki Yusufu.

Kumbuka kile Mungu alichomwambia Ibrahimu hapo awali, “*Nitakufanya wewe.*” Kwa sababu Mungu alikuwa pamoja na Yusufu, huku akimsaidia maishani, alifanikiwa katika kila jambo alilofanya, kiasi kwamba

bwana wake mpagani, Potifa, aliona tofauti kubwa katika uwezo wa Yusufu ilipoltinganishwa na wanaume wengine wengi aliokuwa amewaona. Ninapaswa kutaja hapa kwamba tunapofanikiwa kwa msaada wa Mungu, watu wanaoishi chini ya mfumo wa laana ya dunia huona tofauti! Potifa alivutiwi sana kiasi cha kumweka Yusufu awe msimamizi wa mali yake yote.

Kuna kanuni nyingi za Ufalme zilizofunuliwa katika kifungu hiki cha maandiko, lakini ile muhimu kabisa ni hii. Ninaiita “Nguvu ya Kuwa Mwaminifu,” au unaweza kuiita “Kanuni ya Potifa.” Inapatikana katika Mwanzo 39:5:

*Ikawa tokea wakati alipomweka awe msimamizi juu ya nyumba yake, na vyote vilivymo, Bwana akabariki nyumba ya yule Mmisri kwa ajili ya Yusufu. **Mbaraka wa Bwana ukawa juu ya vyote alivyokuwa navyo katika nyumba, na katika shamba.***

Nataka uwe na picha wazi ya kilichotokea hapa. Siku moja Yusufu hakuwa msimamizi na keshoye akawa msimamizi. Biblia inataja wakati ambapo badiliko hilo lilitukia. Baraka ya Bwana ilikuja juu ya vitu vyote vya Potifa, mali yake yote! Lakini hakumjua Mungu wa Yusufu na hakuwa sehemu ya taifa la Israeli. Kwa hivyo hili liliwezaje kutokea na inamaanisha nini? Jibu ndilo hili. Potifa alipoweka mali yake chini ya mamlaka ya Yusufu, bila kujua, mali yake ilikuwa chini ya agano ambalo Yusufu alikuwa nalo na Mungu.

### **Vitu vya Potifa, mali yake, na vyote alivyovimiliki vilibadili falme!!**

Wajua, mali ya Potifa bado ilikuwa imefungwa kisheria na mfumo wa laana ya dunia hadi wakati ilipowekwa chini ya uanganlizi wa Yusufu. Potifa alipoweka mali yake chini ya usimamizi na mamlaka ya Yusufu, hakutambua kwamba pia alikuwa akiweka chini ya ushawishi wa baraka za Mungu. Biblia inaendelea kusema kwamba kwa kuwa Yusufu alikuwa msimamizi, Potifa hakuhitaji kujali au kuhangaikia kuhusu chochote isipokuwa chakula alichokula. Hakuwa na wasiwasi wowote! Kwa hivyo Potifa alipaswa kukaza mawazo yake kwa kusudi lake na kazi yake tu kama kapteni wa walinzi wa Misri.

Kuna mengi ya kuona hapa, lakini kilichomfanyikia Potifa bila kutarajiwa ni kile Waebrania 4 inachokiita pumzikio la Sabato, na naam, lipo kwa ajili ya waumini wa Agano Jipyia.

Ukisoma kuhusu Sabato, utagundua kwamba Mungu hakuwaruhusu Waisraeli wafanye kazi yoyote siku hiyo; hakuna jasho wala kazi nzito iliyofanywa. Sabato, bila shaka, ilikuwa siku ya saba ya juma, nayo iliambatana na siku ya saba ya uumbaji. Kumbuka kwamba siku ya saba

**ILITWA SIKU YA SABATO,  
AMBAYO NI PICA YA  
SIKU MWANADAMU  
HANGELAZIMIKA KUJITAHIDI  
KIVYAKE KWA KAZI NZITO  
YA TAABU NA JASHO ILI  
KUWEZA KUISHI.**

ya uumbaji ilikuwa siku Mungu aliyoitangaza kuwa siku ya mapumziko. Haikuwa kwa sababu Mungu alikuwa amechoka bali, kwa sababu alikuwa amekamilisha kazi ya uumbaji. Kila kitu kilikuwa kimekamilika. Mwanadamu aliumbwaa aishi katika siku ya saba, siku isiyo na wasiwasi, na kila kitu mwanadamu alichohitaji kuwepo bila kuhitajika. Lakini bila

shaka, twajua kwamba Adamu alipoteza pumziko hilo alipomwasi Mungu. Kwa kumwasi Mungu, Adamu alikata uwezo wa Mungu wa kumruzuku. Hivyo, alipoteza nafasi ya kupokea riziki ambayo Mungu alikuwa amempa hapo awali. Adamu sasa alilazimika kujiruzuku, huku akitumia wakati wake wote kufanya kazi nzito yenye uchungu na jasho ili kuishi.

Lakini Mungu hakumwacha mwanadamu bila tumaini. Alimpa mwanadamu picha ya pumziko ambalo siku moja angelirejesha. Ilitwa siku ya Sabato, ambayo ni picha ya siku mwanadamu hanelazimika kujitahidi kivyake kwa kazi nzito ya taabu na jasho ili kuweza kuishi. Potifa alipoingia chini ya baraka ya Bwana aliyoibeba Yusufu kuititia kwa agano, alipata fursa ya kupokea kutoka kwa Mungu kuititia kwa Yusufu kisha akapata pumziko. Kila kitu kilishughulikiwa; hakuwa na wasiwasi.

*Akayaacha yote aliyokuwa nayo mkononi mwa Yusufu; wala hakujua habari za kitu cho chote chake, ila hicho chakula alichokula tu.*

– Mwanzo 39:6

Ili kuelewa umuhimu wa siku ya Sabato na kile ambacho Mungu alikuwa akimwonyesha mwanadamu, unahitaji kuuliza swali rahisi. Iliwezekanaje kuwa na Siku ya Sabato? Yaani, chini ya mfumo wa laana ya dunia, mwanadamu alikimbida hapa na pale kila siku ili kuishi. Ikiwa hiyo ni kweli, basi ni kwa nini haikumbidi mwanadamu kufanya vivyo hivyo siku ya Sabato? Je, alipewa riziki gani siku ya Sabato ikiwa hakupaswa kufanya kazi? Hilo ni swali zuri linalopaswa kujibiwa, na katika jibu hilo tunapata

ufunuo mzima wa “baraka ya Bwana” iliyokuwa juu ya Yusufu.

Nafikiri mfano mwema wa kanuni hii unapatikana katika Mambo ya Walawi sura ya 25 Mungu alipokuwa akilifafanulia taifa la Israeli kuhusu Mwaka wa Yubile. Ili kukupa maelezo kidogo, Mwaka wa Yubile ulikuwa kila baada ya miaka 50, na ulikuwa muhimu sana lakini sitazungumzia hilo hapa. Hata hivyo, sehemu ninayotaka uelewe ni kwamba hawakutakiwa kupanda mbegu zao mwaka huo wala mwaka wa 49 maana ulikuwa mwaka wa Sabato. Nataka uelewe wazi hali ilivyokuwa: Israeli waliambiwa wasipande mbegu zao katika miaka ya 49 na 50. Iliwabidi wangoje hadi mwisho wa mwaka wa 51, mara watakapopanda mbegu, ili mimea yao ikomae kisha wavune. Kwa hiyo kimsingi, Mungu alikuwa akiwaambia kwamba wangekuwa na kipindi cha miaka mitatu bila mavuno. Ikiwa ningekuambia kwamba hatalipwa kwa miaka mitatu, unaweza kuwa na wasiwasi kidogo. Naam, Israeli ilikuwa na wasiwasi. Kiasili, hili halingewezekana. Lakini Mungu alikuwa akiwaonyesha jambo fulani.

*“Na kama mkisema, ‘Je! Mwaka wa saba tutakula nini? Angalieni hatutapanda mbegu, wala kukusanya maongeo yetu?’ Ndipo nitawaamria baraka yangu iwe juu yenu mwaka wa sita, nayo utaza matunda hesabu ya miaka mitatu. Na mwaka wa nane mtapanda mbegu, na kuyala yale matunda, akiba hiyo ya zamani, hata mwaka wa kenda, hata matunda yake yatakapoletwa ndani, mtakula hiyo akiba ya zamani.”*

– Mambo ya Walawi 25:20-22

Sabato iliwezekana kwa sababu Mungu aliibariki sehemu ya siku ya sita maradufu, au zaidi ya kutosha. Kitafakari kifungu hicho akilini mwako kidogo. Je, hilo silo ambalo kila mtu anatamani, zaidi ya kutosha? Mungu alipompa mwanadamu sehemu maradufu katika siku ya sita, alikuwa akimkumbusha kwamba Yeye ndiye mtoariziki, naye daima hutoa zaidi ya kutosha. Tuseme ukweli; kuwa na zaidi ya kutosha humwondoa mtu kwa mbio za panya. Kunatutoa utumwani na kutupa fursa ya kuchagua. Muhimu zaidi, kunatuweka huru kutafuta na kufanikiwa katika kusudi na shauku yetu. Hiki ndicho ambacho Potifa alifurahia. Hakuna wasiwasi. Kila hitaji alilokuwa nalo lilitimizwa. Jambo pekee alilopaswa kuzingatia ni kusudi lake. Tena, kama mimi na Drenda tulivyosema, “Usiposhughulikia suala la pesa, kamwe hutaweza kupata kusudi lako.” Lakini kuna habari njema! Pumziko la Sabato bado linapatikana leo, na linatuahidi mahali ambapo mahitaji yetu yatatimizwa na tutafanikiwa wala sio kuishi maisha ya manusuru.

*Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha Yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake (kazi yenye uchungu na mfumo wa kudondokwa na jasho la manusuru), kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi Zake.*

Ufalme wa Mungu ulipita sheria ya ulimwengu ya kazi yenye uchungu na jasho kwa Potifa, na utakufanya vivyo hivyo. Tunapo jifunza jinsi ya kuingia katika Ufalme wa Mungu, tunaweza kufanikiwa na kutimiza kusudi letu. Maisha yanaweza kuwa ya kufurahisha, na yenye shauku na furaha kamili, kweli!

*Baraka ya Bwana hutajirisha, wala hachanganyi huzuni nayo.*  
– Mithali 10:22

Baraka ya Bwana hutajirisha, wala Mungu haongezi taabu pamoja nayo!!! Tunaweza kuishi juu ya taabu chungu na mfumo wa kutokwa jasho wa Mwanzo 3:17. Niliishi chini ya mfumo huo wa zamani wa manusuru kwa miaka mingi hadi nilipo jifunza jinsi Ufalme wa Mungu unavyotenda kazi. Unaweza kujifunza hivyo pia. Mungu yu pamoja nawe! Anaweza kukusaidia! Unaweza kufanikiwa. La, acha niseme vyema: Unahitaji kufanikiwa. Akina Potifa wa ulimwengu, wale wasiomjua Mungu na walioinamishwa chini ya laana ya kazi isiyo na matumaini, na ngumu, huku wakijaribu kuishi, wanatazama. Hawavutiwi na dini yako, majengo ya kanisa lako, au maandiko yako kwa sababu hawaoni chochote zaidi ya ukosefu wako wa majibu. Huwezi kutarajia watu wakusikilize unapowaambia jinsi Mungu alivyo mkuu wakati unaishi katika shinikizo lile lile baya la kifedha na ukosefu na kuendelea kuishi maisha ya manusuru kama wao. La, unapaswa kuonyesha jinsi Ufalme ulivyo kama Yusufu alivyofanya. Sitaki kusikika kuwa mgumu, lakini watu sio wajinga. Wanatafuta majibu.

Sikuwa na sauti ya ushawishi kwa miaka mingi. Hakuna mtu aliyenialika kuwa kwenye televisheni; sikuwa kiongozi wa kanisa la maelfu. Kwa nini? Kwa sababu sikuwa na la kusema, masuluhisho, majibu, wala kuwa na uthibitisho kwamba Mungu alikuwa hai na alikuwa pamoja nami. Nilikuwa nikikopa pesa kutoka kwa familia yangu ili kujikimu. Gari langu lilikuwa limeporomoka, nyumba yangu ilikuwa imeporomoka, na maisha yangu yalikuwa yakisambaratika. Mbona mtu ye yeyote atake kusikia kuhusu ukuu wa Mungu wangu? Naam, nilikuwa njiani kuelekea mbinguni, na mbingu ndiyo jambo kuu zaidi, lakini watu hawangesikiliza jinsi mbingu

ilivyo kuu isipokuwa nidhihirishe mbingu papa hapa ulimwenguni. Sikiliza, ninachosema ni kwamba ikiwa Mungu ni Mungu na Neno Lake ni kweli, basi linapaswa kufanya kazi. Maisha yetu yanapaswa kuonekana tofauti na kuwa tofauti! Tunapaswa kufikia kizazi hiki na ukweli wa Ufalme. Akina Potifa wanatazama.

Kwa hivyo kwa nini nilikipa kitabu hiki manukuu, *Nguvu ya Kuwa Mwaminifu?* Ni kwa sababu Potifa aliingia katika Ufalme wa Mungu na kufurahia pumziko la Sabato pasipo kutokwa na jasho na taabu yenyechungu, wala hofu, na ambapo amani inatawala. Ni mahali ambapo kuishi kama manusuru kunabadilishwa na kusudi na shauku, na umaskini unamezwa na riziki. Aliwezaje kufanya hivyo? Aliweka matatizo na mahangaiko yake chini ya mamlaka ya Ufalme wa Mungu. Kimsingi, ingawa hakutambua alichokuwa akifanya, alijipatanisha na Mungu. Alikubaliana na Ufalme wa Mungu kisha akajiweka chini ya mamlaka Yake. Potifa alikuwa mwerevu vya kutosha kuweka mambo yake chini ya uangalizi wa Yusufu kwa sababu aliona majibu. Unaweza kufanya hivyo pia; ndivyo tulivyofanya mimi na Drenda. Hivyo ndivyo kulungu alivyojitezea, pesa, magari, na nyumba tuliyohitaji kupatikana. Basi subiri nikupe pendekezo. Ikiwa unataka kufurahia yote ambayo Mungu anayo kwa ajili yako, badilisha uaminifu wako. Acha kukubaliana na mashaka na kutoamini kuliko karibu nawe. Badili uaminifu wako na ufurahie Ufalme wa Mungu!

## **ACHA KUKUBALIANA NA MASHAKA NA KUTOAMINI KULIKO KARIBU NAWE. BADILI UAMINIFU WAKO NA UFURAHIE UFALME WA MUNGU!**

chini ya uangalizi wa Yusufu kwa sababu aliona majibu. Unaweza kufanya hivyo pia; ndivyo tulivyofanya mimi na Drenda. Hivyo ndivyo kulungu alivyojitezea, pesa, magari, na nyumba tuliyohitaji kupatikana. Basi subiri nikupe pendekezo. Ikiwa unataka kufurahia yote ambayo Mungu anayo kwa ajili yako, badilisha uaminifu wako. Acha kukubaliana na mashaka na kutoamini kuliko karibu nawe. Badili uaminifu wako na ufurahie Ufalme wa Mungu!



## SURA YA 9

# WAPENI NINYI CHAKULA

Nilipokutana na Don mara ya kwanza, alikuwa amekuja ofisini kwangu akiwa amevunjika moyo sana na kushinikizwa na madeni. Hakuna kitu kilichoonekana kuwa sawa katika maisha yake wakati huo. Nilipoketi na kuzungumza naye, niligundua kwamba alikuwa amechelewa kwa miezi mitatu kulipa kodi ya nyumba na bili zingine alizokuwa nazo. Kulikuwa na matatizo katika ndoa—mke wake alikuwa amechoshwa na hali yao ya kifedha na alikuwa ameanza kupoteza heshima kwa Don kwa kuwa hakuweza kumtunza yeye na watoto wao watano. Ukweli ni kwamba Don alikuwa ameacha kujiheshimu. Na alijawa na maswali.

Kazi yake ilihuisha kuuza bima ya afya katika jimbo lote la Ohio, lakini kutofanikiwa kwake kulikuwa kukimpeleka mahali pabaya kifedha.

Licha ya mambo yote kwenda kinyume na Don, niliona uwezo ndani yake. Alikuwa tayari kujifunza na kufanya kazi. Mambo hayo mawili yenye nguvu yalinivutia vyta kutosha kumwajiri na kuiwekeza katika ustawi wa maisha yake ya baadaye. Mwishowe, ulikuwa uwekezaji uliolipa faida kubwa kwetu sote wawili.

Kampuni yangu changa ilikuwa imeshinda safari ya kwenda Hawaii kutoka kwa mmoja wa wachuuzi wetu, na nilihisi hii ingekuwa nafasi nzuri ya kushiriki na Don kuhusu Ufalme wa Mungu. Ingawa Don alikuwa Mkristo, hakuwa na ufahamu kama wangu. Na ingawa nilijaribu mara kadhaa kushiriki kanuni za Mungu pamoja naye katika eneo hili, hakuonekana kama aliamini nilichosema.

Niliendelea kutafuta njia ya kumvutia Don ambayo ingemsaidia kutambua kwamba yeze pia angeweza kufaulu kwa kujifunza jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi. Lakini, moyo wa Don ulikuwa umevunjika

sana kiasi kwamba ilikuwa vigumu kwake kujiamini na kuamini kwamba mabertiliko yanaweza kutokea kweli. Nilijua safari hii ya Hawaii ilikuwa fursa yangu.

Katika majuma machache kabla yetu kusafiri, tulizungumza kuhusu yale ambayo tungeona na kufanya huko. Hakuna jambo lingine lililokamata usikivu wa Don ila kukamata samaki mkubwa mwenye pembe ndefu mdomoni na rangi ya samawati anayeitwa “marlin” (kwa lugha ya kimombo) katika maji masafi ya Bahari ya Pasifiki. “Hawaii ni mji maalum ambapo samaki huyu hupatikana katika dunia nzima,” Don aliniambia kwa furaha. “Maisha yangu yote nimekuwa na ndoto ya kumkamata samaki huyo.” Kwa mara ya kwanza baada ya majuma kadhaa, niliona mwangaza machoni pa Don. Jambo fulani lilimsisimua, na nilijua msisimko wake ungefingua mlango wa kujifunza jambo muhimu.

“Don,” nikasema, “je, unafahamu kwamba unaweza kujua hakika, wala sio kutumaini, kwamba utamkamata samaki huyo huyo kule Hawaii kwa kuingia katika Ufalme wa Mungu?” Alichanganyikiwa lakini akavutiwa, Don alitaka kujua mengi zaidi, nami nikaendelea na maelezo yangu kuhusu Ufalme. Nilinukuu andiko la Marko 11:24 linalosema, *“Kwa sababu hiyo nawaambia, Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.”* Kwake Don, hili likuwa jambo nzuri sana lisiloweza kuaminika. Nilichukua muda kumsaidia kuelewa Ufalme na jinsi ya kuachilia imani yake. Kwa hivyo, kabla ya kuondoka kwenda kwa safari yetu, yeye na mke wake walitoa matoleo kama vile nilivyotoa kwa ajili ya kulungu wangu, wakaomba kwa makubaliano na kuamini kwamba walikuwa wamempokea samaki wao mwenye rangi ya samawati.

## **“KWA SABABU HIYO NAWAAMBIA, YOYOTE MYAOMBAYO MKISALI, AMININI YA KWAMBA MNAYAPOKEA, NAYO YATAKUWA YENU.”**

**- MARKO 11:24**

Siku ya kuvua samaki ilifika, na tulipokuwa tukipanda mashua, tulimwambia nahodha kwa furaha kwamba siku hiyo tungemkamata samaki wetu mwenye rangi ya samawati. Ingawa alitarajia tuwe na siku yenye mafanikio ya kuvua samaki wengine,

alituhakikishia kwamba uwezekano wa kumkamata samaki huyo mwenye rangi ya samawati ulikuwa mdogo siku hiyo. Akiwa na mashua mbili ambazo watu walilipia kila siku kwenda kuvua kwa muda wa miezi minne, wafanyakazi wake walikuwa wameleta “marlin” mmoja tu wa rangi ya samawati. Hii kwa kiasi kikubwa ilitokana na ukweli kwamba bado msimu wa “marlin” haukuwa umefika, maana samaki hawa huhama. Tulimwambia kwa moyo thabiti na heshima kwamba tungemkamata samaki huyo kisha tukaendelea kuanda vifaa vyetu.

Baada ya masaa masita ya kutafuta samaki kwa uangalifu, hatukufanikiwa hata kidogo, na nilianza kuwa na wasiwasi kwamba hilo lingedhoofisha imani ya Don. Katika wasiwasi wangu nilimuuliza swalii kwa sauti ya juu. “Don,” nikamuuliza kutoka mahali nilikuwa nimeketi kwenye daraja lililokuwa juu yake, “hebu nikuulize swalii. Ulimpokea samaki wako wa rangi ya samawati lini, atakapotokea au tulipoomba?” Kwa ujasiri, Don alijibu kwa nguvu, “Gary, hiyo ni rahisi. Nilimpokea nilipoomba.” Nilisisimka na kujituliza niliposikia jibu lake. Hapo ndipo nilipojua Don alikuwa ametilia maanani maagizo yangu na kudhamiria kumkamata huyo “marlin”.

Baada ya dakika chache, kamba ya nguzo ya Don ilianza kutoa sauti huku nguzo ikiinama kwenda baharini na wenziye wakapiga kelele, “Samaki!”

“Usifurahi sana,” nahodha alionya. “Ni samaki mkubwa sawa, lakini sio “marlin” yenyeye rangi ya samawati. Samaki hao huja juu kabisa na kuruka angani kwa nguvu, lakini huyu anakaa ndani kabisa. Dakika zilizidi kuyoyoma huku Don akiendelea kupambana na yule samaki ambaye bado hakuwa amekaribia juu ya maji ili aweze kuonekana. Don na samaki walikuwa wamechoka lakini samaki aliacha kupigana. Mimi na Don hatukustaajabu “marlin” mkubwa mwenye rangi maridadi ya samawati alipojitokeza, lakini kila mtu mwagine katika mashua alipigwa na butwaa.

Picha ya Don na samaki wake imekaa ofisini kwangu hadi leo kama ushuhuda kwa wengine na kumbukumbu ya mara kwa mara kwangu ya ukweli kuhusu Ufalme. Kwa wengine alioneckana kuwa samaki wa kawaida tu. Lakini kwa Don, alimaanisha mengi zaidi. Ikiwa Ufalme ulifanya kazi hivi, bila shaka ungefanya kazi kwa kila kitu kingine alichohitaji maishani. Kwa Don, huo ulikuwa mwanzo tu wa kutambua mabadiliko ambayo Ufalme wa Mungu ungekuwa nayo maishani mwake.

Rudi nyuma miaka elfu chache na utajifunza kuhusu mtu aitwaye Nikodemo, ambaye alimhoji Yesu hasa kuhusu Ufalme wa Mungu. Sura ya

3 ya kitabu cha Yohana inaonyesha jibu la Bwana, “*Upopo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho*” (mstari 8). Siku ile njema ndani ya mashua na Don ni mfano mzuri wa jambo hili.

## **KAMA VILE UPEPO USIVYOWEZA KUONEKANA LAKINI ATHARI YAKE INAONEKANA KATIKA ULIMWENGU WA ASILI, VIVYO HIVYO UFALME WA MUNGU NI HALISI NA UNA ATHARI KATIKA ULIMWENGU WA ASILI.**

za Ufalme wa Mungu, tunabadili maisha yetu kama Don.

Sawa, swali ni hili. Je, huyo samaki alijitokezaje? Kuna jibu la swalii hili. Hatuwezi kusema ni Mungu tu aliyetenda hilo. La, tunahitaji kujua jinsi tulivyojua kwamba angejitokeza. Unahitaji sana kujua hili kwa sababu kunaweza kuwa na siku ambapo unahitaji samaki wako au gari au mboga tu. Ukweli ni kwamba jambo muhimu katika hadithi hii sio uvuvi kama vile ile yangu ya uwindaji isivyohusu kulungu. Hadithi hii inatupa ufahamu kuhusu Ufalme na jinsi unavyotenda kazi. Kulikuwa na sababu ya yule samaki mkubwa kujitokeza! Yesu alitumia muda mwingi kuwafundisha wanafunzi Wake jinsi Ufalme uliviyotenda kazi, lakini zaidi ya kuzungumza kuhusu, aliudhihirisha.

Tafadhalii zingatia jambo hili. Ufalme hautendi kazi kama ulimwengu uliokulia. Kwa kweli hutaweza kuufahamu kabisa kwa akili yako. Unafanya kazi kwa misingi ya kisheria, lakini sheria tofauti na zile tulizozoea hapa ulimwenguni. Lakini tunaweza kujifunza sheria hizo. Yesu alitumia muda mwingi kudhihirisha na kufundisha kuhusu sheria hizi za Ufalme popote alipoenda. Mojawapo ya hadithi ninazozipenda sana ambapo Yesu alidhihirisha Ufalme iko katika Marko 6. Ni hadithi inayojulikana sana ambapo Yesu aliwalisha wanaume 5,000 na mikate mitano na samaki wawili. Ingawa nimesikia hadithi hii mara milioni kanisani tangu utotonii, hakuna mtu aliywahi kunieleza ni kwa jinsi gani Yesu aliweza kufanya hiyvo.

*Hata zilipopita saa nyingi za mchana, wanafunzi Wake walimwenda, wakasema, "Mahali hapa ni nyika tupu, na sasa kunakuchwa; uwaage watu hawa, ili waende zao mashambani na vijijini kandokando, wakajinunulie chakula."*

*Akajibu, akawaambia, "Wapeni ninyi chakula."*

*Wakamwambia, "Je! Twende tukanunue mikate ya dinari mia mbili ili tuwape kula?"*

*Akawaambia, "Mnayo mikate mingapi? Nendeni mkatazame."*

*Walipokwisha kujua wakasema, "Mitano, na samaki wawili."*

*Akawaagiza wawaketishe wote, vikao vikao, penye majani mabichi. Wakaketi safu safu, hapa mia hapa hamsini. Akaituwa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama mbinguni, akashukuru, akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi Wake wawaandikie; na wale samaki wawili akawagawia wote. Wakala wote wakashiba. Wakaokota vipande vilivyomegwa vya kuweza kujaza vikapu kumi na viwili; na vipande vya samaki pia. Na walioila ile mikate wapata elfu tano wanaume.*

– Marko 6:35-44

"Yesu, tuna tatizo. Watu wana njaa na wasipoondoka sasa, watafika manyumbani mwao wakiwa wamechelewa sana; nasi tuna wasiwasi." Yesu aliwaambia nini? Je, aliwaambia "Doh, Mungu wangu, mnasema vyema, nilikuwa nimesahau kabisa kwamba wakati umekwisha; tufunegeni mkutano mara moja?" La, aliwaambia, "Wapeni ninyi chakula." Eti nini? Biblia inasema wanaume 5,000 walikuwepo, lakini ukihesabu wanawake na watoto labda kulikuwa na watu 20,000. Kulisha kundi hilo la watu, hata kama ungekuwa na rasilimali tayari, ingekuwa kazi kubwa, kazi isiyowezekana. Nina hakika wanafunzi hawakuamini alichokuwa akisema Yesu. Jibu lao kwa suluhu Lake linatoa ufahamu wazi wa hali ya kawaida ya mawazo katika ulimwengu. "Lakini, Yesu, kufanya hivyo kutagharimu mshahara wa miezi minane! Je, tunapaswa kutumia kiasi hicho cha pesa kununua mikate?" Kwanza kabisa, tazama jinsi walivyohusisha mara moja tatizo lao la ukosefu wa maandalizi na miezi minane ya mfumo wa laana ya dunia ya kiuchumi, kazi nzito yenyе uchungu, na jasho.

Siku moja nilikuwa nikiomba kisha Mungu akaniambia kwamba nilikuwa na mawazo ya kimwili. Nilichanganyikiwa; hiyo ilimaanisha nini? Je, nilikuwa na tatizo la tamaa mbaya? La, alikuwa akizungumzia mawazo yangu na jinsi nilivyokuwa nikizuiiliwa kwa sababu mfumo wa mawazo ya laana ya dunia ulikuwa ukichuja siku zangu za usoni kwa kuwaza kuhusu

jinsi ningelivyoweza kujiendeleza mwenyewe haraka. Sote hufanya hivyo. Ikiwa tunahitaji nyumba mpya, huwa tunataka kujuwa gharama yake, kisha tunahesabu mara moja ikiwa tunaweza kuimudu. Tuipigeje hesabu hii? Kupitia kwa ufahamu wa laana ya dunia wa jinsi tunavyoweza kukimbia kwa kasi. Hebu tuseme, mimi hulipwa dola 15 kwa saa moja, mara 40 kwa juma nzima ni sawa na ... “Lo, siwezi kuimudu nyumba hiyo hata kidogo.” Kwa hivyo tunaweka jambo hilo kando kama lile lisilowezekana. Tukichuja kila wazo kupitia kwa kichujio cha kasi gani tunaweza kukimbia, KAMWE hatutaingia katika njia ya Ufalme ya kuishi kwa sababu Mungu hafungwi na mfumo huo. Mungu alikuwa akiniambia kwamba ikiwa nilitaka kuhusisha Ufalme, ningepaswa kuanza kuwaza mawazo ya Ufalme—kwamba mambo yote yanawezekana!

Hapo ndipo wanafunzi walikuwa waliposema, “Hiyo ingegharimu mshahara wa miezi minane.” Kimsingi, walichokuwa wakisema ni kwamba haingewezekana kuwalisha watu wengi kiasi hicho.

Hebu nifafanue jinsi maneno ya Yesu, “Wapeni ninyi chakula,” yaliviyosikika kwao. Tuseme mimi ni mchungaji wako, na umepitia nyakati ngumu na umechelewa kulipa rehani yako. Uko nyuma miezi mitatu na uko karibu kupoteza nyumba yako. Kwa hivyo umekuja kwangu na kuniuliza kama kanisa linaweza kukusaidia kwa kukulipia ile miezi mitatu. Kisha nimekuambia kwa utulivu sana, “Nina wazo bora zaidi. Kwa nini usiilipie malipo yote tu, ili usiwe na malipo ya kila mwezi?” Kisha unaniangalia na macho yanayosema, “Sidhani umeelewa ninachosema.” “La Mchungaji, nafikiri umekosea. Hatuna pesa yoyote; ndiyo maana tumekuja kwako. Tunahitaji kanisa litusaidie ili tuweze kulipia ile miezi mitatu tu.” Tena, ninakutazama kwa utulivu sana na kusema, “La, ninaelewa unachosema, na nimekupa suluhisho nzuri. Unapaswa kufanya malipo yote, na hivyo hutakuwa na malipo yoyote.” Kama vile mashine ya mpira wa pini inavyotoa sauti wakati inahitaji kuinamishwa, unaweza kufikiri mimi ni kichaa.

Basi, nafikiri hivyo ndivyo wanafunzi walivyohisi. “Yesu, huna nia ya dhati ya kuwalisha watu hawa 20,000, sivyo? Hilo haliwezekani. Hatuna rasilimali za kufanya hivyo. Na tukipanga mpango wa kwenda kufanya kazi kwa bidii ili tupate pesa hizo, kisha tupange mabehewa na kamati kuenda kununua mikate, tukirudi, kila mtu atakuwa amekufa. Hata kama tungekuwa na pesa, hatuna wakati unaohitajika ili kutekeleza hili. Hivi ndivyo tunavyoitikia mambo yasiyowezekana kiasili wakati hatuoni jinsi yanavyoweza kutokea. Wakati hatuna riziki, maono yetu hufa.

Yesu hakuwaacha wanafunzi pale katika hali hiyo bila majibu, na

hangewaambia wawalishe watu ikiwa hakukuwa na njia ya kufanya hivyo. Alikuwa anataka kuwaonyesha mfumo mwingine—utendaji wa Ufalme. Yesu alishika usukani huku wanafunzi wakiwa wamechanganyikiwa.

“Mnayo mikate mingapi? Nendeni mkatazame,” Yesu alisema. Wanafunzi walirudi wakasema, “mitano na samaki wawili.” Mara baada ya samaki wawili na mikate mitano kupatikana, Yesu aliwaambia wanafunzi wamletee. Alichukua mkate na samaki na kuwabariki kisha akawarudishia moja kwa moja. Kwa macho ya kawaida, hakuna kitu kilikuwa kimebadilika, lakini katika ulimwengu wa kiroho, jambo la maana sana lilikuwa limetukia, jambo ambalo ni muhimu katika kuelewa Ufalme. Kisha Yesu akaagiza wanafunzi wawagawie watu mikate na samaki, nao wakatazama kwa mshangao chakula kikiongezeka mbele ya macho yao na kuwalisha watu wote 20,000 mpaka wasiweze kumeza hata chembe nyingine ya chakula. Ni nini kilichotokea? Kilifanyikaje?

Ili kujua, tunahitaji kurudi nyuma kidogo na kuchunguza kwa ukaribu maelezo ya tukio hili. Neno “kubariki” linamaanisha kutenga au kuweka wakfu. Kwa hiyo tunaweza kusema kwamba Yesu aliponena juu ya chakula na kukibariki, mkate na samaki vilitengwa kutoka kwa ufalme mmoja hadi mwingine. Katika ulimwengu wa asili, kulisha watu 20,000 na mikate mitano na samaki wawili haiwezekani. Lakini katika Ufalme wa Mungu, mambo yote yanawezekana. Hadithi hii haiishii hapa. Kabla ya yote kuisha, wanafunzi walikusanya vikapu 12 vya vipande vilivyosalia. Mikate mitano na samaki wawili ambao hawangetosha viliwalisha na kushibisha watu 20,000 na kukawa na chakula zaidi mwishoni? Hiyo ndiyo njia ya Ufalme, kuwa na vya ziada!

Kama mwanasayansi wa mambo ya kiroho, nilipotazama kwa makini hadithi hiyo, niliona fomula ile ile ambayo Mungu alinipa na kulungu. Kupitia kwa uwindaji wangu wa kulungu, Mungu alinifundisha kutoa kwanza kwa Ufalme wa Mungu sehemu ya chochote nilichohitaji. Hiki ndicho yule kijana alichofanya alipotoa mikate na samaki wake. Aliviweka chini ya mamlaka ya Ufalme wa Mungu, navyo vikazidisha, na kuwalisha watu 20,000 na vikapu 12 vikabaki. Tazama kwamba mikate ilizidisha ikawa mikate, na samaki wakawa samaki. Hivi ndivyo Ufalme unavyofanya kazi. Nikitoa matoleo ya samaki katika Ufalme nitavuna samaki waliozidishwa. Lakini viyi ikiwa ninahitaji samaki lakini sina samaki wa kutoa? Jibu—pesa! Kumbuka, pesa ndizo zinazotumika katika biashara. Mimi na wewe “hutamka” neno pesa kila siku. Tunazitaja tunapotamka vitu kama maziwa, nyumba, nguo, mkate, na kitu chochote kingine tunachohitaji kila siku.

Pesa basi hufanyika kile tunachohitaji. Ndivyo ilivyo tunapotoa matoleo; tunataja pesa. Badala ya kwenda dukani na kununua samaki ili kutoa

**MUNGU ALINIFUNDISHA  
KUTOA KWANZA KWA  
UFALME WA MUNGU  
SEHEMU YA CHOCHOTE  
NILICHOHITAJI.**

matoleo, tunaweza kutoa pesa tu. Hili linawenza kutokea katika utoaji wako tu, lakini sio katika zaka yako, kwa sababu Mungu tayari aliipa jina. Sheria hii hii ya kuzidisha iko dhahiri katika Luka 5.

*Ikawa makutano walipomsonga wakilisikiliza neno la Mungu, Yeye alikuwa amesimama kando ya ziwa la Genesareti, akaona vyombo viwili vimekaa kando ya ziwa, lakini wavyu wametoka, wanaosha nyavu zao. Akaingia katika chombo kimoja, ndicho chake Simoni, akamtaka akipeleke mbali kidogo na pwanu. Akaketi, akawafundisha makutano ali chomboni. Hata alipokwisha kunena, alimwambia Simoni, “Tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki.”*

*Simoni akajibu akamwambia, “Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno Lako nitazishusha nyavu.” Basi, walipofanya hivyo walipata samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika; wakawapungia mikono washirika wao walikuwa katika chombo cha pili, waje kuwasaidia; wakaja, wakavijaza vyombo vyote viwili, hata vikataka kuzama.*

– Luka 5:1-7

Kama wanasayansi wa mambo ya kiroho, hebu tuichunguze hadithi hii kwa ukaribu. Je, samaki hao walijitokezaje? Je, unaliona jambo hili? Yesu alitembea kando ya ufu na akapata mashua ambayo alitaka kutumia kuhuburia umati kutoka humo. Alimuuliza Petro, mwenye mashua, kama angeweza kuitumia na Petro anasema, “Hakika.” Hata hivyo walikuwa wamemaliza kuitumia; walikuwa wamevua samaki usiku kucha na hawakupata chochote. Baada ya Yesu kutumia mashua, alimwambia Petro arudi na avue samaki katika kilindi cha maji. Nina hakika kwamba hili lilimshtua Petro, maana alijibu, “Yesu, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu.” Petro alikuwa mtaalamu wa kuvua samaki. Kulingana na uzoefu wake, samaki hawakuwepo. Haikuwa na maana katika asili kurudi kuvua. Tayari walikuwa wameweka vifaa vyao na kumaliza kusafisha nyavu zao.

Siamini kwamba Petro angefanya hivyo isipokuwa alikuwa amesikia mahubiri ya Yesu ya saa nzima ambayo labda yalimgusa kwa njia ambayo hakuwa amewahi kuguswa hapo awali. Kwa hivyo alisema, "Lakini kwa neno Lako nitazishusha nyavu." Petro alirudi kuvua na kuwakamata samaki wengi sana nyavu zake zilikuwa karibu kukatika na mashua yake karibu izame. Akawaita wenzake waliokuwa bado ufukweni, wakaja na nyavu zao zilikuwa karibu kukatika na mashua yao karibu izame pia. Biblia inasema Petro alishangaa!

Hili lilitokeaje? Je, kuna vidokezo? Je, tunaweza kupata ufahamu? Kwa muhtasari, ni nguvu ya kanuni ya uaminifu tulioizungumzia hapo awali. Petro alipomruhusu Yesu atumie mashua yake ya uvuvi, mashua na biashara zilibadili falme. Biashara hiyo ilitoka chini ya mamlaka ya mfumo wa laana ya dunia na ikawa chini ya mamlaka ya Ufalme wa Mungu. Kwa sababu ilikuwa chini ya mamlaka ya Ufalme, Mungu alikuwa na uhalali wa kumpa Yesu neno la maarifa kuhusu eneo kamili ambapo samaki walikuwa; "huko kwenye kina kirefu cha maji."

Kwa hivyo hebu tuchambue tukio hili. Yesu aliazima mashua ya uvuvi kutoka kwa Petro ambaye alikuwa ametoka kuvua samaki usiku kucha bila matokeo. Katika kubadilishana huku, mashua ilikuja chini ya mamlaka ya Ufalme wa Mungu. Kisha Yesu akawa na ufahamu kuhusu mahali samaki walikuwa kwa njia ya Roho Mtakatifu. Akaielekeza mashua ya Petro mahali hususa. Mashua ya Petro ilijaa samaki kiasi cha kuzama. Jambo hilo hilo liliwafanyikia washirika wake pia. Kwa hivyo samaki walikamatwaje? Kwa maagizo moja kwa moja kutoka mbinguni. Tukubaliane kwamba mtu yejote anaweza kukamata samaki ikiwa anajua mahali walipo. Tafakari kile tulichosema awali. Mungu anajua kila kitu; anaweza kukusaidia na kukuambia la kufanya.

Tulipokuwa maskini mimi na Drenda na tukaanza kujifunza kuhusu Ufalme, alinipa ndoto usiku nianzishe biashara ambayo sikujua nianze vipi. Biashara hiyo bado inaendelea baada ya miaka 28, huku ikizalisha mamia ya maelfu ya dola kwa mwaka ya mapato halisi. Katika miaka hiyo 28, hilo limenipa fursa ya kutoa mamilioni ya fedha katika huduma na kusaidia watu. Kwa jinsi gani? Nilisikia kutoka mbinguni, na wewe unaweza pia! Hebu nikupe mfano.

Nilikuwa na kongamano la jioni tano kuhusu Ufalme wa Mungu miaka michache iliyopita. Baada ya jioni ya pili, mwanamume anayeitwa Chris alikuja kwangu na kuniomba nimuombee. Nilimuuliza alihitaji maombi kuhusu nini. Kisha akaniambia hadithi yake. Alikuwa akifanya

biashara na mtu aliyeiba pesa kutoka kwa biashara yao, na kuiharibu. Alikuwa na umri wa miaka 40 tu, katika ndoa yake ya nne, na mambo hayakuwa sawa. Aliniambia alikuwa amevunjwa moyo sana kiasi kwamba alichukua bunduki iliyojaa risasi kisha akajizungusha kwa gari hapa na pale, na kusimama kwa kituo cha petroli kilichofungwa akiwa na nia ya kujiua.

Ilikuwa yapata saa tisa usiku, akiwa amekaa na ile bunduki iliyosheheni, wakati simu yake ya mkononi ililia. Akaitambua namba hiyo mara moja. Ilikuwa ni mpenzi wake wa zamani. Hakika hakutaka kuzungumza naye, hivyo hakujibu. Ililia tena, na tena, na tena. Ililia mara 11 ambapo hatimaye Chris aliamua kujibu. Maneno ya kwanza kutoka kinywani mwa mpenzi wake wa zamani yalikuwa, “Uko wapi, na unafanya nini?” Chris alipomwambia, mpenzi wake wa zamani alisema, “Usisogee; naja sasa hivi!” Inaonekana, mpenzi wake wa zamani alikuwa ametoa maisha yake kwa Mungu na alitaka kushiriki hili na Chris. Ajabu ni kwamba, alihisi umuhimu wa kumfikia Chris saa tisa ya usiku, na Chris alipokosa kumjibu, aliendelea kujaribu kumpigia simu.

Rafikiye Chris alipojitokeza, alimwongoza Chris kwa Bwana, na maisha ya Chris yalibadilika sana. Kila kitu kilianza kuwa bora. Alipata kanisa zuri, ndoa yake ikaanza kuimarika. Kila kitu kilikuwa kikienda vyema isipokuwa mapato yake. Chris hakuwa na kazi, na hilo ndilo aliloniomba niliombee. Kongamano nzima, nilifundisha hasa kile ninachokuambia katika kitabu hiki, jinsi Ufalme unavyoweza kufanya mambo ya ajabu kupita uwezo wetu wenywewe.

Chris alipofikiria jinsi Roho Mtakatifu anavyoweza kuntuongoza na kutusaidia katika mwelekeo na mawazo, ghafla alipata wazo. Kwa kweli hakuwa na njia nyingine ya kupata fedha lakini alikuwa mtaalam wa kutengeneza keki ya jibini ya kifahari yenye msingi wa kiafya, ambayo alijua ndio bora zaidi aliyojua kutengeneza. Hakika Chris alijulikana na marafiki zake wote kama mtu aliyetengeneza keki ya jibini bora zaidi kushinda zote. Mara nyingi alikuwa ameenda katika maduka ya vyakula vya afya, na kuonja baadhi ya bidhaa zao zilizookwa lakini zote hazikupendeza. Chris hakuwa na njia nyingine, na alihisi huo ndio uliokuwa uamuvi mzuri aliokuwa nao, kuuza keki za jibini. Alikuwa na hakika kwamba ikiwa angepeleka moja ya keki zake kwenye duka hilo la vyakula vya afya na wakaionja, wangetaka kuiuza. Alikuwa na uhakika kwamba ingeuzwa vyema kuliko keki zao. Hivyo ndivyo hasa alivyofanya. Aliandaa keki ya jibini kisha akaipeleka kwenye duka la chakula cha afya bila kuwajulisha kwamba alikuwa akija. Katika wakati huo huo wa kipekee, Mkurugenzi Mtendaji wa maduka hayo

ya vyakula vya afya alikuwa akilitembelea eneo hilo. Mkurugenzi Mtendaji alikubali kuonja keki hiyo na kumpa majibu.

Jioni hiyo Chris alirudi baada ya mkutano kuzungumza nami tena. Aliniambia alichokuwa amefanya kisha akaniomba niombe pamoja naye tena juu ya kuwa na mkataba na duka hilo la chakula cha afya. Naam, siku iliyofuata Chris alikuja tena, na alikuwa na msisimko mwingi sana! Aliniambia Mkurugenzi Mtendaji alimtaka aoke keki za jibini sio tu za duka lile moja bali pia za maduka yao yote. Mkurugenzi pia alimuuliza ni kitu gani kingine alichojua kuoka. Chris alishtuka! Ajabu ni kwamba, Mkurugenzi Mtendaji alikuja kwa kongamano jioni ya mwisho, ambapo alitoa moyo wake kwa Bwana na kubatizwa kwa Roho Mtakatifu. Nilipokea barua kutoka kwake baada ya majuma mawili iliyosema kwamba alitaka kutoa matoleo kwa Ufalme wa Mungu. Alitoa asilimia kumi ya hisa za kampuni yake kwa huduma yetu, *Faith Life Now*. Ajabu! Mungu anaweza kuchukua wazo na kufanya jambo lisilo na kitu kuwa kitu kikubwa.



SURA YA 10

# KUSANYA, WALA USITOKWE NA JASHO

Umewahi kuona farasi katika majira ya joto baada ya kukimbia kwa muda mrefu? Wao hujawa na jasho linalofanana povu. Unaweza kutambua kwamba walikuwa wamefanya kazi kwa bidii. Kila wakati mimi huulizwa, “Gary, unasema kwamba sitakiwi kufanya kazi?” La, sikusema hivyo na wala Neno la Mungu halisemi hivyo. Lakini kuna tofauti kubwa katika jinsi unavyofanya kazi. Kwa mfano, tafakari hadithi tuliyosoma kuhusu Petro na wenzake waliokuwa wakivua na jinsi mashua mbili zilivyojaa samaki kiasi cha kukaribia kuzama. Walikuwa wamehanganya usiku kucha wakijaribu kuvua samaki bila mafanikio. Kisha Yesu akaja akawaonyesha mahali samaki walikuwa kupitia kwa neno la ujuzi. Walifanya kazi lakini ilikuwa kazi tofauti kabisa. Naam, walifanya kazi kwa bidii walipokuwa wakivuta nyavu zilizokuwa zimejaa samaki. Lakini je, walikuwa wakivua samaki?

Najua nabadilibadili maneno kidogo hapa. Lakini kwa lugha ya Kimombo huwa tunatumia neno kuvua kwa mambo mengi. Mwanamke alikuwa akivua (akitafuta) kupata pongezi. Mwanamume aliingiza mikono mifukoni mwake, huku akivua (akitafuta) funguo zake. Huwa tunatumia neno kuvua tunapomaanisha kutafuta kitu. Kwa hiyo je, Petro alikuwa akivua (akitafuta) samaki? Ninapoenda kuwinda, nilikuambia huwa ninapata kulungu wangu baada ya takriban dakika 40. Je, ninawinda? Kwa maneno mengine, ikiwa unajua samaki wako wapi, je, utavua? Ikiwa ninajua nitapata kulungu, je, hiyo ni kuwinda? Ninasema hivi ili uelewe tofauti. Ndio, ninafanya kazi, lakini sifanyi kazi kwa bidii usiku kucha bila

kupata kitu. Kimsingi, ninapokuwa na yale ninayohitaji maishani, ninaanza kujishughulisha na biashara ya Baba yangu na kusudi langu.

### **Naliita Kukusanya!**

Petro alipomjia Yesu kumuuliza jinsi wangelipa kodi zao katika Mathayo 17:27b, Yesu alisema yafuatayo:

*“Enenda baharini ukatupe ndoana, ukatwae samaki yule azukaye kwanza; na ukifumbua mdomo wake uitaona shekeli ichukue hiyo ukawape kwa ajili Yangu na kwa ajili yako.”*

Tazama Yesu hakusema, “Sawa, Petro, tuna kodi ya kulipa. Nitakuambia jambo, nenda mjini kwa muda wa miezi mitatu hivi, utafute kazi, upate pesa, kisha uwasiliane nasi baada ya kupata pesa za kulipa kodi yetu.” La, Yesu hakusema hivyo. Kwa nini? Kwa sababu Petro angelazimika kuacha kazi yake na kuanza kutafuta pesa na hivyo kurudi kwenye mfumo wa mawazo ya laana. Badala yake, Yesu alituonyesha jinsi Ufalme unavyofanya kazi na jinsi tunavyopaswa kutenda tukiwa hapa duniani. Jibu kwa Petro ni jibu lako pia. Yesu alimwambia Petro mahali ambapo riziki hiyo ilikuwa, njia aliyohitaji kutumia ili kuzipata, na kile hasa alichopaswa kutafuta. Kile Petro alichopaswa kufanya tu ni kwenda kuzikusanya.

Tunapomtazama Yesu pamoja na wanafunzi Wake, walishangaa na kushtuka kila mara walipoona Ufalme ukitenda kazi. Yesu alipounyausha mtini kwa maneno Yake katika Marko sura ya 11, Biblia inasema Petro alishangaa. Lazaro alipotoka kaburini baada ya kufa kwa siku nne, walishangaa. Petro, Yakobo, na Yohana walipokamata samaki hao wote, walishangaa. Drenda na mimi tumekuwa tukishangazwa, na midomo yetu kuwa wazi, tukisema, “Je, umeona hilo?” kila mara kwa miaka mingi tunapoendelea kujifunza zaidi na zaidi kuhusu jinsi Ufalme unavyotenda kazi. Tunapozungumza kuhusu kukusanya kwa msaada wa Roho Mtakatifu, sina budi kukupeleka kwenye Mathayo sura ya 6. Biblia yangu ina kichwa kidogo juu ya kifungu hiki, kinachosema, “Usiwe na wasiwasi!” Napenda hilo.

*“Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharaau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali.*

*Kwa sababu hiyo nawaambieni, Msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini; wala miili yenu, mvae nini. Maisha je! Si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi? Waangalieni ndege wa angani, ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi je! Si bora kupita hao? Ni yupi kwenu ambaye akijisumbua aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja?*

*Na mavazi, ya nini kuyasumbukia? Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo; hayafanyi kazi, wala hayasokoti nami nawaambia, ya kwamba hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo la hayo. Basi, ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo, na kesho hutupwa kalibuni, je! Hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba?*

*Msisumbuke, basi, mkisema, ‘Tule nini? Au Tunywe nini? Au Tuvae nini?’ Kwa maana hayo yote Mataifa huyatufuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa. Basi msisumbukie ya kesho; kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyeue. Yatosha kwa siku maovu yake.’*

– Mathayo 6:24-34

Yesu anasema huwezi kutumikia mabwana wawili. Unaweza kufikiri unaweza lakini huwezi. Utampenda mmoja peke yake. Na nitakuambia ni yupi. Ni yule unayeamini atayatosheleza mahitaji yako. Mungu aliponena nami katika ile nyumba kuukuu pale shambani kwamba sikuwa nimetenga muda wa kujifunza jinsi Ufalme Wake unavyofanya kazi, alikuwa akisema Yeye hakuwa Bwana wangu hasa. Sikuwa *nikimwamini* Yeye na kumtumikia kikamilifu. Sawa, nilienda kanisani, nilikuwa mkarimu, nilimpenda Mungu, na nilijua nilikuwa safarini kwenda mbinguni. Lakini sikuwa nimetenga wakati wa kujifunza mfumo wa Mungu kuhusu fedha na jinsi Ufalme Wake unavyofanya kazi.

*Kwa kuwa hazina yenu ilipo, ndipo itakapokuwapo na miyo yenu.*  
– Luka 12:34

Soma andiko hilo polepole, “Hazina yenu ilipo, ndipo itakapokuwapo na miyo yenu.” Watu wengi hupenda kugeuza hilo na kusema, “Miyo yenu ilipo, ndipo hazina yenu iliyopo.” Lakini neno halisemi hivyo, na

halifanyi kazi hivyo. Watu wanafikiri linamaanisha wanaweza kumpenda Mungu Jumapili asubuhi na hapo ndipo itakapokuwa hazina. MAKOSA! Hazina yako huwa katika mfumo unaouamini kutosheleza mahitaji yako.

Yesu anasema tumelielewa neno hili kinyume na ukweli!

Mungu anataka kuwa wa kwanza maishani mwetu, wala si pesa. Ikiwa fedha ndizo hazina yetu, basi zitakuwa za kwanza, na zitachukua nafasi ya kwanza katika wakati wetu, shughuli, na upendo wetu. Hii ndiyo sababu haikumbidi Petro aache kazi yake kwenda kutafuta pesa kodi ilipohitajika kulipwa. Hii ndiyo sababu haikufaa Mungu kutufunza kukusanya badala ya kutafuta kwa jasho. Inamlazimu Yesu atufunze njia ya Ufalme, ya jinsi ya

**IKIWA FEDHA NDIZO  
HAZINA YETU, BASI  
ZITAKUWA ZA KWANZA,  
NA ZITACHUKUA NAFASI YA  
KWANZA KATIKA WAKATI  
WETU, SHUGHULI, NA  
UPENDO WETU.**

kumtumaini Mungu kwa ajili ya riziki yetu, na hivyo kuiweka huru miyo yetu kumpenda Mungu kwa dhati! Yesu alisema, Maisha je! Si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi? Alikuwa akisema kwamba maisha si kuwa na vitu. Kusudi la maisha ni kwamba vitu vikutumikie pamoja na utume wako duniani.

Lakini huwa tunaona nini? Watu wengi hukimbia hapa na pale bila kukoma wakivitumikia vitu. Watu hukimbia hapa na pale ili kulipa rehani, bili, malipo ya gari n.k. Yesu anasema huo sio uzima! Sasa, usirudi nyuma kwa andiko lililo kabla ya hili na kuanza kuniambia, “Tazama hapa, Yesu Mwenyewe anasema kuwa na vitu sio jambo nzuri.” La hakusema hivyo. Alisema katika mstari wa 33 kwamba ukitafuta Ufalme wa Mungu kwanza na haki Yake, mengine yote utazidishiwa maishani mwako. Jambo muhimu si pale tunapopata tatizo; bali ni moyo wetu. Ikiwa Mungu hangetaka tuwe na vitu, Yesu angelisema hivyo. Lakini anasema kwamba tutaongezewa mambo haya yote ambayo ulimwengu unayaafuata kwa maisha yetu ikiwa tutaishi kwa njia ya Mungu.

Kwa maneno mengine, maisha hayahusu kutumikia vitu, lakini kwa bahati mbaya, watu wengi wanafanya hivyo. Hawana njia nyingine tofauti; ni watumwa. Haiwezekani kutumikia mabwana wawili, na kutumikia vitu sio uzima. Yesu aliendelea kueleza kwamba kuna mfumo mwingine, mahali pa amani kifedha na riziki panapokuweka huru kuishi maisha mema. Panaitwa Ufalme.

Katika Mathayo 6 Yesu alitupatia mifano miwili ya jinsi Ufalme ulivyo. Alisema, “*Waangalieni ndege wa angani, ya kwamba hawapandi, wala*

*hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao*” (mst. 26).

### Ndege hawana mashamba ya minyoo!

Hawalifanyi jukumu lao wenyewe kujitutia riziki yao ya kila siku. La, Baba huwalisha. Wanapaswa tu kukusanya kile wanachohitaji kila siku. Je, unaona hili? Hawatokwi jasho la taabu chungu kwa ajili ya maisha yao. Wao hukusanya!

### Maua Hayafanyi Kazi wala Kusokota!

*“Na mavazi, ya nini kuyasumbukia? Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo; hayafanyi kazi, wala hayasokoti. Nami nawaambia, ya kwamba hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo la hayo.” (Mst. 28-29).*

Maua hayapitii taabu chungu na jasho kabla ya kujivisha. La, Baba huyavisha. Yesu aliendelea na kutupatia mimi na wewe jibu letu. Kuna njia nydingine ya kuishi, njia ya Ufalme! Yesu alisema, “utafuteni kwanza ufalme Wake, na haki Yake; na hayo yote mtazidishiwa” (mst. 33). Maana ya “Kuutafuta Ufalme wa Mungu” ni nini? Ni kutafuta jinsi unavyotenda kazi! Kujifunza sheria zake. Kujifunza jinsi mfumo wa Mungu unavyofanya kazi!

Ikiwa ningekuangusha kutoka kwa ndege kwa nchi nydingine ambayo hujawahi kwenda hapo awali, jukumu lako la kwanza litakuwa kujifunza jinsi ufalme huo unavyofanya kazi: jinsi wanavyokula, wanavyonunu na kuuza, na sheria zinazowaongoza. Ndivyo ilivyo katika Ufalme wa Mungu. Unapaswa kujifunza jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi ili uweze kufurahia manufaa za kuhusika nao. Ninajua kutohana na uzoefu wa kibinasi ni kiasi gani nilikuwa nikikosa kupata nilichopaswa kupata wakati sikujua jinsi Ufalme unavyofanya kazi. Suluhu lako ni rahisi. Unahitaji mapinduzi ya kifedha. Katika mapinduzi, watu huasi dhidi ya serikali iliyopo na kuweka serikali mpya. Unahitaji kufanya hilo hilo. Unahitaji kuitupilia mbali serikali hiyo ya zamani ya mfumo wa laana ya dunia wenye ukosefu na kukata tamaa ili ufurahie njia mpya ya kuishi—katika Ufalme wa Mungu, usio na ukosefu, na wenye sheria mpya na shangwe kuu!



## SURA YA 11

# KUSAFIRI KWA NDEGE NI RAHISI KULIKO KUTEMBEA!

Ikiwa ungerudi katika historia na ungetaka kusafiri kutoka mji wa New York hadi San Francisco, ungelazimika kwenda kwa mashua. Kabla ya njia ya mashua inayopitia Panama kufunguliwa ingechukua mwaka mzima kuzunguka Amerika Kusini. Baadaye, njia ya kupitia Oregon ilipowekwa, ungesafiri kwa miezi minne. Leo, unaweza kufika huko baada ya masaa manne. Vipi? Kwa kutumia sheria mpya, sheria ya kuinuliwa juu. Sheria hii ya kuinuliwa juu imekuwepo tangu zama zile—ndege wa angani wameitumia kupeperuka kila siku—lakini watu hawakuielewa. Vile vile, Wakristo wengi hawajui sheria za Ufalme, ingawa wamekuwa wakisoma kuzihusu kwa muda mwangi katika maisha yao. Ufalme wa Mungu uko hapa, umo ndani yako, na wewe una haki ya kisheria ya kufurahia manufaa yake. Katika ulimwengu wa asili, sheria za kuinuliwa juu haziondoi sheria ya mvuto, zinaipita. Kwa maneno mengine, mradi uko chini ya sheria za kuinuliwa juu, unasafiri kwa ndege, ingawa nguvu ya mvuto ingali inafanya kazi. Utakubali kwamba ni rahisi zaidi kusafiri kwa masaa manne kuliko kusafiri kwa mashua kwa mwaka mzima! Ikiwa ni kweli, basi anza kufanya mambo kwa haraka na uache njia zako za zamani za kufanya polepole.

Je, umewahi kuona kipepeo aina ya *Monarch*? Hapa Ohio, wakati wa vuli, utaona mamia ya vipepeo hivi vikiruka kuelekea kusini kwa majira ya baridi. Huwa vinasafiri hadi Mexico, safari ya takriban maili 2,000. Lakini ajabu ni kwamba havijawahwi kwenda huko hapo awali! Vinajuaje jinsi ya kwenda au wakati wa kwenda? Ikiwa Mungu aliandaa njia kwa ajili

ya kipepeo ili kiweze kuwa hai, basi ana njia kwa ajili yako pia. Kipepeo huwezaje kufanya hivyo?

Neno hilo linaitwa *metamorphosis* kwa lugha ya Kimombo. Neno la msingi ni “morph,” ambalo linamaanisha mabadiliko. Watu wengi wanajua kwamba kipepeo hakianzi kama kipepeo bali kama kiwavi. Kikiwa kiwavi huwa kinaishi kwa mmea mmoja na kukua mpaka, hatimaye, kinakuwa tayari kuwa na mabadiliko makubwa. Baada ya kiwavi kukua kwa ukubwa fulani, huwa kinajenga nyumba ambapo kitajifungia ndani kwa siku 7 hadi 15. Baadaye, kipepeo hutoka kwa nyumba hiyo kikiwa na sura tofauti wala hakifanyi vile kilivyofanya hapo awali wakati kilikuwa kiwavi. Kinaanza kuishi katika kiwango kipyka kabisa. Kinaruka! Badala ya kuzuiliwa na kukaa kwa mmea mmoja, sasa kinawenza kuruka na kwenda mahali popote kinapotaka. Kinapendeza na kina urembo na uzuri usioliinganishwa na chochote katika maumbile.

Lakini jambo la ajabu zaidi katika uwezo wake ni kuruka mbali na shida. Wajua, kipepeo hiki hakiwezi kuishi kwa baridi inayogandisha ambalo ni jambo la kawaida katika maeneo ya kaskazini. Kinawenza kufa. Lakini Mungu aliandaa njia ili kiumbe hiki kiweze kuruka mbali na shida, kwa kuruka maili 2,000 hadi mahali ambapo hakijawahi kufika hapo awali. Kinajuje njia ya kufika huko? Je, kinawezaje kufanya hivyo? *Metamorphosis*—yaani Mabadiliko. Na Biblia inasema kwamba kuititia kwa mchakato huo huo unaweza kuruka juu ya shida zako pia, hata katika hali ambazo hujui jinsi ya kuzishughulikia, kama kipepeo.

Usiku mmoja, Steve, rafiki yangu, alikuwa akiendesha gari lake kwenda nyumbani kisha akamgonga kulungu. Gari lake liliharibika kabisa. Kwa bahati mbaya, baada ya juma moja gari lao la familia, ambalo lilikuwa limesalia liliharibika pia. Kampuni ya bima ya Steve ilimpa Steve gari ya kutumia kwa wiki mbili bila malipo ili kugharamikia hasara ya gari lake, lakini gari lao la familia halikuwa na bima yoyote ambayo ingesaidia kulibadilisha. Steve na Karen hawakuju la kufanya. Biashara ya Steve ilimtaka awe na gari maana alikuwa na kazi ya kuuza bima na kila jioni alikuwa akitembelea wateja.

Walikuwa wamejifunza kuhusu Ufalme kwa muda wa kutosha kujua kwamba Mungu ndiye alikuwa jibu lao. Wakati huo, hawakuwa na pesa za ziada za kubadilisha magari. Kwa hivyo walijua kwamba Mungu na Ufalme ndio tumaini lao pekee. Wiki mbili za kuwa na gari bila malipo zilikaribia kuisha na bado hawakuwa na jibu. Ajabu ni kwamba usiku kabla ya Steve kurudisha gari hilo, alipigwa simu na mtu fulani aliyesema kwamba alikuwa

na gari alilotaka kutoa, na kwa sababu alijua kwamba Steve alikuwa mshirika wa kanisa letu, alimpigia simu Steve kumuuliza ikiwa alijua familia yoyote katika kanisa letu ambayo ilihitaji gari. Steve alieleza hali yake haraka na kusema angeshukuru kupokea gari hilo kwa ajili yake na familia yake. Hilo lilikuwa jambo jema, lakini Steve alikuwa na watoto sita, na gari hilo dogo halingefaa. Hata hivyo, gari hili kujitokeza hivyo liliwatia moyo.

Jumapili iliyofuata, wote wawili walikuja mbele ya kanisa na kuniomba nisali pamoja nao kuhusu gari waliloamini kupata. Karen alisema, "Mchungaji, tunaamini tutapokea gari aina ya *Honda Odyssey*, kwa imani, na tunataka ukubaliane nasi tunapotoa toleo hili kama mbegu kwa hilo." Nikasema, "Hakika nitafanya hivyo." Kwa hiyo tuliomba. Kwa kweli sikumbuki sasa ni wiki ngapi zilipita, si nyangi, labda tatu au nne, hadi siku tulipopitia nyumbani kwao. Tuliingia jikoni mwao, na pale kwenye mlango wa jokofu lao kulikuwa na picha ya *Honda Odyssey*. Karen alisema kwamba kila siku alipofungua jokofu lao, aliweka mkono wake juu ya picha hiyo na kumshukuru Mungu kwa kuwapa gari hilo.

Baada ya takriban wiki moja, katibu wangu alinipigia simu na kusema, "Mchungaji, tulipigiwa simu ya kushangaza leo." Mtu fulani alikuwa anataka kutoa gari kwa kanisa. Sasa, wakati huo hakuna mtu aliyejua imani ya Steve na Karen kuhusu gari jipya wala kujua aina ya gari walilolitaka. Kwa hivyo nikamwambia katibu wangu, "Ni gari aina gani?" Akasema, "Ni aina ya *Honda Odyssey*." "Iko katika hali gani?" Akasema mtu huyo alisema ilikuwa katika hali nzuri kabisa bila mkwaruzo wowote na ilikuwa imesafiri kwa maili 70,000 tu. Nikamwambia nilijua gari hilo lilitahili kwenda kwa nani. Nilimweleza Drenda kisha nikamwambia ampigie simu Karen. Drenda alipompigia Karen simu, alimuuliza jinsi mambo yalivyokuwa na ikiwa walikuwa na taarifa yoyote kuhusu hitaji lao la gari. Maneno ya kwanza ya Karen yalikuwa, "Naam, ninakaribia, bado siku moja!" Drenda akasema, "Vema, uko karibu kuliko unavyofikiria. Njoo ulichukue."

Napenda hadithi kama hizi, je, wewe? Hadithi yao iliendelea huku Steve na Karen walipozidi kupata uhakika zaidi katika Ufalme kuwapa riziki yao.

Karibu na wakati huo, Steve na Karen walihitaji nyumba. Walikuwa wamekodisha kwa miaka kadhaa, na sasa waliona ulikuwa wakati wa kupata nyumba yao wenywewe; lakini tena, hawakuwa na pesa za ziada za malipo ya kwanza. Walikuwa wameenda kwenye benki nyangi kuuliza kuhusu kununua ardhi, na zote zilihitaji kitu kimoja, malipo ya kwanza ya asilimia 50. Katika wakati huo maishani mwa familia yao changa, hawakuwa na pesa

kiasi hicho ili kuweza kuhitimu. Karen alivunjika moyo kisha akaniuliza kuhusu jambo hilo. Tulikubaliana kwamba Mungu atafanya njia. Kwa hivyo walianza kuangalia ardhi na nyumba mbalimbali.

Moja ya ardhi walizoangalia ilivutia macho yao. Ilikuwa katika eneo ambalo walitamani kujenga nyumba, na iligharimu dola 55,000 kwa ekari 55. Tena, hawakuwa na pesa za malipo ya kwanza. Hata hivyo, nilikuwa nimesikia kuhusu benki ndogo iliyokuwa mashambani, ambayo haikuwa katika eneo hilo lakini ilikuwa umbali wa masaa wawili, nayo ingekubali hisa za kampuni kuwa sehemu ya malipo ya mwanzo ya ardhi. Hili lilikuwa jambo lisilo la kawaida ilipohusu ununuzi wa ardhi ambayo haikuwa na chochote. Niliwaarifu kuhusu hilo, na wakapanga wakati wa kuzungumza na benki. Ardhi ilithaminiwa kwa zaidi ya \$100,000, na benki ilisema hawakuhitaji pesa yoyote kabisa. Kwa hivyo walinunua ardhi hiyo bila malipo ya kwanza na wakajenga nyumba ya kifahari kwenye ekari hizo nzuri za mashambani, yote bila malipo ya kwanza. Steve na Karen wanaendelea kufanikiwa hadi leo kama mimi na Drenda wanapofanya mambo kwa njia ya Ufalme.

Nina hadithi kama hizi katika kanisa langu lote, na ninatarajia kikamilifu hadithi kama hizi katika maisha yako. Mungu anaweza wakati mwingine kufanya mambo ya ajabu na yasiyo kawaida ili kukidhi mahitaji yetu. Mara nyingi, huwa tunajiwekea vizuizi kwa kupima hatma zetu kulingana na kile tunachofikiri kinawezekana. Lakini mambo yote yanawezekana kwa Mungu, ikiwa tutaliruhusu Neno la Mungu libadili mawazo yetu.

*Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpare kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.*

– Warumi 12:2

Sisi waumini hatupaswi kufuata mtindo wa ulimwengu huu. Paulo alirejelea mfumo wa laana ya dunia na mtindo wake wa maisha, na hasa, jinsi tunayyofikiri. Je, umewahi kushona vazi au kujenga kitu kutoka kwa mchoro? Ikiwa ndio, na hukupenda matokeo yake, ni nini kitakachotokea ukijaribu tena na mchoro uleule? Utapata matokeo yale yale. Kwa hivyo Paulo alisema kwamba tunahitaji kugeuzwa kwa kufanya upya katika nia zetu; tunahitaji kubadilisha muundo tunaotumia kuishi maisha yetu. Tunahitaji kufikiri kwa njia tofauti na ile ya ulimwengu.

Neno hilo “kugeuzwa” ni neno lile lile tulilolizungumzia, “morph,” ambalo linamaanisha mabadiliko. Tunahitaji *metamorphosis*—yaani

**MARA NYINGI, HUWA  
TUNAJIWEKEA VIZUIZI  
KWA KUPIMA HATMA  
ZETU KULINGANA NA  
KILE TUNACHOFIKIRI  
KINAWEZEKANA.  
LAKINI MAMBO YOTE  
YANAWEZEKANA  
KWA MUNGU, IKIWA  
TUTALIRUHUSU NENO  
LA MUNGU LIBADILI  
MAWAZO YETU.**

huo? Ukimtzama kiwavi na kufikiria safari ya maili 2,000 ambayo lazima afanye, utatikisa kichwa chako tu na kusema, “HAIWEZEKANI!” Lakini katika Ufalme wa Mungu, mambo yote yanawezekana. Nitazame. Kipindi changu cha televisheni kinapoanza, huwa kinanirejlea kama mtaalamu wa masuala ya fedha. Wakati mwagine mimi hukumbuka siku zangu nilipokuwa kiwavi na ninasema, “Hilo linashangaza!”

Ninapozungumza juu ya kuruka, nakumbuka mara tu mimi na Drenda tulipoanza kujifunza jinsi Ufalme unavyofanya kazi, niliamua kwamba nilitaka ndege. Nilikuwa rubani tangu nilipokuwa na umri wa miaka 19 na kila wakati nilikodisha ndege, lakini sikuwa nimewahi kumiliki yangu binafsi. Bila shaka unajua kwa nini; sikuwa na pesa za kuinunua. Kwa hivyo siku moja niliamua jambo gumu; huku nikijambia kwamba ndege si kitu kisichowezekana kwa Ufalme wa Mungu. Mbona niuhekee Ufalme vizuizi kwa yale niliyofikiri kwamba yangewezekana kwangu? Kwa hiyo niliandika hundi, niliandika orodha ya maelezo kwenye sehemu ya maelezo, “Kwa ajili ya ndege yangu.” Niliweka mikono yangu juu ya hundi hiyo kisha nikaituma kwa huduma fulani, huku nikiamini kwamba nilipokea ndege hiyo nilipoomba, kulingana na Marko 11:24.

*“Kwa sababu hiyo nawaambia, Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.”*

mabadiliko! Tunahitaji kufikiri kama Mungu. Tunahitaji kuwaza mawazo ya Ufalme. Badala ya kuwa na mawazo yenye mtazamo wa kiwavi, aliyanaswa, na aliyezekumiwa kifo katika majira ya baridi kali, tunahitaji kumtumaini Mungu kwa njia mpya kabisa ya maisha. Hapo ndipo tu tunapoweza kuruka juu ya matatizo yetu na kutayarishwa kujua mapenzi ya Mungu makamilifu na ya kupendeza katika kila hali. Tusipokumbatia mabadiliko hayo ya fikra, mawazo yetu ya zamani yatakuwa yakisema kila mara, “La, hapana, siwezi kufanya hilo. LA, sioni jinsi hilo linavyoweza kutokea.”

Ni nani angewahi kufikiria kwamba kiwavi huyo asiyependeza angeweza kuruka kwa neema na ukamilifu kama

Baada ya majuma machache nilienda kwa daktari kufanyiwa uchunguzi wa kawaida wa kimwili. Nilishangaa daktari aliposema, “Je, unamjua mtu yeoyote anayetaka kununua ndege?” Nilifikiri hilo lilikuwa jambo la ajabu. Nikauliza, “Ni ndege aina gani?” Nilistaajabu na kusisimka maana hiyo ndiyo ndege hasa niliyoaminikupata nilipoomba. Kwa hivyo nilimuuliza ni wapi ningeweza kwenda ili kuiona, naye akaniambia ilikuwa kwenye uwanja wa ndege wa kaunti iliyokuwa karibu na nyumba yangu. Hebu nifafanue. Nyumba yangu iko kwenye upande mmoja wa uwanja wa ndege wa kaunti. Kila ndege inayotua lazima iruke moja kwa moja juu ya nyumba yangu. Kutazama ndege zikija na kuondoka siku nzima na ukweli kwamba njia ya ndege ya kurukia ilikuwa maili moja tu kutoka kwa mlango wangu ilimaanisha kwamba nilipaswa kuwa na ndege!

Kwa hivyo nilimpigia simu rafiki yangu ambaye amekuwa rubani maisha yake yote na pia alikuwa mwali muwa kuendesha ndege ili aende nami kuichunguza. Tulipoitazama ndege, nilijua kwamba hii ilikuwa ndege yangu; ilikuwa maridadi! Ilikuwa ile niliyotaka hasa. Lakini ilikuwa na tatizo moja tu, tatizo lilelile nililokuwa nalo kwa miaka mingi ilipohusu suala la kumiliki ndege—sikuwa na pesa za kuinunua. Umewahi kuwa na tatizo hilo? Lakini safari hii sikukata tamaa kwa woga. Nilijua kwamba hii ilikuwa ndege yangu; lakini bado sikujua jinsi Mungu angeleta pesa hizo.

Miezi michache awali, mimi na Drenda tulikuwa tukitafuta nafasi ya ofisi kwa ajili ya kampuni yetu. Tulijua mahali tulipotaka biashara yetu iwe, lakini hakukuwa na mahali katika eneo hilo; kwa hivyo tulianza kuangalia maeneo mengine. Tulipata majengo kadhaa ambayo tulikuwa karibu kununua, lakini tulisita mioyoni mwetu. Tuliendelea kurejea kwa eneo lile tulilojua ofisi ilipaswa kuwa, huku tukitarajia kupata mahali. Tulipokuwa tukiomba kuhusu uamuzi huo, siku moja babangu alinipigia simu akasema maneno haya, “Najua, utasema ni Mungu, lakini mimi na mamako tumezungumza, na tunataka kukupa jengo tunalomiliki kuwa ofisi yako.” Jengo walilolimiliki lilikuwa mahali hasa nilipotumaini kupata nafasi ya kuhamia. Nilipigwa na mshtuko!

Ili kuelewa kile kilichotokea unahitaji kujua kwamba babangu hakuwa muumini wakati huo. Alikuwa mbishi sana wakati wowote Mungu alipotajwa. Kwa kweli, ilikuwa vigumu sana kiasi kwamba singeweza kuzungumza naye kuhusu Mungu. Hata niliomba kwamba Mungu atume mtu mwingine ili amhubirie kuhusu Kristo. Nilijua kwamba singeweza kumfikia; hakutaka kunisikiliza. Lakini aliokoka baada ya miaka michache akiwa na umri wa miaka 80. Cha kushangaza ni kwamba, aliokoka

alipokuwa akitazama matangazo yetu ya televisheni na kuona mambo yote ya ajabu ambayo Mungu alikuwa akifanya. Alitumia miaka mitatu na nusu ya mwisho wa maisha yake akiwa mtu aliyebadilika na alienda kanisani kila wikendi.

Siku moja punde tu baada ya ibada, nilimwona babangu katika ukumbi wa kanisa akizungumza na mshirika wa kanisa langu ambaye alikuwa amemfahamu kwa miaka mingi. Nilipokuwa nikitembea kuelekea upande wao, nilimsikia mtu huyo akimuuliza babangu sababu alianza kuja kanisani. Babangu alijibu kwamba alikuwa ameona mambo mengi sana ambayo hawezi kueleza. Bwana asifiwe! Hivyo ndivyo inavyotakiwa kuwa.

Lakini tunahitaji kurejea kwenye ile simu kuhusu jengo, kabla ya babangu kuokoka. Mimi na Drenda tulishtuka kwamba alitupatia lile jengo. Tulijua ni Mungu, bila shaka; na Baba alipotupigia simu tulimwambia, “Ndio, Baba, umesema kweli; huyu ni Mungu!”

Jengo hilo lilihitaji kufanyiwa ukarabati mwangi ili lifike kiwango kilichohitajika katika kuweka ofisi ya biashara yetu humo. Baba alinipa jengo hilo mwezi wa Desemba, na nilihitaji kusubiri hadi majira ya masika kabla ya kuanza ukarabati. Jengo lilikuwa limefungwa katika msimu wa baridi, na baba yangu alisema alikuwa amefunga maji. Hivyo ndivyo mambo yalivyo kuwa wakati wa majira ya baridi kali hadi karibu wiki moja baada ya kwenda kuangalia ile ndege. Kisha kakangu alinipigia simu akaniambia nifike haraka kwenye jengo langu, kwa kuwa maji yalikuwa yakiniririka kutoka ndani yake hadi barabarani. Hali ya hewa ilikuwa imepata joto na inaonekana babangu alikuwa amekosea; maji hayakuwa yamefungwa wakati wa majira ya baridi. Nilienda hadi kwenye jengo hilo, na katika bafu iliyokuwa juu kwa ghorofa ya jengo maji yalikuwa yamemwagika kwa siku kadhaa au hata majuma. Ukuta wote wa kadibodi kwenye ghorofa ya chini ulikuwa umeanguka.

Ninajua kwamba hii inasikika kama hadithi mbaya, lakini usichojuua, na kaka yangu hakujua, kwamba tayari nilikuwa nimesaini mkataba wa kuondoa ukuta huo wa kadibodi katika jengo zima, na pande zote za nje kuondolewa, na usanifu kamili wa jengo kuanza baada ya wiki kadhaa. Kwa hivyo uharibifu huu wa maji haukuwa shida hata kidogo maana kila kitu kilichoharibika kilipaswa kuondolewa. Lakini fahamu hili—kampuni yangu ya bima iliniandikia hundi ya kugharamikia uharibifu huo, ambayo ilikuwa pesa za kutosha za kununua ndege yangu!

Je! Hilo lilinitendekea? Naam, nilipokea ndege yangu na jengo la ofisi, bila deni na kukimbia hapa na pale kulifanya litokee. Sasa ninapoendesha

ndege hiyo, na kupaa juu ya shamba letu, huwa nakumbuka kwamba kitendo hiki ni kama Ufalme wa Mungu. Utendaji wake na sheria zake hutupa fursa ya kuishi maisha katika kiwango tofauti kabisa. Kama ule mfano wa kiwavi na kipepeo, kiwavi hangeweza kamwe kufanya miguu yake kukimbia haraka vya kutosha kufika Mexico. Maisha yangu, ambayo yalikuwa yamezuiliwa na unusuru na hofu, sasa yalikuwa yamebadilishwa na Ufalme wa Mungu. Kwa kutumia sheria zake, niliweza kupata maisha yenyewe uwezekano usio na kikomo.

Ninapohitimisha kitabu hiki, nataka kukuachia andiko moja. Nina hakika ni andiko ambalo umesikia maisha yako yote. Lakini nafikiri litakuwa na maana mpya kwako sasa.

*Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenyewe kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira Yangu ni laini, na mzigo Wangu ni mwepesi.*

– Mathayo 11:28-30

Yesu alikuja kuvunja nira yetu, taabu chungu na jasho la mfumo wa laana ya dunia. Sasa tunapaswa kuchukua nira Yake (yote yamekwisha) na kupata pumziko (siku ya saba, Sabato ya kweli) kwa ajili ya roho zetu.

Utaweza kujiona mambo ya ajabu maishani mwako utakapofanya yale ambayo Potifa alifanya, kulingana na mtindo wa maisha ya Ufalme. Fanya uamuza leo kujipatanisha na sheria za Ufalme wa Mungu na utaanza kufurahia nguvu za kuwa mwaminifu. Anzisha mapinduzi yako ya kifedha leo, tupilia mbali njia ya zamani ya kuishi, serikali ya zamani, mfumo wa laana ya dunia ya umaskini, magonjwa, na kukata tamaa. Acha njia zako za zamani za kiwavi na uanze kupaa juu kwa kutumia sheria za Ufalme ambazo Yesu alikutayarishia njia zikufanyie kazi. Wewe ni raia wa Ufalme huo.

Una haki za kisheria!



# **MAPINDUZI YAKO YA KIFEDHA**

# **Nguvu ya kuwa Mwaminifu**

**Soma kitabu hiki ikiwa...**

**UMECHOKA NA HALI YAKO YA KIFEDHA**

**UNATAKA KUTOKA KWA MADENI**

**HUJUI MAHALI PA KUANZIA**

**HUNA MATUMAINI**

Gary Keesee amekuwa katika hali hii mwenyewe. Kwa miaka tisa mirefu sana, maisha yake yalikuwa katika msukosuko mkubwa wa kihisia kutohana na hali yake mbaya ya kifedha. Kupigwa simu na wakopeshaji, madai ya ushuru, kuhukumiwa, na aibu zilikuwa kawaida maishani mwake. Lakini yote yalibadilika siku moja Mungu alipozungumza na Gary kuhusu fedha zake na kumpa siri iliyombadili kwa kiasi kikubwa! Alitoka kwa madeni, akaanzisha kampuni za mamilioni ya dola, na sasa anashiriki mambo muhimu yaliyobadilisha maisha yake kwenye kipindi chake cha televisheni kinachoitwa, *Fixing the Money Thing* kinachoonyeshwa kila siku katika kila eneo ulimwenguni. Gary amefundisha kuhusu dhana hizi kwa mamia ya maelfu ya watu duniani kote katika kongamano na mafundisho ya kibinagsi. Anakubali kwamba kuna kanuni nydingi zinazohitajika katika kuishi maisha yenye mafanikio. Lakini ikiwa atashiriki moja tu, itakuwa ni hii. Gary anakualika ujunge na mapinduzi na ubadilishe fedha zako kwa kiasi kikubwa kupitia kwa *Nguvu ya kuwa Mwaminifu*.



Gary Keesee ni mwandishi, mmnenaji, mjasiriamali, mtaalamu wa fedha, na mchungaji ambaye ana shauku ya kusaidia watu kuwa washindi maishani, hasa katika maeneo ya imani, familia, na fedha. Gary na mkewe, Drenda, wameanzisha biashara kadhaa zilizo na fanaka, na ndio waanzilishi wa huduma iitwayo Faith Life Now, ambayo ina vipindi viwili vya televisheni—*Fixing the Money Thing* na *Drenda*, kongamano kote ulimwenguni, na rasilimali za vitendo. Wao pia ni wachungaji wa Kanisa la Faith Life karibu na Columbus, Ohio.